

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 10 Julai, 2007**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 176

**Matengenezo ya Barabara za Halmashauri ya Nzega**

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ni kiungo muhimu cha mawasiliano kwenye masoko ya ndani na utandawazi kwa ujumla na kwa kuwa, Halmashauri ya Nzega haina uwezo wa kuzihudumia barabara za vijijini:-

- (a) Je, Serikali ipo tayari kuzifanyia matengenezo barabara hizo na baadaye zirejeshwe Halmashauri?
- (b) Je, Serikali ipo tayari kuongeza fedha toka Mfuko wa *Road Toll* kwa kila Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ina mtandao wa barabara wenye urefu wa takriban kilomita 1010 kwa mgawanyo ufuatao:-

- %Barabara Kuu (*Trunk Roads*) km 167;
- % Barabara za Mkoa (*Regional Roads*) km 145;
- % Barabara za Wilaya (*District Roads*) km 207

%Barabara za Mjini (*Urban Roads*) kwa maana ya mitaa, km50;  
% Barabara za Vijiji (*Community Roads*) km 445.

Kati ya barabara nilizozitaja hapo juu barabara za Wilaya na barabara za Mjini zinahudumiwa na fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Funds*).

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara inatoa fedha za matengenezo ya barabara katika Halmashauri zote nchini kwa barabara zilizo katika hali ya kutengenezeka. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega barabara zinazopata fedha za matengenezo ni zile barabara za Wilaya pamoja na barabara Mjini.

Hata hivyo, iwapo Halmashauri inaona ni muhimu kwa baadhi ya barabara za vijijini kupata matengenezo makubwa kutokana na umuhimu wake ni vema Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ikazipa kipaumbele barabara hizo ili ziweze kujumuishwa kwenye baadhi ya miradi mingine kama vile *TASAF* na miradi inayotekelezwa kwa kutumia fedha za Halmashauri.

Iwapo barabara za vijijini zitafanyiwa matengenezo na kukidhi vigezo vya kuwa barabara za Wilaya, barabara hizo zitajumuishwa kwenye orodha ya barabara zitakazopata fedha za matengenezo kutoka Mfuko wa Barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza fedha za matengenezo ya barabara kutoka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwa mwaka 2004/2005 ilipata kiasi cha shilingi milioni 139.25; kwa mwaka 2005/2006 ilipata kiasi cha shilingi milioni 168.55; na kwa mwaka 2006/2007 ilipata kiasi cha shilingi milioni 147; kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008 kiasi kimeongezeka hadi kufikia shilingi milioni 419.61.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega pia kwa mwaka wa fedha 2007/2008 itapatiwa fedha za *Local Government Transport Programme* kiasi shilingi milioni 73,102,930/= kwa ajili ya utengenezaji wa barabara zake. Ofisi yangu itasambaza katika Bunge lako Tukufu orodha ya fedha za Mfuko wa Barabara zitakazokwenda kwenye Halmashauri moja kwa moja. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ongezeko la fedha za Mfuko wa Barabara kwa mwaka huu ni kubwa ikilinganishwa na miaka iliyopita kwa Halmashauri zote nchini.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninaishukuru Serikali kwa ongezeko hilo ambalo wameipa Halmashauri yetu ya Nzega. Nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, upokee orodha ya barabara na hazibadilishwi ni zile zile mwaka hadi mwaka. Je, kuna utaratibu gani mzuri wa kuongeza mtandao wa barabara uko vijijini ambako kuna wananchi wengi, wakabadilisha na kuongeza barabara zingine mpya?

La pili, kwa kuwa katika Bajeti ya mwaka huu 2007/2008 kuna ongezeko kwa ajili ya utengenezaji wa barabara katika mafuta ya petroli na dizeli. Je, ongezeko hilo litazinufaisha vipi Halmashauri zetu za Wilaya na zenyewe zitakumbukwa kwenye ongezeko hilo la mafuta?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, nikianza na swali la pili. Kila Serikali inapongeza mapato yake na ndivyo hivyo Bajeti zetu katika Halmashauri zinaongezeka. Kwa hiyo, hilo ongezeko la mafuta pia tutafaidika hata sisi watu wa Serikali za Mitaa yaani katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, ongezeko la *levy* zetu katika Serikali pia litatufaidisha hata sisi katika Halmashauri. Haitatenga kwamba ni Serikali Kuu itapata tu au watu fulani tu ndiyo watapata. Kwa hiyo, sisi pia tutafaidika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa orodha ya barabara za Halmashauri kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba iwapo Halmashauri inaona kwamba kuna barabara fulani ni muhimu kwa ajili ya uchumi wake, ni wao ambao wanapanga kuiendeleza hiyo barabara na hiyo barabara ikifikia vigezo vya kuingizwa kwenye barabara za Wilaya au barabara za Mkoa basi ni wao wanaanza huko huko kwenye Halmashauri ku-*up grade* hiyo barabara na kupeleka mapendekezo katika Ofisi yangu na baadaye tutahalalisha kwamba iwe ni barabara ya Wilaya kulingana na vigezo ambavyo tumeviweka. (*Makofi*)

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna Halmashauri karibu nane ambazo ni mpya. Je, Serikali iko tayari kuzipangia fedha za barabara tofauti na zile Halmashauri Mama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri mpya zilizoanzishwa mwaka huu zimepangiwa Bajeti yake maalum. Kwa hiyo, vitu vyote kama barabara pamoja na mambo mengine yamepangiwa kulingana na Bajeti yake. Lakini hawatapata mgao wa ziada kulingana na Bajeti ilivyo, mgao unakuwa sawa kwa Halmashauri zote.

Na. 177

### **Uhitaji wa Hospitali ya Wilaya Kishapu**

**MHE. FRED M. TUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Wilaya ya Jimbo la Kishapu wapatao 242,000 wanakabiliwa na matatizo ya kupata matibabu ya kufaa wanapougua kutokana na kutokuwepo kwa hospitali ya Wilaya ya Kishapu; na kwa kuwa, katika Ilani ya

Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, wananchi wa Kishapu waliahidiwa kujengewa hospitali ya Wilaya:-

(a) Je, Serikali ambayo ndiyo inayotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, itatekeleza lini ahadi ya kujenga hospitali ya Wilaya katika Jimbo la Kishapu kama ilivyoahidi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuviboresha na kuvipanua Vituo vya Afya vya Nhobola, Kishapu, Songwa na Bunambiyu ili wananchi wa Tarafa za Nyegezi, Mondo na Kishapu waweze kupata huduma za afya zilizo bora na kwa wakati muafaka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuweka kumbukumbu sahihi, Wilaya ya Kishapu ina watu wapatao 291,000 na siyo 242,000 kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Wilaya ya Kishapu haina hospitali ya Wilaya kwa sasa, bali kuna hospitali binafsi inayomilikiwa na mgodi wa Almasi wa Mwadui. Hospitali hii hutoa huduma kwa wafanyakazi wa mgodi pamoja na jamii inayozunguka mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 juu ya ahadi ya kujenga hospitali ya Wilaya ya Kishapu, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu iko katika maandalizi ya awali ya ujenzi wa hospitali hiyo. Hadi sasa baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kutenga eneo la hekta 43 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo. Eneo hilo limepimwa katika Kitongoji cha Ugunigu karibu na makazi mapya yaliyotengwa katika Mji wa Mhunze. Shughuli zingine ni utayarishaji wa michoro, makadirio ya gharama za ujenzi na fidia ya eneo. Pia ramani ya majengo na makadirio ya gharama (*Bill of Quality*) za ujenzi ziliwasilishwa katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kupata idhini ya kuanza ujenzi wa hospitali hiyo. Shughuli za awali zimegharimu jumla ya shilingi milioni 14,500,600/=.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuviboresha na kuvipanua Vituo vya Afya vya Nhobola, Kishapu, Songwa na Bunambiyu ili wananchi wa Tarafa ya Negezi, Mondo na Kishapu kupata huduma za Afya zilizo bora na kwa wakati muafaka Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(a) Katika Kituo cha Afya Nhobola:-

- (i) Jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje (*OPD*) limekarabatiwa;
- (ii) Nyumba 5 (tano) za watumishi ikiwemo ya Mganga Kiongozi zimekarabatiwa;

- (iii) Wodi za wanaume na wanawake zimekarabatiwa;
  - (iv) Tenki la maji ya kuvuna kutokana na mvua limejengwa; na
  - (v) Shughuli hizi zimegharimu kiasi cha Sh.17,000,000.
- (b) Katika Kituo cha Afya Kishapu:-

- (i) Jengo la kuhifadhia madawa na vifaa tiba limekarabatiwa;
- (ii) Jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) limekarabatiwa;
- (iii) Nyumba ya kuishi daktari imekarabatiwa;
- (iv) Shughuli hizi zimegharimu kiasi cha shilingi 11,004,110/=.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na kukarabati wa Vituo vya Afya vya Binambiyu na Songwa kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, vilevile Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inaendelea kukarabati Zahanati ya Seke – Bugoro iliyopo Kata ya Seke – Bugoro, Zahanati ya Badi iliyopo Kata ya Mwakipoya na Zahanati ya Seseko iliyopo katika Kata ya Itilima. Halmashauri pia ina magari mawili ya kubeba wagonjwa aina ya *Toyota Land Cruiser* yenye namba za usajili SM 4469 na SM 4679 ambayo hutoa huduma ya kuwapeleka wagonjwa wanaopata rufaa na dharura ili kuwapeleka hospitali ya Mkoa ambayo iko umbali wa kilometa 58.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Serikali kwa swali langu nililouliza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, kwa kuwa Serikali inatoa fedha katika Halmashauri za Wilaya kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Afya katika Wilaya mbalimbali hapa nchini. Je, Serikali haioni umuhimu kwa sasa kutoa fedha kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa ajili ya ukarabati wa Vituo vya Afya vya Nhobola, Songwa, Bunambiyu na Kishapu?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kishapu ambayo itajengwa Mhunze itachukua muda mrefu; na kwa kuwa huduma kwa sasa zinazotolewa na Kituo cha Afya Kishapu zinashindwa kukabiliana na msongamano mkubwa wa wagonjwa wanaokuja kutoka katika sehemu mbalimbali katika Wilaya ya Kishapu; na vilevile kutoka Wilaya ya Meatu. Je, Serikali inaweza kuwasaidia wananchi kwa kuongeza huduma ya madawa na huduma nyingine za afya na kuongeza vilevile wafanyakazi katika Kituo hicho cha Afya cha Kishapu ili kiweze kukabiliana na msongamano mkubwa wa wagonjwa kwa sasa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kuanzia mwaka 2002 ilianza mpango wa ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati na ilitoa fedha hizo kwa awamu katika Wilaya mbalimbali. Kwa mwaka huu 2006/2007 Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya Wilaya 35. Kwa mwaka 2007/2008 Wilaya ya Kishapu ni mojawapo ambayo itapata fedha hizo za ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati. Kwa hiyo, namhakikishia programu hii ya ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati inaendelea kwa awamu na Kishapu awamu yake ikifika fedha zitatolewa.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, ni kweli kwa sasa hivi huduma za Afya katika Wilaya ya Kishapu zinatolewa hasa na Kituo cha Afya cha Kishapu. Kwa kweli Serikali inajitahidi kuongeza madawa katika Kituo cha Afya cha Kishapu kulingana na *population* ya wagonjwa wanaohudumiwa katika Kituo cha Afya hicho. Kwa upande wa wafanyakazi Serikali kwa kweli inajitahidi na inafanya kila njia kuongeza idadi ya wafanyakazi wa afya katika Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na Hospitali mbalimbali. Mheshimiwa Mbunge naomba awe na subira wakati Serikali ikiwapanga watumishi mbalimbali katika Vituo vya Afya na Zahanati; na Kituo cha Afya cha Kishapu kitapewe kipaumbele pindi hapo wafanyakazi wengi watakapopatikana.

Na. 178

### **Barabara ya Kisili - Buhigwe na Daraja katika Mto Luiche**

**MHE. MANJU S. MSAMBYA (K.n.y. MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Kisili-Buhigwe katika Mkoa wa Kigoma hupita karibu na Mto Luiche; na kwa kuwa, wakazi wa kijiji cha Che-Nyamihanga kilichopo pembezoni mwa mto huo wanapata taabu kubwa sana ya kuvuka kwani wanatumia kivuko cha kamba ambacho ni hatari sana kwa wakazi wa sehemu hizo:-

Je, Serikali haioni kuwa, ni vema wananchi hao wakajengewa daraja kwenye mto huo ili waweze kuishi kwa amani na kuwa na mawasiliano na wananchi wenzao katika vijiji vya Kinazi, Kimagu, Jande na sehemu nyingine zenye huduma za afya na elimu kama vile Malyazo, Munaile na Kasulu?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogomyi, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara Kasili- Buhigwe yenye urefu wa kilometa 65 ni ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Kigoma. Barabara ndogo inayochepeka kwenye barabara ya Kisili – Buhigwe na kivuko katika mto wa Luiche ambavyo vinaunganisha Kijiji cha Che – Nyamihanga na vijiji vya Kinazi, Kimangu, Jande, na kadhalika. viko chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Hivyo ili kuondoa adha kwa wananchi wanayoipata katika kuvuka mto Luiche nashauri Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (*TAMISEMI*) kupitia

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu wachukue hatua zinazostahili ikiwa pamoja na kupata fedha na kufanya maandalizi ya kujenga daraja hilo katika mto huo. Wizara yangu kupitia Ofisi ya *TANROADS* Mkoa wa Kigoma iko tayari kutoa ushauri wa kitaalam kama utahitajika.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ni kweli kwamba barabara aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri iko chini ya Halmashauri.

Lakini tumeona uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ni mdogo ndiyo maana ombi linaletwa kwa Wizara ya Miundombinu ili iweze kusaidia kujenga daraja hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba itakuwa busara kuisaidia Halmashauri ya Kasulu ili daraja hilo liweze kujengwa na kuwasaidia wananchi hao kutokana na adha wanayoipata?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema barabara iliyotajwa ni ya Halmashauri kama alivyokubali na sisi tunayo hiyo barabara yetu na kama tulivyosema hata *TANROADS* kwa kweli wana upungufu wa fedha si kwamba wao wana kiasi kikubwa sana cha fedha hata barabara zao zingine zina matatizo makubwa. Kwa hiyo, nashauri tu kwa utaratibu ambao Halmashauri itakuwa imeupanga na kwa taarifa nilizonazo kwa kweli Halmshauri wameanza kazi wamejenga kalvati 9 na wanajipanga sasa kutoa *tender* kwa ajili ya kujenga daraja; na kwa kuwa fedha za *Road Fund* zitaongezeka mwaka huu wa fedha; nadhani Halmashauri ikijipanga vizuri na kuweka vipaumbele wataweza kukamilisha kazi hiyo.

Na. 179

#### **Taasisi ya Sayansi na Teknolojia - Mbeya**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, ili nchi iwe na Maendeleo ya kasi ni sharti ijiingize kwa vitendo katika kukabiliana na changamoto za Maendeleo kwa kutumia Sayansi na Teknolojia; na kwa kuwa moja ya vitendo hivyo ni kusimamia na kujenga Vyuo Vikuu ili kukidhi mahitaji ya Taifa:-

Je, ni lini Serikali itatimiza azma ya Baba wa Taifa ya kuitangaza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya (*MIST*) kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mpesya, Mbunge wa Mbeya Vijijini, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo ili kutoa ufafanuzi kuhusu tofauti ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Ufundi:-

Mheshimiwa Spika, majukumu ya vyuo vikuu ni pamoja na:-

- (i) Kufundisha;
- (ii) Kufanya utafiti (*Research*); na
- (iii) Kutoa ushauri (*Consultancy*).

Aidha, Vyuo Vikuu hutoa wataalam walioboea katika fani mbalimbali na hujishughulisha sana na utafiti na uzalishaji wa maarifa (*knowledge creation*). Hata hivyo kufanya utafiti peke haitoshi kwani utafiti hauna budi kuchapishwa ili kuisaidia jamii.

Kwa upande mwingine Vyuo/Taasisi za Ufundi zina jukumu la kufundisha kwa kuweka umuhimu mkubwa katika kukuza stadi (*skills development*) kwa kuangalia mahitaji halisi ya jamii. Wahitimu kutoka katika Vyuo/Taasisi hizo huweza kufanya kazi katika mazingira mbalimbali yaani wako *Flexible*.

Mheshimiwa Spika, mahitaji yetu kwa sasa ni wahitimu wa kada ya kati kutokana na ukweli kwamba kwa sasa tunatoa wahitimu wengi katika kada ya juu (shahada) kuliko kada ya kati (*Technicians*). Mfano kwa upande wa madini, kuna upungufu mkubwa wa kada ya kati (*Technicians*) kiasi kwamba sekta hiyo inabidi iagize wataalam kutoka Kanada, Australia na Afrika Kusini. Vilevile kuna upungufu mkubwa wa mafundi sanifu katika taaluma za:-

- Uhandisi;
- Afya;
- Hoteli ya Utalii; na
- Maabara (mashule na hospitalini).

Viwango vya Kimataifa vinaonyesha kuwa uwiano wa wahandisi na kada ya kati ni 1:2:25 (*1 Engineer - 5 Technicians - 25 Artisans*).

Kwa hiyo, kwa sasa kuna uhitaji mkubwa wa kada ya kati (*Technicians*) katika nchi yetu. Baada ya maelezo hayo mafupi naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mpesya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo niliyotoa hapo juu na kwa kuzingatia matamko ya Serikali ya tarehe 1 Februari, 2006 na 31 Mei, 2007, Serikali haina mpango wa kuigeuza Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*) kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia.



**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya kuanzisha Chuo hicho cha Mbeya na kwa kufuatilia maagizo hata ya Baba ya Taifa huko nyuma ilikuwa ni kukifanya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia; sasa pamoja na maelekezo hayo ya Naibu Waziri kwamba Serikali haina nia. Je, Serikali imepingana na azma nzuri ile ya Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa ya kukifanya Chuo hiki kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia?

La pili, kwa kuwa kulikuwa na timu ya wataalam ambayo ilikuwa imeshateuliwa na Serikali yenyewe na kutoa mapendekezo kuwa Chuo hiki kiwe sasa na hadhi ya *MAST* kutoka *MIST*. Je, Serikali imeyazika mapendekezo hayo wakati yenyewe ilikuwa imeunda timu hiyo ya wataalam?

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pili, nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godfrey Zambi kama ifuatavyo:-

Uamuzi huo uliotolewa haupingani na yale mawazo yaliyokuwepo hapo awali ya Baba ya Taifa kwamba Chuo hicho hatimaye kiwe Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia badala yake Serikali imeweka mpango kamili wa kuanza Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Kimataifa kitachoitwa *Nelson Mandela Institute of Science and Technology* kule Karangai Arusha.

Kwa hiyo, yale mawazo yaliyokuwepo Mbeya sasa yanahamia kujenga Chuo Kikubwa zaidi kule Arusha ili kusudi Mbeya izidi kutoa wataalam wa katikati. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante. Naona watu wa Mbeya na Nyanda za Kusini wanajisikia vibaya lakini ndiyo maamuzi.

Na. 180

### **Utaratibu wa Utungaji wa Mitihani Kwa Wahitimu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia inatoa mafunzo ya Ufundi katika ngazi ya cheti cha Ufundi Mchundo (*FTC*) na Stashahada ya Juu ya Uhandisi (*ADE*) katika fani mbalimbali; na kwa kuwa, taasisi hiyo imekuwa na migogoro mingi sana tangu ikijulikana kama *Dar es Salaam Technical College*, kwa wanafunzi kudai haki zao

mojawapo ikiwa ni kukataa kutungiwa mitihani na *NECTA* hasa kwa wale wanaohitimu Stashahada; na kwa kuwa, Sheria Na. 6 ya mwaka 1997 iliyounda Taasisi hiyo imeipa mamlaka kutunga mitihani na kutoa tuzo kwa wahitimu wake:-

- (a) Je, kwa nini wahitimu kwenye taasisi hiyo wanaendelea kutungiwa mitihani ya kuhitimu na Baraza la Mitihani la Taifa *NECTA* kinyume na Sheria?
- (b) Je, ni nini hatma ya wanafunzi waliofukuzwa baada ya kugoma kufanya mitihani iliyotungwa na *NECTA* mwaka 2005, na kulazimishwa kurejea kwa masharti ya kufanya mitihani hiyo ya *NECTA* na *Projects* kwa gharama zao wenyewe na huo sio uonevu?
- (c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, madai ya wanafunzi hao ni ya msingi na ni sahihi na kwamba Serikali ilishughulikia suala hilo na kuhakikisha kwamba, sheria iliyowekwa kusimamia masuala hayo inafuatwa ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b), (c) kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) ndilo lenye jukumu la kusimamia na kuendesha mitihani ya ufundi. Hata hivyo, kwa kuwa Baraza hilo lilikuwa halijawa na uwezo wa kusimamia na kuendesha mitihani hiyo, liliingia mkataba na Baraza la Mitihani Tanzania (*NECTA*) ili *NECTA* iendeshe mitihani hiyo kwa niaba ya "*NACTA*" na hapo *NECTA* itakapojenga uwezo wa kuchukua jukumu lake. Kwa sasa, *NACTE* imekwishakujenga uwezo wa kutekeleza jukumu lake la kusimamia na kuendesha mitihani ya Elimu ya Ufundi. Aidha, *NACTE* imeweka taratibu na vigezo vitakavyotumiwa ili kuwezesha Chuo au Taasisi iruhusiwe kuendesha mitihani yake. Kwa Vyuo/Taasisi ambazo zimekidhi vigezo vilivyowekwa na *NACTE* zimeruhusiwa kuendesha mitihani yake. Kwa Taasisi ambazo hazijatimiza vigezo vilivyowekwa mitihani yao inaendeshwa bado na *NACTE*.

(b) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi limefuta Cheti cha Ufundi Sanifu kijulikanacho kama *Full Technician Certificate (FTC)* na badala yake limeanzisha Cheti cha Stashahada ya Kawaida (*Ordinary Diploma*) na si Shahada ya Uhandisi. Wanafunzi waliodahiliwa kwenye mafunzo ya Cheti cha Ufundi Sanifu (*FTC*) wamemaliza mafunzo yao (*Phased Out*), ambao wanafunzi wa mwisho walitahiniwa Mei, 2007. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haitaendesha mafunzo ya cheti hicho kwani hayatolewi na Chuo chochote kwa sasa.

(c) Mafunzo ya vyeti vya Ufundi Sanifu (*FTC*) na Stashahada ya Juu ya Uhandisi (*ADE*) yalibuniwa na Wizara ya Elimu katika hiyo miaka ya nyuma na kutahiniwa na *NECTA*. Tuzo zitolewazo na *NECTA* tangu wakati huo hazikuwa na madaraja na zimekidhi matakwa ya soko la ajira na wadau kwa ujumla kwa wakati huo, ingawa

kumekuwepo na manung'uniko madogo, likiwemo la tuzo kutokuwa na madaraja. Kwa sababu hizo, *NECTA* ambayo sasa imepewa jukumu la kusimamia, kuendesha na kutoa Tuzo za Elimu ya Ufundi limefuta Cheti cha *FTC* na kuweka Cheti cha Stashahada ya kawaida ambacho kitakuwa na madaraja.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Serikali imeruhusu kuanzishwa kwa Shahada ya Ufundi baada ya kufuta Stashahada ya Ufundi ya Uhandisi katika Chuo hicho au Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Dar es Salaam. Je, ni sababu zipi za msingi ilizozichukua Serikali kwa kuzuia kuanzishwa kwa programu ya Shahada kwa Taasisi ya Usimamizi wa Fedha *IFM* na Chuo cha Biaashara *CDF*? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoielezwa katika swali lililopita la Mheshimiwa Mpesya ni kwamba sasa hivi nchi yetu ina mahitaji makubwa ya kada hizi za kati. Tumeshaona uwiano uliopo kati ya wataalam wa Chuo Kikuu na kada za kati pamoja na wale tunaowaita kwa Kiswahili Rahisi spana *boys*.

Kwa kweli utaona kwamba tukiendelea kuruhusu Vyuo Vikuu viendeleo kuwepo na tubadilishe Vyuo vya Kati kuwa Vyuo Vikuu tutaendelea kupunguza hii kada ya kati na katika kuendeleza nchi kiuchumi tunawahitaji sana. Kwa mfano huwezi kusema kila chuo kitoe Udaktari wakati tunahitaji Manesi kwa sababu kazi ya Daktari ni *prescribe*. Lakini tutahitaji kada ya kati ambao ndio watoa dawa na ndio watundika damu, hali kadhalika katika nyanja mbalimbali.

Kwa hali hiyo kama kuna chuo kinachotaka kutoa taaluma ya Chuo Kikuu basi wawasiliane na Vyuo Vikuu ambavyo tayari vinatoa taaluma za namna hiyo. Lakini hatuwezi kuendelea kubadilisha vyuo hivyo na hii ndiyo sababu ya kukataza Chuo cha *IFM* kutoa shahada.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda *ni-declare interest* kwamba mimi nimepitia mfumo huo wa Elimu ya *FTC in Engineering*.

Mheshimiwa Spika, lakini moja kati ya madhara makubwa yaliyokuwepo katika mfumo ule ambao mitihani yake ilisimamiwa na *NECTA* ilikuwa ni pale ambapo wanaofanya mitihani yaani watahiniwa wanapofeli hawapati fursa ya kurudia. Je, katika huu mfumo wa sasa watapata fursa wale wote waliofeli kurudia mitihani yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa nini huyu mwanafunzi afeli. Lakini kwa utaratibu huo wa *NTA* wa *levels* mbalimbali mwanafunzi anapewa nafasi ya kurudia lakini tusingependa wanafunzi kwanza wafeli ili waruhusiwe kurudia. (*Makofi*)

Na. 181

### **Umaskini wa Kipato**

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA** aliuliza:-

Kwa kuwa, umaskini upo wa aina nyingi ikiwa ni pamoja na umaskini wa kipato na usio wa kipato:-

- (a) Je, ni Kata zipi katika Wilaya za Tunduru, Songea Vijijini, Mbinga, Namtumbo na Songea Mjini zinaongoza kwa umaskini wa kipato?
- (b) Je, ni nini chanzo cha umaskini wa kipato katika Kata hizo?
- (c) Je, Serikali inatekeleza miradi gani ya dharura ili kukuza uchumi na kuondoa kabisa umaskini wa kipato katika Kata hizo?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola, Mbunge wa Mkoa wa Ruvuma (Viti Maalum), lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Kutokana na hali halisi kiutendaji na gharama kubwa siyo rahisi kufanya utafiti wa hali ya umaskini kwa nchi nzima hadi katika ngazi ya Kata. Serikali imeweza kufanya uchambuzi wa hali ya umaskini hadi ngazi ya Wilaya tu. Ingawa kuna baadhi ya Wilaya chache nchini ambazo zimefanya uchambuzi wa Kikata kwa kutumia utafiti shirikishi. Kwa hivyo Serikali haina taarifa za uchambuzi wa takwimu katika ngazi ya Kata katika Mkoa wa Ruvuma na hivyo, siyo rahisi kufahamu Kata zipi zinazoongoza kwa umaskini katika Mkoa wa Ruvuma.
- (b) Vyanzo vya umaskini wa kipato kama ilivyo katika sehemu nyingi za Vijijini, vinachangiwa na elimu ndogo na ujuzi mdogo katika kilimo ambao unaashiria uzalishaji mdogo na wenye tija duni; uzalishaji usiozingatia maarifa na juhudi katika kufanya kazi; kutokuwa na uhakika wa masoko; uduni wa miundombinu; kuendekeza uvivu, na kukumbatia mila na desturi zinazorudisha maendeleo nyuma.

(c) Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ili kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato katika ngazi ya Halmashauri, Kata na hata vijiji. Miradi hiyo ni kama ile ya MKUKUTA, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) ambayo imeainisha mikakati na programu za utekelezaji wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini miongoni mwa Watanzania. Miradi kama vile ujenzi wa barabara kwa kutumia nguvu kazi itasaidia kuinua vipato kwa watu kwenye ngazi ya kaya zenye vipato duni. Mradi mwingine ni ule wa *SELF (Small Entrepreneurs Loan Facility)* ambao unatoa mikopo nafuu na mafunzo kwa wajasiriamali wadogo wadogo katika Mikoa 14 ukiwemo Mkoa wa Ruvuma. Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi wa shilingi bilioni moja (1 bilion) kwa kila Mkoa ni fursa nyingine ya kuwawezesha wananchi kupata mikopo yenye masharti nafuu ya uzalishaji mali na biashara na hivyo kuupiga vita umaskini.

Aidha, ili kuongeza tija katika Kilimo, Serikali inatekeleza Mpango Kamambe wa Kuinua Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme (ASDP)*) na Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan (NIMP)*). Maeneo yote ya Mkoa wa Ruvuma yatanufaika na Mipango/Programu hizi zikiwemo Lundo, Litumbadyosi, Nakahuga, Ngindo, Mkalachi na Ngingama. Serikali inatoa wito kwa viongozi wa Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji, wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kuwahamasisha wananchi katika kuibua na kutekeleza miradi yao. Serikali pia inatekeleza miradi ya pembejeo za kilimo kwa kutoa ruzuku ya mbolea na kuboresha huduma za ugani ili kuongeza uzalishaji na kuimarisha ushirika wa uzalishaji kwa lengo la kuwa na masoko ya uhakika.

Vile vile inahakikisha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuongeza ajira hasa vijijini, Serikali kwa kushirikiana na asasi za kifedha inaendelea na juhudi za kuhamasisha uanzishwaji na usimamiaji wa Vyama vya Kuweka na Kukopa (*SACCOS*) ambavyo vitatumiwa na wananchi kujiwekea akiba na baadaye kupata mikopo nafuu kutoka katika benki na taasisi za kifedha ikiwemo Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ajili mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa. Kwa kuwa Serikali imeshindwa kufanya utafiti katika ngazi ya Kata na utafiti huo utawasaidia sana wananchi katika kujua hali za Maendeleo ya kipato katika Kata zao. Je, Serikali iko tayari kutafuta wadau wa Maendeleo kama vile *REPOA*, *ERSF* ili waweze kufanya utafiti wa kipato kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Swali la pili, kwa kuwa Serikali inatekeleza Mradi wa Kurasimisha Rasilimali za wanyonge yaani MKURABITA. Maskini wengi walioko vijijini tunawaita tu maskini lakini wao sio maskini kwa sababu wana rasilimali kama vile mashamba, ardhi na nyumba. Je, Serikali iko tayari kuongeza fedha na kuboresha Mfuko wa MKURABITA ili uweze kufanya kazi na maskini waliopo vijijini?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa juhudi anazozifanya za kuhamasisha wakazi wa

Mkoa wa Ruvuma ili kujiletea Maendeleo. Jibu la kwanza, Serikali iko tayari kuhamasisha *REPOA* na *Economic and Social Foundation* ili wafanye utafiti huo. Lakini mwisho ya yote tatizo lao linaweza kuwa lile lile la uhaba wa fedha. Kwa sababu Serikali yenyewe sio kama imeshindwa, Serikali gharama zake zimekuwa kubwa mno kuzifanyia utafiti katika ngazi ile ya Kata; ndiyo maana haijafikia bado. Lakini tunajua kutokana na zile taarifa za ngazi ya Wilaya kwa mfano Wilaya ambayo inaongoza katika umaskini ni Bunda ambayo ina watu asilimia 68 na ndiyo ya 119. Wilaya ya pili ni Musoma Vijijini watu asilimia 24 namba yake katika nafasi yake ni 119. Inayofuata ni Geita asilimia 62, nafasi yake 117, inayofuata Serengeti asilimia 61 nafasi yake 116, inayofuata Singida Vijijini asilimia 56, nafasi yake 115, inayofuata Namtumbo asilimia 55 nafasi yake ni 114.

Kwenye Wilaya nafuu ni zipi? Bukoba Mjini watu 11 nafasi ya kwanza, Arusha Mjini asilimia 12 nafasi ya 2. Mbeya Mjini nafasi ya 3 watu 12. Mbarali asilimia 13 nafasi 4. Morogoro Mjini nyumbani kwetu nafasi ya 5 asilimia 14. Kinondoni asilimia 14 namba 6, Wilaya za Mkoa wa Ruvuma, Mbinga ndio ya kwanza asilimia 28 namba 1, Songea Mjini asilimia 32 namba 2. Tunduru asilimia 39 namba 3. Songea Vijijini asilimia 41 namba 4 na Namtumbo asilimia 55 nambari 5. (*Makofi*)

Kuongeza uwezo wa fedha MKURABITA. Nia iko ya Serikali kuongeza fedha ili kuikamilisha shughuli za MKURABITA. Lakini MKURABITA ni kitu kikubwa sana maana inataka isambazwe nchi nzima. Kwa hiyo, tutajitahidi kuongeza fedha pale zitakapopatikana ili tuweze kutekeleza kwa nchi nzima.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kweli Serikali imeanza Mpango wa Kurasimisha Mali za Watu zikiwemo Nyumba na Vitu vingine vya thamani na tumejaribu katika Mkoa wa Dar es Salaam Wilaya tatu na tayari tumepata mafanikio kwa sababu wamepata leseni ambazo wanaweza kutumia katika Mabenki. Kinachotakiwa sasa nchi nzima na tunamwomba Mbunge atusaidie kuhamasisha Halmashauri za Wilaya zao ziige mfano huo huo kwa sababu tulifanya kama *Pilot Project* ili Halmashauri zingine ziweze kufuatilia kurasimisha mali katika miji yao.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika vijiji Serikali tuko mbioni sana kupima vijiji vyote nchi nzima. Tumekwenda kwa kasi tumeshapima zaidi ya vijiji 8,700 iliyobaki tutavimalizia kwa kipindi kifupi. Ninaomba kumshawishi Mbunge kwa vile ambavyo vimeshapimwa katika Mkoa wa Songea ambao akitaka idadi yake tutampa Mkoa wa Ruvuma Wilaya ya Songea na Kata zake zote akitaka idadi tutampatia ili aweze kuhamasisha wale ambao tayari wana hatimiliki za kimila waweze kutumia katika Mabenki na kupata mikopo kujiongezea uchumi. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la mwisho la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali yetu kwa kweli tunakubali haiwezi kuwa na uwezo mkubwa wa kufanya *research* hizo zote za umaskini mpaka kwenye ngazi ya Kata na Vijijini. Lakini kwa kuwa yako Mashirika mengi yamefanikiwa kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Serikali kwenye maeneo hayo ya vijijini na maeneo ya kwenye Kata. Je, Serikali sasa iko tayari kutengeneza kitengo maalum kitakachoweza kupokea tafiti hizo ambazo zimefanyika na Mashirika mengine ili ziweze kuhusishwa katika mipango na kuona namna gani inaweza kutekeleza katika kuhamasisha Maendeleo ya wananchi na hasa maeneo hayo ya vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majibu. Pengine ingefaa baadaye pia muonane kwa kupata na hakuzitaja. Mheshimiwa hakutaja.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli naunga mkono suala hili la kuonana baada ya kikao hiki. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini vile vile napenda kutambua juhudi za Mheshimiwa Mhagama za kuhamasisha wananchi wake ili wajiletee Maendeleo kwa kuondoa umaskini. Takwimu na taarifa hizo zote tunazo na tunazitumia katika kuandaa mipango yetu ya Kitaifa na ya Kimkoa na Wilaya. Kitu muhimu sasa sio ngazi ya Taifa kitu muhimu ni pale kwenye Halmashauri kuzitumia taarifa hizi kuandaa mipango ambayo itawanufaisha wananchi kuondoa umaskini.

Na. 182

### **Mahitaji ya Maktaba za Mkoa**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mahitaji na umuhimu wa Maktaba vimeongezeka hivi karibuni hususan kwa wale wanaofanya mitihani ya Taifa na ya Chuo Kikuu Huria; na kwa kuwa, Maktaba nyingi za Mikoa nchini hazina vitabu vya kutosha na hufungwa saa 12 jioni muda ambao hauwasaidii wafanyakazi kujisomea:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza muda wa kusoma katika maktaba hizo za Mikoa hadi saa 4.00 usiku ili kukidhi haja ya watahiniwa wanaojisomea wenyewe?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Maktaba za Mikoa ili ziweze kukidhi mahitaji ya sasa ya nafasi ya vitabu?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Maktaba za Wilaya hususan Wilaya ya Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna umuhimu wa kuongeza muda wa kujisomea katika Maktaba zote nchini. Hata hivyo kutokana na ufinyu wa Bajeti, isiyoweza kukidhi gharama za uendeshaji wa Maktaba, hakuna mpango kwa sasa wa kuongeza muda wa kusoma katika Maktaba hizo hadi saa 4.00 za usiku. Kwa kutambua kuwa, wapo wafanyakazi na wanafunzi ambao wanashindwa kuwahi kutumia Maktaba siku za katikati ya wiki, Maktaba zote zilizo chini ya Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, zilianza kutoa huduma siku za Jumamosi kuanzia saa 3.00 hadi saa 8.00 tangu mwaka 1996.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa Mpango Mikakati wa Bodi ya Huduma za Maktaba wa mwaka 2007 - 2012 wenye lengo la kuboresha Maktaba za Mikoa kwa kuongeza nafasi na vitabu katika Maktaba za Mikoa ili kukidhi mahitaji ya sasa. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu imepanga kuanza awamu ya kwanza ya Ujenzi wa Maktaba ya Mkoa wa Singida na kukarabati majengo ya Maktaba za Mikoa ya Tanga, Mbeya, Ruuma, Mtwara na Lindi. Aidha, idadi ya machapisho yataongezwa kutoka 836,428 hadi 956,428, katika Maktaba za Mikoa 18.

(c) Mheshimiwa Spika, mpango wa kuanzisha Maktaba za Wilaya ni mojawapo ya malengo ya Bodi ya Huduma za Maktaba ya kuhakikisha kila Wilaya nchini inapata Maktaba. Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wilaya ya Mpanda tayari inayo Maktaba ambayo tayari imeanza kutoa huduma. Lengo la Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine zikiwemo Halmashauri za Wilaya ni kuhakikisha kuwa Maktaba zinaanzishwa katika Wilaya zote ifikapo mwaka 2015.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nami niwashukuru kwa jitihada zilizofanywa za kuweza kufungua Maktaba Mpanda lakini nilikuwa na swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kutokana na taarifa aliyowasilisha katika Bunge sasa hivi kwamba katika mwaka huu wa fedha kutakuwa na ziada ya machapisho kutoka 836,000 mpaka 956,000 ambayo yatapelekwa katika Maktaba 18 za Mkoa. Je, Maktaba hii mpya ambayo imefunguliwa Mpanda itanufaika na machapisho haya ya ziada ambayo yatatolewa mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI(MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, Wizarayangu ina mpango mzuri tu wa kuweza kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya machapisho katika Maktaba zetu zilizoko Wilayani na Mkoani. Wilaya ina kiwango chake na Mkoa una kiwango chake.



Tutazingatia kiwango kile kinachotakiwa katika kila Maktaba ya Wilaya kiweze kufikiwa kwa ajili ya nafasi zile zitakazotolewa katika lile jengo ambalo ni la Wilaya. Lakini pia na nafasi zile zinazoweza kutumika kwa ajili ya kila Maktaba ya Wilaya. Tunatarajia kwa wakati mmoja walau watu 150 wanaweza wakakaa katika Maktaba kwa wakati mmoja na kuwa na machapisho ya kutosha yale ambayo wanaweza kubadilisha wakati wowote wanapokuwa katika kujisomea. Hilo litazingatiwa ili Wilaya ya Mpanda nayo iweze kunufaika na ongezeko la machapisho.

Na. 183

### **Hali ya Madaktari (AMO)**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Madaktari (*A.M.O.*) ndio tegemeo kubwa katika Hospitali za Mkoa na Wilaya:-

Je, Serikali haioni kuwa, ni haki yao kutambuliwa na kupewa maslahi kama mishahara mizuri, nyumba, usafiri na marupurupu mengine kama Madaktari wenzao (*M.D's*)?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mbunge wa Viti Maalum, kwanza napenda kutoa maelezo mafupi ya ufafanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *AMO* ni kifupi cha neno la Kiingereza *Assistant Medical Officer* na tafsiri yake kwa Kiswahili ni Daktari Msaidizi. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kundi hili la Wataalam ni moja ya kada za afya zinazotegemewa sana katika Hospitali za Mikoa na Wilaya hususan mikoa ya pembezoni. Baada ya maelezo haya sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kutathmini kwa dhati huduma zinazotolewa na watumishi wote wa afya wakiwemo Madaktari Wasaidizi (*AMO*). Kwa kutambua huduma zinazotolewa na watumishi wa afya pamoja na watumishi wengine wa umma, Serikali imekuwa ikiboresha maslahi yao hususan mishahara awamu kwa awamu. Kwa mfano mwaka 2006 mshahara wa Daktari Msaidizi ulipandishwa kutoka ngazi ya mshahara *TGS D* kwenda *TGS E*.

Aidha, kiwango cha mshahara katika ngazi hiyo ya mshahara yaani *TGS E* kiliongezeka tena kufuatia mabadiliko ya mishahara ya watumishi wa umma ya mwezi Julai, 2006. Ni matumaini yangu kuwa kiwango kinaweza kuongezeka zaidi kufuatia

mapendekezo ya Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kushughulikia mapendekezo ya maboresho ya mishahara ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kuwa si rahisi kwa watumishi wote wa umma kuwa na mishahara na marupurupu mengine yanayofanana. Mishahara na marupurupu kwa watumishi wa Umma hutolewa kwa kuzingatia elimu, muda wa mafunzo na majukumu ya mtumishi.

Hivyo, si rahisi Madaktari Wasaidizi wakapatiwa maslahi sawa na Madaktari isipokuwa kama watajiendeleza na kupata sifa ya Daktari. Tunayo mifano mingi ya Madaktari Wasaidizi ambao wamejindeleza wakawa Madaktari na sasa ni Madaktari bingwa.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa *Clinic Officers* wanaokaa vijijini wao ni Waganga Wasaidizi. Sasa hivi kwa vile mishahara yao ni midogo na usafiri wanaotumia ni mabasi. Sasa hivi nauli imepanda mara nne kwenye mabasi hayo. Nilikuwa naiomba Serikali iweze kuwanunulia pikipiki za kwenda mjini. Je, ni lini itawanunulia pikipiki hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kupanda kwa gharama za nauli nadhani haiwagusi *Clinical Officer* tu kwa sababu wanaofanya kazi katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wako *Clinical Officers*, Madaktari, Manesi na wengine.

Lakini nataka nimwambie kwamba Serikali haina mpango wa kuweza kuwanunulia *Clinical Officers* kwa sababu walimu, *Ma-engineer* na wafanyakazi wote wa umma wako vijijini ambako suala kama ni kupanda kwa nauli haliwagusi tu *Clinical Officers* lakini linagusa *cross country* wafanyakazi wote walioko kule kama itapanda nauli ni wote ambao litawagusa. Kwa hiyo, Serikali haina mpango wa kuwapatia pikipiki.

Na. 184

### **Uhaba wa Madaktari Bingwa Hospitali ya Mkoa wa Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hospitali ya Mkoa wa Singida inakabiliwa na tatizo sugu la kutokuwa na Madaktari Bingwa hata mmoja hasa kwa magonjwa ya akina mama na watoto licha ya ahadi nyingi zinazotolewa na Serikali mara kwa mara kuhusiana na tatizo hilo:-

(a) Je, ni lini Serikali itazitekeleza ahadi zake ili wananchi wa Mkoa wa Singida waendeleo kujenga imani na Serikali yao?

(b) Kwa kuwa, hospitali hiyo inakabiliwa pia na uhaba wa dawa na vifaa muhimu kama vile *X-ray*, vifaa vya upasuaji na vya maabara. Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hilo ili kuwaondolea kero wananchi wanaotegemea kupatiwa matibabu kwenye hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya ana Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chilolo, Mbunge wa Viti maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa inaajiri Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali katika hospitali zote za Wilaya na Mkoa ikiwemo hospitali ya Mkoa wa Singida.

Kutokana na uhaba wa wataalam wazalendo, Serikali imekuwa ikituma wataalamu kutoka nchi za China, Cuba na Misri ili kutoa huduma katika hospitali zenye uhaba wa wataalam ikiwemo hospitali ya Singida. (*Makofi*)

Nafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa Serikali imemwajiri Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama ambaye ni mzalendo jina lake anaitwa Dr. Christopher Mgonda, kwenda kufanya kazi katika Hospitali ya Mkoa Singida na tayari amesharipoti. Serikali itaendelea kuajiri wataalam hao kadri watakatavyopatikana na kuwapanga kufanya kazi katika mikoa yenye uhaba.

(b) Kupitia mradi wa *ORET* wa kuimarisha huduma za radiolojia (*X-ray*) Hospitali ya Mkoa wa Singida mnamo mwaka 2004 ilipatiwa mashine kubwa moja ya *X-ray*, *Ultra Sound*, Kitanda kimoja cha Upasuaji, Mashine ya Kutengeneza Hewa ya Oksijeni kwa ajili ya Chumba cha Upasuaji na wodi ya kuzalia; na chombo cha kutakasia vifaa na nguo kwa ajili ya huduma za upasuaji.

Aidha, mashine moja aina ya *Microlab 200* ilitolewa kwa ajili ya huduma za maabara, na vile vile hospitali hiyo imepatiwa mashine "*CD-4 Count*" na *Haematology Analyzer*". Vitendea kazi vingine vikiwemo vitendanishi vya maabara, picha za *X-ray* na madawa yake (*Developer* na *Fixer* na dawa nyinginezo) ni jukumu la Mkoa kuvinunua kutoka Bohari ya Madawa ya Serikali (*MSD*) kwa kutumia fedha wanazopelekewa kwa madhumuni hayo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Vilevile nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutupatia Daktari Bingwa wa akina mama pamoja na Daktari Kiongozi wa Hospitali ya Mkoa. Baada ya pongezi hizo naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa upungufu wa vifaa vya maabara na vifaa vya chumba cha *X-Ray* umeboreshwa kwa kiasi kikubwa na Daktari Kiongozi huyu mgeni kwa

kipindi kifupi cha miezi sita. Je, Serikali itakuwa tayari kumpongeza Daktari huyu Kiongozi kwa kazi nzuri aliyofanya kwa miezi sita na vile vile kumpa ushirikiano ili aipende Hospitali ya Mkoa wa Singida asiondoke kama wanavyoondoka wengine waliotangulia?

Swali la pili, kwa kuwa, Hospitali yetu ya Mkoa wa Singira pamoja na za Wilaya zina upungufu mkubwa wa madaktari wa kawaida kwa mfano Hospitali wa Mkoa inaupungufu wa Madaktari wa kawaida sita na Madaktari wasaidizi saba na wauguzi 54. Je, Serikali itakuwa tayari kuboresha ili Hospitali yetu ipate ufanisi unaoridhisha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyodai yeye mwenyewe kwamba Daktari Kiongozi amefanya vizuri tunampongeza kwa kazi nzuri aliyofanya na naamini ataendelea kukaa Singida lakini vile vile napenda kuwapongeza Madaktari wengine nchi nzima wanaofanya kazi nzuri kama hiyo. Lakini vile vile tumekuwa tukishirikiana na hospitali zote za Mikoa na Wilaya ikiwemo Singida na ndiyo maana tukaona umuhimu wa kuwapelekea Daktari bingwa sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, suala la uhaba wa watumishi kama tulivyokuwa tukizungumzia wakati wote ni kwamba si kwa hospitali ya Singida lakini kwa Mikoa yote lakini napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, Wizara yangu inafanya mkakati kuhakikisha kwamba wataalamu watakaohitimu kipindi hiki kwa kadiri itakavyokuwa tutaweza kuwasambaza kila mahali na ndiyo maana tumempeleka Daktari huyu kama kianzio. Kwa hiyo, watakapopatikana wengine basi Mkoa wa Singida tutaupa kipaumbele.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali hii ya Singida tunayozungumzia ilijengwa katika miaka ya 50; na kwa kuwa wakati ule wakazi wa Singida walikuwa ni watu laki mbili na sasa hivi wakazi wa Singida ni zaidi ya milioni moja na mia moja; na kwa kuwa kikao cha *RCC* tumeamua kwamba kutajengwa Hospitali mpya ya Mkoa wa Singida katika eneo la heka 80 zilizotengwa. Ninaomba nisikie tamko la Serikali kwamba itaungana na uongozi wa Mkoa tushirikiane tujenge Hospitali mpya ya kisasa itakayo-*serve* Mkoa wa Singida.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza sana watu wa Singida kwa kuweza kutumia Hospitali hii ambayo ni kogwe kuanzia mwaka 1950 ambao wengi wetu hawajazaliwa mpaka sasa hivi wakati idadi kubwa imeongezeka. Lakini vilevile kama *RCC* imekaa na ikaona kuwa kuna umuhimu wa kujenga Hospitali hii ambayo ni ya kisasa Serikali yetu haitakuwa na kipingamizi kutoa ushirikiano pale itakapoonekana kwamba inafaa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Matangazo tutaanza na wageni. Wale niliowatangaza jana Walimu

Wakuu sabini wa shule za msingi Manispaa ya Morogoro natumaini leo wamefika. Kwa sababu nimeletewa tena tangazo hili.

Naomba msimame kama mpo, wapo wale pale karibuni sana walimu natumaini jana hamkupata athari yoyote kwa sababu tuliwatangaza lakini hatukuwaona na Morogoro siyo mbali sana na hapa. Lakini tunashukuru kuwaona katika afya nje na tunawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haroub Masoud anao wageni wake mmoja ni bwana Wang Cheon kutoka China, Mr Wang yule pale ahsante sana. Ifraji Haroub na Salim Suleiman, kutoka Koani Jimboni kwa Mheshimiwa na Msaidizi wake Mheshimiwa Haroub anaitwa Suleiman Salum yule pale, ndiyo yule pale ni mlemavu.

Mheshimiwa Haroub nakupongeza sana kwa sababu wengi tunazungumza tu juu ya kujali walemavu, wewe msaidizi wako ni mlemavu. *(Makofi)*

Tunao pia wale vijana wetu kutoka *TAYOA* wakiongozwa na Ndugu Peter Masika, wale pale karibuni sana karibu tena nashukuru kuwaona na pongezi sana Ndugu Masika kwa kazi nzuri unayofanya ya kuongoza taasisi hii.

Mheshimiwa James Lembeli, anao wageni watatu ambao naona ni binti zake, Maria Lembeli, yupo *Form six Kilimanjo Secondary School*, Wizilia Lembeli anasoma *Briblan School* na Kalunde Lembeli anasoma *Shaloom Primary School*. Kama kawaida sisi wazazi wenye vijana wa kiume hili ni suala zuri la kuchangamkia kwa sababu huwezi kujua unaweza....*(Kicheko)*

Mheshimiwa Lembeli ana sifa kule Kahama ya kutunza vizuri sana wanawe. Kwa hiyo, ni jambo zuri sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninayo dharura kidogo ya mkanganyiko wa malipo muhimu sana ya Waheshimiwa Wabunge naomba nikashughulikie. Nitaomba Mheshimiwa Naibu Spika aje ili aendelee na shughuli zinazofuata.

*Hapa (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia kiti.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani tumeamka salama. Sasa tunaendelea na kazi zetu. Katibu shughuli inayofuata:-

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2007  
*(The Financial Bill, 2007)*

(Muswada wa uliotajwa hapo juu ulisomwa kwa mara ya Kwanza Bungeni)

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi

(Majadiliano yanaendelea)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tulipomaliza jana, wale Wabunge ambao hawajachangia mara moja alibakia Ponsiana Nyami. Kwa hiyo atakuwa wa kwanza atafatiwa na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha ajiendae.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia nikiwa wa kwanza siku ya leo. Awali ya yote nami naomba kuungana na wenzangu kwanza kwa sababu muda mrefu nilikuwa sipo naomba kutoa rambirambi zangu kwa hayati Mheshimiwa Juma Akukweti, pia natoa rambirambi zangu kwa aliyekuwa Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kwa kutangulia mbele ya haki na Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nianze kuchangia kwa upande wa elimu nitaje mawili matatu niliyonayo. Nianze na shule za sekondari ambazo kwa kiwango kikubwa mimi ndizo zinazonisikitisha sana. Shule za wananchi ambazo tumeanzisha kujenga lengo lake kubwa ni kutaka kuweka uwiano wa elimu kwa nchi nzima na maeneo yote. Lakini kwa bahati mbaya sana ni rahisi kwamba Serikali haijaweka umuhimu wa hali ya juu kujali shule hizi za wananchi zinazojengwa hasa zile za vijijini kwa kuzipa huduma inayotakiwa kikamilifu. Kwa mfano, shule inaweza ikaanza mwaka huu ikiwa na Mwalimu mmoja lakini ikamaliza kidato cha nne ina walimu wanne au watatu. Mtihani utakaotolewa wa masomo yale yale ni mtihani sawa sawa na shule zilizoanza zamani na zenye walimu wengi na walio mahaili, mtihani ule ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano shule ya Sekondari Mzumbe inapotoa wanafunzi wengi waliopata vizuri kwa daraja zuri la kwanza waliopata *point* tatu, nne hadi tano wapo 30. Lakini shule moja wapo ipo huko Nkasi, Masasi au maeneo mengineyo, ambayo hadhi yake ni hiyo hiyo sawa sawa na Sekondari ile ya Mzumbe, ina walimu 40, shule labda ya Kate au Ntunchi na nyingine yoyote ya wananchi ina walimu watatu tangu ilipoanza hadi *form four*, inapewa mtihani ule ule na wanafunzi 30 wanaopata daraja la kwanza kutoka Mzumbe shule ile itasifiwa sana lakini zile shule kama vile Kate Ntunchi watalaumiwa. Hawakusoma vizuri nakadhalika. Lakini bado hamzingatii kwamba shule zinazokuwa mjini na zinazokuwa maeneo yenye neema shule zina umeme. Kwa hiyo wanafunzi watasoma zaidi, Walimu wake ni wazuri zaidi kwa hiyo watasoma vizuri zaidi lakini pengine watapata hata bahati, bahati kwao lakini hasara kwa Tanzania kuiba mitihani na wakafaulu vizuri sana. Wale walioko porini kule hawana

*access* ya kuiba mitihani wanatumia akili zao na ninavyojua mtoto wa kijiji akifaulu amefaulu kweli kweli, mtoto wa mjini akifaulu mimi namtilia mashaka mara tatu wengi wezi wa mitihani. Ingawa si lazima narudia wengi lakini walio wachache wanatumia akili zao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, na pengine hata Wazazi wengine wanachangia mtoto anamwambia kuna mahali fulani kuna *tuition* lakini tunasikia kuna nywinywira za mitihani, anatoa fedha akanunue hivyo hivyo vitili vya mitihani. Matokeo yake tunakumbana na wengine wanamaliza hata Chuo Kikuu lakini akiongea na baadhi ya waliomaliza hata *form six* au *form four* kingereza wanaweza wakampita. Kingereza chake cha kuandika si cha kujieleza kwa umahili kwa sababu alizoea mabomu ya kuibaiba tangu alikotoka. Hatutendi haki sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri Wizara ya Elimu ifanye utafiti wa kina na pengine kuandaa mitihani tofauti kati ya shule ambazo zimekuwa na matatizo ya Walimu. Kwa hiyo, Wanafunzi wamepata matatizo ya kusoma kwa uhakika baadhi ya masomo hadi kumaliza *form four*. Mitihani hiyo iwe tofauti na ya wale ambao wana walimu wote na wenye sifa zilizotakiwa. Tutatenda haki. Lakini jambo jingine ni suala la walimu wenyewe iweje shule moja Walimu wa somo moja warundikwe hadi kufika kumi na shule nyingine zikose Mwalimu hata mmoja. Lakini wewe iweje unapompeleka Mwalimu katika shule hasa za vijijini na zinazoanza Mwalimu akatae kwenda na mara nyingi akatae wanaopelekwa sisi hapa ni mashahidi ni wale walimu ambao unakuta labda ndiyo wametoka vyuoni au wale ambao walipelekwa kwenye programu maalum.

Nilipokuwa nasoma kwenye Tovuti, niliona kuna shule moja hapa Tanzania ambapo kuanzia kidato cha Kwanza hadi kidato cha Tatu Mwalimu yupo mmoja na Mwalimu Mkuu Msaidizi ni kiranja mkuu. Kwa maana kwamba Mwalimu yule anapoondoka hana mtu mwingine wa kumwachia ni lazima amwachie madaraka kiranja mkuu. Mtihani wa *form four* ukifika hamtajali wale wanafunzi wa Minaki, *Tabora Boys* na kwingineko wote mtawapelekea mtihani sawa na wale wakifaulu mtachekelea shule zile zimefundisha vizuri. Lakini shule ile ambayo kiranja ndiye anakuwa Mwalimu Mkuu Msaidizi mtaicheka sana haokufaulisha. Matokeo yake watoto wa wakulima ambao ndiyo wenye shule hizi wanaojitahidi wataendelea kubakia nyuma na hata wakipata kazi watapata za kawaida si zile kazi za maana kama zile za watoto wa wale ambao tunawajali kuwapeleka shule za maana na Ndugu Nyami akisikia hapa kwamba shule ya Mzumbe inafaulisha vizuri na Mheshimiwa Waziri fulani akisikia hivyo, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Mkoa na hata Mfanyabiashara mzuri zaidi atapenda kwa kweli hata mimi kumpeleka mtoto katika shule hiyo na si kumpeleka katika shule yangu ya kule vijijini ambako Walimu hawapo na ni vigumu kupata vitabu vya kutosheleza, kupata vifaa vya maabara na mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa nguvu zetu wote tujitahidi zaidi kujali elimu kwa vijana wetu wa vijijini na kusaidia wananchi wetu kikamilifu ili tuondokane na tabaka la wale ambao tayari wanacho wamekwisha tangulia wataendelea kuwa nacho na wananchi tunaowaongoza tutaendelea kuwapa lugha tu nzuri ya kujenga shule lakini hawana faida nazo na matokeo yake, mtoto wa kike kwa mfano anapopata mimba tutakaa

majukwaani tukilalama mzazi awe wa kwanza kumfichua ni nani aliyempatia mimba huyu mtoto wa shule.

Kama mzazi mwenyewe anaona anasumbuka kumsomesha mtoto wake shule ya msingi na hata anahaingaika kumsomesha shule ya Sekondari tuliyomwambia yeye mwenyewe ajenge haoni faida ya mbele bado atadhani ni vizuri mtoto wake apate mtoto na ama aolewe, kitu ambacho hatusaidii sana eneo la elimu.

Lakini kama kuna walimu wanakataa kwenda baadhi ya shule na sisi wenyewe tunaona mazingira yale ni magumu zaidi kwanini tusiandae utaratibu kama Serikali wa kuhakikisha kwamba tunatoa maalum kwa walimu hao kuwapa malipo ya ziada ili kusudi wakae katika maeneo hayo na hata kuwavutia wengine kwamba wakienda huko nje ya mshahara wa kawaida wanaoupata lakini kuna aina nyingine ya malipo ya ziada kwa sababu ya mazingira magumu hatuwezi tukakataa.

Mwalimu anayefundisha mjini na Morogoro Mjini huwezi ukamlingisha na yule Mwalimu anayefundisha shule ya vijijini kule inakoanzishwa upya kabisa mazingira ni tofauti. Mahali ambapo utakuta nyumba ya Mwalimu haipo, mwalimu yule lazima apate nyumba ya kupanga tena nyumba ya nyasi lakini mwenzake anakaa nyumba ya bati simenti chini na umeme.

Yeye yupo kijijini kabisa ambapo hata akitaka kuupata huo mshahara ni labda asubirie lori linalokuja mara mbili kwa wiki au kwa mwezi apande lori hilo kwenda kuuchukua mshahara wake. Huwezi ukamlinganisha na Mwalimu ambaye muda wowote anaoutaka anatazama saa Benki itafungwa saa ngapi akimbie aende benki na tena aende na kadi akachomoe tu hata kama ingekuwa ni usiku. Kwa hiyo lazima tuandae mazingira haya hatuwezi tukasema Walimu na si kwa Walimu tu hata kwa watumishi wengine.

Lakini umuhimu wa Walimu kwa sababu katika nchi yoyote huwezi ukaendelea kama hujazingatia suala la elimu hilo halipo. Nchi yoyote iliyoendelea Duniani. Kwa sababu ya watu wake wamejitahidi kajikita katika suala la elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004 nilipokuwa Japan maendeleo ya Japan hata wazungu wenyewe wamekuwa wakiyashangaa wazungu kutoka eneo la Ulaya kwamba wale Wajapan kwanini wameendelea kiasi kile katika miundombinu, ukitazama *style* ya majengo na hata mambo mengine. Sasa nilipomuuliza mjapan mmoja kwamba hivi ni kwanini maendeleo yao yanaonekana kuwa makubwa, yanakwenda kasi hata hawa wazungu wanaanza kuwaogopeni?

Nilidhani nitapewa maelezo mengi, jibu lake lilikuwa neno moja tu “elimu.” Ndivyo alivyoni jibu. Mimi nikabaki nazubaa. Nikamuuliza swali tena Elimu kwanini? Akasema tunaposema elimu ukitaja afya ni elimu na unapotaja maendeleo ya jamii ni elimu, sayansi na teknolojia ni elimu, ukitaja ufanisi wa uongozi au kutokuwepo ufanisi wa uongozi ni elimu.



Kwa hiyo, kama wewe hutaki kuzingatia suala la elimu ukajiona umefika basi wewe ni mfu. Ndivyo alivyonijibu. Kwa hiyo, tukitaka kuendelea tupende tusipende hatuna budi kukazania suala la elimu na mimi naipongeza Serikali ya awamu hii kwa dhati kabisa kwamba hata ukitazama Bajeti yetu imetoa kipaumbele kwa elimu. Hata wenyewe tuliopo hapa tunajulikana wengine tunajulikana wengine ni mahiri sana kwa elimu; na kama huna elimu na hutaki kujiendeleza kwa elimu wewe ni mfu maana wewe si mtu wa dunia hii sasa. Hauendi na wakati na kwa Mbunge nitakushangaa unapokwenda kijijini hata mwananchi wa kawaida ambaye aketegemea si kwamba Wabunge tunaakili sana tunajua sana lakini uwe na uelewa wa kutosha basi lakini sio wewe wakati ndiyo mtu wa kuongozwa na kuelekezwa kila kitu, umepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa mtu yoyote unapokuwa kiongozi wewe ni dira na kama wewe ni dira ili uweze kuwa dira zaidi ni lazima ujikite katika kutafuta mambo yanayofaa kwa ajili ya uongozi na huyapati popote isipokuwa katika kusoma upende usipende. Kwa hiyo, ni lazima tukazanie suala la elimu na hasa elimu ya sekondari ambayo ndiyo inianza kumkomboa binadamu kuelekea maarifa ya juu.

Kwa hiyo, lazima tuandae mazingira mazuri ya shule zenyewe za sekondari na walimu wa kiwango cha juu kabisa na bila upendeleo na hata jinsi gani mitahani inavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsateni sana, sasa tunaielewa kwanini uliamua kwenda kusoma. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea kuwaita wasemaji wengine nina matangazo yafuatayo:-

Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo tarehe 10 Julai, 2007 saa tano. Nadhani baadaye katika Ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Kwa hiyo, chumba namba 219 Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara Mheshimiwa William Shellukindo anawatangazia Wajumbe wake kwamba wakutane kuanzia saa saba mchana katika ukumbi namba 231.

Mheshimiwa Paul Kimiti anaitwa mratibu wa Kikao cha CPT anakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote waliokaribishwa na Baba Askofu Yuda Thadei wa Kanisa Katoliki Dodoma wakutane naye saa saba mchana ofisini kwake. Baada ya hapo naomba nimwite Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha ajiandae.

**MHE. PINDI Z. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kushukuru kwa kupata nafasi na mimi ya kuchangia hoja hii ya masuala ya elimu. Awali ya yote nami niungane na Wabunge wengine wote kutoa pole kwa familia ya mwenzetu Ndugu yetu, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, na wale wote ambao wamepata msiba ya aina moja au nyingine katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wizara hii imefanya kazi kubwa katika nchi yetu na wote tumekuwa mashahidi kwa kazi kubwa ambayo imefanywa, imejitahidi sana sana kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Hata maandalizi ya hotuba ya Wizara yameletwa vizuri sana ukiangalia kitabu chao pale mwanzo wameweka yaliyomo, lakini pia wanakitabu kizuri sana ambacho kinaonyesha takwimu za masuala ya elimu nchini Tanzania. Kwa kweli ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika sambamba na hilo mimi nilete salaam kutoka kwa wananchi wa Mkoa ninaotoka, Mkoa wa Iringa Wilaya zote za Ludewa Makete, Njombe, Kilolo na Iringa. Kwa kweli wanaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa lakini zaidi sana wanaishukuru Serikali kwa uwezo wake mkubwa ulioamua kuondoa ada za shule za misingi. Huko nyuma ada za shule za misingi zilikuwa ni kikwazo lakini baada ya Serikali kuamua kuondoa ada watoto wameweza kwenda shule asilimia 90 kwa wale wenye umri wa kwenda shule.

Mikoa mingi nchini ilikuwa inatoa watoto wa kazi ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Iringa lakini sasa watoto wetu wenye umri wa kwenda shule hakuna kikwazo kabisa. Watoto wetu wote wanaweza kwenda kusoMa na Waheshimiwa Wabunge pia niwashukuru na madiwani kwa kazi kubwa ambayo imekuwa ikifanya kuhamasisha suala hili la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua, elimu ni haki za binadamu na mimi ni muumini wa haki za binadamu. Lakini, yapo bado matukio baadhi ya maeneo ambapo watoto wenye umri wa kwenda shule hawaendi shule kutokana na sababu moja au nyingine. Ninadhani wakati umefika sasa kuchukua jitihada mbali mbali kuhakikisha kwamba watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanakwenda shule. Wasitumike watoto hawa kufanya shughuli za uchungaji. Wasitumike watoto hawa kufanya shughuli za migodi na shughuli nyingine. Nafahamu wazi kwamba tunaszo sheria nyingi sana ambazo zinaelezea kwamba kumtumia mtoto wa shule katika kazi ya aina yoyote ni kinyume. Lakini yamkini sheria hizi bado hazijafahamika vizuri. Kwa hiyo, niombe sana sheria hizi zitumike vizuri ili kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule aweze kwenda shule kwa sababu ni haki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu wazi kwamba nchi yeyote ikitaka kuendelea, suala la kuwa na rasilimali watu ni jambo la msingi sana. Tunaposema rasilimali watu ni watu wenye elimu, wenye uwezo wa kubuni mambo mbalimbali. Kwa hiyo, ni jukumu letu kama viongozi, ni jukumu letu kama wananchi kuhakikisha kwamba watoto wenye umri wa kwenda shule, wanakwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa upande wake imejitahii sana. Ilani imekwishatekelezwa. Ilani imesema kwamba tunatarajia asilimia 50 ya watoto watakaofaulu darasa la saba waweze kwenda sekondari. Lakini, sasa hivi baadhi ya Mikoa imekwishafikisha asilimia mia moja. Kwa hiyo, niipongeze sana ile Mikoa ambayo imekwishafikisha asilimia mia moja ikiwa ni pamoja na Mkoa wangu katika baadhi ya Wilaya, kwa mfano Wilaya ya Njombe, asilimia mia moja wanakwenda shule, Mikoa kama ya Dodoma. Niendeleo kutoa wito kwa ile Mikoa ambayo bado wajitahidi kutekeleza hilo kwa sababu ni haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu zaidi utakaa upande wa ushauri. Ningependa kuishauri Serikali kwamba suala la kuweka umeme katika shule zetu za sekondari pamoja na vyuo, ni jambo la msingi sana. Tunaposema rasilimali watu ambao ni watu wenye elimu, tunatarajia wafahamu mambo mengi sana ikiwa ni pamoja na masuala ya *IT* na masuala ya sayansi, vitu kama *Laboratory* zinahitajika kwenye shule hizo. Sasa, umeme kuwepo kwenye shule hizi ni *structure* ambayo ni ya msingi sana. Ombi langu kwa Serikali, tunapopanga makisio ya kusema kwamba gharama za kukamilisha shule hii ni kadhaa, gharama ya kukamilisha darasa hili ni kadhaa basi suala zima la kuweka umeme lizingatiwe ili tunaposema kukamilisha darasa ni milioni 7 au nyumba ya Mwalimu ni milioni 9 basi kipengele cha umeme kiwe kimezingatiwa ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zetu zina mambo mengi sana. Tukisema tuziachie *Local Government Authorities* kushughulikia masuala haya, utakuwa ni mzigo mkubwa na baadaye itabidi turudi tena kuanza moja kuweka umeme katika kila shule. Wafadhili wengi na sisi wenyewe Wabunge tumekuwa tukijitahidi sana kutoa vitu kama kompyuta lakini, ukifika pale shuleni, wanakwambia Mheshimiwa bado hatuna umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya *Information Technology* yako mambo mengi sana ambayo yangeweza kupatikana kwa kuwa na umeme. Naomba jambo hilo Serikali iliangalie. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini, waangalie zipo Wilaya kweli hazina umeme, basi waangalie kama wanaweza kutumia hata umeme wa *solar* kwa kuanzia. Lakini badaye tuangalia ni jinsi gani tunaweka umeme katika shule zetu. Tutakapokuwa na umeme utasaidia hata wale watoto kusoma kwa muda mrefu hasa zile shule za *boarding* na vitu kama hivyo. Naomba sana jambo hilo tulizingatie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vyuo vingi sana katika nchi yetu ambavyo vinafanya kazi nzuri sana na vyuo hivi ambavyo vingine ni vya Ualimu, vinatoa *Certificates*. Siyo mbaya vyuo hivi tungevi-*up-grade*. Kwa mfano, Chuo cha Ualimu cha Tandala Wilayani Makete. Chuo hiki kimekuwa kikitupa Walimu wazuri sana. Lakini, tuki-*up-grade* Chuo hiki, kikatoa *Diploma*, itakuwa ni jambo zuri sana. Lakini tena watakwambia labda wanahitaji *structure* za umeme. Mambo mengi sana tunapokuwa tunakosa umeme inakuwa ni vigumu kuyatekeleza. Kwa hiyo, jambo lingine tuangalie ni jinsi gani tunaweza tukaimarisha na kuboresha zaidi masuala ya *structures* za shule zetu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine kama nilivyosema kwamba yapo baadhi ya maeneo inakuwa ngumu kupeleka asilimia mia moja ya watoto shuleni kutokana na sababu moja au nyingine. Ingekuwa siyo mbaya tungekuwa na *registers* katika kila kijiji. *Registers* hizi ziwe zina-*monitor* idadi ya watoto wanaozaliwa na ukisha-*monitor* ile idadi, wanashirikiana na kitongoji, inakuwa rahisi kujua baada ya miaka 6 tutakuwa na watoto wangapi ambao wataingia darasa la kwanza. Wale ambao tutaona kuna upungufu mkubwa, kwamba tunatarajia kijiji X kipeleke watoto idadi kadhaa lakini kimepeleka watoto chini ya asilimia 50, hii asilimia 50 imepotea imekwenda wapi? Tunapokuwa na *Registers* inasaidia sana hata masuala mengine mengi ya takwimu. Kwa hiyo, ninadhani suala hili ni la msingi sana na itasaidia pia tunapokuwa tunachukua hata sensa za nchi yetu, tunapopanga mipango na mikakati kabambe ya maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Wizara kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kupitia Vyuo vya Ufundi – Vyuo vya *VETA* na vyuo vingine ambavyo vimekuwa vikifadhiliwa na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali pamoja na Mashirika ya Dini. Wizara imefanya kazi kubwa na katika Ilani ya Uchaguzi, tumesema kwamba tutajitahidi katika kila Wilaya kutakuwa na Chuo cha Ufundi. Bado kitendawili kikubwa kinakuja, inakuwaje ile Wilaya ya Ludewa ambayo haina umeme? Hapo ni jambo la kuliangalia sana ili Wilaya zetu zote ziwe na Vyuo vya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema kwamba sisi wananchi wa Wilaya ya Ludewa, tumefanya maandalizi makubwa sana ya kujiandaa kupokea chuo hicho cha *VETA* kama tulivyohidiwa kwenye Ilani ya Chama Tawala na tumeishaanda eneo lenye ekari zipatazo 30, tumeishafyeka. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa sababu najua atanipa ushirikiano wa hali ya juu na tutafurahi kama atafika kule kuona hilo eneo na kutushauri zaidi kwa sababu tunafahamu vyuo vinahitaji eneo kubwa. Kwa hiyo, tumeishaandaa. Tungeomba kipengele hiki cha Ilani kikatekelezwa kama kipengele kingine ndani ya Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwashukuru sana wafadhili mbali mbali ambao wamekuwa wakichangia Serikalini hasa katika sekta ya elimu na niwahakikishie kwamba mchango wao umetoa matunda makubwa sana na sisi kama Bunge ambao tunasimamia Bajeti hizi kimsingi tunahakikisha kwamba kazi hii inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la shule za mabweni: Shule nyingi za mabweni huwa zinaingia mikataba na watu mbali mbali ku-*supply* vyakula. Wale wanao-*supply* vyakula kwenye zile shule, wamekuwa wakikumba na vikwazo kwamba malipo yao huwa yanachukua muda mrefu. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ilianguilie hilo ili iwape moyo wale wanao-*supply* vyakula kwenye vile vyuo waweze kupeleka vyakula vyenye *standard* na watoto wetu waweze kusoma vizuri na kuwa na afya bora na kupata maisha bora ya kila Mtanzania. Shule hizi ambazo kwa kweli bado zina mzigo mkubwa wa madeni ya kulipa ni pamoja na shule ya Sekondari ya Tosamaganga iliyoko Mkoani Iringa. Shule nyingine ambazo bado zina mzigo, basi ningeomba sana Serikali ianguilie

jinsi ya kuzisaidia. Kulipwa, wanalipwa, lakini wakati mwingine huwa inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la *High School*. Kama tunavyoenda na kasi hii kubwa katika shule za sekondari za *O' Level*, vivyo hivyo tunahitaji kasi kubwa sana za shule za *A' Levels*. Ziko Wilaya ambazo mpaka sasa hazina shule za *A' Level* ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Makete pamoja na Wilaya ya Ludewa. Tunaomba sana Wizara watuletee Wakaguzi ili zile shule ambazo zina *structure* za kutosha tuzi-up-grade, tuongeze yale madarasa ya *A' level*, huduma ile iweze kupatikana. Kwa hiyo, hilo nadhani ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa sasa hivi na tunashukuru sana kwamba katika kila Wilaya wameweka msaidizi au Mshauri wa masuala ya elimu anasaidia sana. Mkoa mingine hatuna Ofisi za Wakaguzi. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa, Mkaguzi lazima atoke *Mbeya Zonal Office*. Lakini tukiweza kuweka wale Wakaguzi wa shule za sekondari pia katika kila Mkoa nalo litakuwa ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru sana Wizara kwa kazi nzuri na mambo mengine makubwa ambayo wanazidi kufanya, hata mtoto akizaliwa, haanzi kukimbia hapo hapo, anaanza kutambaa, anaanza kutembea kidogo na kadhalika.

Lakini, tunaomba tu tuzidi kuongeza kasi za Walimu katika Wilaya za pembezoni na tukiweza tuweke zile *allowance* za mazingira magumu ili Walimu waweze kwenda maeneo ya pembezoni ikiwa ni pamoja na eneo la Ludewa, maeneo ya Makete, Walimu waweze kupenda kwenda kutoa huduma ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nami naunga mkono hoja hii ya elimu kwa aslimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kabla ya hapo, napenda kutoa pole sana kwa familia ya aliyekuwa Mbunge mwenzetu ambaye ametutoka sasa, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Kwa kweli alikuwa mtu mzuri, kila mtu alimpenda, kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu amemchukua. Kwa hiyo, napenda niwape pole sana na naomba roho yake iwekwe mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Waziri wa Elimu, Manaibu Waziri wake na Makatibu Wakuu wake. Kwa kweli kazi nzuri wameifanya. Ukipitia *data* walizotupatia hapa kwenye hivi vitabu, unaona kabisa kazi nzuri inafanyika. Kwa hiyo nampongeza sana na kama msomi nasema kazi nzuri sasa inaendelea huko Wizara ya Elimu, *we are very satisfied*. Tuko *very satisfied*, acha yale mambo tunakuja hapa tunasema *and then* tunaanza kulaumu lakini hii naweza ku-*stand* nayo, kazi nzuri inafanyika huko. Lakini niipongeze vile vile na Serikali yetu inafanya kazi nzuri sana.

Madarasa yaliyojengwa ni *record*. Tuanze hivyo tangu tupate uhuru, leo tungelikuwa kila mtu anafika Chuo Kikuu. Lakini, kuna mahali pa kuanzia. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tugeuze hiki kitabu, *Basic Education Statistics in Tanzania*. Kama unataka kujua elimu ya Tanzania, huyu aliyetuwekea hiki kielelezo hapa, basi amemaliza wala huna haja ya kusoma zaidi. Unaangalia hiyo, unaichambua, unajua hali ya Tanzania kielimu ilivyo. Kilichonipendeza zaidi ni kuona kwamba 1961 tulikuwa na asilimia 14 ya wanafunzi wa kike katika *Form Six*, leo ni asilimia 41. Kweli ni mafanikio makubwa. Uchambua kuja chini, wasichana sasa wanakuja asilimia 50. Wewe usije ukafikiri wanaume tukisoma, sisi hatukai nyumbani, akina mama ndio muhimu sana, ndio wanaojua mtoto ana hali gani, mtoto ameugua nimpeleke hospitali, usafi wa pale nyumbani, mama anahusika sana. Hata angekuwa *Principal Secretary*, Waziri, lakini ukienda pale nyumbani, mama atakuwa anafanya kazi kubwa. Kwa hiyo, tunashauri kwamba Serikali iweke mkazo kabisa tusije tukalegalega, watoto wa kike wasome, ni muhimu sana kuwapeka shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, ukiangalia tena hapa, tuje hapa *primary school*, utaona kwamba pamoja na madarasa yaliyojengwa, tuna kazi kubwa. Watu wanasema tumejenga madarasa, sasa tumechoka. Tusichoke kwa sababu kama mwaka huu watoto watakaofanya mtihani wa darasa la saba ni 816,000 lakini mwaka kesho watakuwa 1,151,000. Tutaongeza watoto 300,000 hapo ambao watafanya mtihani na hao wote wanatakiwa kwenda *Form One*. Sasa, tukisema tumelegea, tutakuwa tumefanya makosa makubwa sana. Naomba sana sana wazazi huko tuliko tujifunge mkanda. Kama kuna kitu cha kujifunga, basi ni kujifunga mkanda ili tujenge madarasa. Tujenge madarasa watoto wetu wasome, hatuwezi kuendelea, wengi tumesema hapa. Mheshimiwa Nyami pale kasema, kila mtu anasema elimu ni muhimu na kwa kweli bila elimu hatuwezi kufika popote. Vile vile ukiangalia hapa *Form Six*, Tanzania kwa leo 2007 ina *Form Six* 20,000 na huku tuna Vyuho Vikuu 33. Hivi tutatoa wapi wanafunzi wa kujaza hivyo Vyuho? Ni wachache mno! Halafu hapa katika *Statistics*, mwaka jana waliopata *Division One* na *Division Two* ni asilimia 20. Ukizidisha mara asilimia 20 na watoto 20,000 walioko *Form Six* ni kwamba watakaofuzu kwenda Chuo Kikuu ni 4,000 tu ndio wanatakiwa. Sasa, kuna haja ya kufanya *Marshal Plan* kuongeza watoto katika *Form Five and Six* ili waweze kujaza hivyo Vyuho. *This is a very serious issue*. Mwaka 2007 unakuwa na watoto 20,000 *Form Five* na *Six*, ni wachache mno. Kwa hiyo, *we need a Marshal Plan*. Sasa hivi tunasema tutajenga madarasa 128. Hapa tutaweza kupeleka watoto 5000 mwaka 2009 ukiongeza na 20,000, ndio unapata 25,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Vyuho Vikuu viwili vinajengwa hapa Dodoma, kimoja nasikia kitachukua watoto 40,000. Kwa hiyo, *intake* ya mwaka ni 10,000 wakati huna watoto wa *Form Five* na *Six*, unatarajia hao watu waende wapi? *We need a Marshal Plan* na ni kwamba *within two years* tuwe na watoto 70,000 *Form Six*, hapo ndio unaweza kusema unajenga Vyuho Vikuu *otherwise* utawapeleka watoto ambao ni *sub-standard* huko Chuo Kikuu kwa sababu Vyuho vinataka kujaza kwa sababu vingine ni *private*, una *Principal* moja, unakwenda lakini, ni elimu gani wanatoa? Elimu ya Chuo

Kikuu, siyo ya lele mama, lazima wawe *well educated*. Acha vihiyo, mtu anasema ana Ph.D. Ukimwuliza amesoma wapi, anapiga chenga. Hatutaki elimu ya vihiyo hapa, tutaua nchi. Lazima uende usome. Kwa hiyo, *Form Five* pale tunapeleka watu ambao wamepata *Division One, Division Two* lakini, *Division Three*, huyo lazima awe mzuri sana. Kwa hiyo, lazima tuwekee nguvu sana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie katika kitabu hiki ukurasa wa 57. Nashukuru kwamba wameleta *data* wenyewe na tunazichambua. Katika mwaka 2006 ni asilimia 4.5 ndiyo iliyopata *Division One Form Four One*. Tunawafundisha watoto, asilimia 4.5! Nchi imekuwaje? Walimu wanafundisha au hawafundishi? Halafu unaambiwa *Division Two* 6.9! Kwa hiyo, hapa tuna 11.4 ndio walishinda. Ndiyo na hesabu walishinda *total* ya walioshinda *First Division* na *Second Division* wanaenda *Form Five*. Hivi kweli huko shuleni wanafundisha au hawafundishi? Naomba Wizara ifanye *examination* kali kujua kwa nini watoto wanaanguka mitihani! Sasa shule ni *industry* ya ku-*manufacture failures! We cannot afford that*. Hii ni nchi yetu, *we cannot afford that! It's very bad!* Halafu asilimia 65 walianguka mtihani! Asilimia ya watoto 2600, 65 walianguka mtihani na sijasikia kwamba Wizara ilichukua hatua juu ya suala hili. Ninaomba maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu sasa angalia viroja. *Form Six* mwaka huu, 7.2. Kweli watoto walioshinda wakachujwa vizuri wakaenda *Form Five*, inakuwaje *Division One* wanakuja kupata 7.2, halafu *Division Two* 18.1. *Total* ya waliofaulu hapa ni kitu kama 25.3. Lakini, kama kweli watoto walishinda kwa sababu mimi nilishinda, nikaletwa hapa Mazengo, tulikuja *stream* yetu tulikuwa *total* 22 wote *First Class*, wote tulienda Chuo Kikuu! Kwa nini tena tuanguke? Sasa kwa nini watoto wanaanguka wakifika *Form Six* kama kweli *selection* ilikuwa vile na tulichukua watoto wazuri? Ama ni vihiyo ambao vinavuzisha mitihani? *We cannot afford* kucheza na elimu! *This is very bad. We cannot afford*. Mimi ni msomi, lazima niwambie hiki, haiwezekani tukacheza na masomo. Lazima tujue kwa nini watoto wanaanguka mitihani! Wanapelekwa shuleni kwenda kuanguka? Kwa kweli mimi nasikitika sana! Sasa tumesikia Kenya imepiga *bingo*, inatoa elimu bure ya sekondari. Kenya imetangaza kwamba elimu ya sekondari inatolewa bure na sisi tufikirie kuitoa bure. Elimu ya darasa la saba imepitwa na wakati. Watoto angalau wakiwa na *Universal Secondary Education* hapo ndio utakuwa tumeboresha elimu. Sasa mtoto akisoma darasa la saba na amesoma huko vijijini, kweli anaweza kufungua *internet*? Hivi mtu wa karne ya sasa akiwa hawezi kufungua *internet*, huyo amesoma? Tupeleke watoto mpaka *Form Four*, uwezo tunao *we can do it!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunafundisha sekondari, ati shule tunakazana nyumba za walimu, madarasa, maabara tunasahau. Ni sayansi tunasomesha hiyo? Tusisahau maabara, elimu lazima ikamilike na elimu ya sayansi huwezi kuifundisha bila maabara! Utafundisha *Physics* ile *Newton's Law, Faraday*, bila kuitazama inacheza pale kwenye *practical*, umefundisha *Physics* gani! *We need quality education!*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna kitu kinaitwa *IT*, sasa hivi kuna vigogo, watoto wao kuanzia *Kindergarten* wanacheza na *Computer*, wanaingia shule za *primary* wanacheza na *Computer*, wanakwenda *High School*, wanacheza na *computer*. Mtoto wa mlalahoi anakuja kuona *Computer University*, utawezana nao? Tunajenga elimu ya

kimatabaka hii! Hakuna hatari kama kujenga elimu ya kimatabaka nchini. Tuna taka *IT* isambazwe. Kuna *Solar*, *solar* iko pale, tuiseme umeme haupo. Siku hizi siyo lazima uweke umeme wa *grid*, kuna *solar* zipo na kompyuta. Sasa mtasema hela hazipo! *One VX* ina-cost more than a hundred million, kama ukichukua hizo hela ukasema kila mtu pale Dar es Salaam *Oysterbay*, chukua *Mark II* nenda kazini. Moja tu inakupa kompyuta 150. Ukizuia mashangingi 10, usiyanunue mwaka huo, una kompyuta 1500. Hujaleta *IT* mashambani? *We need IT* katika shule zetu za vijijini. Tusijenge elimu ya kimatabaka hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kingine, elimu kila Kata. Elimu isitumike hivyo kwamba kila Kata kuwe na shule, hapana. Tuweke *distance radius*, mtoto gani atatembea kama Kata yangu ya Ikoma ni kilomita karibuni 100 na shule iko Bwitengi, wa Lubanda ataendaje? Tuweke kwamba *may be five radius kilometre*, shule ya sekondari iwepo. Sasa nakwenda kwenye Wilaya yangu. Wilaya yangu tuna shule karibuni kila Kata lakini watoto wanaanguka hakuna Walimu, vifaa hamna, shule hizo hazijatembelewa na *senior person* kutoka Wizara ya Elimu. Mwaka juzi nililalamika hapa inakuwaje miaka mitano hatuoni mtu akija kututembelea? Au kwa sababu tuko pembeni, njooni mtuone mtusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri naomba ufike Serengeti ukatungalie huko. Tumejenga mabweni ya wasichana katika shule ya Nata Sekondari, Dr. Omar Juma, Serengeti Sekondari School, Isangula Sekondari, Kambarage Sekondari na Mwachuo Sekondari, lakini hatujapata msaada wowote kutoka Serikalini. Tunaomba Serikali ituangalie. Tumeza ng'ombe tumemaliza, MMES tukiomba hatupewi hela, sasa tunaomba msaada. Vile vile tume-*plan* kujenga mabweni Kisangula mwaka huu tuna Sh.60 milioni na Ikoma tuna Sh.60 milioni. Tusaidieni tumalize, ili watoto wetu wakae bwenini. Tunatarajia kuleta maombi ya shule nne kuwa *high school*. Tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie zisajiliwe. Baada ya kusema hivyo, naipongeza tena Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri iliyofanya. Naomba tuendelee hivyo. Tunalia kwa uchungu na katika uchungu huo ndio tuta-move.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, napenda kusema kwamba *you are doing a good job and we are with you* na ninaamini Bajeti hii itapita bila matatizo. Kazi yako ni nzuri mno na tunakupongeza, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kuungana na Watanzania wenzangu na Waheshimiwa Wabunge kutoa pole kwa familia, marafiki na jamaa kwa msiba uliotokea kwa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia. Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho ya Marehemu, amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii ya awali kabisa, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na viongozi wengine katika Wizara kwa hotuba nzuri iliyowalishwa kwenye Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba madhumuni makubwa ya kuwapa uwezo wananchi katika ngazi ya Wilaya na Serikali za Mitaa ni kuhakikisha kwamba wananchi wanashiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo na utekelezaji wa mipango hiyo kuanzia kuchagua vipaumbele, kubaini matatizo, kushiriki katika utekelezaji pia na kumiliki miradi hiyo baada ya kukamilika. Moja ya nyenzo ya kuwawezesha au kuwajengea uwezo wananchi ni kuwapa elimu iliyo bora. Elimu iliyo bora inatoa ujuzi na kuwapa maaarifa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za Maendeleo. Wahenga walisema: “Elimu ni ufunguo wa maisha”.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi duniani zilizopiga hatua kubwa katika Maendeleo ya kiuchumi, kiteknolojia na kijamii ni nchi zilizozingatia kwanza suala la kuwapa elimu bora wananchi wake. Ni dhahiri kwamba matokeo ya rasilimali watu kutoandaliwa kwa kuwa nyuma kielimu kunaleta athari kubwa sana kwa sababu wananchi hao wanakuwa hawawezi kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo inayokuwa imepangwa na kutekelezwa katika maeneo yao mbalimbali katika nchi yetu hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Tunayo mifano, katika sekta ya maji kwa mfano, kuna miradi ambayo imechelewa kutekelezwa kutokana na kutoshiriki kwa wananchi kikamilifu katika utekelezaji wa miradi hiyo na tuna mifano katika sekta ya kilimo kuna miradi ambayo inachelewa kutekelezwa kutokana na wananchi kutoshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mipango hiyo ya maendeleo. Lakini moja ya tatizo ni wananchi kuwa nyuma kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa elimu katika maisha ya wananchi tumeona elimu inakuwa ni kichocheo kikubwa sana katika maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne, kwa uamuzi wake wa makusudi wa kutoa kipaumbele kwa sekta ya elimu katika bajeti ya mwaka huu. Serikali ya Awamu ya Nne, imetoa kipaumbele sana na sekta ya elimu imepata asilimia 18 ya bajeti nzima. Tunaipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo na ndiyo sababu yangu ya kimsingi ya kuunga mkono hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga shule za sekondari kwa kushirikisha wananchi kupitia Halmashauri zao na Serikali za Mitaa. Ujenzi wa shule za sekondari kwa kutumia nguvu za wananchi umeipa heshima Serikali na nchi yetu kwa ujumla. Nchi inapofanya mambo makubwa kama ujenzi wa sekondari nchi nzima na ujenzi wa mradi wa maji, kwa mfano, kutoka Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Shinyanga na sehemu zingine kwa kutumia fedha zake bila kutegemea wafadhili ni heshima kubwa kwa nchi. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo wa makusudi wenye lengo la kujitegemea ambao umeleta mafanikio na heshima zaidi kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za Serikali kukabiliana na changamoto la ongezeko kubwa la wanafunzi wanaomaliza darasa la saba ni za kupongezwa wala siyo za kubezwa au kudharauliwa/kupuuzwa. Naomba sana Watanzania wenzangu tuthamini jitihada zetu wenyewe tunazofanya kukabiliana na matatizo yetu. Mafanikio yote yana gharama na tunapona nchi zingine zimepata mafanikio makubwa ya kimaendeleo mfano

nchi za Japan, Marekani, Uingereza, wananchi wake waligharamia mafanikio hayo. Kwa hiyo, jitihada za Serikali za kushirikisha wananchi washiriki wenyewe katika ujenzi wa shule za sekondari ni jambo kubwa sana na tulithamini sana pamoja na kwamba tunagharimika na wakati mwingine tunapata machungu. Mafanikio yoyote yana gharama. Kwa hiyo, *there is no pain there no gain. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto mbalimbali zinazokabili nchi yetu hazitaisha siku moja. Ilani ya Uchaguzi ya CCM imetoa mwelekeo bayana na kuungwa mkono na Watanzania wengi. Naomba Watanzania tushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Nina hakika hatua kwa hatua maisha bora kwa kila mwananchi yatapatikana. Nia njema ni zabibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Serikali inajitahidi katika kukabiliana na changamoto mbalimbali katika sekta ya elimu. Nimpongeze Mheshimiwa Margaret Sitta na viongozi wenzake katika Wizara ya Elimu, kwa kazi nzuri inayoonekana kuleta matumaini kwa Watanzania. Lakini naomba nitoe ushauri wangu katika maeneo yafuatayo; ushauri wangu wenye lengo la kuboresha na kuongeza kasi Serikali yetu ya Awamu ya Nne katika kuleta maisha bora kwa kila mwananchi na kuboresha sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali wa kuanzisha Chuo cha Ualimu, mchepuo wa biashara Mkoa wa Shinyanga ni uamuzi wa kupongeza sana. Hata hivyo, kutokana na ongezeko kubwa sana la shule za msingi litakaosababisha kuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaomaliza darasa la saba, upo umuhimu mkubwa kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeza mchepuo wa kufundisha walimu masomo yenye michepuo mingine katika Chuo cha Ualimu chenye mchepuo wa biashara kinachoanzishwa Mkoa wa Shinyanga. Tuna mahitaji makubwa sana ya walimu, pande zote walimu wa shule za msingi na walimu wa shule za sekondari. Wilaya ya Kishapu peke yake ina upungufu wa walimu 608 wa shule za msingi. Hivyo uwiano wa utoaji wa taaluma sahihi kwa Wilaya ya Kishapu ni moja kwa sabini badala ya moja kwa arobaini. Kwa hiyo, tunaona tuna mahitaji makubwa sana. Kwa hiyo, fursa hii ya kuanzisha Chuo cha Ualimu Mkoa wa Shinyanga, kwa kutumia Chuo cha *SHYCOM* ni fursa nzuri na tunaomba Serikali iangalie uwezekano huo wa kuweka michepuo mingine ili walimu wa michepuo mingine waweze kufundishwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kishapu pamoja na kukabiliwa na njaa kwa muda wa miaka mitatu mfululizo lakini tumeweza kushirikiana na Serikali na kuweza kujenga shule za sekondari 17. Pamoja na hatua hiyo bado mahitaji ya shule za sekondari ni makubwa sana na kwa kutambua hivyo Mgodi wa almasi wa Mwadui, uliamua kutoa baadhi ya majengo ili yaweze kutumika kuanzisha shule za sekondari, kidato cha kwanza mpaka cha nne na mengine kidato cha kwanza mpaka cha sita. Nitumie nafasi hii kuupongeza uongozi wa kampuni ya Mwadui na hususan Mkurugenzi Mtendaji, Tony Davin kwa moyo wake wa kiungwana wa kuona aweze kutoa majengo yale yaweze kusaidia Wilaya yetu ya Kishapu na Tanzania kwa ujumla ili tuweze kuanzisha shule ya sekondari ya kidato cha kwanza mpaka cha nne na cha tano mpaka cha sita.

Lakini baada ya ukaguzi Serikali imetoa ushauri tuanzishe kidato cha kwanza mpaka cha nne tu kwa sababu cha tano mpaka sita kutahitajika maabara. Lakini la kusisitiza hapa ni kwamba ni vema viongozi wa Wizara wakaona wenyewe kwa sababu baada ya kufanya ukaguzi na mimi nilikuwepo na uwakilishi wa Wilaya ulikuwepo tuliona kwamba majengo yaliyopo yanafaa kuanzisha shule ya sekondari ya kidato cha tano mpaka cha sita. Kuna fursa nzuri sana, kuna umeme pale na kuna maji. Shule za Sekondari zinazoanzishwa wala hazina fursa hiyo ambayo inawezekana ikapatikana pale mgodini. Kwa hiyo, naomba Wizara irejee uamuzi wake wa kutojenga au kutoruhusu kuanzisha shule ya sekondari kidato cha tano mpaka cha sita kwa sababu fursa hiyo ipo. Sisi wananchi ndiyo tunaibua hiyo na tunasema sasa wananchi waibue wenyewe Serikali iunge mkono. Naomba sana Serikali ilianguzie sana jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipokuwa inajibu swali langu kuhusu uanzishwaji wa shule ya *VETA*, imetoa maelekezo kwamba Wilaya itenge eneo la kujenga Chuo cha *VETA*. Napenda kuchukua nafasi hii kuiarifu Serikali kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, imekwishatenga eneo kwa ajili ya kujenga Chuo cha *VETA*. Naomba Serikali itumie nafasi hii vile vile kuwaeleza wananchi ni lini sasa Chuo cha Ufundi cha *VETA* kitaanza kujengwa katika Wilaya ya Kishapu kwa sababu eneo tayari limetengwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho nafikiri kwa haraka haraka nizungumzie ujenzi wa shule za walimu na ujenzi wa hosteli kwa shule za sekondari zinazojengwa. Kuna matatizo makubwa sana ya nyumba za walimu kutokana na ongezeko kubwa sana la shule za sekondari zinazojengwa. Kuna tatizo la hosteli kwa wananchi wasichana kwa sababu wanakaa mbali sana, shule zingine zimejengwa mbali na makazi ya watu. Naiomba Serikali iangalia uwezekano wa kutumia shirika la nyumba la taifa kujenga nyumba za walimu na iangalie uwezekano wa kutumia jeshi la magereza kujenga nyumba na hosteli na vilevile iangalie uwezekano wa kutumia Jeshi la Kujenga Taifa katika kukabiliana na hilo tatizo kubwa la upungufu wa nyumba za walimu na mabweni kwa ajili ya wanafunzi wasichana katika maeneo mengi na hususan katika Wilaya ya Kishapu ambayo ina eneo kubwa sana na shule zingine zimejengwa katika maeneo ambayo shule hizo ziko mbali na makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kusema yafuatayo: kwanza, matatizo haya ambayo yanatukabili katika sekta ya elimu, Serikali iangalie kushirikisha wadau mbalimbali na ninaamini kwamba tutaweza kuyamaliza na hasa tukizingatia kwamba tukiwa na nia njema ambayo ni zabibu, yote yanawezekana. Baada ya kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwa namna ya pekee sana naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mama Magreth Sitta. Mama Margret Sitta, ana historia kubwa sana katika kuongoza Wizara hii.

Kule alikotoka amefanya kazi kubwa mno akisaidiana na walimu wenzake nikiwemo mimi na walimu wengine katika nchi hii ya Tanzania. Kwa kweli amefanyakazi kubwa sana na ninaamini kwamba sekta hii anayoiongoza iko katika kichwa chake hata anapoamshwa usingizini anaweza akasema matatizo ya walimu, matatizo ya sekta ya elimu kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze pia Naibu Mawaziri hawa wawili, kwa kweli ni watu jasiri, tumekuwa tukiwaona wakijibu maswali yetu hapa Bungeni, lakini wakitimka katika kona zote za nchi hii ya Tanzania kuhakikisha mipango hii yote inafanikiwa vizuri.

Naomba pia nimpongeze Katibu Mkuu, akishirikiana bega kwa bega na Naibu Makatibu Wakuu katika ofisi hiyo. Kwa kweli hata wale wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana kushirikiana na Katibu Mkuu, kuhakikisha kwamba masuala haya ya elimu na masuala ya ufundi stadi katika nchi yetu ya Tanzania na kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau naomba nimshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mheshimiwa Sabaya. Nimshukuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Mheshimiwa Jumanne Nyingo na Madiwani wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea pamoja na wananchi wote wa Jimbo la Peramiho kwa kushirikiana kwa kiasi kikubwa bega kwa bega kuhakikisha tunatekeleza azma ya Serikali ya kuendeleza sekta ya elimu katika Jimbo la Peramiho.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninaanza kuwa Mbunge wa Jimbo hilo tulikuwa na sekondari tatu za Serikali yaani Sekondari ya Mpitimbi, Madaba na Makoselo. Sasa hivi tumeshafikisha kiwango cha sekondari 20 katika muda huu mfupi. Hayo ni maendeleo makubwa sana.

Nawapongeze wananchi wa Uwino kwa kujenga sekondari moja na kuweka matarajio ya kuongeza sekondari ya pili. Mahanje kwa kuwa na sekondari mbili ya kata na ya Kijiji, Gumbilo kwa kuwa na Sekondari moja, Tanga kwa kuwa na sekondari moja, Lilambo kwa kuwa na Sekondari mbili, Maposeni kwa kuwa na Sekondari mbili, Mgazini kwa kuwa na sekondari moja, Litisha kwa kuwa na sekondari mbili, Magagula kwa kuwa na sekondari mbili, Mpitimbi sekondari moja, Ndogosyi sekondari mbili, Matimila sekondari moja. Muhukulu mpakani mwa Tanzania na Msumbiji haijapata kutokea tuna sekondari mbili zimekwishajengwa na wananchi huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni maendeleo makubwa sana, kwa hiyo, nawashukuru wananchi wa Peramiho na mimi nawaambia tuko bega kwa bega tutayafanya maagizo yote ya Serikali kwa maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Peramiho na Halmashauri yetu ya Wilaya ya Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mjadala kwenye suala la elimu. Niseme kwamba maamuzi ya Serikali katika mwaka huu wa fedha kutoa kipaumbele cha bajeti kwenye sekta ya elimu ni suala la msingi kabisa. Mimi ninapozungumza na wananchi

wangu wa Jimbo la Peramiho, mara nyingi ninawaambia bima iliyo bora kuliko bima zingine zote katika dunia ni elimu. Ukiwekeza kwa mtoto wako katika elimu basi umewekeza bima ambayo ni bora kuliko bima nyingine yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha yetu tunayajua. Kuna umri wa utoto ambapo mtoto amekuwa akitegemea sana malezi ya wazazi, kuna umri wa ujana ambapo uwezo wa kufanyakazi na kujitafutia riziki ya maisha unakuwa ni mkubwa sana. Lakini umri wa uzee ni umri tegemezi, unategemea sana msaada na matunzo kutoka katika mtu ambaye anaweza akakuhudumia. Usipomsomesha mtoto huna bima katika umri wako wa uzee, hata kama utakuwa na fedha. Hakuna mtu atakayeweza kukusaidia. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwekeza kwenye elimu ili kuleta maendeleo ya Watanzania. Hilo sina matatizo nalo, ninaamini tumejiwekea malengo, mwakani tutatathmini malengo haya ya kielimu yametufikisha wapi na hatimaye tutahamia katika kipaumbele kingine na baada ya miaka mitano tutaweza kumaliza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kwa kiasi kinachotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa labda niingie katika hoja ya msingi ya Mheshimiwa Waziri. Mimi kama walivyofanya wenzangu nilikuwa najaribu sana kupitia taarifa mbalimbali ambazo zimewasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri katika hoja hii ya elimu. Tumeletewa mgawanyo wa fedha in *blocks*, wapi kitaenda kitu gani, wapi watapata nini na hali kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kuishauri Wizara ya Elimu, Waheshimiwa Wabunge tukitoka hapa tutakutana na wananchi katika maeneo yetu ya kazi, tutawapa taarifa njema ya Serikali kuweka msisitizo wa elimu na kutenga asilimia karibu 18 ya bajeti ili kuendeleza sekta ya elimu nchini. Tunafahamu kwamba suala la elimu limeingiliana katika utekelezaji ama utendaji katika Wizara zisizopungua sana tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini masuala tutakayouliza nina uhakika, “Mheshimiwa Jenista katika jimbo la Peramiho bajeti hii umetengewa shilingi ngapi za kujenga mabweni ya wasichana katika jimbo lako?”

Hilo swali tutalipata. Nitaaulizwa, “bajeti hii ni nzuri ya kuboresha elimu lakini hebu tuambie Waheshimiwa Wabunge ni shilingi ngapi.?” “Hebu tuambie Mheshimiwa Mbunge, ni shilingi ngapi tujiandae kwa ajili ya kukamilisha maabara katika shule zetu za sekondari”, bahati mbaya majibu hayo mpaka bajeti hii inavyoendelea sina.

Nilikuwa nashauri ama kabla hatujaondoka hapa Bungeni Waziri wa Elimu, atusaidie kutupa mgawanyo wa fedha hizo nyingi za kuboresha elimu kimajimbo ama kihalmashauri, tutakaporudi tunapokusanya nguvu za wananchi kujenga mabweni tujue msaada wa Serikali kwenye bajeti hii nono ni kiasi gani. Tutakapokusanya nguzu za kujenga maabara kwenye zile sekondari nilizozitaja hapa Jimbo la Peramiho tujue ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwenye Halmashauri yangu kwa ajili ya maabara. Vinginevyo tutapa kazi sana kufikia malengo haya tuliyojiwekea. Tumeona mfano mzuri kwenye barabara, ukiniuliza fedha za barabara kwenye bajeti ya mwaka huu kwenye jimbo langu ninaporudi nina uwezo wa kuwaeleza wananchi wa jimbo la Peramiho.

Lakini kwenye elimu naomba niwe mkweli, nimeshindwa mpaka dakika hii kulielewa hilo. Kwa hiyo, naomba sana tusaidiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumze kitu kingine. Wizara imekuwa ikileta fedha kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa sekondari zetu kupitia mpango wa MMES, fedha hizo zinapitia hazina ndogo Mkoani. Mimi nafikiri ni wakati muafaka kwa kuwa tumeamua elimu hiyo iwe kipaumbele.

Hebu tuwachangamshe wenzetu wa hazina ndogo, mshirikiane na Wizara ya Fedha, wamekuwa wakichelewesha sana fedha hizo katika sekondari zetu. Kwa hiyo, ninaomba suala hili liangaliwe na ninaamini kabisa kwamba nia njema ya Serikali inatakiwa iendane na nia njema ya usimamizi wa utekelezaji wa mipango na fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya kazi hizo.

Lakini labda nikiliacha hilo niangalie kitabu ambacho kinaonyesha taarifa mbalimbali za kazi katika Wizara yetu ya Elimu. Nilipokuwa nafungua ukurasa wa 52 wa *Basic Education Statistics in Tanzania (BEST)* cha mwaka huu 2003/2007 ukurasa wa 52 nilichogundua watoto wengi wanaojiunga na sekondari ni waliopo kati ya miaka 14 na 17, huo ni umri mzuri sana wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilipokwenda ukurasa wa 66 nimegundua kwamba yako matatizo ya *drop out* katika sekondari zetu. Kitu kikubwa kinachosababishwa watoto hao kutokumaliza kuondoka katika elimu hiyo ya sekondari, cha kwanza ni utoro ambao unaambatana na asilimia 62.6. Cha pili, ni sababu nyinginezo ambazo Mheshimiwa Waziri hajaziweka sawasawa lakini sababu nyinginezo nazo zinachukua asilimia 20.

Halafu linakuja suala la mimba za watoto, hiyo nayo inachukua asilimia 8. Kwa hiyo, hicho ni kiashirio cha tatu na mahitaji madogo madogo ya watoto katika shule yanayowasababisha wasimalize *form four* ni asilimia 7. Ninaomba sana kwa kuwa wenzetu wa Wizara wameshajua matatizo haya, hebu watuambie tuna mikakati gani ya kuhakikisha watoto wanaoanza shule wanamaliza shule wakiwa salama na kwa elimu iliyo bora. Vinginevyo hatutakuwa tunawasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumza umri ule wa miaka 14 na 17, watoto wanapoingia shule ndiyo umri wenye matatizo makubwa sana. Tusipohakikisha kuwa wanabaki shule, wanamaliza shule, ina maana kwamba bado tunaendelea kujenga taifa la vijana ambao watakaa kwenye vijawe huko vijijini na kwenye maeneo mengine. Badala ya kwenda mbele wataendelea kuleta matatizo makubwa kwenye taifa letu.

Sitaki kusema sana tatizo la mimba shuleni, mimi ingekuwa ni uwezo wangu wale wote wanaosababisha mimba hizi kwa kweli wangeshughulikiwa na wangemalizwa kabisa hata nguvu zao wasirudie tena hayo matendo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wazazi wanapata shida ya kuwazaa watoto wao, kuwalea na kuwasomesha na vijogoo visivyokuwa na msimamo vinaharibu maisha ya watoto wa kike. Umuhimu wa suala hili kama ulivyoonekana kwa Waziri nadhani

umefikia wakati wa kujadiliana bila kuonea aibu na kuchukua hatua za dhati na madhubuti. Hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumze kitu kimoja. Watoto wadogo chini ya miaka mitano bado wana matatizo, ubongo wa mtoto mdogo kuanzia umri wa mimba mpaka miaka mitano unakuwa umeshakua kwa asilimia 80. Asilimia 30 zinazobaki kuanzia miaka mitano mpaka unapokufa, lakini nani anahusika na watoto hao.

Wizara ya Elimu inakutana nao wakati wa elimu ya awali, Wizara ya Afya inakutana nao hospitali kwenye matibabu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, inakutana nao kama sekta mtumbuka. Watoto hawa wadogo chini ya miaka miaka mitano ni watoto wa nani?

Nani anatakiwa kuwaangalia kwa jicho la karibu? Nadhani huko mbele tunakokwenda watoto hawa wapewe mtu maalumu wa kuwatazama na kweli wakutane na hayo mengine huku lakini tujue nani kabisa yuko *responsible*.

Tutaharibu ubongo wao katika asilimia zile 80. Hata tukiwapeleka huko sekondari awe na msingi mzuri, ni kazi bure, hakuna kitu kabisa. Huko nyuma tulikuwa na bei kila *centres* zilikuwa zinafanya kazi vizuri sana, sasa hivi zimeanza kupwaya. Tungeendelea kuwa nazo zile tungeanza kuwapa misingi mizuri sana watoto wetu kwa ajili ya kuwajenga kielimu katika siku zinazokuja. Ningeomba sana Waziri aliangalie hili na ili ajue namna gani tunaweza kushughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niwapongeze walimu wangu wote katika jimbo la Peramiho, walimu wakuu wote wa shule za msingi na walimu wengine.

Niwapongeze walimu wa sekondari, wote wanaishi katika mazingira magumu lakini wamekuwa wakifanya kazi na tunashirikiana nao vizuri sana. Ninaomba niwape moyo, tuko pamoja, Serikali inawaangalia na tuendeleo kufanya kazi ili kuwasaidia wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada kusema hayo naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia 100 na nimtakie Waziri wa Elimu, usimamizi mwema wa bajeti hii kubwa ya kwanza yenye fedha nyingi katika kuleta maendeleo ya nchi ya Tanzania. Nakushukuru. (*Makofi*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii nzuri.

Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameifanya, Waheshimiwa Naibu Mawaziri ambao kwa kweli tunawaona jinsi wanavyochachalika katika nchi nzima kusimamia shughuli za elimu lakini na watendaji wa Wizara hii ambao kimsingi wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba kama kuna mahali Watanzania tunaweza tukajivunia kwamba tumekuwa na mikakati mizuri na mipango mizuri basi mipango yenyewe ni hii miwili, mpango wa MEM na mpango wa MMES. Hii ni mipango ya ukombozi wa elimu kwa Watanzania, wote tumeshuhudia kazi nzuri zinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme machache juu ya matumizi ili iweze kuwasaidia. Kwanza, naomba sana kwamba imarisheni ukaguzi wa fedha za MEM. Yapo matumizi mabaya ya mpango wa fedha za MEM. Sisi katika Halmashauri yetu ya Wilaya Muheza tumemweka mkaguzi wa ndani amepitia, ametoa taarifa inaonekana matumizi mabaya yapo.

Sasa taarifa zimefika kwenye Baraza la Madiwani, lakini mnafahamu tena uwezo wa Baraza la Madiwani, walimu ni walimu ile *chain of command*, hivi kweli Baraza la Madiwani linaweza likawatimua walimu wale ambao wamehusika na wizi wa fedha za mpango wa MEM?

Hata hivyo, hata ukiwafukuza haisaidii, jibu linabaki pale pale, fedha za mpango wa MEM zimetumika vibaya na hivyo tunahitaji kufanya maamuzi ya kuhakikisha usimamizi wa mpango wa fedha hizi za MEM. Hivyo hivyo katika fedha za MMES. Utaratibu wa kuwaweka wasimamizi wa fedha kwa ujenzi wa shule ambazo hazijaanza kwenye shule tunazojiita shule za walezi zimetuharibia sana matumizi ya mpango wa MMES. Mwalimu anakabidhiwa fedha, shule inayojengwa iko kilomita 50 kutoka kwenye shule yake na huyo ndiye unayemwambia mlezi wa shule asimamie matumizi ya fedha kilomita 50 kutoka pale alipo.

Hapa hatujakuwa makini. Matokeo yake mwalimu huyu ndiyo anafanya *management*, ananunua vifaa bila kuangalia mahitaji halisi katika eneo la ujenzi anapeleka vifaa, anavifikisha pale, anavibwaga anaondoka, hajakabidhi vizuri. Matokeo yake vifaa vinaibiwa; matokeo yake vifaa vinavyokwenda kwa hatua ya ujenzi analeta mabati kabla ya matofali, analeta matofali kabla ya sementi. Huu utaratibu mbovu, umeharibu fedha za MMES kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, la pili nasema kwamba andaeni taratibu zitakazoondoa mianya hii ya ubadhirifu wa fedha za MMES. Andaeni utaratibu mzuri, huu ulikuwa unaweka mianya na watu wametumia mianya hiyo kutumia vibaya fedha za MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, MMES ilipoanza, ndani ya Bunge lako Serikali ilisema itatoa shilingi milioni 7 kwa ujenzi wa madarasa, kusaidia nguvu za wananchi, shilingi milioni 9 kusaidia nguvu za wananchi katika ujenzi wa nyumba za walimu, shule za sekondari. Sisi Wabunge tumekwenda tumehamasisha. Tumewaeleza wananchi kwamba shilingi milioni 7 madarasa, milioni 9 ujenzi wa nyumba za walimu. Shule nyingi nimekwishasikia Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema hapa, na mimi nitazizungumzia chache katika zile shule zangu.

Shule ya sekondari kwa mfano ya Zirai, wamejenga madarasa manne yamekamilika na sasa hivi wanafunzi wanasoma, wamejenga nyumba ya walimu senti



tano ya MMES hakuna. Alikwenda Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, hivi karibuni, wananchi wakamwuliza, fedha za MMES ziko wapi Mheshimiwa Waziri. Na yeye alishangaa kwa nini shule madarasa manne hawajapata fedha za MMES, akawaahidi atawasaidia. Mimi nilijua kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri nitampa matatizo tu, hataweza kuzipata hizo fedha za MMES kwa sababu zinatoka kwa mpango maalumu. Hazitoki mfukoni kwake.

Kwa hiyo, ninachowaambia ni kwamba tsubiri awamu inayokuja. Kwa sababu nina uhakika mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri hizo fedha za MMES bado hujazipeleka. Ni vizuri Serikali na Wizara hii ikatuambia ukweli bado mnatoa fedha shilingi milioni 7 kwa ujenzi wa kila chumba cha darasa; bado mnatoa shilingi milioni 9 kwa kila nyumba ya mwalimu inayoanza kujengwa. Vinginevyo tubadilishe kauli ile na kazi hii si kazi ya Wabunge kurudi kwenda kubadilisha kauli. Serikali ibadilishe kauli.

Najua tumekumbwa na wimbi la ujenzi wa shule nyingi za sekondari kuliko tulivyokadiria. Ni dhahiri uwezo wa Serikali utakuwa mdogo kuweza kutoa fedha za kutosheleza kwa wananchi wote. Basi tuwaambie wananchi ukweli. Vinginevyo nataka niwaambie Waheshimiwa Mawaziri na nyinyi pia ni Wabunge, lakini mnatuweka mahali pabaya sasa. Sisi tumesema wananchi wangojee shilingi milioni 7, haziji! Kila siku kwenye mikutano tunaulizwa Mheshimiwa Mbunge, shilingi milioni 7 tumemaliza vyumba vitatu, ziko wapi? Sasa msituweke mahali pabaya! Toeni kauli yenye mwelekeo na msimamo na sisi tutaiunga mkono na wala hatutaogopa kuwaambia ukweli wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inakusudia kujenga shule za kitaifa katika ujenzi wa shule za kitaifa, kuhusu suala hilo, ningepomba niseme yafuatayo:- Wapeni kipaumbele au toeni kipaumbele katika ujenzi wa shule za kitaifa katika Wilaya ambazo hadi leo Serikali haina shule hata moja ya Sekondari iliyojengwa na Serikali. Wilaya ya Muheza ni mojawapo. Hatuna shule hata moja ya sekondari iliyojengwa na Serikali, na ninajua zipo Wilaya nyingine nyingi lakini zipo wilaya nyingine zina shule 10 zimejengwa na Serikali.

Sasa ukiwaambia hatuna hata shule moja ya Sekondari iliyojengwa na Serikali, lugha ya rahisi rahisi watakuambia hiyo shule ya m wananchi walimu si wanalipwa na Serikali. Shule ya wananchi walioanza kuijenga kwa nguvu zao na shule ambazo zimejengwa na Serikali kikamilifu mpaka zimekamilika ni tofauti. Sisi tunazungumzia hizo. Kwa hiyo, kipaumbele hapa kipewe zile Wilaya ambazo kwa kweli hazina shule hata moja ya sekondari iliyojengwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie vilevile katika mambo yafuatayo: Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri anaelekezea kwamba kutakuwa na mgao wa fedha, ujenzi wa maabara 84, maktaba 30, majengo ya utawala 14. Naomba Mheshimiwa Waziri kuwe na uwiano wa mgao wa fedha hizi. Tunajua tuna shule nyingi zaidi ya hizi 84. Lakini unapokuwa na mgao wa uhakika kwa mahesabu ya 84 tunaomba fedha hizi zitolewe kwa mgao wa uwiano ili pale ambapo hakujawahi kujengwa maabara hata moja tuwape kipaumbele. Lakini kama mtindo utakuwa mahali kuna maabara 2

zilizokwishajengwa na Serikali na katika 84 hizi mnapeleka huko huko hatutawaelewa. Huu siyo uwiano. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuangalie tunataka uwiano wa uhakika. Katika baadhi ya maeneo katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri umetaja kwa mfano ukurasa wa 15, *sub section* hii 16 (h) pale. Unasema ujenzi wa hosteli na ukazitaja, itajengwa Arusha, shule moja iko Arusha, Tabora, Lindi, Manyara, Singida. Lakini katika haya ya maabara, maktaba, hazikutajwa. Ninafahamu zipo katika orodha yenu ndani ya Watendaji wenu wanayo. Tuambieni na sisi tujue. Tunajua wataalamu wanayo, nikienda mimi Wizarani kule nitaambiw, lakini kwa nini hamtuambii, tuambieni tuzijue ili kama tunaona hakuna uwiano tuseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizingumzie shule ya *High School* ya Muheza. Tumejenga *High School* Muheza ina madarasa 6 yaliyokamilika, safi ya kisasa na madawati yapo. Maabara tatu, nyumba ya mwalimu ipo. *Administration block* ipo shule ile haijafunguliwa, yaani madarasa yamekaa pale. Hatuna wanafunzi *high schools* na mwenzangu amesema sasa hivi kwamba tuna idadi ndogo tu ya wanafunzi *high school* lakini pamoja na *facility* hiyo ipo, madarasa *empty* yako pale. Tunawanyima nafasi watoto 120 si haki!

Ni kweli nakubali kwamba chama kile *Muheza Development Trust Fund* wakati wanajenga shule ile walijenga kwa dhamira ya kuwa shule ya wananchi na walimshirikisha hata Mheshimiwa Rais katika kuchangia. Ni kweli kwamba walifanya makosa kuwa hawakuiarifu eti Wizaru ya Elimu kwamba wanajenga shule? Lakini pale yanapojengwa majengo mengi kiasi hicho haifiki hata kilomita moja kutoka makao makuu, kila mtu anaiona Afisa Elimu anayaona majengo yote. Haiwezekani watu wasijue kwamba wanajenga *high school* pale. Lakini wanafalsafa wanasema hamkutuambia. Sawa nakubali, chama hakikuwaambia. Sasa sijui tunafanya nini? Kinachokosekana pale ili wananchi 120 waingie shuleni ni hosteli tu, basi tumetumia zaidi ya shilingi 320 milioni za wananchi.

Tumejenga *facilities* zile, tumejenga vyumba vinne shule ya sekondari Kerenge. Tumejenga vyumba vitatu na *Administration Block* shule nyingine ya sekondari ya Kilulu. Tumejenga vyumba viwili shule ya sekondari ya *Chief Erasto Mang'anya*. Tumejenga vyumba hivyo sita viko vimekaa pale. *High School* hatuna wanafunzi, vyumba vipo hatuwezi kuwa na programu ya kusaidia watoto 120 Watanzania wakatumia *facilities* zile, madawati yapo. Tumeshindwa kujenga hosteli. Tunashindwa kujenga mahali pa kulia chakula ambapo ukiweka turubai tu na sakafu, watoto watakaa watakula chakula pale.

Sasa *facility* ile itakaa pale mpaka mwaka 2008. Nakubaliana na wazo la Mheshimiwa Waziri tulizungumza. Kaniambia tulifanya haraka, walimu hatuna. Tuna vyumba, tuna mpaka madawati, tuna *facilities* zote lakini walimu hatuna. *Facilities* zikae hivyo mwaka mzima mpaka 2008. Sioni kama tunawasaidia Watanzania. Nafikiri

tukitengeneza *crush programme* watoto 120 wataingia darasani, watasoma, tusiziache *facilities* zikaendelea kuharibika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika ya mwisho inakuja, naomba nizungumzie utaratibu. Boresheni utaratibu wa wanafunzi wanaopata misaada kutoka Serikalini. Juzi wanafunzi wamefukuzwa Chuo Kikuu. Miongoni mwa wanafunzi wale wapo wanafunzi ambao walikuwa wanalipia ada kuanzia sekondari, wakaenda *high school*, wakaenda Chuo Kikuu. Uwezo wa kulipa zile gharama za Chuo Kikuu asilimia 100 kweli hawana. Lakini wao ndiyo wanaambiwa warudi waka-*trace back records* waleta chuo kikuu. Hivi Wizara ya Fedha, tunawalipia kule hatuweki hata rekodi, hebu tujenge *data base* ili isaidie ule mfuko wa elimu waweze kufahamu kwamba tuna watoto wangapi, wapi na wapi na nani. Na kwa majina wako *Form Four* waliopasi *High School*, *Form Six* kwenda Chuo Kikuu tunawajua tuna *data base*. Tunatoa pesa hatuna *data base*, hatuwajui watoto.

Leo ukienda ku-*trace record* zao kuanzia Serikali za Vijiji hazitapatikana. Kwa hiyo, anafukuzwa tu Chuo Kikuu. Naomba tutengeneze *data base* tuwe na mpango wa uhakika wa kisayansi. Tunazungumza sayansi na teknolojia, kompyuta zimejaa, tunashindwa kuwa na programu ndogo tu ya kuweza kuonyesha watoto wanaosaidiwa na Serikali wako wapi, na kama wamepasi *Form Four*, *Form Five*, tunawa-*trace* tunashindwa. Tengenezeni *data base* kwa sababu ninajua mnao uwezo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni ruzuku katika shule ambazo siyo za Serikali. Tunaposema haya tuyatekeleze. Tumesema tutawapa ruzuku ya kununua vifaa vya kufundishia. Basi tuwape, vigezo tuviweke bayana ili wanaoendesha shule hizi Taasisi za dini, na watu binafsi wajue vigezo halafu waombe fedha hizo. Lakini vigezo hawavijui, wataomba kweli fedha hizo? Basi tuweke bayana vigezo hivyo viweze kusaidia, zipo shule zinafanya vizuri sana. Mwaka 2003 shule ya *Muslimu Muheza* ilikuwa ndiyo shule pekee iliyotoa watoto waliopata *division one*. Tunahitaji kusaidia shule kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru sana na niseme dhahiri kwamba naiunga mkono hoja hii. Nawatakia kila la kheri. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe na Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti wetu kwa kuliongoza Bunge katika hali ya uhuru pamoja na kuzingatia Kanuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili napenda kuipongeza Serikali yetu kwa usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, imeweza kutekeleza sera zake za Chama Cha Mapinduzi na tukizingatia kwamba elimu si ya kujitegemea peke yake bali pia inategemea maendeleo ya sekta zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli maendeleo ya matengenezo ya barabara, miundombinu ya barabara, maendeleo ya nishati, upatikanaji wa umeme. Upatikanaji wa maji, ni chachu kubwa katika kuhakikisha kwamba elimu yetu inaboreka na haya yote yanaweza pia kumsaidia mwanafunzi kupata elimu ambayo ni bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze tena Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Naibu Mawaziri, Watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba zao nzuri na maandalizi mazuri ambayo yamewasilishwa hapa Bungeni, na yameweza pia kutupa sisi kianzio katika kuijadili hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru tena Serikali kwa jitihada kubwa sana ambayo imefanya katika kuhakikisha kwamba kunakuwepo na ongezeko la shule za Serikali katika kila Kata na labda niseme tu kwa upande wetu Mkoa wa Mtwara una shule mpya 40 za kutwa na hivyo tunaishukuru sana Serikali. Kwa namna ya pekee sana tunaishukuru Serikali kwa kuhakikisha kwamba imetoa upendeleo wa pekee katika Mikoa ya pembezoni kwa kutoa zuruku kubwa kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa. Hii kwa kweli lazima tukubaliane kwamba bila msukumo wa Serikali maendeleo ya ujenzi wa shule yangekuwa hayapo hapa tulipo katika nchi nzima. Na lazima niseme tu kwamba inanikumbusha ile *Newton's first law of motion* inayosema kwamba *an object will remain at rest or in its state of uniform motion unless an external force acts on it otherwise.* (Makofi)

Kwa hiyo.....!

**NAIBU SPIKA:** Jamani tutafsiri kwa sababu wananchi watahindwa kukuelewa.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kitu chochote hakiwezi kwenda kitabaki katika hali yake hiyo hiyo labda itumike nguvu ya ziada kutoka nje. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwa nguvu za ziada, kwa msukumo mkubwa ambao imeweza kuutoa katika ujenzi wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kipaumbele hiki cha elimu, elimu imepewa bajeti kubwa, asilimia 18, lakini tutakubaliana kwamba ndani ya kipaumbele hiki kuna vipaumbele vingine. Kwa mtazamo wangu basi nafikiri ni vizuri sana Wizara ikaangalia yale matatizo ambayo yapo katika maeneo maalumu. Labda niseme kwamba yale matatizo ambayo ni *location specific* na kwa kuanzia labda niseme matatizo ya walimu. Haya matatizo ya walimu kwa ufafanuzi tu niseme kwamba maeneo ya mijini mara nyingi yanakuwa yanajitosheleza kwa walimu, maeneo ya vijijini hayajitoshelezi lakini kuna maeneo mengine ambayo ni mikoa ya pembezoni. Haya yamekithiri. Pamoja na hayo napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, mwaka jana Mkoa wa Mtwara alitupatia walimu 155. Ukizingatia kwamba Mkoa wa Mtwara kwa sasa una shule za kutwa 106, kwa bahati mbaya walimu waliofika ni 79 tu. Walimu 76 hawakufika na kwa namna hiyo basi tuna upungufu mkubwa wa asilimia kama 56 hivi ya mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuiomba Wizara iliangalie hili na labda kwa kuelezea ukubwa wa tatizo, kuna shule ambazo ziko karibu na mpaka wa Msumbiji, kwa mfano, kuna shule ya Sekondari ya Mkundi ina wanafunzi 160 lakini kuna mwalimu mmoja tu. Huyu ndiye mwalimu mkuu, ndiye mwalimu wa zamu, na ndiye anayefanya kila kitu. Anafundisha masomo yote. Sasa sijui elimu hii wanafunzi kama kweli wataipata inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haishii kwenye shule za sekondari tu, lakini pia hata shule za msingi. Mfano mwingine ni shule ya msingi ambayo ipo Kata ya Michenjele, ina wanafunzi zaidi ya 740 lakini ina walimu watano tu. Ukihusisha tatizo la ukosekanaji wa walimu hapa kuna tatizo kubwa sana la maji katika maeneo haya. Kwa hiyo, kama nilivyokuwa nimekwishasema mwanzoni kwamba elimu haijitegemei yenyewe tu inategemea pia maendeleo ya sekta zingine. Hivyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na kujaribu kulihusisha na sekta zingine kama itawezekana kushirikiana na kutatua matatizo haya ili kusudi tuweze kupata walimu wa kutosha katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya upungufu wa walimu yanakwenda mpaka Chuo cha *VETA*. Nadhani hata Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakubaliana na mimi kwamba Chuo cha *VETA* Mkoani Mtwara kinafanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na kutokuwa na walimu wa kutosha wa fani zingine.

Kutokana na haya nitoe mapendekezo kwa upande huu, kwanza, kwa kuzingatia kwamba upungufu mkubwa uko katika walimu wa sayansi, katika Mkoa wetu kuna chuo kile kinachotoa diploma ya *arts*, napendekeza ikiwezekana kitoe pia diploma ya sayansi kwa sababu walimu wanaomaliza hapa, wanaohitimu ni rahisi kwao kubaki Mtwara kuliko kuleta walimu wapya. Hawa wanaweza wakatusaidia sana kufundisha masomo ya sayansi. Pendekezo jingine katika kutatua hili, ni kuboresha mazingira. Kama Serikali ilivyokuwa imeamua kutoa upendeleo kwa ruzuku ya madarasa basi tunaomba tena upendeleo kwa ujenzi wa nyumba za walimu na maeneo mengine ili kusudi walimu hawa waweze kupata kivutio na kuja kufundisha katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala jingine la *Mtwara Girls* ambalo kwa kweli sasa hivi naona kama lisipochukuliwa hatua za haraka shule hii inaweza kushuka kiwango mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo hapa la ongezeko kubwa la wanafunzi ambalo limepelekea wanafunzi kulala wawili wawili kutokana na ufinyu wa hosteli. Vilevile samani hazitoshi na wanafunzi wakati mwingine hukaa juu ya meza. Hiki ni kikwazo kikubwa sana kwa mwanafunzi kujifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sambamba na ongezeko la wanafunzi kwa sababu ukiangalia mwaka 2006/2007 zimeongezeka *combination* za *HGK* na *CBG* bila ongezeko lolote la hosteli wala samani. Kwa hiyo, tunaomba hosteli ijengwe pale na hata *reserve* za maji. Visima vya maji havitoshelezi mahitaji ya wanafunzi. Tunaomba pia na samani zinunuliwe yaani vitanda pamoja na viti vya kuwatosheleza wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee tena suala la mishahara ya walimu. Mishahara ya walimu wapya wale wanaokwenda kuripoti, mishahara yao inacheleweshwa sana. Kwa kiasi fulani kumekuwepo na maboresho kidogo lakini bado inachelewa na hata wale walimu wa zamani bado madai yao ni mengi na hii imepelekea walimu kukopa kwa wanyabiashara mahitaji yao. Jambo ambalo pia limepelekea kukosana kutokana na kutokuamiana na vilevile hata kudharauliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie tena suala hili la wanafunzi kurudishwa nyumbani kutokana na kukosa karo. Hili suala nadhani tunamwadhibu mwanafunzi pasipo na sababu, ni vizuri Wizara ya Elimu ikaliangalia kwa sababu si mwanafunzi anayetafuta pesa hizi za karo bali ni mzazi. Wizara iangalie utaratibu mwingine wa kumwezesha mzazi kulipa karo au kutoa michango mingine badala ya kumrudisha mwanafunzi nyumbani akipoteza masomo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wanafunzi kupanga vyumba wanapokuwa wakitoka mbali na maeneo ya shule. Kwa upande wangu suala hili naliona ni la hatari na ni ukweli usiojificha kwamba tunampa mtoto majukumu ambayo ni zaidi ya umri wake.

Mtoto wa miaka 13, au 14 anapopanga chumba lazima tu itamkwaza katika masomo, hataweza kufuatilia masomo vizuri. Yeye huyo huyo ndiyo mtafutaji wa chakula, mtafutaji wa maji, mfanyaji wa shughuli zote za nyumbani, na vilevile ahudhuri shule. Ni vizuri Serikali ikaliangalia upya ili kusudi kuweza kuwanusuru hawa watoto kutokana na majaribu mbalimbali ambayo yanaweza pia yakasababisha ukosefu wa nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimalizie tu kwa kuomba Wizara ifuatilie wale wanafunzi wenye vipaji maalumu, itunze kumbukumbu zao. Kwa sababu wakati mwingine wanaibuka watoto wenye vipaji lakini inafika mahali fulani katikati hapo vipaji vile haijulikani vimeishia wapi. Kwa kweli vikifuatiliwa kumbukumbu zikatunzwa inaweza ikasaidia baadaye hata kuwapata watu ambao ni bora wanaoweza wakatusaidia katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa kutupatia Waratibu wa Elimu katika Mkoa wetu wa Mtwara.

Wanafanya kazi vizuri kwa kushirikiana na Halmashauri zetu katika Wilaya zote isipokuwa Wilaya ya Nanyumbu ambayo haina waratibu na hivyo wamekuwa ni kiungo kizuri sana kati ya Wilaya na Serikali Kuu.

Kabla sijagongewa kengele niseme tu naiunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 na namtaka kila la heri Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante nashukuru. Sasa nitamwita Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Benadeta Mshashu na Mheshimiwa Losurutia. Lakini kwanza kabisa Mheshimiwa Susan

tunashukuru Mungu umepona kutokana na ajali ambayo jana walipata wakitoka Dar es Salaam kuja huku.

**MHE. SUSAN A J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa pole na namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutuepusha na ile ajali kwa kweli ilikuwa mbaya lakini nashukuru kwamba tumenusurika bila kupata majeraha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru kwa kunipa hii nafasi lakini naomba sana nimpongeze Waziri na Manaibu wake pamoja na Watendaji wake wakuu. Kwa kweli hotuba hii ni nzuri. Lakini kimsingi toka mwanzo tunasema wanawake wanapopata nafasi wanafanya vizuri sana na hata tukiangalia vitabu vyenyewe vinajieleza, sijaona Waziri yeyote ambaye ame-*present* vitabu viwili lakini pia vina *table of contents* ametupa takwimu. Kwa hiyo, mtu yeyote anayesoma ataelewa kwa mara moja. (*Makofi*)

Lakini Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwenzetu alipofariki sijasimama kuongea, hivyo, nilikuwa naomba kutoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Chifupa. Nawatakia wazazi wake kila la heri, Mungu awape nguvu ili waweze kuendelea na maisha yao ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, hii hotuba ni nzuri lakini kuna sehemu ambazo naomba niongee ili ziweze kuboreshwa. Labda nianze na maneno ya Mheshimiwa Rais au Baba wa Taifa wa Nchi hii. Alisema kwamba tuna maadui wakubwa watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Lakini alienda mbele na kusema kwamba katika maadui hawa watatu ujinga ndiyo baba yao. Kwa maana ya kwamba ukishaondoa ujinga basi hayo mengine yote yanaondoka yenyewe (*automatically*) na njia pekee ya kuondoa ujinga ni kwa kumwelimisha mtoto. Lakini kama ambavyo wenzangu wamekwisha yaongea, kwa kweli Tanzania sasa hivi tumekuwa na matatizo makubwa katika elimu.

Nalizungumzia hili nikiwa namaanisha kwamba sasa hivi Tanzania tumekuwa na matabaka ya elimu. Jambo ambalo mwanzilishi wa taifa hili Baba wa Taifa alilikataa na tunakumbuka kwamba baada ya Uhuru, Mwalimu Nyerere aliweza kutaifisha shule zililizokuwa za binafsi.

Pamoja na kwamba alikuwa Mkatoliki lakini aliweza kubinafsisha shule ambazo zilikuwa zinaendeshwa na Kanisa Katoliki. Licha ya kwamba hali hii iliwashangaza wengi lakini nia yake ilikuwa ni kuhakikisha kwamba hakuna matabaka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kumeibuka makundi matatu ya matabaka katika nchi hii. Kimsingi ukiangalia katika makundi haya kuna yale ambayo ni ya vigogo, ambao ni watoto wa viongozi hasa wa kisiasa. Hawa utakuta watoto wao hawasomi Tanzania, kama wanasoma Tanzania basi wanasoma kwenye shule ambazo tunaziita *International Schools* ambazo zina walimu wazuri sana, maabara nzuri sana, lakini pia zina vifaa vya kusomea.

Pamoja na hayo kuna mabasi maalumu kwa ajili ya kuwapeleka na kuwarudisha shuleni. Lakini kundi lingine ambalo linafanana nalo sana ni la wafanya biashara wakubwa ambao nao hupeleka watoto wao kuanzia chekechea nje ya nchi na kama ni hapa nchini basi kwenye shule hizo ambazo nimezisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi la tatu ni la walalahoi ambapo kwa kweli watoto hao wanasoma katika mazingira magumu sana, hawana vifaa, hata walimu waliopo pamoja na kwamba wana sifa ya ualimu lakini ni wachache, na shule hizi ziko ndani kabisa vijijini lakini pia hawana usafiri, na maabara. Hapo hapo tunazungumzia suala zima la sayansi na teknolojia!

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunajenga hizi shule kwa kweli ni wazo zuri watoto wote waweze kwenda shuleni. Lakini shule ya sekondari kama haina maabara kwa kweli inakuwa mtoto hajasoma. Najua wenzangu watakuwa wamechangia lakini kwa kweli kama hakuna maabara hawa watoto watatoka, mtakuja kuwaita maprofesa, profesa maji mafupi, profesa nani, lakini hawatakuwa na uwezo wa wowote wa kuweza kuingia katika karne hii ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ujenzi wa shule hizi tumeona kwa kiasi kikubwa sio tu Dar es Salaam, lakini hata mikoani, unakuta shule ilikuwa moja wanajenga ya pili A na B katika viwanja vilivyokuwa vya michezo. Kwa hiyo, ile dhana ya kwamba michezo pia inaboresha afya ya mtoto na pia ni ajira kwa baadaye inakuwa haipo. Naiomba Serikali iangalie ni jinsi inaweza kuongeza shule lakini pia iangalie pia umuhimu wa michezo ili watoto nao waweze kucheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilikuwa nataka kukizungumzia ni kuhusu suala zima la mishahara ya walimu. Ni kweli kuwa walimu siku za nyuma walikuwa wanaonekana kama walivyo wafanyakazi wa *TRA* kwa hivi sasa. Wakati huo ilikuwa ukisikia fulani ni mtoto wa mwalimu au mtu fulani ni mwalimu kwa kweli unamheshimu, na hii ilikuwa kwa sababu walikuwa wanaishi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba sasa hivi walimu wa Tanzania hasa wa shule za msingi na sekondari maisha yao ni magumu sana. Hawapati mishahara kwa wakati, lakini mishahara hiyo pia ni midogo, ukizingatia kazi ngumu sana wanazofanya hasa kusomesha lakini pia kusahihisha madaftari na kuhakikisha watoto wanakuwa katika maadili ya kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Dar es Salaam nimepata taarifa kwamba walimu wanatakiwa wakatwe mishahara yao kwa ajili ya ujenzi wa shule. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri atuambie kama hili ni kweli, kwa sababu kwa kweli nimepata malalamiko kutoka kwa walimu kwamba kulitoka tangazo walimu watakatwa mishahara kwa ujenzi wa shule. Sasa najiuliza, hivi shule ni za walimu, ni watoto wa walimu pekee watasoma? Na kwa nini tumkate mwalimu ambaye mishahara wake bado ni mdogo tuwaache wafanyakazi wakubwa, wafanyabiashara na katika mashirika makubwa



makubwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kufafanua hili kama hili ni kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala zima la shule. Sasa hivi kumeibuka shule za aina mbalimbali. Utakubaliana nami kwamba sasa hivi kuna shule zimeibuka za madhehebu mbalimbali, lakini pia zimeibuka za kutoka nchi mbalimbali, mfano utakuta *Yemen Secondary School*, au *Feza* na unakuta hizi ni za watu wa nje. Naomba kujua hivi ni vigezo gani Wizara inatumia kusajili shule, na je, kama hivyo vigezo vipo, baadaye wanaenda kuangalia kama masharti yanafuatwa? Kwa sababu napata wasiwasi kwamba tunaweza kuendelea tukaja kuambiwa kwamba kuna shule hii ni maalumu kwa ajili ya wachaga, hii kwa wakurya kitendo ambacho kwa kweli kitalitumbukiza taifa letu katika hali ngumu sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba wakati wanaangalia vigezo wawe pia wanapitia kuona kwamba kweli hayo masharti waliyoingia mkataba yanatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nililosimamia hapa zaidi ni kuhusu utoro shuleni. Awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunitua kwenda kwenye mkutano uliokuwa unahusu masuala ya ujauzito shuleni. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba watoto wetu wa kike wanapata mimba shuleni na hili limekuwepo sio leo wala jana, imeanza siku nyingi lakini Serikali bado haijalitolea tamko. Labda nieleze tu kwamba ni kweli Tanzania imeridhia mkataba wa *Beijing* wa *SADC* ambao una lengo la kumsaidia mtoto wa kike akipata mimba arudi shuleni, lakini bado katika nchi yetu haujatekelezwa. Nakumbuka kuwa kipindi cha nyuma Serikali ilisema mtoto akipata mimba hapaswi kurudi shule, hana maadili na pia anaweza akasababisha wenzake wapate mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuelewe kwamba huyu mtoto anapata mimba katika mazingira gani. Takwimu zinaonyesha kwamba wengi wanaopata mimba sio wale waliobakwa, waliobakwa ni wachache sana. Lakini tunajiuliza wanapewa mimba na watu gani? Ukiangalia asilimia kubwa sana hawapati mimba kutoka kwa wanafunzi wenzao, wanapata mimba kutoka kwa watu wazima wafanyakazi, wafanyabiashara, wanasiasa, na labda nikazie, kwa sababu juzi tu tumepata taarifa kwamba kuna Diwani mmoja amecharazwa viboko baada ya kukutwa na mtoto shule kwenye *guest*, kwa hiyo, tunaona kabisa...!

**MBUNGE FULANI:** Wa Chama gani?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Sitaki kusema chama, wananiambia ni chama gani lakini kimsingi ni diwani, kwa hiyo, tunaona ni jinsi gani watu wazima wenye staha au ni viongozi wanavyoweza kuwarubuni watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuelewe kwamba mtu anakuwa na uwezo wa kuamua jambo (*rational decision*) anapokuwa mtu mzima kuanzia miaka 18, lakini watoto wa shule za msingi ni watoto wa umri ya chini ya miaka 15, kwa hiyo, kimsingi yule ni mtoto na hivyo, hana kosa kwa maana kwamba hajawa na ile *rational decision*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea ni kwamba takwimu zinaonyesha kwamba kuanzia mwaka 2003 mpaka 2006 wasichana au watoto wa kike 10847 wamepata ujauzito na wamefukuzwa shule. Hawa ni wa shule za msingi, lakini hapo hapo wa sekondari kuanzia mwaka 2003/2006 wanafunzi 3209. Sasa pamoja na kwamba sababu ni nyingi ikiwemo ya umaskini, umbali kutoka shule, mila na desturi, ndoa za lazima na pia ubakaji, bado sisi tunaamini kwamba Serikali ya Awamu ya Nne hata na awamu zilizopita lengo lake kubwa ni kuondoa umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kabisa katika hawa watoto waliopata mimba, zaidi ya asilimia 95 wanatoka katika familia maskini. Kwa maana hiyo basi kama kweli tuna nia ya kupunguza umaskini ni lazima tumsaidie yule mtoto arudi shule ili kuondoa ile *vicious circle* ya umaskini. Kwa sababu kama huyu mtoto amepata mimba halafu unamfukuza shule, ina maana hata yule mtoto aliyezaliwa bado ataingia kwenye lindi la umaskini, na ukiangalia familia za kitajiri, mtoto wao akipata mimba sana sana ama yule mama anaweza akahakikisha yule mtoto wake anaendelea akajifungua lakini akampeleka Ulaya au hapa hapa kwenye shule nyingine akaweza kumsomesha. Kwa sababu watampa maziwa ya kopo, lakini huyu maskini ni lazima yule mama yake amnyonyeshe kwa sababu hakuna jinsi bibi yake akaweza akanunua maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuondoa suala zima la umaskini, mimi nafikiria Serikali ifikie mahali sasa itoe tamko ni jinsi gani inaweza kuwarudisha watoto shule. Kwa sababu kuna nchi nyingi tu majirani zetu kama Zambia ambayo toka mwaka 2001 wameweza kurudisha watoto shule, sheria kabisa imetungwa. Vilevile Malawi, Kenya wanawarudisha watoto shuleni, kwanini sisi tusifanye hivyo na tunamwadhibu binti yule wakati ukiangalia kimsingi hana kosa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itoe tamko. Najua *NGO* haziwezi kutoa tamko, Serikali ndio inapaswa kutoa tamko ili hao watoto waweze kurudi shuleni. Lakini kuna suala zima pia la sheria. Ukiangalia Katiba yetu haelezi chochote kuhusu haki ya elimu, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kuna haja pia ya Wizara ya Katiba na Sheria kuangalia na kurekebisha sheria ili elimu iwe ni haki ya Mtanzania, na hii itasaidia watoto wote waweze kusoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiria kwamba kisheria kwa kweli tufute sheria zote ambazo zinamfukuza mtoto wa kike shuleni aliyepata ujauzito lakini pia turekebishe zile sheria kandamizi. Lakini cha muhimu sana ni kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Wanawake, Jinsia na Watoto, kuliangalia suala zima la kuwa na mtaala wa elimu ya afya ya uzazi (*reproductive health*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tunasema kuwa kwa shule za msingi kuweka elimu ya afya ya uzazi tunawakwaza watoto, lakini nataka nikuhakikishie kwamba watoto wa sasa hivi wanajua mambo makubwa kuliko sisi tunavyoyajua. Kwa hiyo, naomba kabisa hii elimu ipelekwe kwa sababu tuna mifano mingi kama ya mtoto wa miaka minne anaweza akakuambia jambo ambalo wewe mwenyewe unajiuliza mara tatu mtoto huyu kalijuaje. Hivyo tusijenge dhana kwamba watoto hawa wakifundishwa

kwamba wataenda kutenda, basi ni afadhali atende wakati anajua madhara kuliko kutokumwelimisha halafu akafanya ikaonekana sisi ndio tumemkosesha. Mimi nafikiri kwamba kuna haja kwa Wizara kuwa na mtaala wa elimu ya afya kwa uzazi ili watoto wetu waweze kuelewa kwa uwazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu watoto kurejeshwa nyumbani. Naomba kusema kwamba watoto wa kike au wanawake kwa ujumla kibiolojia ndio wanaobeba mimba hilo halina ubishi. Lakini pia tuangalie mazingira wanamotoka, kwa mfano, kuna shule tumeambiwa mtoto anakwenda shuleni, inabidi alale kesho yake ndiyo arudi nyumbani, na kule anakolala analala na walimu na watoto wa kike na wa kiume. Kwa hiyo, kuna mazingira yote yale ya kijamii ambayo tunayaona. Lakini pia mimi nakumbuka zamani ilikuwa kwa kweli mtoto wa mwenzio ni wako na namshukuru mke wa Rais Mama Salma Kikwete kwa hiyo *organization* yake ambayo ameanzisha huo mkakati, mwone mtoto wa mwenzio kama wako. Nadhani tukiweza kuendeleza ile ni nzuri kwa sababu sasa hivi kila mtu anamjali mtoto wake, lakini baba yule yule ambaye ni mkali sana kwa binti yake ni huyo huyo anaenda nje kuchukua mabinti wa wenzake! Kwa hiyo, naomba pamoja na kwamba sheria zipo, lakini kwa kweli nadhani elimu ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia mila na desturi. Kuna mila na desturi ambazo kwa kweli zinawafanya watoto wa kike wakapate ujauzito mapema. Kwa mfano, katika jamii mbalimbali, mtoto wa kike ataambiwa labda lazima uwe na mafiga matatu, kuna suala la kwenda kuteka maji lazima uwe na chungu cha kuchotea, maana yake ni kwamba lazima uwe na bwana mmoja halafu kuna mwingine wa nje. Kuna mila kwa kweli zinachochea sana mtoto wa kike. Au utakuta baba anamwambia mtoto wa miaka 13 nenda ukatafute chakula, sasa mtoto wa miaka 13 anaenda kutafuta wapi na huyu ni binti? Kwa hiyo nafikiria kwamba Wizara ya Katiba na Sheria ina haja ya kuangalia haya mambo nakuona ni jinsi gani tunaweza kuyarekebisha. Lingine la mwisho ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la kisheria kuhusu watoto hawa. Mimi nafikiri kwa kweli hata ile sheria ya kutoa shilingi mia moja kwa mtoto ni ndogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa asante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya elimu. Nasimama hapa kwa niaba ya kata zangu katika Jimbo langu: Kata ya Marika, Mnavira, Mbuyuni, Mkululu, Lulindi, Nanjota, Lipumbulu, Mkundi, Chiwata na Malenga, Sindano, Mchauru, Chiungutwa na Mpindimbi. Hawa ndio walionipigia kura mimi na kuweza kuwa Mbunge na kuingia katika ukumbi huu ili niweze kutoa maoni yao, ushauri wao ili na wao waweze kupata nafasi ya kupiga hatua katika maendeleo.

Kwa kuwa tunazungumzia hotuba ya elimu, kwanza kabisa ningependa kuipongeza Wizara. naipongeza Wizara ya Elimu kwa hotuba yao nzuri yenye kuleta matumaini katika suala zima la mapinduzi ya elimu katika nchi yetu. Haya mapinduzi yanaendelea, natamka yanaendelea kwa sababu tumeanza na MEM, tumekuja MES

leo hii tumeona jinsi Serikali ilivyoamua kuongeza pesa nyingi katika Wizara hii ya Elimu. Lakini pia ningependa kuwapongeza viongozi wenzangu wa wilaya yangu ya Masasi ambao wamefanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba wanatimiza malengo ya kuwapeleka watoto katika shule za sekondari. Nampongeza Mheshimiwa DC, nampongeza Mkurugenzi mtendaji, wengine wote walioshiriki kikamilifu kutaka kuhakikisha kwamba shule zinajengwa katika wilaya yetu na hasa katika jimbo langu la Lulindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu mengi yatakuwa maombi tu ama kuongeza hapa na pale. La kwanza, wakati nikichangia katika hotuba ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nilizungumza kwamba mikoa ya Kusini ambayo iko pembezoni mwa nchi yetu inategemea sana zao la korosho. Ili mikoa hiyo iweze kujiletea maendeleo pamoja na kutoa ada katika shule za sekondari wanaomba; na mimi kwa niaba yao naomba tena, kwamba kwa kuwa kwetu kule korosho zinaanza kuvunwa mwezi Oktoba, Novemba, Desemba, mpaka Januari, ili waweze kutoa ada wanaiomba Serikali itazame uwezekano wa kutoa matokeo hasa mkupuo wa pili kati ya mwezi Desemba na Januari, kipindi ambacho wao wanapesa za kulipia ada za sekondari. Wanasema hivyo kwa sababu sasa hivi wana mwamko wa kupenda kuelimika. Naomba sana sana Serikali kupitia Wizara yake ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi suala hili walifikirie hasa ikizingatiwa kwamba Mheshimiwa Rais amekwishazungumza kwamba mikoa hii ya pembezoni ipewe kipaumbele. Kwa hiyo, kwa mikoa ya Kusini hasa Mkoa wa Mtwara hili ni tatizo ambalo Wizara ya Elimu lazima mlitazame kwa macho ya huruma, hilo ya kwanza.

La pili, pale Chihungutwa, pana shule ya sekondari. Katika msimu uliopita ama katika kipindi kilichopita niliambiwa kwamba kitaanzishwa kidato cha tano na sita. Lakini kwa sababu ya kutaka kukidhi haja ya kupeleka watoto wa shule za sekondari, uamuzi huu ulisimama kwa muda. Naomba Wizara ya Elimu ione kwamba sasa wakati umefika kwa shule ya sekondari ya Chiungutwa kuanzisha kidato cha tano na cha sita, maana shule hizi za sekondari zilizojengwa ni nyingi. Sisi hatuna kule kidato cha tano na cha sita, kuna shule moja tu ambayo inachechemea, tunawaombeni sana kwa hili kusiwe na mambo mengine tena ya kuchelewesha kuanzishwa kwa shule ya Chiungutwa kidato cha tano na cha sita ili watoto watakaomaliza katika sekondari hizi zilizojengwa waweze kuingia kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia napenda nichukue nafasi hii niwapongeze wananchi wa Jimbo la Lulindi, wamefanya kazi kubwa kweli kweli ya kuchangia ujenzi wa shule za sekondari ambazo sasa hivi wanafunzi wanasoma. Nilikwenda kule na viongozi wenzangu tukawahamisha, wamehamisika na wanasema wako tayari kuchangia jambo lolote lile la elimu, liwe ni ujenzi wa shule, nyumba za walimu, maabara wako tayari. Kwa hiyo, kwa kuwa wao wameshahamasika basi naomba hamasa hii iende moja kwa moja kwa kujenga kidato cha tano na cha sita katika shule ya sekondari ya Chiungutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niungane na wenzangu wote ambao wameelezea matatizo ya walimu katika shule zetu za sekondari na hata shule za msingi. Kule kwetu kama nilivyosema kuna shule nyingi tu za sekondari, lakini utakuta mwalimu ni mmoja shule yote ya watoto karibu 80 tena wanaoanza ufanisi wa elimu utakuwa wa

chini sana. Naomba sana sana Serikali katika upendeleo huu na hasa kwa kuzingatia historia ya mikoa hii ya Kusini basi katika mgao huo wa walimu tupelekeeni walimu wa kutosha katika shule za sekondari ili elimu hii ya sekondari ipatikane kwa ukamilifu. Kama nilivyosema wananchi wako tayari kujitolea wakishirikiana na Serikali yao kujenga nyumba za walimu. Lakini hapo hapo naomba nitilie mkazo katika ujenzi wa maabara. kila anayesimama anazungumza matatizo yaliyopo yanayowapata wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi, lakini sayansi bila maabara hiyo sio sayansi, kwa sababu kule ndiko wanakofanya mafunzo kwa vitendo ( *practicals*), wanathibitisha waliyosoma yale darasani.

Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Elimu, suala la maabara litiwe mkazo kweli kweli ama sivyo tutakuwa tunaimba nyimbo tu kwamba wanafunzi hawapendi kuchukua masomo ya sayansi. Naomba tuwape chachu kwa kujenga maabara katika shule za sekondari. Tatizo la mimba ni kubwa kweli kweli, naomba nitolee mfano wa mimi mwenyewe. Kijijini kwangu pale Mholela, mjukuu wangu wa darasa la tano amejazwa mimba, ukimkuta yule mtoto amembeba mtoto wake, unaweza ukafikiria mama yake yuko shamba yeye anamlea tu. Unaweza kumwuliza kwamba “wewe mama yako yupo wapi” mwenye mtoto huyu, kwa sababu ni mdogo sana, darasa la tano. Atakwambia, “hapana, huyu ni mtoto wangu!” Kwa kweli suala la mimba ni tatizo kubwa sana katika elimu kwa watoto wa kike. Naomba Wizara ya Elimu kama hizi sheria hazitoshi, tungeni sheria nyingine, tena zileteni hapa Bungeni tuzipitishwe ili hawa wanaojaza mimba watoto wapewe adhabu kali kwa kweli inatia huruma sana! Tunasema watoto wa kike lazima wasome huku wanajazwa mimba, watasoma saa ngapi? Na mimi hapa naomba nisisitize suala la kuwarudisha shule waliojazwa mimba, warudishwe shuleni lakini adhabu iwe kali ili watoto wa kike nao wasome, wakisoma watoto wa kike ndio kusoma kwa familia nzima, naomba sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilipochangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nilizungumzia suala la historia. Naomba Wizara ya Elimu, somo la historia litiliwe mkazo, lisiwe na hiyari i li vijana wajue historia yao. Wanaposhindwa kujua historia hawajui nchi yao, wasipojua nchi yao wanakuwa hawana nguvu, naomba sana hili lizingatiwe. Wenzetu nchi nyingine somo la historia linakwenda mpaka chuo kikuu pamoja na taaluma yako unayochukua lakini historia inabaki pale pale, matokeo yake kunakuwa na uzalendo wa hali ya juu kweli kweli. (*Makofi*)

Tulikuwa hapa na JKT ikafa kwa sababu mbalimbali. Katika JKT tulikuwa tunajenga uzalendo, anayetoka Mtwara, anayetoka Arusha, Kigoma, wanakutana katika kambi moja, wanajenga uzalendo. Sasa hapo naomba turudishe uzalendo kwa kutumia somo la historia linajenga uzalendo wa kiwango cha hali ya juu. Haya yote tunayozungumza yanaweza yakafanyika vizuri vijana wetu watakuwa wazalendo, naomba sana hili lipewe umuhimu na ikiwezekana na sisi tuige kwa wenzetu, somo la historia lipelekwe mpaka Chuo Kikuu ili kijana akitoka pale awe ameiva kweli kweli, anayejua kweli kweli nchi yake. Nimesema hapa kwamba mengi nitazungumza, ni maombi tu. Nakumbuka nilipeleka ombi langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mwananzila. Pale Lupaso pana kituo cha vijana kinafanana na *VETA*, lakini pana matatizo makubwa kabisa ya walimu na mambo

mengine, naomba atakaposimama kujibu hoja hizi basi anieleze lile ombi langu limefikia wapi maana kila nikienda jimboni wananchi wananiulizia, na maana ni ile ile na wao wanataka kupiga hatua katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa nipigiwe kengele narudia tena ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa sababu inaleta matumaini makubwa ya kupiga hatua katika elimu katika nchi yetu hii ya Tanzania, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba hii. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba iliyoandaliwa vizuri sana.

Pili nawapongeza Naibu Mawaziri wote wawili, Afisa Elimu Kiongozi, Wakurugenzi wote, Makatibu Wakuu na watendaji wote ambao wamehusika kwa njia moja au nyingine katika kuandaa hotuba hii kwa sababu imeandaliwa kitaalamu. Napenda kumpongeza na kumshukuru Rais wetu ambaye alitamka bayana kwamba kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Nne ni elimu, na naishukuru Serikali kwa kuliona hilo na kuipangia elimu bajeti kubwa. Kwa hiyo, kuonyesha kwamba kweli kipaumbele cha Serikali hii ni elimu, sasa naishauri Serikali kwamba tangu sasa angalau kwa miaka minne, mitano kipaumbele cha kwanza kiwe elimu, kusudi sehemu mbalimbali au mambo mbalimbali katika sekta ya elimu yaweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningeanza ku-*declare interest* kusudi ninapoanza kukupongeza watu wajue kwamba ni mwalimu *by profession* na nimekuwa mkuu wa shule kwa miaka kadhaa inayotosha. Naipongeza sana Wizara ya Elimu kwa mipango mizuri na kwa mafanikio makubwa sana yaliyopatikana katika kipindi kifupi. Wote tumeshuhudia madarasa yameongezeka na shule zimeongezeka, idadi ya wanafunzi katika shule za misingi imeongezeka, idadi ya wasichana katika shule hizo imeongezeka, uwiano kati ya wasichana na wavulana katika shule unakabiliana na kwa ujumla idadi ya walimu katika Tanzania imeongezeka.

Matatizo tunayoyaona sasa hivi ambayo yako katika sekta ya elimu ni matatizo ambayo yanatokana na mafanikio makubwa ambayo tumeyapata katika muda mfupi. Nipende basi kumshukuru Waziri Mkuu kwa msukumo wa pekee ambao ameuweka katika mradi huu na kuhakikisha kwamba unafanikiwa mara kwa mara. Tulikuwa tunaona anawaita wakuu wa mkoa na kwa kufanya hivyo kumewezesha huu mpango kufanikiwa. Nawashukuru sana Naibu Mawaziri ambao wamezunguka Tanzania nzima, wakahakikisha kwamba wanaweka msukumo wa pekee na kuchochea kasi ya ujenzi wa shule hizo mpaka tukafanikiwa. (*Makofi*)

Napenda basi kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Mkoa wa Kagera, *Col. Enos Mfuru* pamoja na Wakuu wa Wilaya wote wa Mkoa wa Kagera, maafisa elimu wote, wakurugenzi na watendaji wote, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Waheshimiwa Madiwani ambao walihamasisha wananchi, na wakakubali wakachangia ujenzi wa shule mpaka Mkoa wa Kagera ukaweza kupeleka wanafunzi walioshinda kutoka darasa la saba kwenda kidato cha kwanza kutoka kwenye asilimia 48.11 kwenda kwenye asilimia 93.86, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo matatizo bado yapo. Nikianza na MMES, ruzuku inayopelekwa au iliyokuwa inapelekwa mpaka sasa hivi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ni sh.7,000,000.00=, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu ni sh.9,000,000.00 lakini ukienda kwenye mkoa kama ya Kagera ambayo ni pembezoni, utakuta vifaa vya ujenzi vinavyopatikana madukani kwa maana ya mabati, sementi na kadhalika viko juu sana. Hizi sh.7,000,000/= na sh.9,000,000/= kwa hiyo, unakuta hazitoshi. Ningependa Waziri atusaidie wakati anafanya majumuisho atueleze kwa Mkoa wa Kagera, hata Wabunge wengi wameshachangia, kwa mkoa ya pembezoni ukiwemo Kagera, sasa hivi kwa darasa moja tutapewa ruzuku ya shilingi ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mradi mkubwa sana. Ujenzi wa madarasa hauwezi kwisha leo. Tukimaliza madarasa tutaboresha vitu vingine, kwa hiyo, tumekubaliana kwamba ni mradi utakaoendelea. Msimamizi mkuu wa mradi huu katika mkoa ni Afisa Elimu wa Mkoa, huyu Afisa Elimu wa Mkoa anategemewa azunguke katika wilaya zote lakini hana gari anategemea magari yaliyo kwenye *cluster*, akikuta *RAS* amelipangia kazi nyingine ina maana kwamba kazi za Afisa Elimu haziwezi kufanyika. Napendekeza kwa Serikali kwamba Maafisa Elimu wa Mkoa wapewe magari kusudi waweze kuratibu hii mipango vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari unapeleka hela moja kwa moja shuleni kwa ajili ya ujenzi lakini ule wa Elimu ya Msingi ulikuwa unazipeleka kwenye Halmashauri. Zikishafika kwenye Shule ya Sekondari, hizo shilingi milioni saba hazitoshi, inabidi wananchi wahamasishwe wachangie na ili kupata huo mchango inabidi Diwani aende kuhamasisha. Sasa kunakuwa na bodi mbili, kuna Mkuu wa Shule huku na Diwani ambaye anapaswa kuhamasisha uchangiaji. Hii imeleta malalamiko makubwa sana hasa kutoka kwa Madiwani na Wakuu wa Shule wengine wakafikiriwa kwamba labda hizi hela wamezitumia vibaya. Lakini mimi ninaloliona ni kwamba ni kwa sababu Mkuu wa Shule hana wananchi wa kuwachangisha Diwani ndio anao. Sasa naishauri Serikali kwamba badala ya kuzipeleka hizi hela kwenye shule hizi hela za MMES na zenyewe ziende kwenye halmashauri na Madiwani wahamasishwe wananchi waongeze mchango wao. Madiwani washughulikie pamoja na kamati husika wajenge shule, Wakuu wa Shule za Sekondari wabakie kusimamia taaluma pamoja na uendeshaji wa shule wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huku nyuma walimu walioajiriwa wangeweza kukaa hata mwaka kabla hawajapata mishahara. Ninampongeza sana Waziri kwa sababu sasa hivi kwa mara ya kwanza hawa walimu wetu ambao wamepostiwa mwezi wa tatu kwenda kuanza kazi walikuta tayari kule kuna hela za kujikimu na walikuta tayari kuna mishahara miwili. Kwa hiyo, walioajiriwa mwezi wa tatu walipata hizo hela za kujikimu, wakapata mishahara wa mwezi wa tatu, wakapata na mishahara wa mwezi wa nne na biashara ikaishia hapo. Sasa wanashawishika kuona kama hii ilikuwa ni ile danganya toto! Mwezi wa tano mishahara hawakupata, mwezi wa sita mishahara hawakupata!

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inaweza ikawafanya watu wakaacha kupenda ualimu na ninavyojua mishahara ni haki ya mtu kwa hiyo ninapendekeza kwa Serikali kwamba wahakikishe kwamba walimu wanaowaajiri wanawalipa mishahara yao na stahili zao kama wafanyakazi wengine. Matatizo ya walimu jamani yamekuwa kero kila bajeti, kila mtu akisimama iwe kwa Waziri Mkuu lazima utakuta anazungumzia matatizo ya walimu, malimbikizo huwa hayalipwi, mtu anaenda likizo halipwi, uhamisho unahamishwa unakuja kulipwa baada ya miaka miwili. Ukienda kwenye matibabu unalipwa baada ya mwaka mmoja, mishahara mipya ndio unaona imeanza kuwa na matatizo. Kwa nini ni katika Wizara hii tu ambapo haki hizi hazilipwi *on time*? Kila tukikaribia mwaka wa uchaguzi, utasikia Tume imeundwa ya kushughulikia masuala ya walimu. Mbona hatuzisikii zinazoenda kushughulikia masuala ya mainjinia au ya Maafisa Kilimo? Kwani kuna nini kwenye hii Wizara ya Elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwa Serikali kwamba kwanza Wizara yenyewe nafikiri imekuwa kubwa sana, shule zimeongezeka maradufu, ualimu upo pale pale, vyo vya ualimu, sasa hivi na *VETA*. Nilikuwa napendekeza masuala ya ualimu yaishie kwenye ngazi ya wilaya, ya halmashauri na ngazi ya mkoa. Kwa kufanya hivyo haya matatizo labda yataweza kupata ufumbuzi wa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia madeni shuleni. Mnakumbuka kwamba karo ya shule kwa mwanafunzi wa kutwa Serikali ilipunguza kwa nia njema kabisa mpaka sh.20,000/=, kumpunguzia mzazi mzigo kusudi wanafunzi wengi waende shule lakini Serikali ikaahidi kwamba itakuwa inapeleka hela kuongezea pale *capitation grant*. Kwa miaka kama mitano, sita iliyopita Serikali ikapanga kwamba karo ya bwani ni sh.70,000/=, sh.70,000/= ilionekana zilitosha kwa wakati huo. Ni miaka mingi imepita, kwa hiyo, ina maana kwamba hiki kiwango kimepitwa na wakati, inazungumzia vitu ambavyo nafikiri kwamba vinachangia madeni ndani ya Wizara hiyo kuongezeka. *Capitation grant* haijapelekwa tangu Januari na sasa hivi tunapoongea ni mwezi wa saba na shule haijapata *capitation grant*. Kuna watoto wale wanaotoka katika familia ambazo ni maskini, watoto wanaotoka katika mazingira magumu, kuna watoto wanaoitwa yatima wale ambao Serikali imeona matatizo yao na sasa hivi wanachangia kwa elimu yao. Fedha tangu Januari mpaka sasa hivi zilizopelekwa ni za kidato cha tatu na kidato cha nne, kidato cha kwanza na cha pili hawajapata hela mpaka sasa hivi. Wameanza *term* ya pili na hawa watoto ndio tunasema kwamba wanasoma katika mazingira magumu. Naomba Serikali ingeliangalia hili kusudi iweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2002 (*Procurement Act*) ambayo ilirekebisha mwaka 2004 inasema, hakuna kununua kama huna fedha. Lakini huyu Mkuu wa Shule pale shuleni inabidi ahakikishe kwamba ananunua vifaa vya kufundishia, ananunua madawa, ananunua chakula wakati hana fedha anawatumia wazabuni. Wizara ya Elimu nafikiri hela za kuwalipa wazabuni zilitoka kama mwezi wa pili hadi wa tatu. Zile hela zikatumiwa, zikalipa baadhi ya madeni yaliyokuwepo, lakini tangu wakati ule mwezi wa pili na wa tatu mlivyopeleka hela wanafunzi wameendelea kula, wameendelea kufanya mitihani kwa hiyo, madeni yanaendelea kuongezeka siku hadi siku. Hawa wazabuni wengi ni wajasiriamali wadogo ambao wamekopa fedha kutoka kwenye *SACCOS* au kutoka kwenye mabanki, kwa kuwa Serikali haiwalipi *on*



*time* riba zinaongezeka mpaka wengine wamefilisika. Je, ni lini Serikali italipa madeni haya? Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba sasa wakati umefika aidha, Serikali itoe kwa makusudi kabisa hela kusudi iweze kupunguza matatizo ya madeni na mrundikano wa madeni katika Wizara ya Elimu ziweze kusaidia na labda kwenye bajeti hii tuambiwe kwamba ni kiasi gani kimetengwa kuweza kulipa hizo hela za wazabuni. Kama nilivyosema siyo siri kuna mafanikio makubwa sana katika Sekta ya Elimu na matatizo yaliyopo ni kwa sababu mafanikio yamekuja kwa haraka sana. Mwisho kabisa, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hii hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo. Kwanza, nimpongeze kabisa Waziri wa Elimu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo tumeipata, tumeisoma na imeandaliwa vizuri sana. Nampongeza pamoja na Manaibu wake na wataalamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonipendeza sana katika hotuba hii imerahisisha kazi, utakuta huna haja ya kwenda sana, bajeti ya 2006/2007 imeunganishwa pale pale na bajeti ya 2007/2008, yaani hapo hapo kwa hiyo, ni rahisi kuelewa. Baada ya kusema hayo yote wenzangu wamezungumza mengi sana kuhusu hotuba hii na inanipa tabu sana kwamba hakuna kuongeza ila tunajaribu kujazia jazia tu na kutoa maoni na kutoa hoja zetu kuboresha hotuba hii na mimi naomba leo niende Kiteto. Ninafurahi sana katika ukurasa wake wa 17 katika hotuba yake amejaribu kuangalia sehemu zote, ukurasa wa 17 ni muhimu sana nitarudia baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya za wafugaji tunayo matatizo makubwa sana, ni kwamba wote tunazungumzia kwamba suala la elimu ni ufunguo wa maisha, bila elimu huwezi kufanya hiki lakini sisi bado tuna matatizo makubwa sana. Ukiniona nimesimama hapa nikiongea katika jumba hili nikiwa Mbunge nimepitia katika sehemu ngumu sana. Mimi nimekwenda shule mzazi wangu alikuwa hataki niende shule, nimepelekwa shuleni na polisi na nimesomeshwa na *missionaries* na nikalipiwa shule. ukiwaona hapa akina Mheshimiwa Lekule Laizer na wengine ujue wamepitia katika ngazi hizo. Mzazi wangu aliwekwa ndani halafu akatolewa na mimi nikawekwa ndani ndio nikaenda sekondari. Sasa tunapozungumzia watoto wetu sasa hivi wa *primary* kwamba wako katika Shule za Bweni tunawanyang'anya wazazi, mtoto anapopelekwa shuleni familia nzima inalia kwamba mtoto anaenda kupotea mpaka dakika hii tunapozungumza kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuna kazi kubwa kwamba watoto tuna shule za bweni za *Primary School* naomba ndugu zangu mtuelewe hizi shule za bweni sasa hivi ukienda kule unafikiri kabisa ni jela. Kama ni *kabweni ambacho* tumejenga *kadogo* namna hii cha watoto 40 wanalala kama watoto 120, wanabanana kama tunavyosema jela. Sasa hivi naomba Waziri wa Elimu atembelee shule zetu za bweni, japokuwa zipo chini ya halmashauri lakini shule za msingi zipo katika wizara yake na nimemwomba Naibu Waziri, nikamwomba na Waziri aende Kiteto akaangalie Shule za Bweni. Hawa watoto wakoje, wana hali mbaya sana, tuna Shule za Bweni sita *catering* pesa

tunazotengewa ni Sh.200,000,000/= watoto wanakulaje pale? Mtoto anapofunga shule anakwenda nyumbani, anapewa kibuyu cha maziwa anakunywa, unapompeleka shuleni kwa Serikali anapewa bakuri ya uji mkavu. Sasa *contrast* iko wapi? Uji hauna sukari, hauna nini anasukumiwa mtoto na anapokwenda nyumbani anapewa kibuyu cha maziwa, anakunywa anafurahi, sasa ataenda shuleni au atakaa nyumbani. Kule shuleni inakuwa ni mahali pa matesa, ni lazima tuangalie mahali pa shuleni pawe mahali pa kuvutia pa kulala vizuri, pa kula vizuri na mtoto atasoma, nina hakika mtoto wa kifugaji akisomeshwa vizuri hana mahali pengine popote mpaka Chuo Kikuu tu, hana kipingamizi kingine chochote ataenda Chuo Kikuu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndio tunachosema, tukishamaliza *primary* tumeshawaweka, angalau sasa hivi asilimia 30 au asilimia 40 ya watoto wa kifugaji wako shuleni, hatuumii tunashukuru Serikali yetu, tunaisifu sana na imekazana sana. Tunaomba tu iweke juhudi sana kwamba kama Rais alivyozungumza ziongezwe Shule za Bweni. Hizi Shule za Sekondari tumeshazijenga. Juzi nilikuwa na Mkuu wangu wa Wilaya, namshukuru sana Jona Njolewele, tunahamasisha, wanajenga sekondari kwa kila kata. Tumekuwa na Kata ya Sunya, tumekuwa na Kata ya Kijungu, Kata ya Matui, Kata ya Machimbo, tuna sekondari nne nzuri tu, tunaomba hosteli. Mwaka jana nilikuwa mgonjwa ulitenga hela 2006/2007 lakini Kiteto haijapata hela, naomba safari hii unitengee hosteli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama watoto wa *primary* tunawaweka bweni kwa sababu ya kukosa mahali wazazi wao wanahamama, mtoto wa sekondari utamweka wapi, hosteli kwetu sisi siyo suala la hiari kama hujengi hosteli mtoto atalala darasani ataenda wapi? Tunakuomba Waziri wa Elimu katika hizo hosteli utuanzie hatuna hata Sekondari ya Bweni ya Serikali tangu ukoloni.

Rais Mkapa alituhidi kwamba atajenga Shule ya Sekondari moja Ngorongoro, ataweka sekondari nyingine Longido, ataweka sekondari nyingine ya Serikali Monduli, ataweka sekondari nyingine Simanjiro na mwisho ataweka Kiteto. Basi muda wake umeisha tunamshukuru kwa kazi nzuri sana anayoifanya lakini sasa muda umekwisha sasa utujengee hizi sekondari moja moja angalau tujue au kama umeshindwa kabisa utujengee hizi hosteli mama yetu utakuwa umetusaidia. Hizo 10 ambazo umesema utugawie tupate, utujengee na sisi tutawahamasisha. Suala zima sisi siyo umaskini, hatuna umaskini na umaskini upite mbali usitukaribie, suala ni mwamko, tuna ng'ombe wa kutosha, tuna ardhi ya kutosha hatuna umaskini na umaskini uende mbali na sisi lakini ule mwamko na elimu hatuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu huwezi kuwa na ng'ombe 200 au 300 ukashindwa kujenga sekondari lakini kwa vile huna akili hujaenda shule basi tatizo letu ni elimu. Tungepata leo elimu tungekuwa matajiri kabisa hapa, (*the richest people here*) tungekuwa hatuna shida ya pesa, pesa yetu ni elimu mtupe. Kwa hiyo, katika suala hili la sekondari tunaomba hosteli kwa watoto kike. Pili, hawa watoto wa kike, mwaka jana sisi tumepata watoto 20, walipewa mimba na kwetu wale ambao hawataki shule wanaona ni raha kwa sababu watoto wanarudi. Tunashukuru Serikali yetu kwamba wale watoto wanaopata mimba wanarudi shuleni lakini hivi vijogoo mnavifanyaje ambavyo vinakaa

njiani, kazi yao kubwa ni kupandikiza pandikiza mimba. Mbona mimi sijasikia *solution* yao ambao wamekuwa mzigo mkubwa kila mahali kwa shule za sekondari, shule za kutwa na shule za msingi, hivi vijogoo tutavifanyaje? Tuiambie Serikali itumie sheria na hakuna dawa yoyote ni kuwahasi tu, vikipatikana mvitwange, vitaogopa kwenda huko, watapita kusema kweli siyo utani, ni kuwashika kabisa na kuwashughulikia kwa sababu wameshakuwa tatizo ndani ya jamii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, napenda niwapongeze walimu wangu wa Shule za Msingi kwa kazi nzuri wanayofanya licha ya maisha magumu waliyonayo, halafu kwa kuinua taaluma katika wilaya yangu. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana, ninawapongeza Afisa Elimu pamoja na Afisa Taaluma na timu yote na ambao wamefanya jitihada kubwa sana. Napenda kuungana nao kabisa katika jitihada hizi na Serikali ianze kuangalia juu ya maslahi ya walimu, wao hawana posho nyingine zaidi ya mshahara. Sisi tunaokota okota hapa na pale, nimelala Arusha na huko, walimu wataokota wapi? Kwa nini tusiungalie huu uzito wa kazi ya mwalimu? Ikija sensa ni wao, ikija kitu kingine ni wao, ikija kuhamasisha umma ni wao, tunawatumia lakini suala la kusema tuangalie maslahi yao, kilio chao, hakuna. Kwa nini tusiwaangalie? Siyo kwamba tunatafuta kura kwao hapana tunaangalia thamani ya kazi ambayo wanaifanya. Maana kuna mwingine anasema kuzungumzia mwalimu ni kupata kura, hapana wanaumia! Sisi tunabahatika kila mahali, leo ukilala namna hii unapokea, ukienda Dar es Salaam unapata, unaenda nyumbani mke wako ni mwalimu hana kitu chochote anakuangalia tu, anakwenda darasani, anakuja kusahihisha daftari basi, kwisha habari yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwaongeze hata *kamshahara* au hata mazingira magumu tukatoa, tukawaondolea adha, hata haiwezekani? Watumishi wengine wana raha, lakini mwalimu huyu anasahihisha mpaka saa sita usiku, nani anafanya kazi mpaka saa sita usiku? Ukifanya hivi idara nyingine itadai kwa nini hakwenda ualimu ni ngumu! Hawa wanajitolea. Naiomba sana Serikali iangalie kwa makini sana.

Baada ya kusema hayo napenda tu niseme kwamba naomba mpitie ukurasa wa 17 kuna mambo mengi tu, madarasa, nyumba za walimu halafu kuna maeneo magumu kwa Wilaya za wafugaji. Wafugaji wako wengi tu kila mtu anaangaliwa, kwa huruma yako tuangalie tu na sisi katika kipindi kijacho cha bajeti nyingine, tuone kwamba umetusaidia kiasi gani. Nachukua nafasi hii kuwashukuru na nasema kwa moyo mkunjufu kabisa kwamba naiunga hii hotuba mia kwa mia, ahsante sana! (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, unasema unaiunga mkono hotuba, wafugaji wanaunga tu. Naomba niwashukuru sana, muda tulionao ni mfupi sana kwa kumpa mchangiaji mwingine, tulikuwa na wachangiaji wengi lakini tumeshindwa kuwafikia wanne, nao pia walishazungumza mara nyingine. Wale ambao hawakufikiwa kama wanne basi watapata nafasi, waombe Wizara nyingine bado ya elimu ya juu ipo wanaweza kuweka huko.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mchana tukurudi tutaanza kuwapa Naibu Mawaziri wawili kuchangia kwa nafasi yao kama wachangiaji wengine dakika 15. Kama tulivyoamua mtoa hoja atapewa muda wa saa moja kujaribu kujibu hoja ambapo atakuwa tayari amesaidiwa na Naibu wake, halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. Kama kawaida nawaombeni anayetaka kufanya kazi yake akajiandae vizuri, si vizuri wewe unataka kitu chako halafu unaambiwa kanuni haijafuatwa unakosa nafasi. Mkajiandae vizuri.

Mambo ya sera yanaingia katika kifungu cha walimu, mambo mengine ndio mtaenda huko, kitabu cha maendeleo ni mambo *specific* huwezi kusema kitu Njombe hukupewa shule unaanza kusema kwa nini shule ya Njombe haiko katika kifungu kilichopewa shule ya Kiteto, haiwezekani! Kwa hiyo, mjiandae vizuri. Baada ya kusema hivyo naomba niwatakie mchana mwema na naisitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Naibu Mawaziri wote wawili kwa kujitoa kwao katika kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa MEM umekuwa na mafanikio makubwa, pia matatizo ya hapa na pale hasa pale kasi ya kuongeza madarasa ambapo haikidhi idadi ya wanafunzi waliopo hasa baada ya Wizara kuagiza shule zilizokuwa na idadi kubwa ya wanafunzi na kuzigawa kuwa shule mbili na hasa shule za mjini na kujengwa madarasa mawili kwa fedha za MEM lakini madarasa hayatoshelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiomba Wizara kwa sasa kufanya tathmini ya shule hizo na kuzisaidia ili ile dhamira njema ya kupunguza msongamano na kuzipa muda wa kutosha wa wanafunzi kujisomea kwa shule za msingi za Majengo, Katavi, Uhuru, Makanyagio, Nyerere na Mkapa zilizopo Mpanda Mjini katika Jimbo la Mpanda Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la malipo ya madai ya walimu ya mafao, likizo na uhamisho kwa muda mrefu sasa na jambohili limekua likishughulikiwa kwa taratibu mno na kero hii haijaisha kabisa. Ni vema sasa Serikali ikaweka bayana kuwa Wizara hii itashughulikia masuala ya walimu wote hata wa shule za msingi au utaratibu bora zaidi kuliko ilivyo sasa unashindwa kufuatilia uanzie wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utunzaji wa kumbukumbu za walimu pale *TSD* ni vyema ukaboreshwa na kuwekwa katika *Data Base* kwenye kompyuta kuliko majalada

kama ilivyo sasa kwani tunatumia muda mrefu kufuatilia taarifa za walimu hasa za mirathi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuishauri Wizara kufuatilia na kujua kwa nini upandishaji wa madaraja kwa walimu unachelewa, tatizo ni nini? Nakushukuru sana, changamoto kwa Wizara hii ni kufanya tathmini ya kina juu ya MEM na kukamilisha kwa kusaidia miradi iliyokwama kwa sababu yeyote ile. Aahsante sana.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu na timu yake ya watendaji kwa kazi kubwa na nzuri sana mnayoifanya katika kuendeleza elimu nchini, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uongozi wenu, kufanya *SHYCOM* iwe Chuo cha Ualimu cha Biashara na ziara zenu Jimboni na Mkoa wa Shinyanga kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shule ya Sekondari ya Rajani, naomba kibali cha shule ya Sekondari Rajani kuwa na kidato cha tano na sita (*A Level*) kitolewe mwaka huu kwa kuwa shule hiyo inazo sifa stahili ya kuwa *High School*. Barua ya maombi iliwasilishwa mapema mwaka 2006, ahsante.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kuboresha elimu ya sekondari kwa mpango wa MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nina tatizo kwenye maabara na maktaba bado huduma hii haipo katika shule nyingi nchini. Naomba Wizara kuzingatia na kuona umuhimu wa huduma hizi ili tuwe na elimu bora, Serikali ione hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni huduma ya maji safi na salama kutokana na tatizo la kukosa maji safi na salama huko shuleni. Mimi ni Mbunge wa Kilwa Kusini na kuna matatizo kubwa la maji shuleni kwa mfano kwenye Kata ya Kivinje/Singimo, Majirinje, Pande Lemariao, Meteja na kadhalika. Tunawatesa watoto wetu kusoma bila maji kutoka asubuhi mpaka jioni wanaporudi nyumbani ndipo wa waweze kunywa maji. Naomba Wizara itilie mkazo wa kupata maji katika kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna uhaba wa walimu katika shule zetu, naomba tupewe walimu wengine haswa katika Wilaya yetu ya Kilwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuwa na mpango wa kila Wilaya kuwa na Vyuo vya Ufundi. Nashukuru mpango huu unasaidia watakaomaliza sekondari kuwa na taaluma mbalimbali baada ya masomo. Mzigo mkubwa tutawapunguzia wazazi wao na watapata ajira haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Wilaya yetu ya Kilwa kupatiwa maabara na maktaba katika sekondari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BALOZI KHAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Margaret Sitta kwa hotuba yake makini kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza jitihada zake na wasaidizi wake katika kurekebisha mambo mengi na muhimu katika sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Margaret Sitta na wasaidizi wake wanasaidie katika haya yafuatayo ambayo yanahusu Jimbo langu la Bukoba Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko mengi kutoka kwa walimu kuhusu malimbikizo ya mishahara yao. Naomba jambo hili litafutiwe ufumbuzi wa haraka. Walimu wengi katika Jimbo langu wanadai malipo yao ya malimbikizo ya likizo. Hawakuwezesha kwenda katika likizo zao sababu pesa za mishahara zilicheleweshwa sana. Pia walimu ni wachache wakati wanafunzi ni wengi. Zipo shule nyingi unakuta mwalimu anafundisha darasa moja na wapo wanafunzi mia moja. Hii ni idadi kubwa sana kwa mwalimu. Naomba idadi hii itazamwe na kazi za *homework* na mitihani mwalimu mmoja kwa idadi hii ya darasa moja, hataweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara itazame shule ya Mugeza Viziwi. Shule hii haina huduma nzuri. Naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie matatizo ya shule hii. Hii ni shule ya walemavu na ningeomba ifuatiliwe kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Serikali, ahsante.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nichangie katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuchelewa, naomba niende moja kwa moja katika kupongeza agizo la Waziri Mkuu na wananchi wa Jimbo la Bukene, wakishirikiana na Mkurugezini Mtendaji, Bi Sylvia Siriwa na Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Mheshimiwa Betty Machangu, bila kuwasahau Waziri, Naibu Mawaziri wake wawili na watendaji pale Wizarani kwa kazi nzuri waliyofanya kwa ujumla wao hadi kupata shule za sekondari Kata saba kwa muda mfupi sana. Hongera sana kwa ushirikiano huo (*team work*), nasema hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu lina Kata 16 kati ya Kata 16 zilizokuwepo sekondari tatu na *in fact* mbili ya *Kili Secondary School* na *Itobo Secondary School*. Ile ya *Mwamala Secondary School* imefunguliwa awamu hii ya nne na sekondari saba zimejengwa na kufunguliwa tarehe 15 Machi, 2007. Hongera sana kwa Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa kuwa nina Kata 16 na sasa ina sekondari 10, zimebakia sekondari sita kwa Kata sita zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizi zilizobaki zipo katika hali nzuri yaani ninakuhakikishia kwamba mwakani nazo zitakuwa tayari yaani mwaka 2008. Kwa

taarifa, nami nimechangia matofali ya chumba kwa Kata ya Mwangoye, Sigili, Igusule na Ikindwa ili kuhamasisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za sekondari Kata ndio hizo, tuna upungufu wa walimu, maabara ili wanafunzi hawa wapate elimu ya karne ya 21 ya sayansi na teknolojia. Tunaomba kupata maabara na vifaa vyote husika, bila kusahau walimu wa kutosha angalau watano kwa kila sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule hizi ni *co-education* yaani ni za wavulana na wasichana lakini hazina *hostel*. Kwa misingi hiyo, tunaomba tupatiwe *hostel* kwa ajili ya wasichana hasa katika shule za mbali vijijini zaidi (maporini) kama Semembela, Maambali, Isagenhe, Mogwa na hata zile ambazo ziko kwenye *centers* mfano Itobo na Bukene.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile za maporini ni sababu ya wanafunzi hasa wasichana, wanatembea maili na maili porini *anything can happen* hapo katikati kabla ya kufika nyumbani/shuleni kunaweza kutokea mimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *centers* kama Itobo, wanafunzi wanawekwa unyumba na walimu au wanaume/wafanyakazi/wafanyabiashara. Hivyo wanakuwa akinamama wa nyumbani (*temporary housewives*) na baada ya muda wanapata mimba. Ili kuzuia hii, tunaomba *hostel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisha sema zamani nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Waziri Kivuli wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na leo nasisitizia adhabu kali zaidi ili kwa wale hasa walimu wanaowapa mimba wanafunzi basi wahasiwe. Wakihasiwa wawili/watatu kama mfano naamini kabisa, mchezo huu mchafu utaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipotembelea Jimbo langu la Bukene aliahidi misaada katika shule mbalimbali, hapo baadaye. Nilipata taarifa kwamba fedha zilifika lakini ukweli ni kwamba fedha hizo hazijafika. Hivyo namwomba au namkumbushia Waziri apeleke fedha hizo au kwa kifupi atimize ahadi zake. Walimu wa shule kwa mfano Kidete wameniomba nifikishe suala hili la ahadi hii ili kukumbushia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kwako kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Hii ni faraja kwetu kama Wabunge, kwao kama wafanyakazi lakini kubwa zaidi ni Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu ni mtambuka na lina dhima kubwa hasa kwa watendaji wa Wizara hii. Elimu inaweza kuligawa Taifa hili vipande vipande kwa wale wajuzi na wajinga na kwa wale maskini na matajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka mizani ya mtandao wa elimu nchi nzima ni jambo la lazima. Kwa kweli Wizara hii ni tegemeo la ustawi wa Watanzania kwa sasa na hasa kwa siku za baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya lakini lazima muelekeze juhudi hizo pia sehemu ya pili ya Muungano (Zanzibar). Mfano suala la mtaala tumelifuatilia muda mrefu sasa zaidi ya miaka nane. Si busara Mheshimiwa Waziri kulitizama suala la elimu kana kwamba sio la Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani mitihani ya kidato cha nne na kuendelea iwe ni ya Kitaifa wakati mitaala ya mafunzo ya madarasa ya chini (elimu ya msingi) tukawa tunatofautiana. Hii ndio inapelekea kwa wanafunzi wengi kutoka Zanzibar kufeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wasiwasi sisi wananchi wa Zanzibar kuwa Taifa hili linagawanyika. Nasaha zangu kwa hili ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Bara na Zanzibar waanze kuandaa mtaala mmoja na hata inapowezekana Vyuu vya Ualimu (kusomea Ualimu) viunganishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Tanzania Bara wanalenga kuwa na *secondary school* kwa kila Kata, Zanzibar haina hata shule kwa kila Wilaya. Je, tunakwendaje? Namuomba kwa hili nalo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Bara akutane na Waziri wa Elimu Zanzibar au kwa usemi mwingine Serikali ya Muungano iingilie kati angalau kwa Zanzibar nako basi kuwe na *secondary school boarding* mbili kwa kila Wilaya.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Yapo masuala machache ambayo ningependa yazingatiwe na Serikali ili utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2007/2008 uwe wa ufanisi mkubwa na uwaguse Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 17 wa hotuba ya Waziri, imeelezwa kuwa Wizara katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 itatekeleza pamoja na mambo mengine ujenzi wa hosteli kumi kwa ajili ya wasichana katika maeneo ya wafugaji na yaliyo nyuma kielimu. Ujenzi wa madarasa 128 ya kidato cha tano na sita na ujenzi wa maabara 84 na maktaba 30 na majengo ya utawala 14 pamoja na kukarabati shule 15 za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyachagua masuala haya matatu kwa kuwa ni nyeti na yanahitaji uadilifu na uangalifu katika kuteua maeneo ya utekelezaji wa miradi hiyo. Ujenzi wa hosteli za wasichana ni suala muhimu sana ambalo itabidi litengewe fedha zaidi kutokana na upana wake. Ni hitaji ambalo halihusu jamii za wafugaji tu bali vile vile za wakulima zenye mila potofu zisizompa nafasi sawa mtoto wa kike kama vile Kyela. Matokeo yake ni kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wa Kyela. Mwaka 2005 wanafunzi wa kike 258 sawa na asilimia 11 hawakumaliza darasa la saba na mwaka 2006 watoto wa



kile 452 sawa na asilimia 16.4 hawakuweza kumaliza darasa la saba kwa sababu kuu mbili za utoro na mimba zinazochochewa na mila potofu. Takwimu za kufaulu watoto wa kike ni mbaya na asilimia 31 ya watoto wa kike waliofanya mtihani mwaka 2006 walifeli.

Aidha, mwanafunzi wa kike ambaye alishika nafasi ya kwanza Wilaya ya Kyela mwaka 2006 alishika nafasi ya 599 Kimkoa. Hii ndiyo hali halisi ya Kyela na imesababishwa na mila potofu za miaka nenda, rudi zinazomthamini mtoto wa kike kwa kigezo cha kuolewa na kuzaa watoto tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelazimika sasa kuazimisha kila mwaka Wiki ya Mtoto wa Kike yenye kauli mbiu isemayo: “Mtoto wa kike anaweza, mpe nafasi,” kwa lengo la kupiga vita mila potofu. Hatua ya pili ni kujenga hosteli kwa ajili ya watoto wa kike, azma ambayo tunaweza tukaifikia ikiwa Wizara itatusaidia. Kyela ichukuliwe kama moja ya maeneo yanayohitaji msaada maalumu toka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya Serikali ya ujenzi wa madarasa 128 ya kidato cha tano na sita na maabara, izingatie Wilaya ambazo hazina kabisa shule za aina hiyo. Kyela ni moja ya Wilaya ambayo haina shule hata moja inayotoa masomo ya kidato cha tano na sita na bila juhudi za makusudi, Wilaya itapata matatizo makubwa sana ya kuwapokea wahitimu waliofaulu kidato cha nne kutoka kwenye shule nyingi sana za sekondari ambazo tumejenga. Natoa ombi kwa Wizara kuipa Wilaya ya Kyela kipaumbele katika ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita na vile vile maabara stahili. Ahsante na narudia kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupata nafasi ya kuchangia kwa kusema Bungeni, nimeshawishika kutoa mchango kwenye maeneo mengine ya hotuba kutokana na kutoweza kuyachangia awali kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya ualimu kwa vile mpaka sasa chuo kinachotoa mfunzo ya elimu maalumu ni Patandi peke yake, hivyo kutoweza kukidhi mahitaji ya walimu wa taaluma hiyo, nilishauri Serikali kwa mwaka 2006/2007 na bado naishauri kuwa elimu maalumu iwekwe kwenye mitaala ya mafunzo ya ualimu ili kila amalizae masomo ya chuo basi awe na ujuzi wa masuala ya ulemavu na hasa ikizingatiwa kuwa nchi yetu sasa inaendelea na maandalizi ya kutumia mfumo wa elimu jumuishi kuanzia elimu ya msingi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukosefu wa ufahamu wa jamii juu ya mfumo wa elimu jumuishi. Napongeza Wizara kwa dhamira ya kuandaa walimu wa elimu jumuishi mwaka 2007/2008 na kwamba mfumo utasaidia watoto wenye ulemavu na wasio na ulemavu kupata fursa ya kujenga umoja na maelewano kati yao, lakini yaelekea Wizara bado haijaandaa mwongozo madhubuti kwa jinsi ya kuielimisha jamii ili iweze kushiriki kikamilifu katika mfumo huu wa elimu.

Hivyo, naishauri Wizara kuwa na Mratibu wa Elimu Maalum katika ngazi ya Wilaya ambako ndiko maamuzi mengi hufanyika na umiliki wa shule ndiko ulipo pia.

Kwa msingi huo utegemezi wa kusubiri wataalamu wasiozidi sita toka Makao Makuu kuhudumia nchi nzima utatoweka. Wao wabakie kuwa waratibu ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara kuhakikisha kuwa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa watoto wenye ulemavu wa aina zote vinapatikana na kusambazwa kwa wakati ili kuwawezesha watoto hao kumudu masomo sambamba na wenzao katika haki yao ya msingi ya kupata elimu bora kwani ulemavu si sababu ya kukosa kupata maarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo kikubwa cha mawasiliano ni lugha kwa viziwi. Hivyo Wizara au Serikali kwa ujumla ione umuhimu wa kutumia lugha ya alama kama lugha rasmi ya kufundishia hapa nchini. Kinyume chake viziwi wengi wanakosa fursa ya kumudu elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetueleza kuhusu ufufuaji wa michezo shuleni na hata kujenga shule za kufundishia michezo. Napongeza Serikali kwa uamuzi huo. Hata hivyo, naikumbusha Wizara isisahau kabisa michezo ya watoto wenye ulemavu. Ipo na wataalamu wa michezo wanaijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya naendelea kuunga mkono hoja.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mawaziri wote kwa kazi nzuri na kwa kuweza kujenga hoja hadi Serikali ikakubali elimu kupewa kipaumbele cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kudokeza siku za nyuma kwamba shule ya sekondari ya Tunduru ambayo mwaka huu umefunguliwa mkondo wa *High School* yaani *form five* na *form six*. Shule hii hadi leo haina walimu hali inayotatanisha maendeleo ya wanafunzi kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuelekeza nguvu (rasilimali) kwa maeneo ambayo yako nyuma sana. Naamini kabisa Wilaya ya Tunduru ni miongoni mwa Wilaya zitakazonufaika na utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Tunduru linakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu. Shule za msingi na sekondari zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa walimu. Tutashukuru sana kama Wizara itatusaidia kupata walimu wa kutosha haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwapongeza sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. Nawatakia kila la kheri na msikatishwe tamaa.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wa

Wizara kwa kuandaa hotuba iliyojaa mwelekeo wa Wizara ya Elimu na imeonyesha mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne. Mafanikio haya yameenea nchi nzima hasa ujenzi wa shule za sekondari. Nasema Wizara hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Wizara kwa mkakati mzuri wa kuendeleza elimu ya ufundi ambayo itasaidia vijana kujiajiri na kujipatia kipato cha kusaidia kujikwamua na maisha. Tatizo linalojitokeza ni mitaji ya kuanzia miradi. Tunaomba Wizara iandae utaratibu mzuri wa kuwakopesha vifaa ili wakaanzishe miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanapata mimba wakiwa shule, naungana na Wizara warudishwe shuleni baada ya kujifungua na aliyempa mimba apate adhabu kali. Adhabu hizo ziangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za walimu zijengwe ili kukidhi mahitaji ya kila shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri wote wawili na watendaji wote kwa hotuba nzuri ya Bajeti, lakini zaidi kwa utendaji mzuri Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *enrolment*, kazi nzuri imefanyika. Tunasikitika hatukuanza miaka iliyopita, tungekuwa mbali sana kama tungeanza zamani kuzijenga hizi shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba shule zimeongezeka sana. Tafadhali imarisha usimamizi, ufuatiliaji, ukaguzi, uongozi wa kila aina ili shule hizi ziwe za mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgawanyo wa pesa, hakikisha usawa katika mgawo ya pesa za ujenzi wa mashule ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule na wanafunzi watajinunulia vitabu. Fanya mawasiliano na wasambazaji vitabu muhimu wawe na *presence* kwenye angalau kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mafanikio makubwa sana yanayopatikana katika sekta ya elimu katika kipindi hiki. Wananchi na viongozi wao nao wanastahili pongezi kwa michango yao katika mafanikio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa lililopo ni jinsi ya kudumisha mafanikio haya. Historia ya nchi hii inaonyesha kwamba katika vipindi viwili vilivyopita, tumewahi kufanikiwa kwa viwango vikubwa kuongeza idadi ya wananchi wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu lakini mafanikio hayo yalififia baada ya muda kutokana na kutokuwepo kwa mipango endelevu ya kugharamia mafanikio hayo. Inabidi Serikali ichukue hatua za haraka kubuni njia endelevu za kugharamia elimu ili kudumisha mafanikio yaliyopatikana na upanuzi wa aina zote za elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeweka uzito mdogo sana katika mafunzo ya ufundi. Aidha, hakuelekei kuwepo mipango mikubwa kama ile ya aina nyingine za elimu ya kuendeleza elimu ya ufundi. Watoto wanaomaliza shule ya msingi na sekondari wanapaswa kugawanywa katika makundi mawili, kundi moja lenye uwezo mkubwa wa kumudu mafunzo ya nadharia wataendelea na elimu ya aina hiyo wakati kundi kubwa linapaswa kuelekezwa katika mafunzo ya ufundi ya ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Elimu ya Ufundi ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa hususan ya viwanda na aina nyingine za uzalishaji. Naishauri Serikali iandae mpango mkubwa na kuendeleza elimu ya ufundi. Kutokana na mahitaji yake, elimu ya ufundi ina gharama kubwa kuliko ile ya msingi, upili na hata ya juu. Inabidi rasilimali hizo zitafutwe na zipatikane. Inabidi kwa kuanzia, kila Wilaya iwe na chuo au shule ya ufundi na baadaye kujenga vyuo hivyo katika ngazi za chini ya ile ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa Wizara wa kupeleka fedha za kujenga shule ya sekondari Wilayani sio mzuri na unachelewesha kazi na kusababisha ujenzi wa majengo yenye ubora wa chini. Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, wakati wa kujadili hotuba ya Waziri Mkuu, ilishauri kwamba fedha hizo zipitie mkondo ule ule wa fedha za MEMM yaani zipitie kwenye Serikali za Mitaa kiasi kinachotolewa na Wizara ni sehemu tu ya mahitaji ya ujenzi na Serikali za Mitaa na wananchi hulazimika kujazia pengo linalobaki.

Aidha, Serikali za Mitaa zina watumishi wenye ujuzi au utaalamu unaohitajika ili kufanya kazi hizo kwa ufanisi. Kutumia utaratibu wa MEMM kutachangia katika utekelezaji wa kuhamishia madaraka, rasilimali na kadhalika katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iangalie utaratibu mzuri wa kusimamia walimu bila ya kuvuruga mpango wa kuhamishia madaraka katika Serikali za Mitaa. Hakuna manufaa yatayopatikana kwa ku-*centralize* sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza wote kwa ujumla kwa kusimamia vizuri Wizara ya Elimu. Elimu ni ufunguo wa maisha. Yaliyomo ndani ya hotuba hii naomba yatekelezwe. Mipango ni mizuri na malengo ni mazuri, tunasubiri utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita sana katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) au *IT*. Katika kitabu chake Mheshimiwa Waziri amelizungumzia na kulitamka mara kadhaa neno TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni mkombozi mkubwa sana, ni nyenzo ya kufanyia kazi endapo Wizara yako italisimamia vizuri, TEHAMA ikisimamiwa vizuri inaweza kusaidia sana hasa kutokana na upungufu wa walimu, upungufu wa vitabu vya kujifunzia hasa katika ngazi ya sekondari, vyo vya ualimu na vyo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, TEHAMA endapo zitafungwa katika maeneo husika zitasaidia kufundishia kwa kutumia mwalimu mmoja ambapo anaweza kufundisha masomo kwa kuziunganisha shule au vyo zaidi ya kimoja kwa kutumia mkongo wa mawasiliano. TEHAMA ikisimamiwa vizuri na kufikishwa kwenye maktaba zetu kila mkoa na makao makuu pale Dar es Salaam zitasaidia wanafunzi wengi zaidi kujifunza lakini kuweza kudurusu laini hizi kila anachokihitaji kuliko kwenda kutafuta kitabu cha *Chemistry, Biology, Physics* chenye kurasa zaidi ya 400. Mkazo mkubwa kwa sasa uwe ni kuwafundisha wanafunzi somo la *computer* ikiwezekana kuanzia kidato cha kwanza, kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaendana na wakati wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niombe Wizara kwa hali ya sasa upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na hesabu. Somo la hesabu na masomo ya sayansi kwa teknolojia ya huko tuendeko endapo tutalitilia mkazo, tutabaki nyuma, dunia inabadilika na imebadilika, hivyo mkazo wetu uwe katika masomo ya sayansi na hesabu, tukifanya hivyo na ikiwezekana somo la *computer* likawa moja ya somo kuanzia kidato cha kwanza, nchi yetu ule utandawazi kiteknolojia tutakuwa tunaendana nao. Mkakati uandaliwe ili tuwe na walimu wengi wa kufundisha masomo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitamishe kwa kurudia kusema TEHAMA (*IT*) tukisimamia, ikafundishwa kuanzia ngazi za sekondari, vijana wetu kuanzia kidato cha tano hadi vyo vikuu hawatapata taabu ya kwenda kurundikana darasani, mwalimu na mwanafunzi watajifunza au kufundishwa hata wakiwa kwenye makazi yao, hii ni kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Tutaomba Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu iweke au ihimize uwekaji wa *fibre optic*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza Wizara nzima ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri waliyofanya kwenye kipindi hiki cha Awamu ya Nne. Siwezi kuelezea ni mengi mmefanya kulingana na tulikotoka. Kwa muda uliopita tuliambiwa tusijenge sekondari mpaka idadi ya shule za msingi zijulikane au shule tano tu kwa kila Wilaya. Jambo ambalo ni kuzuia wanafunzi wasiendeleo sambamba na kunyima michezo shuleni, nawapongeza kwa kuachana na mawazo potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Longido ni Wilaya mpya, hatukuwa na shule za sekondari tuna Longido Sekondari tu. Kwa sasa tunajenga sekondari saba, mwaka huu mbili zimefunguliwa na tano zitafunguliwa mwakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amegusia maeneo ya wafugaji wa maeneo yenye mazingira magumu ambayo Longido ni eneo mojawapo kwa ugumu wa maeneo na ni Wilaya ya wafugaji.

Kwa hiyo, basi naomba hosteli kumi ulizotangaza kwenye hotuba yako mojawapo ijengwe kwenye shule mpya ya Jimbo la Longido kwani hali ya wafugaji ni mbaya sana kutokana na mifugo kufa mwaka jana. Pamoja na madarasa, nyumba za walimu mtusaidie ili watoto wa wafugaji wasome badala ya kwenda mjini kulinda jambo ambalo halitawasaidia kwenye maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni wanafunzi wanaosaidiwa kulipiwa masomo, wale wanaofaulu kupata *division one*. Suala hili liangaliwe kwa sababu itawagawa wanafunzi kwani wale wanaotoka shule za *private* ndiyo watakaopata *division one*, ni vigumu wanafunzi toka vijijini shule zenye uhaba wa walimu, uhaba wa madarasa, uhaba wa vifaa vya kufundishia kupata daraja la kwanza. Naomba hili liangaliwe upya kwani watoto wa watu wenye uwezo wa kuwapeleka watoto *tuition* na shule za gharama ya juu ndio wengi hupata *point* zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ni muhimu sana kwenye shule za sekondari hasa za vijijini na ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha utoaji wa taaluma na ushauri kuhusu uendeshaji wa shule pamoja na kutoa ushauri wa ufundishaji kuwa na semina ya walimu ili wazingatie utawala bora. Kwa kuwa Wizara inajitahidi kumaliza tatizo hili la upungufu wa walimu kwa muda mrefu walimu wanaopangiwa Longido wanapitia tu kwa kuomba ajira, wote wakishaajiriwa wanatafuta uhamisho huku idadi ya walimu inabaki kuonekana kuna walimu Longido huku wote wamehamia maeneo mengine na kuacha pengo kubwa sana. Naomba Wilaya ya Longido ipangiwe walimu wa kutosha kwani ni muda mrefu tuna upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni chakula kwenye shule za bweni, ni ukweli usiopingika kwamba wafugaji hawawezi kusoma kwenye shule za kutwa kutokana na kuhama kufuata malisho. Naomba chakula cha kutosha kwani kuna wakati mwingine uhaba wa chakula unaleta matatizo kwenye shule na bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda huu mfupi aliokaa Mheshimiwa Waziri kwenye Wizara hii pamoja na Naibu Mawaziri na watumishi wengine akiwepo Katibu Mkuu, Mkurugenzi wamefanya mengi lakini tulikuwa mbali, ongezeni bidii miaka ijayo kazi itaonekana kwa wale wanaotaka kuona na wanaojua tulikotoka historia inajieleza. Ahsante.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze sana Waziri Mheshimiwa Margaret Sitta, pamoja na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na watendaji wote

wakiongozwa na Katibu Mkuu Dr. Dihenga. Ninayo machache tu ya ku-*share* nanyi kama mdau wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu waratibu wa elimu wa sekondari, napongeza kuwepo kwa waratibu wa elimu ya sekondari huko Wilayani. Nimebahatika kuongozana na mmojawapo katika moja ya ziara zangu Mkoani Mara. Wanayo kazi kubwa sana na nyeti na ndiyo msaada wa wakaguzi wa shule. Kwa hali hiyo wanahitaji sana usafiri wa angalau pikipiki iwapo uwezo wa gari haupo. La sivyo, kwa nini wasiongozane na wakaguzi wa sekondari ili waweze pia kutoa *input* ya yale wanayoyafahamu kwa wakaguzi na ripoti iweze kufika Wizarani kwa wakati mmoja? Nashauri pia wapewe mafunzo pamoja na wakuu wa shule wapya ili kuwaweka sawa katika majukumu yao ikiwemo *financial regulations* ili waweze kufuatilia pesa za Serikali zikiwemo ada shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wakuu wa shule wapya, pongezi kwa kuwaandalia mafunzo ili kuwapatia maarifa na stadi za uongozi. Hata hivyo, nashauri shule hizi mpya zisipewe wakuu wa muda wakisubiri *appointment* za wakuu wa shule wa kudumu. Baadhi ya hawa hawawajibiki ipasavyo wakijua kuwa wapo kwa muda tu. Mbaya zaidi wengine ni wezi wa fedha hasa za michango ya wananchi, ada na kadhalika mfano hai ni shule ya sekondari ya Nyaibara iliyoko Kata ya Pemba, Tarafa ya Indugu, Wilayani Tarime ambayo mwalimu huyo wa muda aliyekuwepo kuanzisha shule ameiba fedha za michango ukiwemo mchango wangu wa shilingi 500,000/= nilizochangia mwezi Februari, 2007.

Lakini pia ametoroka hata bila ya kukabidhi shule kwa Mkuu mpya akiwa pia ameiba pesa za mtihani wa *form two, just imagine!* Sina hakika kama ameshawekwa chini ya sheria au bado anakula *life* mitaani kama nilivyoikuta hali mwezi Mei, 2007 niliporudi huko. Tatizo kubwa haijulikani ni nani anamwajibisha huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo cha Ualimu Butimba, hakikuonyeshwa kati ya vyuo vitakavyokarabatiwa lakini kinahitaji mno ukarabati wa miundombinu karibu yote hasa ikizingatiwa *capacity* yake, idadi ya kozi ikiwemo fani maalumu za michezo, muziki, sanaa za maonyesho na ufundi. Aidha, nashauri chuo hiki kiendeleo kufundisha fani nilizozitaja hapo juu kwa ngazi ya cheti kwa walimu wetu wa shule za msingi (*in-service*) kama ilivyokuwa awali kwa faida ya shule zetu za msingi katika taaluma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja hamsini. Hongereni sana.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kunipa uwezo kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wake pia niwapongeze watendaji ambao wamemsaidia Mheshimiwa Waziri kutengeneza hotuba hii aliyoiwasilisha mbele ya Bunge letu Tukufu hotuba ambayo imetupa matumaini ya leo na yale ya baadaye kwa kweli hotuba ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzuri wa hotuba hii nina mchango mdogo sana. Ushauri wangu ili tufanikishe yale yote tuliyo udia kwanza kabisa ni kujenga nyumba za walimu shuleni Serikali ielekeze nguvu zake kwenye nyumba hizo katika sehemu mbalimbali kwa kuleta uwiano mzuri na upatikanaji wa elimu kwa sababu walimu wengi kukimbia sehemu wanazo pelekwa kwa ukosefu wa nyumba na hukimbilia sehemu ambazo zina maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, motisha kwa walimu, walimu wengi wana malalamiko kucheleweshwa posho zao. Kazi hii ya ualimu ni ngumu na walimu wanaishi katika mazingira magumu kwa hivyo, ili vijana wengi waipende kazi hii ya ualimu Serikali haina budi kuboresha mishahara, likizo pamoja na posho yao wapewe kwa wakati. Pia Serikali itekeleze maombi ya muda mrefu ya kuwaondolea urasimu na usumbufu mkubwa wa matatizo yao na mfumo wa ajira zao pia ni vyema malimbikizo ya madai ya walimu yalipwe yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa niaba ya wananchi wangu wa Wilaya ya Hai kwa kuanzia kwa Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwani inaonekana ni dhahiri kuna hali ya amani na utulivu ndiyo maana mafanikio ni makubwa sana. Pia nitoe pongezi nyingi sana kwa kazi kubwa iliyofanyika na inayoendelea ya kusajili shule nyingi sana pamoja na maelekezo mazuri yanayotolewa na wataalamu wenu, hongereni sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunazo changamoto nyingi sana kwa kipindi hiki lakini tunazidi kuwatieni moyo kwa kuelewa hiki ni kipindi cha mpito tu hivyo msikate tamaa hata kidogo, endeleeni na kazi kwa kasi kubwa zaidi na baada ya muda si mrefu matunda na faida yake itaonekana kutokana na maandalizi na mipango mizuri iliyopo na inayoendelea kutayarishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kuwepo na chombo kimoja cha kuwahudumia walimu ili kuwaondolea kero ambazo siyo za lazima na kuwapa nafasi ya kuendelea na kazi kwa ufanisi zaidi. Pia napendekeze tuzidi kuboresha elimu yetu kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu na tuwe tunapewa taarifa zote za pesa zinazotumwa Mikoani kwetu hadi kwenye Halmashauri zetu ili tuweze kufuatilia na kusimamia vizuri utekelezaji na matumizi. Naamini sina sababu ya kuziorodhesha changamoto zote tulizonazo kwenye elimu kwani naamini kuwa mnazifahamu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru na kuwapongeza kwa mapinduzi makubwa ya elimu nchini. Hongereni sana na Mungu awabariki nyote pamoja na wananchi wetu waliotuunga mkono sana kwa michango yao ya hiari. Ahsanteni sana na karibuni Hai.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma ni kati ya Mikoa isiyokuwa na huduma za Maktaba ya Taifa. Ni lini Wizara



kupitia Maktaba ya Taifa, itajenga jengo la Maktaba Kigoma? Naona katika hotuba yako huduma hii haionekani kusemwa kwa Kigoma. Kigoma imesubiri sana inahitaji huduma ya Maktaba. Naomba ufafanuzi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Nianze na pongezi, awali ya yote nichukue nafasi hii kuwapongeza kama ifuatavyo, Mheshimiwa Margret Sitta, Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wote, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Katibu Mkuu, Profesa Hamisi Dihenga na wakurugenzi wote na watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi, naomba shule ya wasichana Tabora iangaliwe jinsi ya suala zima la ukarabati ili wapewe fedha kwa ajili ya uzio wa shule kwani shule hiyo ni ya Kitaifa ambayo inayo historia ya tangu mkoloni hivyo kutokana na wananchi kuvamia na kujenga kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya shule, kwa kuwa ni sehemu ya kati ya mji ni tatizo. Vifaa vya kisasa kama vile *computer, television, fax*, ili kuendana na wakati wa sayansi na teknolojia.

Kuhusu shule za awali, kwanza nipongeze sana Wizara kwa kubuni matangazo kwenye redio ambayo yanahamasisha wananchi kujua umuhimu wa shule ya awali na kuelewa kupeleka watoto maeneo yaliyo ya karibu. Ningeshauri Serikali iangalie kuanzisha shule hizi kwenye maeneo ya kata ili yaweze kusimamiwa na wananchi kama walivyojenga shule za msingi, sekondari, kwani wazazi wengi hawawezi kumudu gharama za shule za watu binafsi kwani bila shule za awali au msingi, shule za sekondari haziwezi kuwepo. Serikali ichukue nafasi ya kuwafundisha walimu hao na shule za awali na angalau kufikiriwa kupewa posho ili twende pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Serikali itoe fedha za kuendesha shirika hili ili waibue tena na kwa nyenzo za kisasa kwenye masomo ya elimu kwa njia ya posta, ili wananchi wengi waweze kujiendeleza, kama ilivyokuwa zamani. Pamoja na hayo waliweza kuandaa masomo mpaka ya walemavu wasioona. Ningeshauri kuwa siku zijazo kuwe kuna shirika au chombo ndani ya Serikali, ni vizuri likawa shirika linalojitegemea badala ya kuwa chini ya Wizara, ili isiwe mzigo kwa Serikali.

Kuhusu mishahara. Mishahara ya taasisi za ngazi za chini ni midogo sana, hailingani na mishahara ya mashirika mengine au marupurupu ya watumishi ndani ya Wizara hii, ingawa nao wako ndani ya ualimu. Naunga mkono hoja kwa asilimia kwa mia moja.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri ya kuendeleza elimu ya msingi na sekondari, pia kwa hotuba ya Bajeti inayoleta matumaini makubwa. Pamoja na pongezi hizi napenda kutoa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu mitaala ya elimu ya kujitegemea. Mitaala ya elimu yetu hivi sasa inawaandaa vijana kifikra kwa kazi ya kuajiriwa, tena

Serikalini kwa kazi za mezani (*white collar jobs*). Mitaala hii ibadilishwe ili iwaandae vijana kujiajiri wenyewe kutoka sekta binafsi. Somo la elimu ya kujitegemea liwafundishe stadi za kilimo, ufugaji, useremala, ujasiriamali, ualimu na kadhalika. Kwa kifupi elimu tunayoitoa hivi sasa ilenge kuwasaidia vijana kuingia katika soko la ajira na mahitaji halisi katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi (*VETA*), tamko la Wizara katika hotuba ya Bajeti kwamba lipo lengo la kuwa kila Wilaya kuwa na chuo cha *VETA* ni jambo jema sana. Katika kutekeleza azma hii sio lazima katika kila Wilaya pajengwe majengo mapya ya vyuo hivi. Ushauri ni kwamba Wilaya zipewe fursa ya kupendekeza taasisi zipi za ufundi zilizomo katika Wilaya hiyo ambayo moja wapo inaweza kukarabatiwa, kupanuliwa na kuwa chuo cha *VETA*. Kwa mfano katika Wilaya ya Manyoni tunayo shule ya sekondari ya ufundi ya Mkwese yenye majengo mengi lakini mmiliki wa shule hiyo (Jumuiya ya Wazazi) haina uwezo wa kuiendesha hivyo majengo hayatumiki kwa ukamilifu. Shule kama hiyo inaweza kuboreshwa na kuwa chuo cha Ufundi (*VETA*) ili vijana wapate manufaa makubwa zaidi na taasisi hiyo itumike kwa ukamilifu zaidi.

Kuhusu *skills and development levy* kupitia kodi hii waajiri hulipa 6% ya matumizi yao ya mishahara kwa kila mfanyakazi. Mwaajiri huyu tayari huendelea kutoa kodi hii isipokuwa wanalalamika kwamba ni 2% ndiyo inayokwenda katika mafunzo, fedha zinazobaki hawaelewi zinakwenda wapi? Vile vile wanalalamika kwamba pamoja na kutoa kodi hii, wafanyakazi wao wanapohitaji mafunzo, hawaoni wanapewa kipaumbele. Ahadi ya Wizara ya kuanza kutoa motisha kwa waajiri ni jambo jema na inajibu baadhi ya malalamiko ya waajiri.

Kuhusu upungufu wa walimu katika maeneo yenye mazingira magumu, Wizara itazame namna ya ku-*retain* walimu wanaopangiwa vituo vya kazi ambavyo havina vivutio kwani hawakai na baadhi yao wapo tayari kwenda katika *private schools*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kurudia kutoa pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii. Ahsante.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na wataalam wao wote kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini makubwa. Hata hivyo napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, pamoja na jitihada za Wizara kupeleka walimu kwenye shule za sekondari lakini bado kuna uhaba/upungufu mkubwa wa walimu katika shule za sekondari hasa kwa masomo ya sayansi. Kwa mfano, katika jimbo langu kati ya sekondari 27 zilizopo karibu sekondari 13 zina mwalimu mmoja tu kwa masomo ya sayansi hasa *physics, chemistry, biology* na hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuishauri Wizara iweke mkakati wa makusudi wa kuongeza idadi ya walimu kwa masomo ambayo nimeyataja hapo juu. Vinginevyo wanafunzi watamaliza elimu ya sekondari bila kuwa na elimu nzuri kwa masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu baadhi ya walimu kushindwa kuishi na jamii ambako shule zimejengwa, shule za sekondari nyingi sasa zimejengwa maeneo ya vijijini na kwa kweli ni shule za jamii zinazohusika (*Community schools*). Bahati mbaya sasa walimu wengi hawajui kwamba uendeshaji wa shule hizi kwa sehemu kubwa ni tofauti na zile za bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi ambako shule hizi zimejengwa wanahusika kwa sehemu kubwa sana katika kuziendesha shule hizi kwa mfano Kamati zinazohusika na ujenzi wa shule hizi ni wana vijiji ambako shule hizi zipo. Pili, Kamati au Bodi za Shule hizo huundwa pia na wananchi ambao wapo katika maeneo ambako shule zipo. Matatizo hujitokeza pale wananchi hao wanapohoji matumizi ya fedha za MMES au uendeshaji wa shule hizo baadhi ya walimu hawapo tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili naomba nimtaje mwalimu Mbwambo ambaye ni mkuu wa shule ya sekondari Msense iliyopo Kata ya Isansa, Tarafa ya Igamba Wilayani Mbozi. Mwalimu huyo ni tatizo kubwa, kwanza hajui dhana nzima ya uongozi. Hashirikishi walimu wenzake kwenye masuala mengi ya kuendesha shule, akisafiri hufunga ofisi yake na funguo humwachia mkewe. Haelewani kabisa na Mwenyekiti wake wa bodi ya shule ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Isansa mahali ilipo shule, matokeo yake vikao vya bodi havifanyiki! Nimewahi kwenda shuleni hapo na mwakilishi wa ofisi ya elimu kujaribu kumaliza tatizo lakini mwalimu alikuwa mkaidi. Mkoa na Wilaya kwa upande wake wamejaribu kuchukua hatua mbalimbali lakini bado mwalimu huyo hawezekaniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwalimu Mbwambo ahamishwe na mimi ningeshauri kwamba awe *demoted* kwa sababu akihamishwa na cheo chake itakuwa ni kuhamisha tatizo. Hili lipewe uzito unaostahili na kwa mujibu wa Afisa Elimu wa Mkoa suala hili limefikishwa Wizarani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji shuleni. Shule nyingi za Kata hasa kule jimboni kwangu zimejengwa bila kuchimbwa visima vya maji. Wanafunzi wengi wamekuwa wakifuata maji mbali na shule, maeneo mengine hadi kilometa tatu. Hali hiyo pia huwafanya wanafunzi wake shuleni saa kumi bila kuwa na maji. Nimefuatilia hotuba ya bajeti vizuri lakini sijasikia kama kuna mkakati wa kutatua tatizo la maji katika shule za sekondari. Nashauri sasa baada ya kuwa na mkakati mzuri katika maeneo mengine, sasa ni wakati muafaka kuliweka kwenye mipango suala la kuzipatia shule hizo maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme shuleni, baadhi ya shule za sekondari kule jimboni kwangu kwa mfano, Myovizi, Mlowo Nalyelye (Kata ya Mlowo) Ilolo, Ihanda, Isangu na Isandula ziko jirani sana njia ya umeme. Hivyo ili kurahisisha maisha ya walimu na wanafunzi wawapo shuleni, basi shule hizo zipatiwe umeme. Nashauri

Wizara iliweke hili katika mipango yake. Tumezungumzia ujenzi wa hosteli, lakini hosteli hizo bila umeme wanafunzi wataishije? Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuipa sekta ya elimu kipaumbele cha kwanza kwa kuitengea asilimia 18. Nampongeza tena Waziri Mkuu kwa kuhamasisha ujenzi wa mashule mengi ya sekondari. Lakini lazima tukiri kuwa mfano uliotumiwa wa kuhamasisha ujenzi wa shule haukuwa wa kiungwana wananchi walilazimishwa kutoa michango mikubwa kinyume na uwezo wao, cha msingi sasa ni kutayarisha walimu wenye uwezo ili elimu itakayotolewa iwe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaopewa mimba wasifukuzwe shule kwa sababu elimu ni haki ya Kikatiba kwa kila Mtanzania, baada ya kujifungua warudishwe shuleni kuendelea na masomo. HakiElimu kwa maoni yangu inatoa mchango mkubwa wa kuwaelimisha jamii masuala mbalimbali yanayohusu elimu. Serikali iwe na uvumilivu wakati kasoro zinazotolewa na HakiElimu zitaigusa Serikali kwa namna moja au nyingine.

Kuhusu mishahara ya walimu, walimu ni kioo cha Taifa. Heshima ya walimu ni muhimu kwa kujenga maadili ya wanafunzi. Inasikitisha kuona walimu wanafanya kazi zinazowavunjia heshima kutokana na kutokuwa na mishahara inayokidhi mahitaji yao ya msingi. Hivyo naiomba Serikali iwaangalie sana walimu kimshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *tution*, elimu inayotolewa kwa mfumo huu ina mwelekeo zaidi wa kibiashara. Lakini zaidi inawagawa wanafunzi wenye uwezo na wasio na uwezo na hili linachukua mwelekeo ule ule wa shule za binafsi ambazo ni wenye uwezo tu ndio wanaosoma, ili watoto wa wanyonge wajione kuwa na hadhi sawa Serikali lazima izifanye shule za Serikali ziwavutie wanafunzi kwa kila hali.

Kuhusu mitihani ni tatizo. Tatizo la mitihani kuvuja linaelekea kupatiwa ufumbuzi. Lakini Serikali inapaswa kuwa macho na hili. Kwa sababu mitihani iligeuka kuwa kitega uchumi kwa baadhi ya wajanja wachache. Lakini bado kuna tatizo la kutoa matokeo yasiyo sahihi kwa baadhi ya watahiniwa. Serikali isisitize uangalifu kwa Baraza la Mitihani sambamba na hili shule ziwe na vitabu vya kutosha vinavyolingana na mitaala.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyo vya *VETA* viwepo kila Wilaya na ikiwezekana kila Kata ili vijana wengi wanaomaliza shule ya sekondari waweze kupata nafasi ya kiufundi ili waweze kujiajiri wenyewe. Ahsante.

**MHE. FELISTA A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya kwa lengo la kuimarisha Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini. Pia natoa pole kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa, kwa kifo cha mpendwa wetu Marehemu Amina Chifupa, Mungu aiweke mahali pema peponi roho yake, *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika shule za sekondari za watu binafsi. Shule nyingi za sekondari binafsi zinapoanzihwa zinakuwa na walima wanaokidhi vigezo lakini baada ya muda aidha, kutokana na malipo ya mishahara kuwa midogo wengi wao wanaacha kazi na shule zinabaki bila walimu wanaokidhi mahitaji na vigezo. Matokeo yake wanafunzi wengi wanashindwa mitihani na kuleta hasara kwa wazazi na Taifa kwa ujumla. Ni vizuri pia Serikali kuweka vigezo vinavyohitajika kwa mtu kuwa mwalimu wa shule ya sekondari kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri sasa Serikali kufuta leseni kwa shule za binafsi zisizofanya vizuri kwa miaka mitatu mfululizo. Ni miaka 46 sasa tangu tupate Uhuru na bado kuna Watanzania ambao hawajui kusoma wala kuandika. Nilishuhudia hiki kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2005. Naishauri Serikali kufanya tathmini kujua ni wananchi wangapi waliojua kusoma na kuandika na ufanywe mkakati wa makusudi kabisa kwa lengo la kila Mtanzania kujua kusoma na kuandika hasa katika maeneo ya vijijini na kuwalipa wale wanaojitolea kuwafundisha hasa watu wazima walipwe kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Watanzania kwa kuitikia wito wa ujenzi wa shule za sekondari za Kata nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutapata mafanikio makubwa katika elimu iwapo mabweni yatajengwa katika maeneo ya shule. Wanafunzi wengi wamepata nafasi ya kujiunga na shule za sekondari lakini wengi wao wataishia njiani aidha, kwa kupata mimba au kwa kuvuta bangi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyohamasishwa na Serikali katika ujenzi wa madarasa, uhamasishaji huo ungeendelea pia katika ujenzi wa hosteli. Watoto wengi wanatembea mwendo mrefu sana kwenda na kurudi shule. Mfano mzuri ni shule ya sekondari Chunyu - Mpwapwa, watoto wanatoka Mpwapwa kilomita 20 kwenda kusoma sekondari ya Chunyu, huu ni mtihani mkubwa kwa wanafunzi na hasa wa kike wanaweza kushawishika au kuchoka na kutembea mwendo mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie sasa kuhusu upungufu wa walimu katika shule zetu za msingi na pia shule za sekondari, katika maeneo ya vijijini kuna upungufu mkubwa wa walimu. Mfano ni Shule ya Msingi Mbalawala. Nilipotembelea shule hiyo mwaka huu nilikuta shule hiyo ina walimu nane tu na darasa la kwanza na la pili, hawakuwa na walimu kabisa. Pia shule ya sekondari ya Mbuga, Mpwapwa in walimu wawili tu. Je, kwa hali hiyo tutafikia lengo la kila mtoto kupata elimu stahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa nia nzuri ya kuanzisha vyuo vya Ufundi Stadi kila Wilaya. Elimu ya Ufundi Stadi itawasaidia sana vijana wetu katika kujitegemea kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri watoto ambao wataonekana wana uwezo kiakili lakini hawata bahatika kupata nafasi aidha ya kujiunga na sekondari au kuendelea

na kidato cha tano basi waruhusiwe kujiunga katika vyuo hivyo vya ufundi kwani wengi wa waliomaliza darasa la saba na waliomaliza kidato cha nne na sita wako mitaani wanazurura na wengine wamejiingiza katika uvutaji bangi na pia ukahaba. Watakapopata nafasi ya kusoma katika Vyuo vya Ufundi Stadi wataweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja ya Serikali.

**MHE. SVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana Wizara hii kwa kazi mnazozifanya. Pamoja na mazingira magumu nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mapendekezo pamoja na ushauri, nashukuru kuwapongeza Wizara imekumbuka kupongeza wananchi kwa kuchangia ujenzi wa shule.

Kwanza mimi pamoja na wananchi wote wa mkoa wa Kagera kuna shule ya Ngeza Walemavu na Viziwi, Serikali kwa kutowakumbuka hao watoto kuwapa angalau vifaa kulingana na ulemavu wao. Naomba Serikali iwakumbuke hao watoto pamoja na walimu wao wapatiwe usafiri pamoja na huduma za matitabu, wanapata shida sana wale watoto, naomba sana Wizara ione huruma sana kwa watoto.

Pili, hizo pesa zilizotengwa naomba Wizara hii zifuatilie sana kwa sababu hazifiki zinakotarajiwa. Watendaji wengi wamekula pesa za wananchi walizokuwa wanachangia. Kwanza zikichangwa wanagawana wenyewe, unakuta wanajenga kwa kusuasua mchanga unapukutika ama simenti ndogo nyingine wanapata mtaji, naomba wanaopata mimba au kuwatorosha sheria ikaze kamba, siyo kuwalegezea kamba Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wasiwaharibie kwa kazi mnayoifanya nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwalisha. Ahsanteni.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza mchango wangu huu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Ufundi, halikadhalika pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wataalamu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo napenda kuchangia kwa kuipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kuhamasisha ujenzi wa shule za sekondari za Kata kitu ambacho kimeuiba msisimko mkubwa wa juhudi za kujitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyojua mimi nia ya kujenga sekondari za Kata ni kuwawezesha watoto wa kata hiyo kwenda shuleni na kurudi nyumbani jioni. Kwa bahati mbaya sana, katika Wilaya ya Morogoro Vijijini suala hili lina mkanganyiko. Pamoja na Afisa Elimu kuwa katika msimamo huo, *DEO* wa Morogoro Vijijini ameamua kufanya kinyume cha hicho. Wanafunzi kutoka Kolelo wamepelekwa kwenye Kata ya Selemala na Mvuha. Wale wa Selemala wamepelekwa kwenye Kata ya Mvuha, hapa sizingumzii wale wanafunzi wa *second selection*. Suala hili nimelipeleka kwa *REO* naye ameahidi kulichukulia hatua kwa kumuelekeza *DEO* arekebishe dosari hiyo. *DEO* hataki, hii

inasababisha watoto hawa wahangaika na kutafuta nyumba za kupanga. Hapa mambo mengi ya matatizo yanajitokeza. Suala hili bado ni kero kubwa na linawakatisha tamaa wazazi kujitolea kujenga majengo ya sekondari. Hili ninalitolea taarifa ingawa nina imani kubwa sana na ofisi ya *REO* Morogoro. Lakini kama *DEO* wangu ataendelea na hili basi usije ukashangaa nami nikaanza mgogoro na *DEO* wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kuwapongeza sana wananchi wa mkoa wa Manyara kwa kujitolea kwa hali na mali kuchangia elimu hususan elimu ya msingi na sekondari. Aidha, naipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa kuhimiza sana suala zima la elimu nchini. Kipekee, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu maana hii hamasa ya elimu tulikuwa tunaiona zaidi kwenye jimbo lake la Monduli na sasa tangu awe Waziri Mkuu ameweza kutekeleza hamasa hii kwa nchi nzima. Hongera sana Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi, naomba sasa nichangie hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyelewa dunia ya leo kwamba elimu ndiyo msingi bora wa maisha na elimu ni ufunguo wa maarifa. Elimu bora ni msingi wa taaluma bora, kwa maana ya kuwa na walimu bora, madaktari bora, mahakimu na majaji bora, wahandisi bora na kadhalika. Nianchotaka kusema ni kwamba ubora wa shule zetu za msingi na sekondari ni kielelezo cha kuwa na wataalamu wengi na bora wa fani mbalimbali kama nilivyotaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima basi Serikali izingatie kwamba sambamba na uhimizaji wa kujenga shule ni budi shule hizo zijitosheleze tangu mwanzo kwa kuwa na walimu wa kutosha, mazingira bora ya shule, vifaa vya kutosha vya kufundishia na uongozi bora (shule nyingi hazina walimu wakuu).

Mheshimiwa Naibu Spika, kushindwa kwa Watanzania kumudu ushindani katika usaili mbalimbali unaowahusisha watu kutoka nje ya nchi inatokana na elimu yetu duni tangu ngazi ya chini (msingi na sekondari) lazima tuelewe kuwa tuko katika dunia ya utandawazi kitu ambacho hatuwezi kuepuka. Ndiyo maana hata suala zima la kuungana Afrika Mashariki tunasema sisi bado tusubiri kuboresha hali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali izingatie kuboresha elimu ili Tanzania nayo tufikie *level* ya ushindani wa ngazi ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine sugu katika elimu yetu ya sekondari ni mimba na utoro shuleni. Mimi naomba nizungumzie kwa maeneo ya wafugaji na hususani Mkoa wa Manyara. Mkoa huu una maeneo mapana sana na ubali wa kata hadi

kata ni kubwa na umbali wa shule hadi shule au kutoka shule hadi makazi ya watu ni mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanalazimika kukodisha mabanda ili wajipikie na kuishi humo ili wawe karibu na shule. Mabanda hayo hayana umeme, hayana maji na mazingira yake yanatisha na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Serikali isigawanye haya maeneo mapana, igawanye Kata, Tarafa na hata Majimbo kwa mfano Jimbo la Kiteto ni kubwa kuliko hata mkoa wa Mtwara. Kwa nini Serikali isigawanye maeneo haya mapana ili kupeleka huduma kwa karibu zaidi kwa wananchi na kupunguza mimba na utoro shuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi imefafanua sana maeneo mengine niliyotaka kuchangia, nampongeza sana kwa moyo wa dhati. Hongera sana Mheshimiwa Margret Sitta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa jana hapa Bungeni na kuonyesha jitihada za Serikali na nguvu za wananchi katika kuleta mapinduzi ya hali ya juu ya elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi wa Siha tumeridhika kabisa na mipango iliyoainishwa katika hotuba ya Waziri na tunaunga mkono yote ambayo yameletwa kwetu. Ombi letu, ambalo tumekuwa tunalikumbushia mara kwa mara ni lile la kutuongezea walimu katika shule mpya za sekondari zifuatazo, Suumu, Dahani, Nuru, Kamarage, Kilingi, Magadini, Oshara, Namwai, *Sanya Day* na kadhalika. Uhaba wa walimu katika shule hizi ni kero kiasi kwamba wazazi wengi wanaamua kuwahamisha watoto wao na kuwapeleka katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za Wizara katika kutafuta walimu tunazitambua na kupongeza, hata hivyo, tunaomba sana shule nilizozitaja hapo juu ziongezewe walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri inayofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja na nina machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kufufua na kuelekeza nguvu kwenye Mafunzo ya Ufundi hasa vyuo vya *VETA*, taaluma hii ya



ufundi ni muhimu sana kwenye maendeleo ya nchi. Napendekeza hivi vyuo ya Ufundi viendeleze mafunzo hayo siyo kuishia cheti tu. Viweze kutoa hata shahada lakini katika taaluma hiyo na wataalamu wenye shahada ya ufundi sambamba na wle wenye shahada za nadharia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie namna ya kukuza lugha ya Kiingereza shuleni. Wanafunzi wanaomaliza sekondari na kwenda vyuoni wana upungufu wa ufahamu wa lugha ya Kiingereza. Hii inawafanya vijana hawa kushindwa kutoa mawazo yao fasaha sababu ya lugha hiyo na ndiyo maana vile vile vijana wetu wako tofauti na wale wa Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie njia muafaka ya kufikisha mishahara kwa walimu wa shule za msingi na sekondari za kata. Walimu wngi wako pembezoni mno na wanapata shida sana kufuata mishahara pale benki ilipo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuipa elimu umuhimu wa kwanza. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa usimamizi wa operesheni sekondari kata ambayo imewezeshwa karibu watoto wote waliofaulu darasa la saba mwaka 2005/2006 kwenda sekondari. Hii ni historia kwa nchi yetu, haijapata kutokea. Pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Mama Margaret Sitta na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa ambayo Serikali imefanya katika elimu ya sekondari, yapo mambo kadhaa ambayo tumejifunza ambayo ningependa kuyawasilisha kwa nia ya kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa elimu ya sekondari ulikuja kidhamira, naainisha mambo yafuatayo ambayo n pamoja na idadi ya shule zinazotakiwa kujengwa, idadi ya nyumba za walimu, idadi ya walimu, idadi ya maabara, kwa kiasi gani hosteli zinahitajika na ni ngapi Kitaifa, kiasi cha vifaa vya maabara, viwanja vya michezo, gharama za kuyatimiza haya yote, wadau au wachangiaji wa gharama hizo, uwezo wa wananchi kushiriki na *timeframe* ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na shule za *A-Level* kutokuwepo kwa mpango huo kunafanya zoezi liwe gumu na watendaji Serikalini kama Ma-DC na kadhalika wamekuwa wakifanyakazi vigumu. Wananchi wanashindwa kupanga vipaumbele mfano kati ya hosteli na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoainishwa kwa wachangiaji kumefanya kwa baadhi ya maeneo wananchi wametakiwa kuchangia hadi shilingi 22,000/= kwa mtu. Hili limetokea katika Kata za Lunguya na Segere, Jimboni Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi hawajui Serikali inachangia kiasi gani na kwa shughuli gani kwa kila shule, tunaomba Serikali itoe mchanganuo wa fedha zitakazotolewa na Serikali Kuu. Mfano, nyumba ngapi za walimu kwa kila shule au Kata

zitagharamiwa? Pia ni vizuri Serikali ifafanue ni nini Halmashauri zinapaswa kugharamia na kwa muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Serikali itoe kipaumbele kwenye Mikoa iliyo nyuma kielimu. Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa idadi ya watu nchini na kwa idadi ya shule za msingi kwa sekondari. Tatizo hili kwa mkoa huu ni la kihistoria, hivyo Serikali inapaswa kuangalia mkoa huu kipekee sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada ambazo wananchi wa Kahama wanafanya kuimarisha elimu hasa sekondari, bado wananchi hawa wameelemewa na umaskini, wanaumia na kulalamika sana wanapotakiwa kuchangia shilingi 22,000/= kwa mtu ni kikubwa mno. Hawana pamba kama zamani na hali ya hewa imebadilika sana kwani kilimo hakiwalipi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali wawaangalie wananchi hawa kwa jicho la huruma. Tuna nia ya kukimbia kuwafikia wenzetu walio mbele kielimu, lakini uwezo ni mdogo. Sababu ni umaskini wa kipato ambao hautokani na wananchi wenyewe bali ni hali ya hewa (*global warning*) iliyoathiri kilimo na wakati mwingine ni mipango mibaya hasa iliyoathiri zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iimarisha usimamizi wa fedha za MMES. Pia Serikali iwachukulie hatua wanaofuja michango ya wananchi. Wabadhilifu hawa wengi ni watumishi watendaji vijiji na kata. Tunaomba Serikali iwasaidie wananchi kuwepo kwa *audit* ya miradi ya elimu iliyochangiwa na wananchi. Kuna maeneo zimefujwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalize kwa kuunga mkono hoja hii. Nashukuru sana.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu uchakavu wa majengo ya shule, nadhani ni wajibu wa Wizara kusimamia majengo ya shule yanakuwa katika hali nzuri. Kwa mfano majengo ama usimamizi wa shule utaelezwa kuwa umeachwa kwa Maafisa wa Elimu wa Mkoa. Hawa wameonyesha kushindwa kumudu kuwa na usimamizi madhubuti. Ni kwa mantiki hii, majengo ya shule zilizo nyingi yameharibika. Kwa mfano shule iliyokuwa na majengo mazuri kama vile shule ya wasichana ya Msalato majengo yameharibika mno na inasikitisha ukiyaona. Nashauri kwa makusudi mazima majengo ya shule hiyo yafanyiwe ukarabati wa hali ya juu.

Pili, shule ya nyingi za sekondari hazina umeme na hasa kwenye Mikoa ile ambayo haina umeme kama vile Kigoma. Matokeo ya mtihani kwa shule hizi yamekuwa yakishuka siku hadi siku kwa sababu wanafunzi hawapati nafasi ya kujisomea. Nashauri Wizara ijipange katika mwaka mwingine wa Bajeti kuhakikisha kunakuwa na makadirio ya kuweka *solars units* kwenye shule za sekondari na hasa

*boarding* ili wanafunzi waweze kupata nafasi ya kujisomea wakati wa usiku badala ya kuzurura ovyo na kujiingiza katika vitendo vya anasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la nyumba za walimu kimekuwa ni kikwazo kinachowaogopesha hawa walimu wapya kukimbia baada ya kukosa nyumba. Hili nalo naomba lipewe kipaumbele katika Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewa kwa mishahara kwa walimu ni kitendo ambacho kimekuwa kikipigiwa kelele na wahusika. Nashauri hili lisimamiwe vizuri na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujua uhalali wa uwezo wa walimu kuja kufundisha hapa nchini wakitoka nchi jirani kama vile Kenya na Uganda. Lipo wimbi kubwa la ujio wa watu hawa ikiwa ni pamoja na kuwarubuni walimu wenye uwezo (wazawa) kufundisha shule binafsi. Hawa walimu wageni wanaziba nafasi za wazawa. Pia kuchelewa kwa pensheni kwa walimu wanaostaafu limekuwa ni kero kubwa. Nashauri Wizara ilisimamie hili ili kuepusha malalamiko.

Kuhusu usafiri, shule nyingi hazina usafiri na kusababisha wakati wa dharura na hasa mwanafunzi anapougua kukosa huduma. Ni vema Wizara ilisimamie hili, pia kuendeleza mashindano ya insha pamoja na mambo mazuri yanayofanywa na Wizara, nashauri mashindano haya yarudi shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda niwapongeze sana Wizara ya Elimu kwa *budget speech* nzuri sana. Mheshimiwa Waziri mama Margaret Sitta, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote hongereni kwa kazi nzuri. Pia niwapongeze kwa utekelezaji bora wa Ilani ya Uchaguzi angalau ndicho kitu tunachoweza kusema kwa kujiamini na kinaonekana elimu kwa ujumla nashukuru kama Mbunge wa Kawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye hotuba yenu ya mwaka huu napenda kuchangia eneo la (21) D Idara ya Ukaguzi, *set up* ya ukaguzi Kanda zote ni nzuri sana na madhumuni ya kuanzisha hizo idara ni mazuri. Ukweli ni kwamba wanazingatia kupata ubora wa elimu wa wanatoa ushauri. Hiki ni kitengo muhimu sana katika kufanya maamuzi ya elimu nchini hasa uanzishaji wa shule mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba wasaidiwe vitendea kazi vikiwemo ofisi, usafiri, *computer* na kadhalika, wanafanya kazi mfano Kanda ya Mashariki Pwani katika mazingira magumu kidogo. Wataalamu wake ni wazuri sana na wahitimu wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba pamoja na kudhibiti ubora wa shule hasa wakati wa uanzishwaji, wazingatie *basics* na kuhakikisha malengo ya Wizara

yanafanikiwa. Watumie busara ili shule nyingi ziweze kuanzishwa kwa ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kabisa kwa busara zao wanaweza kusimamia ubora na wingi wa shule badala ya kukatisha tamaa wawekezaji. Wasaidiwe hivyo vitendea kazi ili waweze kutembelea shule kwa urahisi na kutoa ushauri. Baada ya kusema hayo naomba kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea nakala ya barua ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Babati ikionyesha kuwa Halmashauri ya Mji bado haijapokea fedha ya mgao wa *Capitation Grant* na kwamba kuna uwezekano wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati kutumia fedha ambayo ingepaswa kupewa Halmashauri ya Mji. Nimeona kuwa wahusika wamepewa barua na kuandikiana (*Att. Mr. J. Sagini* – Wizara ya Elimu na Ndugu Sudi – TAMISEMI). Pengine ni vizuri nipate ufafanuzi wa mgao huo na kama fedha zimetolewa kwa Halmashauri ya Wilaya, basi ni vema fedha hizo zirejeshwe kwa Halmashauri ya Mji ambayo imeshindwa kuendesha shule zake kwa kukosa hiyo *Capitation Grant* kwa 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nimeona majina ya walimu wanafunzi waliopangwa Halmashauri ya Mji wa Babati kwa mwaka 2007. Sasa sijui nao fedha zao hazijatumwa au vipi kwa sababu sioni maelezo ya ziada na kwa kuwa nimetumiwa nakala hii bila maelezo ya ziada, naomba nipate maelezo. Naambatanisha nakala ya barua niliyotumiwa hapa Dodoma jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa mchango wangu, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na kwa niaba yangu binafsi, kufuatia msiba mkubwa wa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa salamu za rambirambi kwa familia na marafiki, kufuatia msiba wa marehemu Steven Kazi aliyekuwa Mbunge wa Mwanza Mjini na wenzake waliofariki katika ajili ya gari Mkoa wa Singida. Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri wote, Katibu Mkuu wa Wizara, Maofisa wote na walimu wote nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya kuelimisha Taifa letu. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuamua kuipa elimu kipaumbele cha kwanza. Jitihada za Serikali zimechochea wananchi kuthamini elimu. Serikali ikaze mwendo na kupuuzwa wale wanaobeza juhudi zetu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao ushauri ufuatao, kwanza naishauri Serikali iwekeze zaidi katika kusaidia ujenzi wa maabara katika sekondari zetu. Pili, mikoa ya mbali na Dar es Salaam ipewe mgao zaidi wa fedha kwa sababu bei ya vifaa vya ujenzi ni ya ghali sana ukilinganisha na Dar es Salaam. Tatu, shule kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu (walemavu) ziongezwe kwa mfano Mkoa wa Kagera tunayo moja tu ya bweni pale Mugeza. Nne, naishauri Serikali iwalipe zaidi walimu wa shule za walemavu kwa sababu kazi wanayoifanya ni ngumu sana. Tano, walemavu wapewe muda mrefu sana zaidi ya wale ambao sio walemavu wa mikono na macho wakati wa kufanya mitihani, napendekeza saa moja zaidi na sita, walimu wetu wapewe mishahara mizuri sana na posho nzuri ili kuwamotisha hasa wakati huu ambapo kazi yao ni ngumu sana. Walimu wachache sana lakini wanafunzi ni wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza tena mtoa hoja kwa hotuba nzuri iliyoeleza mambo muhimu kwa ufasaha. Naunga tena mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya elimu na ufundi. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia yafuatayo. Kwanza, ni kuhusu elimu ya msingi, miradi/mpango wa MEMM unafanya kazi nzuri ya kujenga madarasa na ofisi za walimu. Tatizo kubwa ni nyumba za walimu bado kuna upungufu mkubwa sana na nyumba za walimu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Walimu wapewe vyombo vya usafiri ili kuwawezesha kufuata mishahara (pikipiki) hata kama ni mkopo, maslahi ya walimu yaboreshwe, walimu wapewe mafunzo ya kujiendeleza mara kwa mara ili kuboresha taaluma yao, walimu walipwe posho ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu elimu ya sekondari, nawapongeza wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kwa kujenga shule za sekondari 23 na wanafunzi wanasoma katika shule hizo. Shule za sekondari za kutwa (*Community Secondary Schools*) zina matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza shule nyingi hazina hosteli kwa ajili wanafunzi wasichana ambao wapo nje ya *catchment area*. Serikali isaidie nguvu za wananchi kujenga hosteli, mpango wa MMES ni mzuri, nashauri fedha za kujenga madarasa, nyumba za walimu, ofisi na matumizi mengineyo zipelekwe moja kwa moja shule inayohusika badala ya kupeleka Hazina Ndogo, zinaleta usumbufu mkubwa kuzipata, shule za sekondari za Mpwapwa, Dodoma na Kilakala zinahitaji ukarabati mkubwa na kujenga uzio kwa ajili ya ulinzi na usalama wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuzifanyia ukarabati mkubwa shule za sekondari za Mpwapwa, Dodoma na Kilakala? Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kujenga maabara katika shule za sekondari za kutwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia shule za sekondari za kutwa usafiri; shule za sekondari za Mima, Godegode, Kimagai, Berega, Vinghawe, Ihala, Chungu, *Mount Igovu*, Mazae, Mwanakianga na Matomondo hata kama ni kwa awamu shule nyingi zipo mbali na Makao Makuu ya Wilaya. Walimu wa shule hizo wapewe usafiri kama vile pikipiki na wale ambao hawajalipwa mishahara tangu waajiriwe walipwe mishahara yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mratibu wa shule za sekondari katika Wilaya angekaa katika Halmashauri za Wilaya kwa kuwa shule nyingi za sekondari za kutwa zipo chini ya Halmashauri za Wilaya ili aweze kupata msaada katika kuratibu shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inaweza kutoa maelezo ya kina kuhusu wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na kuchukua mafunzo ya mwezi mmoja na kupeleka shule za sekondari za kutwa kuwa walimu baada ya kupata leseni ya kufundisha? Je, mafunzo wanayopata mwezi mmoja (*Induction Course*) yanatosha kumfundisha mwanafunzi na kuboresha taaluma inayotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Vyuo vya Ualimu, kwa kuwa majengo ya Chuo cha Ualimu cha Mpwapwa na nyumba za walimu yanahitaji ukarabati mkubwa. Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo kwani nyumba za walimu wa *TTC* zimechakaa sana zinahitaji ukarabati mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule ya sekondari ambayo itakuwa chini ya *TTC* Mpwapwa kwa ajili ya walimu wanafunzi wa *Diploma* kufanya mazoezi ya kufundisha (*BTP*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutamka kuwa naunga hoja mkono. Pamoja na hayo ni vyema nianze kushauri kuhusu matatizo yanayopatikana katika ujenzi na uendeshaji wa shule za sekondari. Zipo bodi za shule za sekondari kama zilivyo kamati za shule za Mdingi. Jambo la kushangaza ni kwamba Kamati za Shule za Msingi katika mfumo wa MEM zinashirikisha watu wa kamati wote katika uendeshaji, usimamizi na ununuzi wa mahitaji ya elimu. Upo ushirikishi wa kamati ya shule hasa upande wa ununuzi wa vifaa katika shule za msingi. Kamati inaamua yote yanayofanywa kwa maendeleo ya shule ni mara chache sana kupata malalamiko ya uongozi kwenye kamati za MEM.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lipo kwenye MEM, hapa zipo bodi za shule lakini yaelekea hizi ni bodi jina tu. Mwalimu Mkuu wa shule ya sekondari amepewa madaraka makubwa kuliko hata Mwenyekiti wa Bodi na bodi yake katika maswala ya usimamizi wa fedha na ununuzi wa mahitaji muhimu ya shule. Mwalimu Mkuu anapenda madaraka ya kumiliki na kudhibiti fedha za ujenzi wa madarasa na kwa kweli yamekuwepo malalamiko toka kwa wajumbe wa bodi kufuatia mwenendo wa walimu wakuu kushirikisha wanabodi katika shule. Nashauri Bodi ya Shule ya Sekondari ipewe madaraka ya usimamizi wa fedha kama ilivyo kwa Kamati za Shule za Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu ujenzi wa sekondari za Kata, ni jambo la kupongezwa sana. Kwa sasa tumeona jinsi shule hizi zilivyoweza kuokoa watoto wengi ambao kama isingekuwapo tungekuwa tunaandaa jeshi la wahalifu, wapo watu wanaoanza juhudi zilizofanywa. Ni vyema ieleweke kuwa hatua tunayopitia sasa wenzetu wa Uturuki na Uyahudi walipitia zaidi ya miaka 30 iliyopita. Wenzetu hao wamepiga hatua kubwa katika mapinduzi ya elimu.

Napenda ieleweke kuwa ujenzi wa sekondari za kata kwa sasa ni hatua ya kujenga jeshi la wasomi na wanataaluma wa kesho. Ushauri wangu hapa ni juhudi za makusudi na haraka za kupata walimu wa uhakika ili maana ya hizi sekondari za kata iweze kuwepo hasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu Elimu ya Watu Wazima, elimu ya watu wazima ni muhimu katika maendeleo ya Taifa. Elimu hii ikitolewa kwa uangalifu itasaidia kama ilivyokuwa kwa miaka ya 1970 kuwezesha wananchi kuchangia katika kipato chao wenyewe na cha Taifa pia kwa kupatiwa elimu sababu ya uzalishaji. Hivyo basi naishauri Wizara izingatie kuwepo kwa malipo yanayovutia walimu wanaotoa elimu hii kwa watu wazima. Yamekuwepo malalamiko toka kwa walimu kulipwa malipo kidogo kulingana na kazi wanayofanya. Wakati huo huo malipo hayo hayatolewi kwa wakati. Hivyo umuhimu wa kuendesha elimu ya watu wazima unaelekea hauonekani. Elimu hii ikipewa umuhimu inaostahili itasaidia kuifanya jamii kuchangia uchumi wao binafsi na ule wa Taifa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia tena kwa kusema kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kumpa pongezi zangu nyingi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na wale wote wanaomsaidia katika kazi hii ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kumpa mwanadamu elimu li umjenge kwa maisha ya baadae ni kazi ngumu, lakini hapo hapo natoa wito kwa wazazi tushirikiane ili shughuli hii ya makazi ya vijana wote yawe rahisi kwani tunaelewa ushirikiano hutoa tunda jema. Nianze na elimu ya chekechea, kwa ninavyoelewa mwanadamu anasoma na kutaka kuelewa akiwa na umri mdogo kati ya miaka miwili hadi miaka saba, mtoto huwa anakuwa kiakili kwa 70% kati ya umri huu na 30% hupata baada ya miaka saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ilivyoweze kufaulu katika kuandikisha watoto shule za msingi na pia kuweza kuboresha elimu ya sekondari, basi sasa turudi nyuma kidogo kwa kufanya kila bidii kwa njia yoyote, watoto wadogo wote wapate elimu ya chekechea. Elimu ya chekechea ndio hasa msingi wa makuzi ya mtoto kielimu, nyumba imara ni ile yenye msingi imara. Walimu wa chekechea wapatiwe elimu ya kutosha, kwa kweli kama tunatoa elimu nzuri chekechea basi nina hakika itakuwa wepesi kuinua vipaji vya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya msingi kama ilivyo chekechea kwa upande mmoja sio elimu tu ya chaki na ubao lakini pia kuwakuza watoto wetu ili wajuwe wao ni

akina nani, kwa makuzi ya kuelewa mila na desturi za Mtanzania, uraia mwema, uongozi ni nini na nani ni kiongozi, tujitahidi sana kuwaelimisha watoto wetu kwani hii leo ukiwauliza wazee walio wengi kiongozi ni nani, haki zake ni zipi kwa Serikali yake, yeye umuulize unategemea Serikali ikufanyie ni nini na yeye anatakiwa aifanyie nini Serikali basi jibu hajui, ni aibu na hii yote ni kuondoa elimu ya uraia shuleni leo inatugharimu. Elimu ya shule za msingi iwe na mitaala ya kufanana kwa Tanzania unapokwenda shule moja kwa wakati fulani mitawala iwe sawa kwa shule nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya sekondari ni elimu ya mtu mzima anayetaka kupata uelewa wa kazi ambayo ndio itayomtunza yeye na pia kuanzia hapo anakua yupo tayari hata kufikiria atalisaidiaje Taifa lake. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulivalia njuga suala la kujenga madarasa na hapo hapo zaidi wananchi kwa kuitikia wito. Lakini je, madarasa bila ya walimu ni madarasa? Je, madarasa bila maabara ni madarasa na je, madarasa bila *laboratory equipment* ni madarasa? Ninachosisitiza ni kwamba Serikali ielewe bila ya haya ni vitu vya ajabu, tunauhaba sana wa madaktari wa viumbe lakini nimeangalia kitabu cha maendeleo (*Volume IV*), kwa kweli nilishtuka sana kuona sifuri zimeongozana. Naiomba Serikali tuwe makini sana tunapoangalia elimu ya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na walimu, kwa kweli walimu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu sana kama kuna wanaowalaumu walimu kule simo kwani walimu wangeangaliwa kwa jicho la pekee, hawa ndio chanzo cha maisha ya Taifa lolote, walimu mpaka leo mishahara wanayolipwa haikidhi haja hata kidogo ndipo inapomfanya mwalimu ajihusishe na miradi midogo midogo ili aweze kuishi, mwalimu anafanya kazi bila vitendea kazi, hakuna vitabu vya kiada wala hakuna meza wala kiti, wanafunzi wenyewe mpaka leo hii Tanzania wanakaa chini hakuna madawati, mwalimu anaishi mbali sana na shule anayosomesha hata mikopo ya baiskeli inawashinda, inamchukua saa mbili na zaidi kufika shule, kama ilivyo shule ziko mbali sana na maeneo wanayoishi ndipo hapo wanafunzi wasichana wanapopatikana kuharibiwa maisha yao, mradi wote walimu na wanafunzi wanaendelea kuteseka, ni elimu gani utampa mchovu, mwalimu kachoka na mwanafunzi hoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya nne imelenga moja kwa moja kujenga elimu nzuri na bora basi tusiharibu kwa kurukaruka kabla hatujamaliza hili tunashika lingine hatutafika. Tujitahidi kuwajenga walimu wetu kama zamani mwalimu akija kijijini, wanakijiji hutoka na kumshangilia mwalimu, hata zawadi za vikuku na ndizi hakosi kwa sababu walikuwa na ari ya kufundisha, siyo leo walimu wanashindana na wanafunzi mpaka kufika kuingiana maungoni. Hebu turudi na tutafakari na kujiuliza tumetoka wapi, nini kilichoharibu leo?

Kuhusu dawa za kulevya, wanafunzi wetu wake kwa waume wanajihusisha kwenye matumizi ya dawa za kulevya, walimu wajenge ari ya kugundua mwanafunzi wake anapoanza kubadilika kitabia. Vijana wetu walio wengi wamekuwa watoro, wanatumia bangi na walimu kwa sababu ni wachovu hawashughuliki, wanaangalia tu. Wazazi wanapita kwenye maeneo ya vilabu wanaona watoto wapo pale hawajishughulishi kuuliza kulikoni wanashirikiana nao. Hii ndio ile niliyoanza kuiongea



mwanzo lazima sisi wazazi na walimu tushirikiane kulea watoto wetu, vikao vya wazazi na walimu viwe ni vya mara kwa mara shuleni, walimu wapewe agizo la kuitisha vikao mara kwa mara ili pande mbili hizi ziwe zinawasiliana. Narudia kusema nawaenzi walimu ili tupate tija ili malengo yatimie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alikuwa kwenye ziara Monduli, alikemea sana mimba za wasichana shuleni, hivi kuna nini na ukiangalia unaweza kukuta mwalimu ndiye aliyempa mwanafunzi mimba ile, tuhakikishe sheria kali zinatungwa hapa Bungeni kuwakomesha hawa wanaohusika, kule Unguja, Zanzibar kuna sheria, ukimpa mimba mtoto wa shule miaka mitano jela kwa aliyepewa mimba na aliyeweka mimba hiyo, ilisaidia kupunguza mimba shuleni, watu waliogopa na kuheshimu, ila kwa Zanzibar mwanafunzi anaweza kufunga ndoa na kuendelea na masomo, kwa upande wangu mimi siungi mkono hilo, tuwaache wasome halafu tuwaozeshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ombi langu pia tukitaka kurudisha heshima shuleni basi tuisahau kwanza kuwakumbusha watoto wetu maadili mema ya kumjua na kumpenda Mungu, Mwenyezi Mungu ndio kila kitu basi tujitahidi pia kurudisha elimu ya dini katika shule zetu hususani shule za msingi. Tumpende Mungu, tuwajenge watoto wetu kumpenda na kumtukuza na yeye atatusaidia kuwalea ili Taifa letu liwe Taifa zuri lenye maadili mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naomba kuwasilisha na pia sina pingamizi kuiunga mkono hoja hii muhimu. Ahsante.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri, Katibu Mkuu na Wizara nzima kwa hotuba safi, yenye kina, ufundi iliyosheheni mambo yote muhimu. Nashindwa kupata maeneo ya kutosha kuielezea. *It is the best so far both in terms of substance and the calm and the professional manner and in which it was delivered by Honourable Sitta. This is not to mention the momentous and historic strides made during the year. I can only say "full steam ahead."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nina pointi mbili tu japo hotuba hii haikuacha nafasi ya mijadala zaidi. Nilizisemea katika kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu tarehe 26 Julai, 2007 (tazama ukurasa 43 wa *Hansard*). Nazo ni kama ifuatavyo:- Kwanza kitendo cha Wizara kutuma fedha za mchango wa ujenzi wa sekondari kwa Hazina Ndogo Mkoani au shule mlezi kunasababisha usumbufu na urasimu mkubwa. Nashauri fedha hizo zipelekwe moja kwa moja kwa Halmashauri za Wilaya kama ilivyo kwa mishahara.

Pili, ni kuhusu mfumo wa Kanda pia unapunguza kasi ya utekelezaji. Nililalamika kwamba mpango huo unatusababishia usumbufu wa matumizi ya ziada sisi mikoa isiyo na ofisi za Kanda hasa pale tunapohitaji ukaguzi wa ujenzi wa shule. Hapa tulipofikia hatuna tena tatizo la upungufu wa *trained manpower*. Iliyopo ni kubajeti fedha zaidi. Nashauri mtindo wa Kanda uondolewe, japo taratibu na kupeleka rasilimali fedha na watu ili mikoa yote iwe sawa. Isitoshe utaratibu wa Wakuu wa Idara Mikoani kubadilishwa, kubadilishwa na wakuu wa washauri hauna msingi wa sheria. *Regional*

*Education Officer* kama anatekeleza sheria za elimu lakini akifanywa mshauri anapoteza mamlaka yake ya kisheria. Natumaini Wizara italionga hilo na kurekebisha.

Mwisho, mkoa wa Iringa umeanzisha mfuko wa *harambee* na umekwishafikia takriban shilingi bilioni moja, kwa lengo la kujenga mabweni ya wasichana ili kuepusha matukio ya mimba. Pamoja na kwamba Waziri amekwisha wapongeza wote popote walipo, nashauri kuwa mkoa huo unastahili pongezi za pekee. Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya zote, Wabunge wote na Halmashauri zote wameshiriki na wanaendelea kushiriki. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi yeye binafsi, Manaibu Mawaziri pamoja na Watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri inayolenga kuboresha elimu kwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hiyo nzuri napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Wanafunzi wengi wanaofaulu kuingia kidato cha kwanza wanapofika kidato cha pili wengi wao wanashindwa mtihani kuendelea na kidato cha tatu, katika ufuatiliaji wangu nimegundua mambo mawili. Kwanza, mitihani ya darasa la saba inapofanyika, walimu huchukua mitihani na kui-*solve* kisha kuwapatia watoto majibu ya mitihani na matokeo yake watoto hao huonekana wamefaulu na wanapofika kidato cha pili ndiyo maana wanashindwa kuendelea.

Pili, pamoja na jitihada za Wizara yako kupeleka walimu wa kutosha, lakini walimu hao hawafundishi. Vipindi vingi vinapita pasipo walimu kuingia darasani na matokeo yake ni kushindwa kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuelewa ni jitihada zipi Wizara inachukua katika kukabili tatizo hili kubwa la watoto kushindwa mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni madeni makubwa ya chakula katika shule za bweni. Mfano katika Jimbo langu la Musoma Mjini, shule kama *Musoma Technical* na Mara Sekondari zinadaiwa madeni makubwa ya fedha za chakula. Ningependa kufahamu mpango wa Wizara kushughulikia tatizo hilo, maana shule zinakosa chakula kwa kudaiwa madeni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa yenye changamoto nyingi. Nasema hongera na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maoni au mchango wangu katika Wizara hii. Kwanza, napenda kutoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Manaibu wake wote wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Elimu ya Msingi kwani katika shule zetu kutoka darasa la kwanza hadi la saba, tunatumia lugha ya Kiswahili kwa masomo yote ila somo la Kiingereza tu; na mara waingiapo kidato cha kwanza wanakutana na lugha ya Kiingereza kwa masomo yote isipokuwa Kiswahili tu. Hali hii hamwoni kama ni mpango mgumu kwa watoto hao kuweza kufanya vizuri? Hamwoni kama hali hii ndiyo husababisha watoto wengi wanapofika kidato cha pili kufeli. Je, Serikali inasema nini au ina mkakati gani ili elimu iende sambamba toka awali?

Pili, napenda kujua ni watu wa umri gani ambao wanatakiwa kuchangia michango ya shule? Kwani mtu mwenye umri wa miaka 65 au 70 naye anatakiwa kuchangia? Kama ni hapana, ni kwa nini watu hao wanachangishwa tena kwa nguvu na kudhalilishwa watu hao? Pia Watendaji hao ni maelekezo gani ambayo wamepata? Kama kufanya hivyo wanakwenda kinyume ni hatua gani wamewachukulia? Wananchi wanapoonewa washitaki wapi au watoe taarifa kwa nani? Nitaomba majibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuwajali walimu wanaokubali kufanya kazi katika mazingira magumu na kuwapa motisha ili kuwajengea moyo wa kufanya kazi. Pia walimu ambao ndiyo wanaanza kazi walipwe mishahara yao kwa wakati husika kwani kama hawatafikiriwa na kutekelezewa mishahara yao kwa wakati muafaka watawunjika moyo na kutokuwa na ari ya kufundisha. Hivyo, tunaiomba Wizara kufanya msukumo huko Wilayani ili kufanya msaada kwa vijana walio wageni kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupokea mchango wangu. Ahsante.

**MHE. DR. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Margaret Sitta, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Watendaji wote kwa kazi nzuri sana.

Pili, kilio changu ni juu ya ukosefu wa ardhi ya ujenzi wa shule Jimboni kwangu na Majimbo jirani ya Hai, Vunjo na Moshi Mjini. Mojawapo ya mapendekezo ya kutatua tatizo hili ni kutafuta ardhi maeneo ya tambarare (Mwanga, Same na kadhalika) na kujenga shule kubwa kwa ajili ya wanafunzi kutoka Mkoa mzima wa Kilimanjaro. Naliona pendekezo hili kuwa nzuri sana, tatizo tu ni kwamba sisi Wabunge ndio tumeachiwa kazi ya kulipendekeza kwa *RCC* na tumeshalifanya hili, lakini naona mwendo ni mdogo sana. Naomba Wizara ilichukulie kama *agenda* yake kutokana na umuhimu wa suala lenyewe.

Tatu, ipo dhana inayoenea kwa kasi kuwa Mkoa wa Kilimanjaro umeendelea kielimu na kwamba eti hauhitaji kupewa kipaumbele. Mtazamo huu ni hasi hasa ukizingatia shule hizi zinafundisha watoto kutoka Tanzania nzima bila kubagua. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Mahiza, alijionea binafsi hali duni ya shule katika Jimbo langu na katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa jumla alipokagua ujenzi wa shule mwanzoni mwa mwaka huu.

Hali hii inatokana na umaskini uliosababishwa na kuanguka kwa zao la kahawa Mkoani Kilimanjaro. Mkoa hauna ardhi ya kutosha, hauna mifugo mingi na tegemeo pekee ni elimu. Tafadhali Wizara isiutupe Mkoa huu kwani nyie ndio Wizara mama kwa Mkoa wa Kilimanjaro.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Napenda kufahamu ombi la Mkuu wa Chuo/la wananchi wa Kigoma kuomba Chuo cha Ualimu Kasulu, pamoja na kupokea vijana wa mafunzo ya Diploma na nafasi kubaki, ni kwa nini Wizara yako isitoe kibali cha Chuo hicho angalau kwa miaka 5 kikatoa cheti cha Ualimu daraja la “A”? (2007-2012).

Hali hii itasaidia sana kupunguza tatizo sugu la ukosefu wa walimu katika Wilaya za Mkoa wa Kigoma na Mikoa mingine ya jirani na pembezoni.

Tatizo la maabara ya sayansi kwa shule za sekondari za Mkoa wa Kigoma, historia ya Elimu Mkoa wa Kigoma inafahamika. Kigoma ilisahaulika, haikupata rasilimali watu na fedha katika Sekta ya Elimu mapema. Kigoma ilibweza kwa sababu nyingi tu za kihistoria. Mheshimiwa Naibu Spika, Kigoma iko pembezoni, walimu hawataki kwenda huko na kadhalika.

Je, nyote hayo pamoja na Wizara ya Elimu haioni ipo sababu sasa ya kuupa Mkoa wa Kigoma kipaumbele, upendeleo wa makusudi ili shule zetu nyingi sasa za Kata (maana ndiyo zilizopo sasa) zijengwe maabara ya sayansi?

Tatu, walimu wa sayansi –Chuo cha Ualimu Kasulu. Hoja na ombi hili limeleta kwako miezi mitatu iliyopita. Jengo safi wamejenga, tatizo ni walimu wa kufundisha vijana. Ni lini walimu wa sayansi utawatuma waende Chuo cha Kasulu? Naomba jambo hili ulipe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu Mawaziri wote wawili na Watendaji wa Wizara kwa hotuba nzuri na hasa jinsi hotuba ilivyogusia kila eneo. Mchango wangu utahusu hali ya elimu kwa ujumla kwenye Jimbo la Songwe.

Moja, ni kuhusu mishahara ya walimu kucheleweshwa. Nashauri utaratibu ufanyike uwawezeshe walimu kupata mishahara yao mapema kama watumishi wengine wa umma wanavyofanyiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usumbufu wa kero wanazopata walimu kwa mfano kuchelewa kurudi kazini wakati wa kusubiri mishahara yao. Kujiingiza kwenye

matatizo mengine hasa walimu wa kike, wanafunzi kukosa huduma ya mafunzo kwa kipindi ambacho walimu wakiwa wamefuata mishahara na kadhalika.

Pili, *hardship allowance*. Serikali itoe motisha kwa walimu wanaofanyia kazi kwenye mazingira magumu kama Jimboni kwangu baadhi ya shule ziko umbali wa zaidi ya kilomita 170 kufika Makao Makuu ya Wilaya. Sehemu hizo hakuna umeme, hakuna maji wala nyumba za walimu.

Tatu, madai ya walimu kuhusu malipo ya bima zilizoiva. Jimboni kwangu ipo idadi kubwa ya walimu ambao bima zao zimeiva, lakini hawajalipwa madai yao hadi sasa. Kila wanapofuatilia wanaambiwa fedha zimekwisha. Serikali inachukua hatua gani za makusudi kuwasaidia hao walimu?

Nne, upungufu wa walimu. Hili ni tatizo la kitaifa. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kutatua tatizo hili. Naomba Jimbo la Songwe liwe miongoni mwa maeneo ya kupewa kipaumbele wakati wa kuwapangia kazi walimu.

Tano, walimu kujiingiza kwenye siasa. Jimboni kwangu wapo baadhi ya walimu ambao wanajiingiza kwenye siasa katika ngazi mbalimbali za uongozi. Matokeo yake muda wa kufundisha darasani unakuwa ni mdogo kuliko ule wanaoutumia kwenye siasa. Ni vyema kukatolewa mwongozo juu ya suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote. Salamu za pongezi ziende zaidi kwa walimu wote nchini kwa kazi nzito yenye matatizo mengi. Katika kitabu cha hotuba na cha *BEST* hakuna mahali hata pamoja nilipoona idadi ya wanafunzi walioko katika madarasa isipokuwa kuna idadi ya walioandikishwa tu. Hivyo, Waziri naomba atupe takwimu za wanafunzi wanaoingia madarasani na kusoma badala ya kuwa na idadi ya walioandikishwa katika ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vifaa, katika hotuba ya Waziri sikuona idadi halisi ya vifaa vya elimu kwa mfano *desks*, vifaa vya maabara na kadhalika. Hata katika kitabu cha *BEST* hakina. Waziri atueleze idadi ya vifaa vinavyohitajika kutokana na ongezeko la shule na wanafunzi na mpango wa kukabili tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu walimu, naomba Waziri atueleze idadi halisi ya walimu katika fani zima husika na upungufu uliopo ili kujua hasa mahitaji ya walimu katika kipindi cha miaka 10 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Serikali katika Elimu. Katika kitabu cha *BEST* page 91, inaonesha kwa 1999 elimu ya juu ilikua kwa asilimia 23.4 wakati 2006/2007 ni asilimia 21.9 wakati huo shule na wanafunzi waliongezeka na thamani ya

shilingi imepungua. Je, Waziri haoni kwamba bajeti ya Elimu haikidhi kufika kuendeleza elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia *E-Education*, Waziri atueleze Wizara inatumia vipi fursa zinazotolewa na *NEPAD* katika programu yake ya *E-Education* ambapo zipo nchi za Afrika zinafaidika na programu hii ambayo inaziba pengo la ukosefu wa walimu kwa shule ambazo wana fursa za kutumia *Internet*? Mpango huu unaweza kupunguza tatizo la idadi ya walimu katika shule ambazo haziwezi kutumia mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwazi katika bajeti. Ni vyema Serikali ikaweka utaratibu wa kutathmini na kujua hasa thamani ya michango ya wananchi kama vile tunavyojua thamani ya misaada ya nje, lakini ya wananchi haijulikani. Aidha, kujua viwango vya michango ya wananchi ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa shule na nyumba za walimu. Ni vyema Serikali kutumia JKT, Magereza kwa kutumia vikosi vyao vya ujenzi na kwa kushirikiana na makampuni ya nje yenye teknolojia ya *Pr-fabricated* ili wawapunguzie mzigo wananchi na kuharakisha ujenzi zilizokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Financing of Basic Education*. Mwaka 2002/2003 *budget allocation* kwa mlinganisho na bajeti jumla ya Serikali ilikuwa kwa asilimia 1.3 na *sector budget* ilikuwa kwa asilimia 31.1 wakati 2006/2007 kwa asilimia 25 na kwa *GDP* haipo. Ni wazi kuwa itakuwa chini. Hivyo, sio kweli kuwa katika mgao wa fedha kwamba umeongezeka hasa tukiitilia maanani ongezeko la wanafunzi, shule, walimu, vifaa na kuporomoka kwa shilingi. Waziri atueleze, ongezeko hilo kwa nini liwe chini kwa mwaka 2002/2003?

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini Mheshimiwa Waziri atatupatia maelezo ya kina.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kunipa uwezo wa kuchangia hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Fuoni kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi na kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jimbo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niishukuru Serikali kuipa Elimu kipaumbele katika bajeti yake na kuipa fedha nyingi kuliko mahali pengine popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafuta kiwanja Zanzibar. Wizara imefanya jambo nzuri la kutafuta kiwanja kwa ajili ya ofisi ya Baraza la Mitihani. Hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa hasa ikizingatia malalamiko mengi yanayotolewa na wanafunzi kwa kukosekana ofisi na kusababisha usumbufu mkubwa hasa wakati wa ufuatiliaji wa matokeo ya mitihani na wakati wa kufanya mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa ofisi huko Zanzibar pia ninaiomba Wizara kufikiria uajiri wa wafanyakazi katika Taasisi hiyo kwani hivi sasa nafikiria hawazidi wafanyakazi wawili walioko Zanzibar na hili lipewe kipaumbele kwa sawa kwani walioko hawakidhi haja kushughulikia shida za wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mitihani Kitaifa, niishukuru Wizara kwa kusimamia vyema suala la uvujaji wa mitihani ambayo ilikuwa ni kero na aibu kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili, ninaiomba Wizara isilegeze kamba. Mikakati iendeleo na kila atakayebainika sheria ichukue hatua bila ya kumwonea huruma kwa sababu anayefanya jambo hili anadumaza wanafunzi, pia kusababisha kupata wataalam wabovu wasiokidhi katika soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kupiga vita suala hili pia hulazimika kufuta matokeo ya wanafunzi wanaobainika wamehusika na kuona mitihani kabla ya wakati pia kuwazuia kufanya mitihani ya Kitaifa kwa muda wa miaka kama mitatu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wangu, naomba adhabu hii ya kuzuia kufanya mitihani kwa muda huu iondolewe, kwani muda huo ni mrefu na inawadumaza kielimu na hasa ukizingatia gharama za masomo zilivyo na hali za wananchi wetu zilivyo kimaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wanashindwa kusomesha watoto kwa kipindi chote hatimaye watoto watakuwa hawana la kufanya na kujiingiza katika mambo yasiyofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba za walimu, ninaiomba Wizara katika bajeti hii izingatie sana ujenzi wa nyumba za walimu. Walimu wengi wanaishi katika nyumba za kupanga na hupata manyanyaso mengi kwa wamiliki wa nyumba hizo na mara nyingine walimu hukimbia katika sehemu walizopelekwa na kusababisha ukosefu mkubwa wa walimu kwa baadhi ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua fedha hazitoshi kutokana na idadi ya shule zetu, lakini msukumo uliotumika katika ujenzi wa madarasa kwa kila Mkoa ni njia pekee inayofaa kwa ujenzi wa nyumba hizo. Tukifanikisha suala hili na kutokana na vijana wengi kuhamasika shida ya walimu itamalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusoma hotuba yake kwa upole; makini na unyenyekevu wa hali ya juu kiasi kwamba kila mtu ameielewa kweli kweli, hasa yeye ni mwalimu na ualimu ni wito. Hongera sana. Mimi ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza ni kuhusu *VETA*. *VETA* nchini zilikusudiwa kujengwa katika kila Mkoa na sasa linakuja wazo la kujenga *VETA* kila Wilaya kama ilivyotajwa katika hotuba yake ukurasa wa 59 – 60 na tayari Wilaya zingine wameshajengewa *VETA* ndani ya Wilaya. Ombi langu ni kwamba, kabla zoezi hilo halijaendelea, kwanza malizeni kujenga katika Makao Makuu ya Mikoa. Bado kuna Mikoa ambayo *VETA* hazijajengwa. Wizara inaweza kutuambia sababu za msingi za kuacha kujenga *VETA* katika Mikoa hiyo na kurukia Makao Makuu ya Wilaya? Suala la Lindi kuwa karibu na Mtwara ambako kuna *VETA* sisi watu wa Lindi hatuliafiki kwani bado kuna ukiritimba wa aina fulani hivi, kiasi kwamba watoto wa Lindi wanakosa au wanapata nafasi chache. Tunataka *VETA* yetu Lindi. Serikali ituambie ni lini *VETA* itajengwa Lindi.

Pili, ni kuhusu ukaguzi wa shule. Katika Wizara ya Elimu, Kitengo cha Ukaguzi kinasahaulika sana kiasi kwamba kitengo hiki kujiona kipweke. Kwanza hawana nyenzo za kufanyia kazi; wakipata magari, basi hawapati mafuta. Tunashauri Wilaya zile ambazo watapewa magari, basi wapewe na uwezo wa mafuta. Si hilo tu; ukaguzi unaofanywa na wakaguzi mashuleni ni muhimu sana kwani wao ndiyo wanaohimiza elimu bora. Lakini utakuta taarifa zao nzuri za ukaguzi ambazo mwishowe hupelekwa kwa waajiri wa walimu husika waliokaguliwa, hazifanyiwi kazi. Mkurugenzi badala ya kufuatilia yale mapungufu, basi kwao huwa kama ni kitu cha kuwafurahisha. Hawafuatilii mapungufu yaliyotajwa na taarifa ya ukaguzi kwao ni kama usanii tu. Wakurugenzi au wahusika wa kufuatilia mapungufu yatolewayo na ukaguzi, basi wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Tatu, kesi za walimu kuchukua muda mrefu. Kuhukumiwa suala hili nililizungumzia mwaka 2005/2006, pia wakati walimu wanapopata kesi, aidha ya kutia mimba mtoto wa shule; kubaka mtoto wa shule; wizi wa mali za shule; wizi wa fedha za MEM/MMES; kupigana walimu *staff room* na kadhalika, kiasi kwamba mwalimu hukaa pale shuleni kwa muda mwingi mpaka wanamwona sasa ni kinyago tu; na kuanza kudhalilika. Tunashauri kesi za walimu zinapotokea, basi Baraza la hukumu limalize hukumu zao ili kuwapa nafasi kutafuta kazi nyingine walimu kama hawatarudishwa tena kazini.

Nne, ni elimu duni, Shule chache Kusini/Lindi. Moja ya matatizo ya Kusini ni kutokuwa na shule za kutosha za msingi na za sekondari; za elimu ya juu hadi Kidato cha Sita na *VETA*. Hii sio kwa sababu watoto wa Lindi hawana akili, hapana. Hili ni kwa sababu kwanza ni kutokana na mfumo wa kikoloni tuliorithi huko nyuma wa kuifanya Mikoa ya Kusini kuwa akiba yao *Reserve* wasipate elimu ili waendeleo kutumika kama Manamba; na la pili ni pale Tanzania mwaka 1972 ilipoamua kuwa na sera mpya ya elimu ya kwamba; shule zote nchini kuzifanya ziwe shule za Kitaifa; hivyo Mikoa ile yenye uwezo zaidi kielimu na kiuchumi kupata nafasi zaidi popote nchini na Mikoa ile yenye uchumi duni kukosa uwezo na nafasi hata kama shule ya sekondari ipo Mkoani pale kwa mtindo huo, watoto wengi wa Kusini ambao wenye uchumi duni walikosa nafasi ya kupata elimu na watoto wengi wa Mikoa tajiri walipata elimu kupitia shule nyingi za Kitaifa.



Mheshimiwa Naibu Spika, ombi tafadhali sana, Serikali haioni sasa kuwa ni wakati muafaka wa kusaidia Mikoa hii kwa makusudi kabisa kwa kuongeza shule za sekondari na za elimu ya juu kama *High School, Secondary, VETA* na kadhalika ili twende sawa ukizingatia kuwa sasa watu wa Mikoa hiyo wana mwamko wa kujitolea kujenga sekondari na hivi sasa wameshajenga ma-boma 78 ya sekondari? Tunaomba upendeleo maalumu wa makusudi kabisa na vilevile uhamasishaji wa kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kupewa kipawa cha awali katika bajeti ya Serikali kwa kutimiza asilimia 19. Ni matarajio yangu kuwa yale yote yaliyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2007/2008 yatafanikiwa kwa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, Barala la Mitihani linafanya kazi yake kwa ufanisi wa kutosha pamoja na hali ngumu na uchakavu wa vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani ndio kigezo cha ubora wa watahiniwa na ni kigezo cha ubora wa vyeti katika nchi yetu. Hivyo basi, naomba chombo hiki kiangaliwe na kupewa msukumo wa kutosha pamoja na kupatiwa mitambo ya kutendea kazi inayolingana na karne hii ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Baraza la Mitihani ndio chombo kinachotunga mitihani yote ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, hivyo basi, tukiombe chombo hicho na Wizara husika kuwa na mfumo wa mitaala kwa wanafunzi wa form IV na form VI ili kwenda sambamba wakati wa kutahiniwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara inatarajia kuwarudisha shuleni wale wote waliopata mimba. Napenda kujua ni kwa awamu ngapi ya mimba? Je, mwanafunzi aliyezaa mara ngapi ataweza kurudishwa tena?

Mheshimiwa Spika, kuwapongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, hasa Vyuo vya *VETA* jinsi walivyo wabunifu na wanavyofanya kazi zao kwa hali bora ni mategemeo yangu ni kwamba vitapewa msukumo wa kutosha ili kuendelea na kazi walizopangiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa MEM, Mpango huu umefanikiwa kwa madarasa na ongezeko la wanafunzi. Hivyo basi, ukiongeza unga unaongeza na maji hivyo basi ni wakati wa kufikiria tena bado mapema, ongezeko la vijana ambao watajiunga na sekondari mwishoni watakapomaliza elimu ya msingi, isiwe tena mshike mshike kutafuta wapi vijana watapelekwa kuendelea na masomo.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri na kazi nzuri na naunga

mkono hoja. Katika kuchangia, namwomba Waziri afafanue na kutoa tamko la Serikali katika maeneo yatuafayo:-

- (1) Ibara ya 17(a) mgao wa wanafunzi hao kimkoa na kiwilaya na (f), (g), (h), (i) mgao wa kila wilaya.
- (2) Umiliki na usimamizi wa shule za sekondari, Je, Serikali ina mpango au la wa kuhamishia umiliki na uendesaji wa sekondari uwe chini ya Serikali za Mitaa kwa kuziongezea uwezo wa wataalamu na fedha chini ya sera ya *D by D*.
- (3) Vyuho vingapi vimepanga kuanza 2008? Je, Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Lushoto kitakuwa kati ya hivyo?
- (4) Sekondari za A Level Wilayani Lushoto, Wilaya ya Lushoto imefaulu kusajili asilimia 100 ya wahitimu wa *STD VII* kuingia *Form I* katika sekondari 50 za wananchi.

Je, Serikali iko tayari kuanzisha angalau sekondari tatu za A Level zianze mwaka 2008 Wilayani Lushoto? Naunga mkono hoja.

**MHE. LAWRENCE K. MASHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niseme wazi kwamba ninaunga mkono hoja asilimia mia moja. *I would like to take this opportunity to congratulate the Ministry on a job well done in terms of increasing the possibility of thousands of young Tanzanias to enjoy the benefits of secondary education through the bulding of hundreds of new secondary schools throughout the country.*

*Whereas I wholly support the idea of mass secondary education, I believe that it is necessary for the development of this country. The Ministry also focuses on the development of Academic centres of excellence at the Regional level to catch for the best brains we have within our country. These centres of Academic excellence should be well equipped with materials, facilities and manpower so as to enable a child who has completed studies as a secondary school designated as a centre excellence to complete on an equal footing with his as her age mates anywhere in the world.*

*These schools of developed would be boarding schools accepting both boys and girls where the Government would be moulding the future political, business and scientific leaders of this country.*

*If initially government could set aside Tsh 1 bilion per region on an annual basis for ten years we would have schools which could complete with the best of schools in the world.*

*In the 1950's and 1960's Pugu, Tabora Boys, Marian College and other were academically equivalent to the best of schools in Europe, and it is graduates of these secondary schools which we still rely on today.*

*These schools should be relatively large schools accommodating between 800 and 1000 students geared at nurturing the best of our students notwithstanding financial ability. The future of our country lies not in mass education alone; however it must be supplemented by centres of excellence. Whereas I am aware that we do have some special schools, these schools are not being given the support they require.*

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niwashukuru Mawaziri wote na walioko chini yao waliyoweza kuwaona watoto walemavu wa Halmashauri ya Kigoma walioko shule maalumu ya Uvinza ambayo ni ya watoto wasioona na wenye mtindio wa akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba wajengewe bweni la kukaa bila kurudi nyumbani na Serikali imeweza kufanya hivyo. Serikali imetuma shilingi milioni tisa wananchi wanashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pesa hiyo ni kidogo kutokana na maisha ama vifaa jinsi vilivyopanda bei Mkoani Kigoma. Vilevile halitakiwi bweni moja tu kwa sababu watakaohudumiwa pale sio hao tu walioko pale bali watakuwa ni watoto wote walioko Mkoa wa Kigoma wenye matatizo hayo hayo ambao walikuwa hawana pa kukaa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ituongeze pesa ili iweze kujenga mabweni hata matatu.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa maandalizi mazuri yaliyofanywa na Mheshimiwa Margaret Sitta akisaidiwa na Manaibu wake wawili, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila chini ya Mtendaji wao mahiri Katibu Mkuu Ndg. Prof. Hamisi O. Dihenga na Wasaidizi wake Wakuu wa Wizara. Nimeamua kuchangia kwa maandishi kwa sababu ya msingi, yote yameelezwa vizuri sana ikiwa ni pamoja na majedwali yote muhimu ya elimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninayo maombi kadhaa ambayo nitaiomba Wizara inisaidie, lakini pia kuiomba initolee hofu kwa yale ninayoona yanaweza kuathiri nia nzuri ya Wizara katika malengo yake.

Pamoja na nia nzuri ya kuendeleza Vyuo vya *VETA* katika kila mkoa lakini kuwepo Chuo hicho Wilayani Mpanda, unakifanya kionekane cha wilaya. Makao Makuu ya Mkoa ndiko kwenye msongamano wa vijana wengi, ni mahali ambapo stadi mbalimbali zinahitajika kwa vijana wengi kuendelea kuhudumiwa bila kulazimika kuishi mabwenini mfano wa *VETA* – Chang’ombe inahudumia wengi sababu wanaokwenda hapo hawalazimiki kulala hapo hapo.

Mkoa wa Rukwa hasa mji wake wa Sumbawanga una Chuo cha Ufundi kidogo cha Katandala. Kwanini kwa kuanzia tusikiimarishe Chuo hiki ili kihudumie fani zote muhimu kwa vijana na wananchi wa mji huo mkuu wa mkoa? Ombi ni hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara inisaidie na kulieleweshwa Bunge hili nini azma ya baadaye ya Vyuo hivi vya *VETA*? Je, wazo la kubinafsisha *VETA* limefikia wapi? Wengi wetu bado tunadhani jukumu la *VETA* kwa nchi maskini kama yetu bado ipo pale pale kusaidia vijana wa aina zote na hasa kwa familia maskini waweze kupatiwa utaalumu wa kujitegemea hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la pili ni kuiomba Wizara ipandishe hadhi Chuo chetu cha Ualimu Kantalamba kiweze kutoa pia vyeti vya Ualimu na pia Diploma, pia tuombe Kasima maalumu kwa kuwafundisha walimu kwa ajili ya mahitaji yetu ya Mkoa wa Rukwa. Mzigo tunaendelea nao na kuwapa motisha walimu kwa kuwachangisha wananchi umetuwekea mazingira magumu yenye madeni mengi. Mpaka sasa zaidi ya shilingi milioni 68 zinabaki kama deni kwetu kwa kuendelea kuwahudumia walimu hao. Pamoja na majukumu ya ujenzi wa Shule za Sekondari kila Kata mzigo huu tunaomba Wizara itusaidie kuubeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kupitia Wizara hii kwa fedha tulizoletewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa shule zetu. Kwanza tunaomba Wizara iangalie upya bei za vifaa hivyo mkoa kwa mkoa ili angalau pawepo na *top-up* ya fedha kwa mikoa yenye matatizo ya usafiri pamoja na umbali wake toka Dar es Salaam.

Pili, tunaomba Wizara itoe miongozo ya awamu inayofuata ya ujenzi wa shule za *High Schools* ili angalau kwa mikoa iliyo nyuma kielimu ipewe kipaumbele kwa kuwa na *high school* kwa kila Jimbo. Kazi hii ni budi ikafanyika kwa hali ya ustadi wa hali ya juu na ya uchambuzi wa kina ili nia na madhumuni ya pendekezo hili isilete utata. Yote hii ni katika kutekeleza azma na nia ya Mheshimiwa Rais ya kutaka maeneo na mikoa iliyo nyuma isaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya watu wazima inaonekana kupewa kisogo ukilinganisha na miaka ya nyuma. Hivyo kweli tumefikia viwango kwa kuridhisha kuwa elimu hii siyo muhimu tena? Msingi ulikuwa iwe pia ni elimu ya kujiendeleza kiuchumi. Elimu ilikuwa ikifundisha pia stadi za maisha na kadhalika, nini hatma yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania (*TIE*) ndiyo hivi sasa imeanza rasmi Mkoani Rukwa. Ni kwa misingi hiyo ninaiomba Wizara itoe kila aina ya msaada kuimarisha Ofisi hiyo. Mwakilishi wa ofisi hiyo ameanza vizuri na hivyo anastahili kupewa kila aina ya msaada ikiwa ni pamoja na kupatiwa vifaa vya kazi zikiwemo kompyuta na *photo copying machines*.

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri M. Sitta na timu yake lakini naendelea kumkumbusha Waziri kuwa suala la nidhamu ya walimu athari za UKIMWI na maslahi yao vipewe kipaumbele katika kazi zake za kila siku. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natoa pole kwa ndugu/jamaa wa familia ya Mbunge mwenzetu Amina Chifupa aliyefariki tarehe 26 Juni, mwenyezi Mungu amuweke pahala pema Peponi. *Amina!*

Naipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuwa mahiri katika kuwasilisha hotuba yake ya makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2007/2008.

Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wa ngazi ya Mkoa wa Pwani hadi Kata kwa kuitikia uzito wa Serikali katika ujenzi wa Shule za Sekondari, vilevile kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Pwani kwa kujitokeza kwa wingi kwa hali na mali katika ujenzi wa shule hizo na kuweka Mkoa wa Pwani kuwa katika orodha ya waliofanya vizuri nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kwamba elimu ni ufunguo wa maisha, hivyo ndio maana Serikali imelipa kipaumbele suala la ujenzi wa shule na kuhimiza kila mtoto aende shule. Hili ni suala zuri, lakini swali la kujiuliza ni Je, ni mazingira gani tuliyoaandaa baada ya ujenzi wa shule hizi? Naomba nipatiwe majibu.

Shule zetu nyingi zimejengwa mbali na maeneo ambayo wanaishi watu mfano shule inajengwa umbali wa zaidi ya nyumba za walimu na hata huduma muhimu kama maji na hata chakula kwa wanafunzi. Mwanafunzi analazimika kupanga.

Hapa tunauhakika upi wa usalama wa huyu mwanafunzi mfano anapaswa aamke asubuhi atafute maji, ajipikie na atembeke kwa umbali wa zaidi ya kilomita 15 – 20, akifika amechoka hata uwezo wake wa kufuatilia masomo unakuwa mdogo. Hali kadhalika hata mwali naye ni hivyo hivyo.

Naomba nipatiwe majibu, ni lini angalu kila wilaya itakuwa na shule za mabweni? Mkoa wa Pwani una maeneo ya visiwa na *delta*, ni lini walimu wa maeneo hayo watatengenezewa mazingira mazuri ambayo yatawawezesha kufika mashuleni au kuishi huko bila ya matatizo kama usafiri, nyumba za walimu, maabara na maktaba? Mfano wa maeneo hayo ni Nyamisali baadhi ya Kata za Mafia, Mkuranga na kadhalika. Shule nyingi za Mkoa wa Pwani hazina umeme: Je, ni lini Wizara inafikia kupeleka umeme wa *solar* ili kuweza kuwakomboa wanafunzi na walimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo linachangia mdondoko wa wanafunzi ni wasichana ambao wanapewa ujauzito. Kwa uchungu kabisa naomba Wizara yako ishirikiane na Wizara nyingine ambazo ni Sheria na Katiba, usalama wa Raia na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kuweza kuziangalia tena sheria ambazo zinatoa mianya ya wanaowapa ujauzito wanafunzi wasipewe adhabu kali.

Hii ni kutowatendea haki watoto wa kike na kuwanyima nafasi ya kujiendeleza. Naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kuibua mjadala wa kitaifa ili kuona ni vipi watoto wanaopata ujauzito waweze kurudi shuleni. Hili ni suala zuri na linakubalika hivyo ni vyema mjadala huo uharakishwe na kuweza kuweka mazingira ambayo yatawasaidia wasichana (wanafunzi) wanapojifungua kurudi shuleni, lakini itakuwa bora zaidi kama atarudia kwenye shule nyingine badala ya ile aliyokuwa anasoma.

Kwa kumalizia, naomba nipatiwe jibu, ni lini Wizara nilizozitaja zitakuwa tayari kuanza maandalizi ya kurekebisha sheria ambazo zinatoa mianya za kuwa na adhabu ambazo zitawabana wale wote wanaowapa ujauzito wasichana. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kuipongeza Serikali yetu kwa jitihada za makusudi inazochukuwa kuboresha elimu nchini hasa kwa maelezo yake thabiti yaliyowezesha ujenzi wa Shule za Sekondari nchi nzima na pia mgawo wa fedha katika bajeti ya mwaka huu na fedha 2007/2008 ambapo elimu pekee itapata karibu asilimia 18 ya bajeti nzima unadhihinisha nia thabiti ya Serikali kuboresha elimu na kupambana na adui ujinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za kipekee ziwafikie Rais Jakaya Kikwete na Waziri Mkuu Lowassa kwa kuwa dira thabiti ya kutuonyesha njia ya kupita ili tuweze kufika huko kuliko na neema tele. Nawaombea maisha marefu na afya njema ili waendeleo kutuongoza vyema.

Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri Sitta na wasaidizi wote hasa Naibu Mawaziri wa Elimu - Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Mwananzila kwa jitihada zao za kuboresha elimu nchini na hasa kwa kuweza kuwa kiungo madhubuti kati ya Serikali na wananchi na hivyo kufanikisha ujenzi wa shule nchini. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa nichangie yafuatayo:-

- (a) Kujenga maadili mazuri ili tuweze kuwa na Taifa lenye maadili (*ethics*) mazuri inatupasa tuwalee watoto wetu (wanafunzi) kwa kuwafundisha maadili mazuri. Hivyo naiomba Wizara iangalie uwezekano wa kuongeza somo la maadili (*ethics*) katika mitaala ya elimu kuanzia Darasa la Kwanza. Elimu hii muhimu itasaidia vilevile kufanikisha vita dhidi ya rushwa na hivyo kuwa na jamii inayowajibika kimaadili.
- (b) Mabweni, Vitabu na Maabara. Pamoja na kufanikiwa kujenga madarasa mengi yatupasa sasa tuvipe kipaumbele mabweni ya wasichana na wavulana kwa wale wanaotoka mbali na shule zao; vitabu vya kusomea (*text books*) na maabara ili watoto wetu waweze kupata elimu bora itakayowawezesha kujitegemea ama kukabiliana na changamoto za maisha barabara, lakini kwa vile jamii zetu nyingi ni masikini, naiomba Serikali yetu iangalie uwezekano wa kujenga mabweni maabara katika shule zote.
- (c) Uwiano wa misaada na Wingi wa wanafunzi, tatizo linalojitokeza hivi sasa ni ugawaji wa madawati walimu vyumba vya madaraasa na nyumba za walimu bila kutilia maanani idadi ya wanafunzi walioandikioshwa.

Kwa mfano wakati Mkoa wa Luna uliweza kuandikisha wanafunzi wengi wa Shule za Msingi, ulipata idadi kidogo ya madawati, nyumba za walimu na walimu kuliko baadhi ya mikoa ambayo ilikuwa na idadi ndogo ya wanafunzi. Ugawaji huu kuongeza kero badala ya kutatua. Naiomba Wizara itilie maanani idadi ya wanafunzi walioandikishwa wakati wa mgao wa misaada.

- (d) Kero za Walimu. Walimu bado wanakabiliwa na kero nyingi zinazowakwaza kufanya kazi zao vyema. Baadhi ya kero ni pamoja ucheleweshaji wa mishahara na ucheleweshaji wa kupandishwa madaraja ya kazi. Kero kama hizi huwafanya kupoteza ya kufanya kazi na hivyo kuwakosesha watoto wetu elimu bora itakayowafanya wajitegemee ama kuwa wataalamu na viongozi wetu thabiti na makini hapo baadaye.

Naiomba Wizara kwa kushinikiza na wadau wengine, ibuni mikakati ya kumaliza matatizo hayo.

Naomba kuishia hapa kwa kuipongeza Serikali yetu kwa kazi nzuri inayofanya katika kuwaondolea kero wananchi wetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Waziri - Mheshimiwa Mahiza na Mheshimiwa Mwananzila kwa kazi nzuri yenye tija na ufanisi katika kuendeleza elimu hapa nchini.

Aidha, shukrani za pekee zimwendee Mheshimiwa Mwantumu Mahiza – Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuweza kufika Wilayani Kilindi na kutoa msukumo wa hali ya juu katika masuala mbalimbali ya elimu, ziara ambayo imeibua ari mpya kwa wananchi wa Kilindi na iliyoleta chachu kubwa ya kufufua elimu wilayani humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali katika jalada la kijitabu cha bajeti yako ya mwaka 2007/2008 iko picha inayoonyesha watoto wanaosoma wakiwa na kompyuta kila mmoja: Je, hiyo ni *private school*? Kama ni ya Serikali, ni lini angalau wanafunzi wa Kilindi watapata angalau kompyuta nne (4) kwa shule zote za sekondari na wala siombi kwa kila mmoja. Halmashauri tutachangia gharama za Jenereta.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona wanafunzi wamekuwa wakimaliza masomo ya sayansi bila maabara wala vifaa: Je, hawa wanafunzi wafaulu vipi, kwa mfano Sekondari ya Seuta, Kwediboma na Mkuyu? Aidha, maktaba hakuna kabisa! Kweli Kilindi itaweza kusonga mbele? Wizara naomba mtusaidie, sisi wananchi tuko tayari kuchangia pale tutakapopata msukumo.

Kwa vile tatizo la Kilindi kuwa miongoni mwa wilaya za pembezoni ambazo ziko nyuma kimaendeleo, waalimu hawaendi Kilindi. Tumejitahidi kuweka mazingira ya

kuwavutia ila ni kwa kiwango kidogo sana. Je, Wizara itatusaidiaje? Kwa sababu kwa kipindi hiki bado inabidi tukamilishe madarasa, jengo la utawala na kadhalika.

Kutokana na umbali wa makazi na shule, wanafunzi wanaingia katika mitego ya kupata mimba au kutoroshwa na kasi inaongezeka siku hadi siku. Mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Kilindi naomba Wizara yako ituangalie kwa jicho la huruma ili tuweze kusaidiwa kupata *hostel* wilayani na hivyo kuzuia wingi wa mimba. Elimu ya watu wazima na Vyuo vya Ufundi ni ndoto nzito Kilindi. Japokuwa kuna mipango mliopanga na kuweka vipaumbele, mimi naomba nipatiwe mtaalam ili waweze kutuhamasisha. Naomba sana wataalam waje na kuelimisha wananchi waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kidato cha sita mwaka huu kwa kiwango kikubwa yalisikikitisha sana, lakini lichosikitisha zaidi ni pale ambapo wanafunzi walilipa Sh. 20,000/= kwa ajili ya *appeal* kusahihishia mitihani. Je, kinachosubiriwa ni nini endapo wamechangia Sh. 20,000/= kwa ajili ya kazi hiyo? Mwisho wa kupokea maombi Vyuo Vikuu (*admission*) ni hivi karibuni. Sasa ni nini ambacho kitatuwezesha kuwahi hizo *deadlines*. Naomba ufafanuzi ili hawa waombewe kibali maalum ili waweze kufanya masahihisho na kutoa alama halali. Nashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Margaret Sitta - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Naibu Mawaziri wake, pia Katibu Mkuu na watumishi wenzake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeleta mapinduzi makubwa ya elimu katika kipindi kifupi hasa katika kushirikisha wananchi kila Kata kujenga shule za sekondari. Shule hizi ndizo zitakazokomboa Watanzania kutoka katika Lindi la umaskini. Hivi sasa ni faraja utembeapo nchini kuona shule hizi zipo kila sehemu, yaani zimezagaa kama uyoga. Hongera sana kwa Wizara na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Wizara imejitahidi sana katika kueneza sekondari hizi, bado tuna shida kubwa ya walimu hasa katika shule za kusini mwa nchi na Mikoa mingine ya pembezoni. Katika Mkoa wa Mtwara hali ni mbaya sana hasa katika uwiano wa kati ya walimu waliopangiwa kwenda Mtwara na wale walioripoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna visingizio vingi, mimi naviita visingizio hasa vya mahali pa kuishi. Kuna maeneo mengi walimu wanaonyeshwa sehemu za kuishi lakini hawaingiii katika nyumba hizi kwa sababu zao binafsi. Mpango wa ujenzi wa nyumba za walimu hauwezi kukamilika upesi kwa nchi nzima. Wakati sisi tukijitahidi kuanzisha shule nyingi zaidi, wenzetu walimu nao wavute subira na kuelewa hali halisi tuliyonayo. Hivyo wanahitaji kuwa wavumilivu zaidi ili hatimaye tuweze kufika huko.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwafafanulie vijana wetu hawa wanapokuwa mafunzoni umuhimu wa kuwa na uzalendo hasa hapa mwanzoni. Inawezekana, mradi waweke uvumilivu mbele. Naunga mkono hoja.



**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ianzishe utaratibu wa kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi zote kuliko utaratibu wa hivi sasa wa shule chache kupatiwa huduma hiyo.

Katika Wilaya ya Manyoni, upande mmoja wa Wilaya wanapatiwa chakula (Jimbo la Mashariki) wakati upande mwingine Jimbo la Magharibi hawapatiwi chakula. Hii inaleta manung'uniko yasiyofaa kwa Serikali. Hali hii irekebishwe ili kujenga usawa na pia kuboresha huduma za shule za msingi. Miaka ya 1960 na 1970 tulipata huduma ya chakula/uji bure na kila mwanafunzi alikuwa mwepesi kwenda shule pamoja na mwamko mdogo.

La pili, ni uhaba wa vifaa vya maabara kwenye shule za sekondari. Sekondari nyingi na hasa Mkoa wa Singida na Wilaya ya Manyoni hazina vifaa vya maabara. Kama kweli tunataka kuimarisha michepuo ya sayansi, hatuna budi kuwa na maabara kwa kila shule na vifaa vya kutosha. Nashauri Serikali ijikite kusimamia ujenzi wa maabara na kutoa vifaa kila maabara na vitabu vya sayansi.

La tatu, nashauri Serikali ije na mkakati wa kuanza na mafunzo ya komputa mapema kwa kila shule ya msingi na siyo sekondari tu au vyuo. Nchi ya Rwanda sasa hivi inaongoza kwa taaluma ya *computer technology* kwa nchi zetu za Afrika Mashariki na hata Afrika kwa sababu shule zote za msingi zinafanya mafunzo haya *ICT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kuendeleza mapinduzi ya elimu nchini.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watalaam wote kwa kazi nzuri na utayarishaji wa hotuba nzuri.

Napenda kukumbusha kwamba kuna mapendekezo ya kuanzisha shule ya sekondari ya bweni katika iliyokuwa Kambi ya Wakimbizi Karagw, Kibondo. Mheshimiwa Mwananzila anajua suala hili. Naomba Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ishauriwe *on way forward* ili majengo yaliyopo yatumike.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza shule yenye mabweni, maji ya bomba na ardhi  $\frac{1}{2}$  - 1 *Acre*, ziweke miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation*). Bustani za namna hii zitasaidia mambo wawili:

- (a) Kuwa na eneo linalofaa kufundisha somo la kilimo na elimu ya viumbe (mimea).
- (b) Shule itapata mazao (mboga na matunda) kwa ajili ya wanafunzi wanaohitaji *special diet*.

Gharama za *drip irrigation kit* ni kati ya shilingi milioni mbili na shilingi milioni 3.5 kwa eneo nililolitaja. Nashauri Wizara ya Elimu ishirikiane na Wizara ya kilimo ili *drip kits* nilizotaja ziwekwe katika bustani za Shule na Vyuo.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu wake wote wawili, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri iliyoandaliwa kwa makini na ikawasilishwa vizuri mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipochangia kwenye bajeti kuu, niliomba na kushauri Serikali igawe fedha za MEM na MES kwa kuzingatia gharama na bei za bidhaa kama vile saruji, mabati na kadhalika. Bei za bidhaa hizi zinatofautiana Mkoa hadi Mkoa kiasi kwamba bei ni kubwa sana Mkoa Kagera ukilinganisha na Dar es Salaam na Mikoa iliyo jirani na Dar es Salaam. Je, Mheshimiwa Waziri atazingatia hilo wakati wa kugawa fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu ya kujipongeza. Serikali, Wabunge na wananchi kwa ujumla kwa jinsi ambavyo vimekupa ushirikiano mkubwa katika ujenzi wa shule za msingi na sekondari. Kuhusu shule za sekondari zinahitaji kuboreshwa kwa:

- (a) Kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wanaotoka mbali na shule;
- (b) Uandaliwe mkakati wa makusudi wa kuweka umeme hasa wa *solar* katika shule zote;
- (c) Uwepo mpango wa kukinga maji kwenye majengo ya shule ili yasaidie wanafunzi na walimu baadhi;
- (d) Mpango wa kuzifanya baadhi ya shule kuwa za bweni ili watoto toka Mikoa mbalimbali wachanganyike ili kuimarisha umoja wa kitaifa. Ni muhimu sana;
- (e) Huduma ya chakula cha mchana katika shule za kutwa ni muhimu ili kuhakikisha watoto wanapata afya ya kutosha kufuatilia masomo; na
- (f) Nyumba za walimu ni muhimu sana ili kuwatia moyo walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa chakula cha mchana katika shule za msingi katika baadhi ya Wilaya wanaonekana kuleta maendeleo ya kitaaluma, hivyo ningeshauri utekelezwe kila shule nchi nzima kwa vile wanaboresha afya za watoto na kuwezesha kujifunza vizuri. Kwa hayo mafupi, naunga mkono hoja.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba nzuri sana. Aidha, niipongeze Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri iliyofanyika katika mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kutoa shukrani. Ninaishukuru sana Wizara na hususan Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa kuipatia Wilaya ya Kondoa gari kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi wa Elimu. Ahsante sana. Ni imani yangu kuwa gari hili litasaidia kuboresha elimu Wilayani Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara imekusudia kutoa kipaumbele katika ajira ya walimu, ujenzi wa nyumba za walimu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya elimu ya sekondari. Ninaipongeza sana Wizara kwa uamuzi huo. Ni matumaini yangu kuwa kama utekelezaji utakwenda kama ulivyopangwa matatizo ya upungufu wa walimu, nyumba za walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia yatapungua sana na hivyo kuboresha elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri imezungumzia kuhusu miradi ya mazingira yanayomjali mtoto. Kwa kuwa miradi hii inasaidia sana kuboresha elimu, ninashauri miradi hii ipanuliwe ili Wilaya nyingi zaidi ikiwemo na Wilaya ya Kondoa zishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri katika hotuba yake ameeleza kuwa mwaka huu ametenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli kumi tu kwa nchi nzima. Kwa maoni yangu kiasi hiki ni kidogo sana kwa sababu mahitaji ni makubwa mno. Ninashauri miaka ijayo Wizara itenge angalau hosteli moja kwa kila Wilaya. Aidha, ninaomba Wilaya ya Kondoa katika bajeti hii ifikiriwe na kipaumbele kitolewe kwa Jimbo la Kondoa Kusini kwa sababu ina mazingira magumu sana. Jimbo la Kondoa Kusini sehemu kubwa inakaliwa na jamii za wafugaji na wawindaji ambao huhamahama kufuata malisho na mawindo. Wazazi hufuatana na watoto wao na kusababisha watoto hao kushindwa kufuatilia masomo. Hivyo hosteli ni muhimu kwa watoto wa jamii hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa kushughulikia ajira mbaya ya watoto nchini. Wilaya ya Kondoa ni moja ya Wilaya zinazonufaika na mpango huu. Jimbo la Kondoa Kusini ndilo limenufaika zaidi na mpango huu, hivyo ninaomba Serikali ipokee shukrani za wapiga kura wangu kwa msaada huu. Ombi lao ni kwamba msaada huu wa kuboreshwa ili kuondoa kabisa tatizo la ajira mbaya ya watoto jimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa maabara, wananchi wa Kata za Mondo, Chandama na Kwamtoro wamejenga majengo ya maabara katika shule za Mondo Sekondari, Soya Sekondari na Kwio Sekondari katika mpangilio huu. Pamoja na ujenzi huu, majengo haya hayatumiki kwa sababu hayana vifaa. Kwa heshima zote ninaomba Wizara ikamilishe maabara hizi ili zitumike na kuboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni nyenzo muhimu katika kutoa elimu ngazi ya sekondari. Ninaomba Wizara iangalie uwezekano wa kuzipatia shule zote umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, ninaomba kuunga mkono hotuba ya Waziri.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Karatu wameitikia sana wito wa Taifa wa kujenga shule za sekondari kila kata na kata zote 13 sasa hivi zimejenga shule zao; Wilaya kwa sasa inaendelea na utaratibu wa kujenga sekondari kwenye ngazi ya vijiji vya sasa hivi. Tayari sekondari 12 za vijiji ziko kwenye hatua mbalimbali za ujenzi na kufanya jumla kuwa sekondari 25 za wananchi. Wananchi pia wamejenga mabomu kwa ajili ya maabara katika sekondari hizo hadi kwenye lenta. Sasa je:

- (i) Serikali inatoa kauli gani kuwapa motisha wananchi hao ambao sio tu wameitikia wito wa Serikali, bali wamekwenda mbele kwa kujenga sekondari karibu kila kijiji nusu ya vijiji kati ya 45 sasa vitakuwa na sekondari na hivyo kupunguza adha ya usafiri na malazi kwa wanafunzi? Motisha tunayoomba hapa ni angalau Serikali kuu kuchangia gharama za kupanua maabara kwa kuanzia ya sekondari ya Welwel na Ganako ambazo ziko kwenye maandalizi ya kufikisha *forum* V na VI.
- (ii) Kwa vile sekondari ya Welwel ipo mjini Karatu, naomba Serikali isaidie ujenzi wa hosteli angalau kwa watoto wa kike ili kuweza kuhimili wanafunzi wanaotoka mbali ili kuwaondoa watoto hao kutokana na adha, inayotokana na watoto hao kupangisha kwenye *Ghetto* na hivyo kuhatarisha usalama wao, pamoja na adhabu nyingine.
- (iii) Ni lini sasa Serikali itafanyia marekebisho makubwa sheria inayosimamia Shule za Sekondari ya Ufundi ili kutokana na hamasa waliyopata wananchi na kujenga shule nyingi za wananchi? Halmashauri za Wilaya ziwe na mamlaka kamili ya kusimamia shule za sekondari tofauti na sasa ambapo Halmashauri hazina mamlaka ya kisheria pamoja na utaratibu wa kiutawala wa kuwa na mratibu katika ngazi ya Halmashauri.  
  
Ni tatizo gani linaifanya Wizara kusita kukabidhi mamlaka ya kisheria kwa Halmashauri ikizingatiwa kuwa kwa sasa sekondari za wananchi ni nyingi zaidi kuliko za Serikali moja kwa moja? Hali hii inazifanya Halmashauri kushindwa kusimamia fedha nyingi zinazopelekwa kwenye shule hizo?
- (iv) Ili kuboresha maisha na mazingira ya walimu na hivyo kuboresha utoaji wa elimu katika ngazi ya shule za msingi na sekondari, Serikali ina mpango gani wa muda wa kati na muda mrefu wa kumaliza kabisa

tatizo la nyumba za walimu? Kwa hesabu za haraka haraka kwa utaratibu wa sasa wa kudunduliza mathalan nyumba 1500 zilizopangwa 2007/2008 itachukua miaka 40 kabla hatujatosheleza mahitaji ya nyumba. Elimu haiwezi kuwa bora kama walimu wa shule za msingi na sekondari hawatakuwa na mazingira bora.

Ninapenda mpange mkakati wa kuondoa tatizo hili kuliko kungojea bajeti ya kila mwaka. Natangulisha shukrani.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii kunipa ili nitoe mchango wangu. Kwanza naunga mkono kwa asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Misungwi inaipongeza Wizara ya Elimu kwa juhudi za kupunguza matatizo ya Sekta ya Elimu nchini. Yapo baadhi ya mambo yanayohitaji ufumbuzi.

Kwanza, madai mbalimbali ya walimu yakiwemo kupanda kwa madaraja kati ya 230,000,000 zinakisiwakuwa ni madai yao. Wilayani Misungwi.

Pili, mishahara ya walimu wanaoanza kazi inachelewa, ni nini hasa kinasababisha tatizo hilo? Naomba Bunge lielezwe sababu za msingi za kuchelewesha haki yao.

Tatu, Wilaya yetu bado ina upungufu wa walimu. Naomba Wizara iongeze walimu ili kuifanya Wilaya ikamilishe kazi yake kwa ufanisi. Juhudi za kuboresha elimu katika Wilaya ya Misungwi ni kubwa hadi sasa Wilaya ya Misungwi inazo shule za sekondari 20 na pia ipo shule moja ya sekondari ambayo iko tayari, tatizo ni wanafunzi, walipelekwa shule jirani kutokana na idadi kuwa ndogo, hivyo 2007/2008 itafunguliwa.

Ombi, Serikali/Wizara isaidie ukamilishaji wa jengo la maabara la shule ya sekondari Paul Bomani. Ujenzi huo ulianzishwa na mfadhiri *LIVEMP* ameishia hapo lilipo. Naomba watalaam waje waone mahitaji yanayohitajika wakamilishe ili jengo lianze kutumika, kwa wananchi kuchangia. Naomba sana wasaidiwe kwani kazi walizonazo za uchangiaji ni nyingi.

Tunaoimba pia Serikali itoe msaada wa kukamilisha ukumbi mkubwa wa mikutano ambao utatumika pia kwa chakula cha wanafunzi wa Misungwi sekondari.

Jengo hilo linahitaji kukamilishwa Mfadhili ni *NGO* ya Sakina, wamefikia mwisho wa msaada wao. Ili kuanza kilitumia tunaomba Serikali/Wizara ifike kujionea na kutuunga mkono katika kulikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie elimu maalumu. Naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali ilizotekeleza mwaka 2006/2007. Wilaya ya Misungwi inayo shule ya msingi inayotoa elimu maalumu kwa wasioona na wenye uoni hafifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hii ya Mitindo inahitaji kupanuliwa kwani sasa hivi jamii imeishaanza kuona umuhimu wa kuwaelimisha watu wa aina hiyo. Mwamko huo unapaswa kupokelewa haraka wakati Serikali inaangalia uwezekano wa kuwachanganya na wanafunzi wa kawaida. Shule zilizopo ziimarishwe, pia ni vyema nikaambiwa ni nini kitakachofanyika Mitindo Shule za Msingi ili iwe rahisi kusaidia ufuatiliaji wa utekelezaji. Ni vyema walimu wanaofundisha watu hawa wakaboreshewa masilahi yao ili neno maalumu liendane na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ukaguzi wa shule. Wilaya ya Misungwi ni Wilaya iliyoanzishwa mwaka 1997 bado ina upungufu.

Wilaya haina gari, hivyo ni vigumu kuzunguka shule za msingi ukizingatia jiografia ya Wilaya pia idadi ndogo ya wakaguzi kwa sasa wakaguzi wawili wamehama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anieleze kama nitapata gari katika Wilaya hii na watumishi wa kutosha. Nimechoshwa na kuwa wa mwisho kimkoa katika matokeo ya shule za msingi, hii ni sababu tosha kuwa walimu wa shule ya msingi kwanza ni wachache, pili hawana mtu wa kuwashitua, yaani mkaguzi hafiki katika shule za msingi kutokana na kukosa usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali ione umuhimu wa kunipa/kuniruhusu baadhi ya shule zangu za sekondari tatu ziwe za A- Level kati ya hizo moja iwe kwa watoto wa kike tu. Nazo ni Misungwi Sekondari, Paul Bomani Sekondari watoto wa kike na Misasi Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kumpongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri. Ni imani yangu kati ya yote hayo niliyozungumza kwa niaba ya wanaMisungwi nitapata majibu ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninampongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta kwa hotuba yake nzuri inayoeleweka na ninamwomba Mungu ampatie afya njema ili aweze kusimamia utekelezaji utendaji mzuri katika elimu. Mungu awabariki Naibu Mawaziri wa Elimu na Watendaji wote tukianzia na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuipatia elimu kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2007/2008. Kipekee ninampongeza Waziri Mkuu kwa juhudi za ujenzi wa Madarasa ya Sekondari kila Kata.

Pongezi hizi ziwafikie Wabunge wote kwa ufuatiliaji mzuri, Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Makatibu Tarafa, Katibu Kata na wananchi wote kwa juhudi zao na moyo wa kujitolea walioonyesha.

Mheshimiwa Spika, changamoto. Pamoja na kukamilisha ujenzi wa madarasa ya dharura, madarasa au shule mpya hizo za Sekondari hazina maabara. Kukosekana kwa maabara hayo ni mapungufu makubwa sana kwani wakati wa mitihani ya *Form IV* mambo yatawawia magumu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa vile mtihani wa *Form IV* ni mmoja nchi nzima bila kujali upungufu huo, ninaiomba Serikali iendelee kuongeza muda wa kipaumbele kwa elimu, kwa miaka mingine miwili zaidi ili tuimarishe ujenzi wa maabara na vitu muhimu kwenye shule mpya. Ukosefu wa maabara utatukosesha wahitimu wa sayansi siku za baadaye na hii itafanya Watanzania washindwe kuhimili kwenye soko la ushindani wakati wa ajira na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanapata mimba wakiwa kati ya *Form I* mpaka *Form III* inapotokea wanafunzi wawili yaani wa kiume amempa mimba msichana, yule kijana anaendelea na shule lakini yule msichana anafukuzwa shule moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Umefika wakati sasa tuliangalie jambo hilo kwa upana zaidi na kumtendea haki mwanafunzi wa jinsia ya kike kwani wao ndio wanaobeba lawama.

Mheshimiwa Spika, hapa ninamwomba kila mmoja wetu aangalie balaa lililomsibu binti aliyepata mimba.

- (i) Atafukuzwa shule
- (ii) Anaitwa Malaya
- (iii) Atafukuzwa nyumbani
- (iv) Atakuwa mama bila maandalizi
- (v) Ndoto yake ya kimaisha itazima ghafla
- (vi) Jamii itamnyanyapaa na kumwita kiherehere, yaani hajatulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali iwapatie vijana hawa fursa nyingine tena na kuendelea na masomo baada ya kujifungua lakini kwenye *Special School* na sio hizo za kawaida.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**MHE. MWANAKHAMIS K. SAID:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima wa afya na kunipa uwezo kuchangia katika siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba yake ambayo ameisoma kwa ustadi kabisa.

Pia niwapongeze Manaibu Waziri pamoja na Watendaji wote waliomsaidia Mheshimiwa Waziri kutengeneza hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ustadi wa bajeti hii ya Elimu jinsi ilivyoeleza kila kitu, sina budi kuchangia mchango mdogo tu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika ukurasa 66 katika kitabu chake katika maamuzi muhimu ameeleza kutoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za walimu na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, suala hili utekelezaji wake ni hatua nzuri kwa sababu hiki ni kilio kikubwa kwa walimu na wananchi kwa ujumla na itapunguza walimu kukimbia kimbia katika sehemu wanazopangwa. Pia kuwapunguzia mzigo mzito unaowakabili wazazi kuhangaika kutafuta vifaa vya kusomeshea watoto wao.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa hili ni kwamba nyumba zinazojengwa zijengwe kwa uwiano katika vijiji vyote bila kubagua, kwani huko ndiko kwenye matatizo zaidi. Pia vifaa vitakavyonunuliwa naomba kipaumbele kiwe vijijini ndiko kwenye shida kubwa sana kwa sababu Mzee anaweza kuwa na fedha za kununulia vifaa, lakini vifaa upatikanaji wake ikawa shida.

Mheshimiwa Spika, kwa mchango wangu huo mdogo naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. BINLITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi nazitoa kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo kwa kazi nzuri aliyofanya yeye na Manaibu wake hasa kuongeza idadi ya watoto kwenda Kidato cha Kwanza.

Naomba kupewa maelezo kuhusu kutokuwepo Mkakati wa kuendeleza michepuo katika Sekondari hususan ufundi. Serikali katika hotuba yake mwaka jana ilieleza dhamira yake kubwa ya kurejesha michepuo sekondari iliyofutwa awamu ya tatu.

Lakini cha ajabu, kitabu kizima cha hotuba ya Waziri mwaka huu hakuna kabisa Mkakati wa Elimu ya Ufundi Sekondari. Mikakati iliyopo ni ya ufundi stadi katika ngazi ya *VETA*. Kwa hiyo, naomba Waziri wakati wa kuhitimisha hoja aseme kuhusu kutokuwepo mikakati hii katika Shule za Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu chote hakijaainisha waziwazi mikakati ya Wizara ya kuboresha maabara za masomo ya Sayansi kama vile Fizikia, Kemia, Biolojia katika ngazi ya Kidato cha Nne. Hakuna mikakati ya wazi ya kuongeza Shule za Sekondari zenye Mikondo ya Sayansi.

Zamani kulikuwa na Chuo cha Walimu wa Ufundi Kleruu na wale wa Sayansi Mkwawa, Wizara katika hotuba yake hawaonyeshi Mikakati ya kuboresha sekta hii. Kwa hiyo, naomba Serikali iwaeleze wananchi dhamira yake ya kuongeza idadi ya watoto katika mikondo ya Sayansi pamoja na kuboresha au kujenga maabara na vifaa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa MMES umesaidia sana kuongeza idadi ya Sekondari nchini, lakini toka mpango huu uanze hawajawahi kuweka mahesabu ya



matumizi waziwazi. Ni vizuri Serikali itoe maelezo kwamba ni lini itaweka wazi mahesabu ya MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwavutia watoto wengi kujiunga na Vyuo vya *VETA*, ni vyema mitaala ya *VETA* (Stadi za *VETA*) ikawa na masomo kama Hisabati, Fizikia na Kiingereza. Masomo haya yatawawezesha kuwa na sifa za kuingia katika Vyuo vya Ufundi, yaani *Technical Colleges*. Kwa sasa vijana wengi wa *VETA* hawapati nafasi hizi na hivyo kufanya wazazi wengi kutopenda kupeleka watoto katika Vyuo vya *VETA* kwa kuwa vinakosa *Vertical Progression*.

Mkakati wa kuongeza idadi ya wanafunzi kuingia Kidato cha Kwanza uende sanjari na mkakati wa kuongeza idadi ya walimu, maabara, madarasa na kadhalika. Kama *ratio* ya Mwalimu kwa wanafunzi haijafikiwa, basi ni vyema tukaongeza nguvu na juhudi zaidi kwa upande ule ambao kuna mapungufu kama walimu kwa hali ya sasa.

Muundo wa Utawala wa *VETA* katika Wizara ujitegemee, kuwe na Kurugenzi ya *VETA* badala ya kuwa Idara. Hii itotoa nafasi ya *VETA* kutekeleza majukumu yake vizuri na kwa kasi zaidi.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi yao nzuri waliyoifanya ya maandalizi ya bajeti hii ambayo kwa uhakika inawakilisha vyema na kwa uwazi utendaji na malengo yake iliyojipangia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ndio mratibu mkuu wa shughuli zote zinazohusu elimu nchini zikiwemo na zile shule za binafsi, ninaishauri Serikali isimamie kwa ukaribu suala zima la mitaala itolewayo na shule hizo za binafsi ili ziende sambamba na zile za Wizara. Aidha, Wizara pia haina budi kuwa mratibu wa karibu wa shule hizo kwa suala zima la malipo ya ada yanayolipwa ambayo kwa kweli hutofautiana kati ya shule moja hadi nyingine na tena kwa kiwango cha juu.

Gharama hizi za juu huwavunja moyo sana wazazi wa watoto wanasoma kwenye shule hizo na wakati mwingine hushindwa kuwaendeleza kutokana na kupanda kwa holela kwa ada kwenye shule hizo bila ya Serikali kuingilia kati.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ujenzi wa Shule za Sekondari nyingi kwa kila Kata na mikakati ya MMES, ni dhahiri kuwa kutakuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi watakaofaulu Kidato cha Nne ambao watahitaji nafasi za masomo ya Kidato cha Tano na Sita baada ya miaka michache ijayo. Hivyo ni vyema Serikali ikaanza maandalizi mapema ya kujenga Shule za Sekondari kwa ajili ya Kidato cha Tano na Sita angalau mbili kwa kila jambo badala ya kusubiri muda ufike ndipo Serikali ianze ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, katika Shule za Sekondari zinazojengwa kila Kata, ni vyema itengwe shule moja kila Wilaya kama sio Jimbo ambayo ni maalum kwa watoto wenye

ulemavu tu badala ya kuwachanganya na wanafunzi wasiokuwa walemavu kama utaratibu ulivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mtindo wa baadhi ya wafanya biashara kuchapisha vitabu kwa ajili ya Shule za Msingi na Sekondari kiholela. Ni vyema Serikali ikawachagua wakala wachache watakaosambaza au kuuza vitabu hivyo ambavyo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itakuwa imevihakiki na kuviruhusu rasmi kutumika shuleni.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la muda mrefu sana la uvujaji na ugushi wa mitihani ya Taifa kwa watahiniwa ambapo baadhi ya walimu hushiriki kwa kiwango fulani kwa tamaa za binafsi. Aidha, kuna mtindo wa baadhi ya wananchi wa kuchapisha mitihani isiyo rasmi (*fake-examination papers*) hasa ile ya Kidato cha Nne (*Form IV*) na kuuzwa mitaani kwa wanafunzi watarajia watahiniwa ambapo wengi wao huzamia zaidi kwenye *papers* hizo na hata kusitisha masomo kwa muda wakisubiri kufanya mitihani tu.

Kwa kawaida *papers* hizo huuzwa muda wa mitihani ya Taifa inapokaribia. Ni vyema Serikali ikalifuatilia suala hili kwa ukaribu kwani linashusha na kupotosha elimu kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Elimu ya Ufundi kwa kila Wilaya ni jambo la kupongezwa sana. Hata hivyo wasiwasi wangu ni upatikanaji wa zana za ufundishaji ambavyo vingi hugharimu fedha nyingi. Elimu hii isiwe ya nadharia tu bali kwa asilimia kubwa iwe ni ya vitendo na ikiwezekana wahitimu wanapomaliza mafunzo hayo wapewe na vifaa kwa ajili ya kuanzisha miradi yao ili kukidhi malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mafao kwa walimu ni muhimu sana kwani bila motisha walimu wengi wataendelea kuishi katika maisha magumu na hatimaye hali ikizidi kuwa ngumu wanaweza kuacha kazi na hivyo Serikali kuendelea kubaki na uhaba wa mara kwa mara wa walimu katika shule zake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa asilimia zote.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi inatambua kuwa rasilimali watu ndio nyenzo kuu ya maendeleo yote ya nchi. Watu walioelimika na wenye afya ndio chombo na lengo la harakati za kukuza uchumi na kuutokomeza umaskini. Ndiyo maana katika harakati za Taifa za kuondokana na uchumi ulio nyuma na tegemezi suala la elimu bora ya aina na fani zote na la huduma bora za afya kwa wananchi wetu linapewa umuhimu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika katika kila Tarafa na Kata kuwa na Shule ya Sekondari, kweli Serikali imetambua Ilani na kufanya kazi nzuri sana. Hata mtoto akizaliwa anaanza kutambaa ndio anatembea kwa muda mfupi Serikali imejenga mashule na inaendelea kujenga na kuboresha vifaa pia. Niwahakikishie wafadhili wetu wanaowekeza katika elimu nchini kuwa Serikali imelisimamia vizuri sana jambo hili.

Mheshimiwa Spika, uandikishaji wa watoto wa shule, lengo la Ilani ni asilimia 100. Katika hili Serikali imeondoa ada, vyema. Lakini bado kuna maeneo hawapeleki watoto shule. Maeneo hayo yatazamwe maeneo ya wachungaji.

Natoa ushauri kwamba kila kijiji kiwe na rejista ya kuandika watoto wanaozaliwa katika kijiji husika, ni rejista ile itasaidia kujua baada ya miaka sita wanatarajia watoto wangapi wataingia darasa la kwanza. Suala la takwimu ni muhimu sana ili wale ambao watakuwa hawajaingia kuangalia sababu zilizopelekea hilo kwa mfano ni kuhama na sababu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni haki ya kila mtoto. Sisi wananchi wa Iringa tunashukuru sana kwani Mkoa wa Iringa tulikuwa tunatoa sana watoto wa kazi majumbani na baada ya Serikali kufuta ada mimi Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, Makete, Njombe, Mufindi, Iringa na Kilolo nawatangazia kuwa watoto wetu wote tunawapeleka shule, hivyo hatuna watoto wa kufanya kazi za ndani. Wanaotaka wapo waliosoma *VETA, house-keeping* na tunaomba Serikali ipange mishahara ya watoto wasomi (wataalamu) wa kutunza nyumba na watoto mishahara yao. Maana wengi wanafanya kazi bila mikataba na mishahara inayofaa.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi imesemwa kuongeza idadi ya wanafunzi watakaoundelea na Elimu ya Sekondari kufikia asilimia 50 ya watahiniwa darasa la saba. Sababu za watoto kutoendelea na Elimu ya Sekondari ni kadhaa ikiwa ni pamoja na utovu wa nidhamu, mimba kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, “elimu ni hati ya binadamu.” Nimeshuhudia watoto wakifukuzwa shule kwa utovu wa nidhamu kwa mfano kuondoka bila kuaga shuleni. Kosa kwa mfano hili mtoto ananyang’anywa haki ya elimu lingeangaliwa (*Secondary Schools*).

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mimba (ujauzito). Watoto wa kike bila shaka Mheshimiwa Waziri atatolea maelezo. Tunaiomba shule ziwe na Vitengo maalum vya *Discipline* suala la Nidhamu (maadili) ni taaluma tuwasaidie watoto wamalize shule kwani rasilimali watu wenye elimu ndio nyenzo kuu ya maendeleo. Kuwafukuza shule ni tatizo zaidi, Sekondari ziwe na walimu wa *Discipline*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya kazi nzuri sana ya kuelimisha walimu pia wa Sekondari na wa Msingi.

Mheshimiwa Spika, aidha vipo vyuo ambavyo ni muhimu, Serikali iangalie jinsi ya ku-*upgrade* viweze kutoa *Diploma* badala ya *Certificates* ikiwa ni pamoja na Chuo cha Ualimu Tandala kuki-*upgrade* kilichopo Makete Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado shule nyingi na Vyuo vya Walimu havina umeme ipo haja ya Wizara kuweka mikakati kabambe kwenye Taasisi za Elimu zote nchini kuziwekea umeme. Kuna umeme wa *solar*, tukianzisha na Mchuchuma katika bajeti hii kwa mfano tulivyokubaliana itasaidia sana.

Hivyo Wizara iweke mikakati kabambe mapema, kwani sisi Wabunge huwa tunachangia *computer, Dish TV* lakini shule unakuta nyingi bado hazina umeme. Serikali ilianganilie hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuongeza kasi ya upanuzi wa mafunzo ya ufundi stadi, kuanzisha vyuo vya *VETA* angalau kila Wilaya kimoja. Wilaya ya Ludewa, Makete, Njombe hazina vyuo hivyo muhimu. Ninaomba sana Serikali ianzishe vyuo hivyo mapema hasa Wilaya ya Ludewa iliyoko pembezoni sana. Ni imani yangu kuwa ifikapo mwaka 2008 Serikali itaweka Chuo cha Ufundi/*VETA* Ludewa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya imekwishafanya maandalizi ya awali ikiwa ni pamoja na kuandaa kiwanja kikubwa na naomba Mheshimiwa Waziri afike kuona jitihada hizo za wananchi wa Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza hasa kwa maandalizi mazuri sana ya hotuba nzuri. Naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kunijaalia na kupata fursa hii kwa siku ya leo kuchangia kwa maandishi hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa bajeti ya mwaka 2007/2008.

Aidha, nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mama Margareth Sitta. Nampongeza Waziri kwa umahiri wake, umakini wake, usikivu wake, ushirikiano wake na jinsi anavyoweza kuishughulikia Wizara na hata kuwa na utayari muda wote kutenda kwa vitendo na kuona sekta yetu nyeti ya elimu inashika hatamu nchini mwetu Tanzania.

Nichukue nafasi hii pia nitoe pongezi kwa Manaibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa karibu na Waziri na kufanikisha malengo ya milenia yale yanayosisitiza juu ya kuondokana na ujinga ikiwa ni kuhakikisha kila mtoto anayefikia umri wa kwenda shule lazima aende kupata elimu ili kuondoa ujinga.

Mwisho, niwapongeze watendaji wote wa Wizara kuwa dhamira yao ya kutenda kazi na hata kufanikisha matarajio tunayokusudia Watanzania juu ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni ufunguo wa maisha. Maneno haya yana eneo kubwa sana. Tunaposema elimu ni ufunguo wa maisha, tuna maana kwamba kila aelimikaye ni sharti kwamba atakuwa na uelewa wa mambo yote yaliyo muhimu yanayohusu maisha. Aelimikaye atakuwa na uelewa na kuona umuhimu wa kufanya kazi, kupinga ubora wa maisha yake, atapiga vita maradhi na atajishughulikisha katika kujiondolea umaskini wa kipato chake na familia yake na hata jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani kwa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete - Makamu wake Dr. Ali Mohamed Shein na Kamanda Mtendaji,

Waziri Mkuu - Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kukubali na kutoa kipaumbele na kufanya sekta hii ya elimu kuwa namba moja katika bajeti ya mwaka huu ya Taifa mwaka 2007/2008 na kutenga kiasi cha trilioni 1.086 sawa na asilimia 18 ya bajeti ya Taifa. Hili ni wazo zuri.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Serikali inayo makusudi mazuri kabisa na sote yatupasa kuunga mkono juu ya juhudi ya Serikali yetu katika kuiendeleza sekta hii muhimu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze wananchi wa Jimboni kwangu Iramba Magharibi, kwa kuwa na moyo wa kujitolea na kusikiliza miongozo ya Serikali yetu, wameitikia mipango yote muhimu ya kuboresha elimu, Mpango wa MMEM na hivi sasa MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iramba Magharibi mwaka 2006 tulikuwa na shule nne za Sekondari zile za Ndago, Shelui, Kisasa na Lulumba achilia mbali ile shule ya Kitaifa ya Tumaru.

Mheshimiwa Spika, Iramba Magharibi hadi hivi ninavyowasilisha taarifa hii tayari tunazo Shule za Sekondari zipatazo 18 zinazofanya kazi. Achilia mbali Kata za Kaselya, Ndago, Shelui, Kiomboi, Kisitiri na Ulemo ambazo zinaongeza Sekondari ya pili hivyo kufanya jumla ya Sekondari ni 24. Kwa kipindi cha miaka miwili hii ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya ya awali, naomba sasa nichangie yafuatayo kama kipaumbele na kuyatilia maanani kwa kuboresha zaidi elimu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kazi nzuri ya kujenga hizi Shule za Sekondari kila Kata, naiomba Wizara katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha itilie mkazo juu ya kuwapeleka walimu katika shule hizi mpya za Sekondari. Kazi iliyofanywa na wananchi ni vizuri sana kwa ushirikiano wa Serikali, sasa Wizara ihakikishe walimu wanapatikana. Tusipofanya hilo, basi shule hizi zitakuwa hazina maana yeyote na nguvu kazi nyingi itapotea bure.

Malipo na marupurupu mengine muhimu kwa walimu yatolewe kama motisha itakayowafanya wavutiwe zaidi kufanya kazi hii ya ualimu kwa Mamlaka ya Serikali Kuu na kuondokana na dhana ya kukimbilia sekta binafsi ambako hufikiri kwa maslahi zaidi kuliko Serikalini.

Wizara ihakikishe inakamilisha miundombinu muhimu katika shule hizi nyingi, kama vile vifaa vya kufundishia, ujenzi wa maabara (*laboratory*) nyumba za walimu, vyombo vya usafiri, ujenzi wa mabweni – kadhalika shule zenye ukaribu na umeme zipatiwe huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia elimu ya VVU (UKIMWI) itolewe kuanzia ngazi ya Shule ya Msingi hadi Sekondari.

Pia kuwadhibiti walimu, watoto na wale wezi wa fedha za elimu wachukuliwe hatua kali pale zinapotokea dalili zinazoonyesha kukiuka maadili ya kazi yao hii ni pamoja na walimu wanaofanya mapenzi na wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, elimu ya Ufundi, wanafunzi wenye vipaji vya ufundi wawe *Identified* toka Elimu ya Msingi na Wizara iwe na taarifa vipaji vyao viendelezwe kwa maslahi ya kuondoa usumbufu wa ajira mara wanapomaliza masomo yao.

Wizara ione umuhimu wa kufaulisha wanafunzi walimu ambao wataingia Sekondari huku wakichukua mafunzo ya Ualimu. Hii tutakuwa na kitu kiitwacho “*Teachers Resource Centre*” idadi ya wanafunzi/walimu itategemea mahitaji ya Kitaifa badala ya kutegemea wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne na baadaye kujiunga na Vyu vya Elimu.

Pamoja na maoni yangu na ushauri kwa Wizara, Mheshimiwa Waziri naomba atupe muhtasari wa yale malengo ya Wizara ya mwaka 2006/2007.

- (a) Utekelezaji wa utafiti juu ya maendeleo ya taaluma ya uongozi, mwenendo wa mdondoko (*drop-out*) wawanafunzi wa Msingi na Sekondari;
- (b) Utekelezaji wa Ukarabati baadhi ya Sekondari na Vyu vya Elimu. Nataka nifahamu kuhusu Sekondari ya Tumaini na Chuo cha Elimu Kinampanda;
- (c) Vipi kuhusu utekelezaji wa dhana ya utunzaji wa majengo na mazingira ya Wakuu wa Shule na Vyu vya Elimu? Je, Wilayani Iramba au Mkoa wa Singida utekelezaji ulikuwa wapi?
- (d) Utekelezaji wa walimu 1200 wa Shule za Msingi juu ya elimu ya UKIMWI. Je, Iramba Magharibi imepewa walimu wangapi? Pamoja na idadi ya vitabu vya UKIMWI vilivyotolewa Jimbo la Iramba Magharibi.

Nimalizie kwa kutoa angalizo kwa Wizara juu ya kusajili, Shule za Binafsi zile za Msingi na Sekondari, Wizara iwe makini sana kwa hizi shule zinazoibuka ghafla namna zitakavyoweza kukidhi yale malengo muhimu ya elimu Kitaifa na lazima shule hizi zifuate mitaala ya Taifa na sio kuibua kama wanavyodhani wao.

Pia Wizara ihakiki viwango vya ada zao za mwaka na namna ya mishahara wanayolipa kwa walimu hii itatunza maadili ya elimu (Pamoja na kwamba hivi sasa ni soko huria) katika elimu lazima maadili Kitaifa yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. Naipongeza sana Wizara na Serikali kwa ujumla kwa dhamira njema ya kutoa

kipaumbele kwa Sekta ya Elimu. Matunda ya MEM na MMES ni ushahidi wa dhamira hiyo njema.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2006/2007 niliomba nifahamishwe ni lini ujenzi wa Chuo cha *VETA* Mkoani Lindi ungeanza? Hadi leo hakuna jibu na eneo lililotengwa pale Mitwero, Lindi limebakia kujengewa uzio tu ambao nao waya za seng'enge zimeanza kutafunwa na chumvi. Kwetu sisi Wabunge kukaa kimya bila ya kutoa maelezo yoyote kwani tunakuwa hatuna majibu wala maelezo ya kuwapa wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitapenda wakati wa majumuisho yake Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ya kina kuhusu mosi; ni lini ujenzi huu utaanza? Tunayahitaji maelezo haya kwa sababu kwanza Chuo hiki ni haki yetu sisi kama sehemu ya Watanzania na pili hii ni ahadi ya Serikali tangu awamu ya tatu.

Hatuna sababu ya kuifikisha Serikali ya CCM katika hatua ya kuonekana kuwa inatoa ahadi hewa. Vyama vya Siasa Mkoani Lindi vimeligeuza suala hili kuwa mtaji wa kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuongezeka kwa idadi za shule za msingi na wanafunzi wanaosajiliwa hapana shaka kuwa idadi ya walimu nayo inahitaji kuongezeka kwa kasi kubwa.

Kwa minajili hii, naomba kutoa rai kwa Serikali kuwa mafunzo ya ualimu yasitowe karo. Kwa rai hii siyo tu matatizo ya uhaba wa walimu yatapungua bali tatizo la ajira kwa watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwalipia karo ya mafunzo ya ualimu nao litapungua.

Mwisho napenda kuiomba Wizara hii iwaunge mkono wananchi wa Kata za Mchinga na Milola katika ujenzi wa Maabara katika Sekondari za Kata hizo mbili. Tayari katika mpango wa MMES, wananchi wa Kata hizi za Mchinga na Milola wameshajenga madarasa mengi, vyoo vya kutosha na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie mchango wangu kwa kumhakikishia Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa kutoka kwangu binafsi na kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Mchinga katika mipango ya MEM na MMES.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu kwa kukamilisha azma ya ukuzaji wa elimu nchini.

Napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Naibu Mawaziri wote wawili pamoja na Makatibu na Wataalam

wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Mkoa wa Ruvuma una Chuo cha Matogoro ambacho hapo awali kilikuwa kinatoa Diploma ya Uwalimu (*GRDA*) kwa sasa kinafundisha tu walimu wa Diploma ya Juu. Chuo hicho kina uwezo wa kutosha kubeba walimu wa tabaka zote mbili, matokeo yake kwa sasa baadhi ya majengo ya Chuo hicho yameazimwa kuingiza watoto wa *primary school*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijana wengi ambao wanahitimu sekondari na wana pointi 27 kushukua chini ambao wangeweza kusoma na kufundisha katika maeneo yale ambayo Walimu kutoka mbali hawataki kwenda. Naomba Chuo hicho tafadhali kirudishwe na kuweza kutoa pia Diploma ya kawaida. Hayo ni maombi ambayo yalitolewa na akinamama wa Ruvuma wakati wa mkutano.

Kuhusu watoto wa kike, utaratibu uandaliwe kwa kuwa na shule maalum za kuwapa elimu ya sekondari wale waliopata mimba shuleni. Mitaala ya shule iangalie jinsi ya kuweka somo la *values* ambalo litasaidia kumpa tena mtoto nafasi ya kujifunza kuhusu maisha yake ili kuepuka vitendo vingine vyenye athari mbele yake ili aweze kutambua nafasi yake katika jamii kuepuka *violence* na kadhalika pamoja na kukuza tabia ya ujasiriamali.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa pongezi za dharti kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wengine wote wa Wizara hiyo na taasisi zake kwa hotuba nzuri sana, kazi nzuri na mafanikio makubwa yaliyopatikana pamoja na mwelekeo thabiti uliozingatia kero na changamoto halisi na kujielekeza kwenye ufumbuzi wa takribani kero zote.

Aidha, napenda kumpongeza kiongozi wetu Mkuu, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutoa kipaumbele kwa sekta hii na kusimama kidete katika kutoa kipaumbele kwa sekta hii na kusimama kidete katika kutoa msukumo na ufuatiliaji madhubuti uliowezesha kupata mafanikio makubwa katika ujenzi wa madarasa, ofisi na nyumba za walimu takribani kata zote nchini. Msukumo wao huo umehamasisha ushirikiano, mshikamano na wivu wa ushindani miongoni mwa viongozi na wananchi katika ngazi zote; hivyo kuleta mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango iliyobuniwa katika hotuba ya Waziri inaleta faraja kubwa na matumaini mapya, ujenzi wa madarasa mapya, nyumba za walimu, maabara, mabweni pamoja na mikakati ya kuongeza idadi na ubora wa walimu na vitendea kazi, ndiyo njia sahihi ya kuelekea kwenye mafanikio yanayotarajiwa. Vilevile dhamana ya kuboresha mitaala, kurejesha michezo mashuleni na kuimarisha nidhamu kwa walimu na wanafunzi kutachangia katika kuleta mafanikio zaidi. Hata hivyo ningependa kushauri kwamba uboreshaji wa mitaala uambatane na masuala makuu mawili. La kwanza ni kujenga uzalendo kwa ujana wetu kuanzia elimu ya awali, elimu ya msingi, sekondari hadi elimu ya juu.

Pili, nashauri elimu yetu ilenge kwenye kujitegemea. Sehemu kubwa ya elimu iwe kwa vitendo na yenye shabaha ya kujenga misingi mizuri kwa utaratibu wa fani



mbalimbali. Muhimu zaidi ni kujenga Wajasiliamali na vijana wenye kujiamini hasa kwa kuzingatia utandawazi.

Zaidi ya kuboresha mitaala, ipo haja za kuboresha mazingira na motisha. Miundombinu muhimu ni pamoja na umeme uwe wa *grid*, *diesel*, jua, upepo au *biogas*, maji safi na salama, barabara za kuaminika, huduma za afya na huduma za mawasiliano kwa walimu. Motisha muhimu ni pamoja na kupata mishahara yao na kupandishwa daraja bila usumbufu bali kwa uwazi na vigezo rasmi. Mashindano ya aina mbalimbali pamoja na zawadi kwa wanaofanya vizuri na adhabu kwa wanaovurunda ni miongoni mwa matosha muhimu.

Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkingi, ningependa kuishukuru sana Serikali kwa jinsi ilivyoshikamana na wananchi katika kuboresha Elimu ya Msingi na hasa Elimu ya Sekondari Wilayani Mkinga. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana na mwelekeo wa Bajeti ya Wizara, itapata maendeleo ya kasi kubwa zaidi. Zaidi ya hayo ya juu kwa jumla, Wilaya ya Mkinga ina uhaba sana wa elimu. Mpaka sasa haina shule ya sekondari maalum ya Serikali.

Ni matumaini yetu makubwa kwamba kwa kuzingatia ukame huo wa Wilaya hii changa iliyo pembezoni, jirani na Kenya, itapewa kipaumbele maalum ili iweze kusonga mbele kwa kasi kubwa sio tu kwa kulingana na Wilaya nyingi zilizoendelea, bali pia kuwa kioo cha nchi kule mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika naamini kwamba wananchi wa Mkinga chini ya uongozi wa Mkuu wa Wilaya shupavu na makini pamoja na viongozi wengine, tuko tayari kutoa ushirikiano wetu kamili katika kupokea sera, mipango na miongozo ya Wizara hii katika kufanikisha mapinduzi ya elimu kama sekta ya kipaumbele cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkonoo hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margareth Sitta, Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mwantum Mahiza, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Watendaji wengine wote walioshiriki katika kuandaa hotuba ya Bajeti hii kwa umahiri mkubwa. Ni hotuba ya kina hasa katika kuonyesha mikakati mikubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, sanjari na pongezi hizo kwa Wizara, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Singida Ndugu Parseko Kone kwa umahiri wake katika kusimamia shughuli za miradi mbalimbali ya maendeleo Mkoani Singida hususan miradi ya Elimu. Kwa kipindi cha mwaka mmoja aliokaa Singida ameweza kufanikisha ujenzi wa shule 70 za Sekondari akisaidiana na wananchi wa Singida. Juhudi zake kubwa zimeufanya Mkoa wetu kuwa na jumla ya shule za sekondari 103. Ikiwa ni shule 31 zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi katika awamu mbili za

Serikali zilizopita shule mbili zilitaifishwa na Serikali kutoka kwa wa misionari shule ya sekondari Mwenge na Tumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi kubwa aliyofanya Mkuu wa Mkoa wa Singida Ndugu Parseko Kone, napenda kuishawishi Serikali itambue juhudi zake kwa kumpongeza hadharani ili kumtia moyo na kumwongezea juhudi ya kazi. Baada ya pongezi hizi napenda nianze kutoa mchango wangu kuhusiana na bajeti hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya asilimia 50 ya watumishi wa umma nchini ni walimu japokuwa mpaka kufikia hivi hawana uhakika na mwajiri wao kuwa ni yupi kati ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Waziri ya Fedha. Jambo hili limeongeza urasimu mkubwa katika utekelezaji au utatuzi wa matatizo mengi sana ya walimu.

Kwa kuwa ni muda mrefu sana tangu tatizo hili lilipofikishwa Serikalini na Chama cha Walimu (*CWT*), nafikiri sasa itakuwa ni wakati muafaka kwamba Serikali itamke rasmi ni chombo kipi kimoja kitakachokuwa kinashughulikia matatizo ya Walimu kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu ni kwamba endapo Serikali itatekeleza ushauri huu ari, nguvu na kasi ya walimu wetu katika kutekeleza wajibu wao vitaongezeka zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa muda mrefu sasa ambapo pamoja na juhudi ambazo walimu wetu wamekuwa wakizifanya kujiendeleza kielimu, wengi wamekuwa wakifanya kazi na kulipwa mishahara kwa ngazi ama madaraja ambayo siyo stahili yao. Yaani madaraja ya chini kuliko wanavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zoezi la upandishaji vyeo au madaraja kwa walimu wetu lilisitishwa kwa nia njema, ni vyema basi Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake akatambua hadi sasa. Ni Walimu wangapi wamekwishawekwa katika madaraja wasiyostahili baada ya *OPRAS*? Ni jitihada gani Wizara inafanya kurekebisha mfumo wa *OPRAS* ili uendane na kazi ya Ualimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwezi Januari, 2007, Serikali imekuwa na zoezi la kuhakiki madeni ya walimu wote ili kubaini madeni halali yanayostahili kwa Walimu. Kwa kuwa zoezi hili limekamilika, naishauri Serikali itamke ni kiasi gani cha fedha kinachodaiwa na walimu? Itamke ni lini fedha hizo zitalipwa kwa walimu? Na itamke mkakati au iunde mkakati maalum wa kuzuia malimbikizo ya madai ya walimu ili yasijirudie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika natambua vyema uwezo mdogo wa kifedha unaoikabili Serikali yetu kiasi kwamba ni vigumu kutekeleza kila jambo linalohitajika katika elimu yetu kwa wakati mmoja. Hata hivyo, ninaishauri Serikali yetu kutenga shule zetu katika mchepuo, yaani ziwepo shule za mchepuo wa masomo ya sanaa na masomo ya Sayansi

na mtihani wa Kidato cha Pili uwe kigezo cha kuwapata wanafunzi wanaostahili kuingia katika kila mchepuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu ukitekelezwa katika kipindi hiki cha mpito utaisaidia Serikali kujenga Maabara chache kwa shule za mchepuo wa sayansi, kwani natambua kuwa kujenga maabara moja tu ya sayansi ni sawa na kujenga shule za sekondari tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu ni kwamba endapo Serikali haitachukua jitihada za makusudi na za haraka katika kujenga maabara hizo upo uwezekano mkubwa kwa Taifa letu, siku za usoni, kukosa kabisa wataalam wa mambo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ushahidi wa wazi kabisa kwamba katika shule zetu nyingi hasa hizi tunazozijenga na zile zilizotangulia upo upungufu mkubwa wa walimu wa kufundisha masomo ya sayansi na hesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ninaishauri Serikali kutafuta walimu wa masomo hayo hata ikiwezekana kutoka nje ya nchi ili watusaidie kuzalisha wataalam wa fani hizo nchini kwetu. Wataalam hao wapelekwe kwenye shule za Sekondari na vyuo vya walimu. Natumaini kuwa endapo utaratibu huu utatekelezwa, shule zetu zitatoa taaluma inayostahili katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa za Serikali kujenga shule za Sekondari hadi vijijini, bado inakabiliwa na tatizo la walimu walio wengi kutokuwa tayari kwenda kufundisha katika shule zilizoko vijijini kwa madai kuwa shule hizo ziko mbali na hazina barabara, hazina nyumba nzuri za kuishi, hazina huduma za afya, hakuna maji safi na salama wala huduma za benki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili walimu wetu waweze japo kukabiliana na mazingira hayo magumu, naishauri Serikali iwe inawapatia motisha fedha ya kukabiliana na mazingira magumu, wakati Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali ionyeshe kwa dhati na vitendo kwamba imedhamiria kuinua kiwango cha michezo nchini kwa kurudisha shughuli za michezo na mashindano ya aina mbalimbali ya michezo hiyo katika shule za msingi, sekondari na vyuo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Margareth Sitta na Manaibu Waziri Mheshimiwa Mwantum Mahiza na Mheshimiwa Ludovic Mwananzila kwa maandalizi mazuri ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Ufundi na kufanya Serikali na Wabunge kuipa kipaumbele bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu wa Wizara uliopewa katika bajeti ya mwaka 2007/2008 naomba pia usimamizi mzuri wa *allocation* ya vipaumbele vilivyopelekea Serikali nasi Wabunge kuipa Wizara ridhaa ya kupata asilimia 18 ya bajeti nzima ya Serikali upewe umuhimu wa kipekee ili zisitumike *formula* nyingine na kusahau maeneo yaliyo nyuma na yanayokusudiwa kuinuliwa kielimu ili iende katika kasi angalau inayokaribiana kama sio sawa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara na Serikali hususan Waziri Mkuu wa ubunifu na mbinu mbalimbali ya kuhimiza, kusimamia na kufanikisha uanzishaji Shule za Sekondari kata kwa nchi nzima na hivyo kufikia lengo kabla ya wakati ulio kusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zetu za sekondari zimeanza na tumefanikiwa kiasi kikubwa, naomba tukumbuke kuwa huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali Kuu hususani Wizara ya Elimu na Ufundi nazo zinaongezeka kwa mfano huduma za malipo ya *bills* mbalimbali zinazolipiwa na Wizara i.e *utility bills; electricity, water, telephone etc.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuongezeka kwa shule, nadhani pia umefika wakati wa ku-*decentralise* malipo yake ili kuongeza ufanisi. Nashauri malipo yake yafanyike huko huko mikoani na yawe *controlled* na *sub-treasury* (Hazina Ndogo) za Mikoa ni matumaini yangu itaongeza ufanisi kwani ufanisi wakati *process* za *bills* hizo mpaka ziletwe Wizarani kunatokea ucheleweshaji ambao unaziletea usumbufu Shule hizo za Sekondari hasa zikikatiwa malipo ya *bills* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuendelea kuomba Wizara kuangalia kwa jicho la huruma Wilaya ya Namtumbo kama tuonavyo ni Wilaya ya tano katika umaskini kati ya Wilaya zote nchini. Kikubwa hapa ni ukosefu wa elimu ya kutosha ili kuweza kupata upeo wa kupambanua mambo ya kujiletea maendeleo na hatimaye kuondoa umaskini. Elimu ndio ufunguo wa maendeleo, hivyo tukiiboresha elimu kwa kutupatia walimu watakaotosheleza mahitaji yetu vitabu, vitendea kazi kwa waratibu wa elimu kata na Wilaya kwa mfano pikipiki, gari ili kuweza kurahisisha ukaguzi kwa utendaji kwa shule zetu. Naamini tutapiga hatua kielimu hivyo kuwa rahisi kupiga vita umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naiomba Serikali ituongezee kulipia idadi ya watoto wasiojiweza na yatima waliofaulu ili tupate watoto wengi watakaopata elimu, kuja kuwasaidia wenzao kielimu na kuendeleza Wilaya na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWADINI A. JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii kuchangia japo kwa uchache hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kuipongeza Serikali kwa kuuona umuhimu wa elimu kwa Watanzania. Suala la kuipa kipaumbele sekta ya elimu ni

jambo la msingi kabisa. Kadhalika hatua ya Serikali kuhamasisha wananchi kujenga sekondari za kata ni la busara sana, ingawaje katika kuteleza azma hiyo baadhi ya maeneo wamekuwa wanawatoza wananchi michango kwa kiwango kikubwa na baadhi ya maeneo nguvu hutumika katika kudai michango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kima cha kuchangia kimekuwa kinatofautiana baina ya sehemu na sehemu na kwa bahati mbaya viwango vinavyowekwa havizingatii uwezo wa wananchi wenyewe. Mara nyingi michango inayochangishwa inakuwa ni mingi na yenye malengo tofauti; Kwa mfano ujenzi wa madarasa, madawati, kusogeza miungombinu ya maji na kadhalika. Huu ni mzigo kwa Mtanzania wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azma ya kumsaidia Mtanzania huyu aweze kuchangia elimu ni vyema basi Serikali ikaandaa na kutoa mwongozo mahususi ikiwezekana kwa nchi nzima ili kila mzazi aweze kujua anatakiwa kuchangia nini, kwa wakati gani na kiwango cha uchangiaji. Hii itawasaidia wazazi kujipanga vizuri na kumwondolea usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na azma ya Serikali kuhakikisha angalau asilimia ya wanafunzi wanaofaulu darasa la saba wanajiunga na Shule za Sekondari. Madarasa mengi yamejengwa katika kata kukidhi haja hiyo. Kwa bahati mbaya shule hizi zimejengwa pasi na kuzingatia sambamba na ujenzi huo, ujenzi wa maabara na nyumba za walimu. Aidha idadi ya walimu waliopo hawatoshelezi kukidhi ongezeko la Shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii, ni dhahiri kwamba elimu itakayotolewa mashuleni haitokuwa ya kiwango kizuri. Kwa maana nyingine tusije tukadhani wingi wa mashule yaliyojengwa ndio kuna maendeleo katika elimu. Maendeleo ya elimu hupimwa kwa kiwango cha ubora wa elimu inayotolewa. Ni dhahiri kwamba zingatia muhimu zaidi katika mipango ya maendeleo ya jamii ni ubora wa huduma inayotolewa na sio wingi wa mashule. Katika elimu pasitamwe shule ngapi zilizopo au zimejengwa au wanafunzi wangapi wanasoma, patazamwe shule ina vifaa kiasi gani, kiwango kipi cha wastani kufaulu kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikahakikisha kwamba shule zote zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa zinapatiwa walimu walioandaliwa vizuri na ambao mazingira yao ya kazi yameboreshwa. Aidha, shule hizo zipatiwe vifaa na zana za kutosha katika maabara pamoja na vifaa vya kufundishia na kujisomea tuweze kufanya hivyo kiwango cha elimu atakayoipata mtoto wa Kitanzania itakuwa ni ya kiwango cha hali ya juu.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Mheshimiwa Margaret Sitta - Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Naibu Waziri wake wote wawili pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwa matayarisho mazuri ya hotuba ya ya Wizara yao ya Makadirio ya matumizi ya

fedha ya mwaka 2007/2008 yenye kulenga utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala ya Uchaguzi 2005 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Kigamboni kwa tatizo kubwa la usafiri wa wanafunzi kutoka nyumbani kwenda shuleni wanafunzi wanalazimika kupanda malori ya michanga au mawe pamoja na kuombaomba usafiri kwa wenye gari ndogo binafsi. Malori yanahatarisha maisha ya watoto kwa kuwa mara nyingi hupakia wanafunzi hao huku gari likiwa linatembea. Ni hatari zaidi kwa watoto wa kike hasa ukizingatia maumbile yao watoto wetu hawa. Hali hii inaweza kusababisha watoto wa kike kuharibika na kupata mimba, maradhi hasa janga la UKIMWI, ajali na kupungua nidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kwamba ugawaji wa wanafunzi upewe kipaumbele kwa kuwapeleka/kuwapangia watoto/wanafunzi katika maeneo yaliyokaribu na makwao hasa kwa kuzingatia wingi wa shule uliopo ambao nina hakika kupatikana nafasi inawezekana, tatizo kubwa na ni vyema likafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa maabara, nyumba za walimu na ugawaji wa walimu yapewe kipaumbele kama yalivyo kwenye mpango wa Taifa na Wizara ya Elimu. Hii itasaidia wanafunzi kufanya mafunzo ya vitendo na walimu kudumu katika shule wanazopelekwa kwa kuwa nyumba za kuishi zitakuwepo. Umuhimu upewe maeneo ya nje ya mji, jiji badala ya mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujenzi wa uzio katika shule zetu ni jukumu la Kamati za shule, naiomba Serikali kuangalia uwezekano wa kuamua kujenga uzio katika shule zote za bweni mijini na vijijini kutokana na mazingira yenyewe pamoja na gharama kubwa za ujenzi na uzio kutokana na ukubwa na milki wa shule zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VETA* ni vyo muhimu na kwa kuwa Tarafa ya Kigamboni inakuwa kwa haraka, naomba kutoa wito kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kufikiria kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Ufundi katika Jimbo la Kigamboni ili kuwanusuru watoto wetu na balaa la ukosefu wa kasi na mafunzo hayo yatakuwa kichocheo kwa wanafunzi wanaomaliza Shule ya Msingi na Sekondari kujifunza na kujiaraji binafsi.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Awali ya yote, napenda kipekee niwapongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Margreth Sitta na Naibu Waziri Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza kwa jinsi walivyoshughulikia kifo cha mwanafunzi David Steven Kimabo wa shule ya Sekondari Panga Hill. Jina la mama wa mwanafunzi huyo ni Edna Kimabo. Napenda niwafikishie shukrani za dhati kutoka kwa familia ya Marehemu. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kutoa pongezi kwa Wizara kwa jinsi wanavyoendeleza walimu kazini (*Primary*) kwa masomo ya *module* hadi kufikia *grade A*. Natoa changamoto kwamba sasa Serikali izidishe kasi zaidi ili waweze kujiendeleza zaidi

ili waweze kufikia stashahada na hatimaye kupata shahada ili wanafunzi wetu wapate walimu ambao wana uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule hizi wanazojenga, ningeshauri wanao-*plan* wafikirie kuweka mahitaji ya walemavu. Kwa mfano; njia za kupitia, *Wheel Chairs*, aina za vyoo kwa ajili ya walemavu, madawati, meza na vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia hata kwenye vyombo vya habari, hasa shule za *primary*, kwamba kumekuwepo na ongezeko la wanafuzni wengi kupata mimba. Kuna haja ya kufanya utafiti wa kina na kujua sababu za hizi mimba ni nini na hatimaye kutatua tatizo hilo ambalo ni kikwazo kwa maendeleo hasa kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo katika Wizara nyingine, miongozo bado ni mingi ya kisera, haijafika mashuleni. Ningeshauri uimarishaji wa Kitengo cha Wakaguzi waangalie ni miongozo ipi ipo kama *Cecular* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanaajiriwa na TAMISEMI, shule na walimu ni wa TAMISEMI. Lakini, kinachofundishwa ni mitaala ya Wizara ya Elimu. Kuna haja ya kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi ili kuweza kumaliza matatizo ya kiufundi ya walimu na hatimaye kuyatatua kwa kupitia zile Bodi, *Ward Resource Centres* ambazo zinahitaji ziimarishwe ili ziweze kuwepo na *continuous training* ya walimu kwa sababu ya mabadiliko ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shule kujengwa, lakini bado maabara zinahitajika kuwa na vifaa vya kufunzia *practical*. Kwa mfano Shule ya Sekondari ya *Mbokomu One*, chumba cha maabara hakina kifaa chochote cha kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kujenga shule, pia kumekuwepo na mesi ya kulia chakula wanafunzi na sehemu za kupikia chakula cha wanafunzi. Kuna sehemu nyingi za shule wanapikia nje huku chakula kikizingirwa na inzi na hapo hapo tunafundisha wanafunzi, *especially primary* somo la afya. Hivi hapa tunafanya nini? Bajeti ikiruhusu na hili pia liwekwe kwenye orodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha!

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi nzuri sana waifanyayo na kwa hotuba hii nzuri ya bajeti ya mwaka huu iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie eneo moja tu nayo ni fedha za MMES. Fedha hizi zinazopitishwa Hazina Ndogo kwenda Halmashauri zina matatizo makubwa kwa Wakuu wa Shule na jumuiya hususan Kamati za Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba fedha hizi kama wafadhili watakubali, zipite katika Halmashauri za Wilaya. Wakuu wa shule wakabidhi mafunzo ili waweze

kusimamia taaluma katika shule zao. Zoezi hili litawasaidia sana Wakuu wa Shule wasieleweke vibaya mbele ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nakushukuru wewe kwa kuweza kusimamia Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili, sina budi kwa makusudi kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu na Watendaji wake wote kwa kuweza kuwasilisha hotuba ya Wizara. Nasema hongera!

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ni msingi wa maendeleo, elimu ni dira, kwa hiyo, naomba Serikali hii ya Awamu ya Nne itoe nguvu zote ili elimu itolewe kuliko nchi nyingine zozote. Sina shaka panapo nia, pana njia! Namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuiendeleza Wizara na kuijenga nchi yetu na Mungu ambariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wa ndani ya nchi yetu waliosomeshwa na Serikali yetu, hukimbia baada ya kujiona kuwa tayari wamepata ujuzi na elimu na kisha kwenda kufanya kazi nje ya nchi na kuacha nchi yao. Naomba suala hili lifuatiliwe na wadhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya juu inatolewa vizuri, lakini bado ipewe kipaumbele kuwa iwe inatolewa sawa kwa kuzingatia kuwa Serikali hii ni ya Muungano. Kwa hiyo, Zanzibar iangaliwe kwa walimu, majengo ya vyuo, wanafunzi na taratibu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuwekeza, wekeza kwenye elimu. Kwa Awamu hii chini ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Sitta, tuanze kuwekeza. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi mwenyewe, naunga mkono hotuba hii!

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ukaguzi, natoa pongezi nyingi kwa ujenzi wa shule toka msingi hadi sekondari. Kinachonikera ni kule kukosa ukaguzi wa mara kwa mara na uwe wa kushitukiza ili waone kama kweli mahudhurio ya wanafunzi na walimu ni asilimia ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Pre-Form One*, Serikali imesitisha utaratibu huu wa kuanza elimu ya sekondari mwaka mmoja kabla. Inasikitisha kuwa katika Mkoa wa Mwanza, bado kuna baadhi ya shule zinaendelea na taratibu hizi. Naomba Wizara iwe na msimamo nchi nzima. Pia, niombe uongozi husika ufike huko kuthibitisha hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu majengo ya shule, naipongeza tena Serikali kwa kutoa pesa nyingi sana katika shule zetu kupitia MEM na MMES. Tatizo kubwa ni jinsi gani majengo hayo wanavyoyajenga bila usimamizi bora. Kati ya Bodi za Shule na Wahandisi ambao ndio wasimamizi wakuu wa ujenzi wa majengo kama sheria inavyowataka kuwa.



Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara itoe utaratibu kwa nchi nzima Wahandisi hawa wawajibike vipi katika ujenzi wa shule hizi. Iko siku yataleta madhara aidha kwa kuanguka au kufumka mapaa ovyo pasipo hata upepo mkali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *VETA*, yafanyike yafutayo:-

- § Kila Jimbo la Uchaguzi liwe na shule za namna hii pamoja kuhamasisha nguvu za wananchi.
- § Ikibidi, wanafunzi wanaofuzu mafunzo hayo toka fani mbali mbali waweze kukopeshwa vifaa vya kuanzia maisha baada ya elimu hiyo. Wazazi wao/walezi wao wawadhamini katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lugha ya Kiingereza, Shule nyingi za Msingi hufelisha wanafunzi au kupelekwa shule zisizo bora kwa sababu ya kufeli tu kiingereza. Niombe Wizara ilione hili kwa kubuni mbinu ya jinsi gani tuweze kuwapata walimu wazuri wenye vipaji maalum vya lugha hiyo ya kiingereza tu ili waweze kusambazwa kwenye shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja!

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naomba waendeleo hivi hivi ili tufanikiwe upande wa elimu. Pia, nawapongeza kwa hotuba nzuri na ya kina iliyowasilishwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msaada wa Mheshimiwa Waziri, kwenye shule za sekondari zilizoko Iramba Mashariki. Iguguno Shule ya Sekondari tuliitembelea tuliposafiri na na Waziri Mkuu. Shule hiyo ni nzuri na inaendelea vizuri sana. Wanafunzi, walimu, wananchi na mimi Mbunge wao, wote tunatoa shukrani kwa mchango wa fedha alizotoa Mheshimiwa Waziri kwa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa tulilonalo katika shule hiyo ni umeme. Tunahitaji shilingi milioni 12.5 ili tuvute umeme ambao nguzo ziko karibu sana na shule. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule za sekondari za Gumanga, Ilunda, Chemchem, Mwanga, Nkinto na Mwangaza, zina upungufu mkubwa wa walimu. Naomba msaada wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefika wakati sasa wa kuanzisha mradi wa uvunaji wa maji ya mvua kwenye sekondari zote ambazo zimejengwa na zile zote mpya zitakazojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna tatizo sana la fedha zinazotumwa kutoka Hazina kwenda shuleni kupitia Hazina Ndogo zilizoko Makao Makuu ya kila Mkoa. Badala ya fedha hizo kwenda kwenye akaunti za shule ili Kamati za Shule ziweze kuzitumia, Hazina Ndogo nyingi, kwa mfano ya Mkoa wa Tabora, fedha zinabaki hapo

na kuwataka Walimu Wakuu wawe wanakwenda hapo na kupeleka mahitaji yao ili waandikiwe *LPO* na kuulizwa mahitaji tao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtindo huu unaleta usumbufu mkubwa sana hasa kwa shule zilizo mbali na Makao Makuu ya Mkoa. Namwomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na Hazina ili fedha za MMES ziende shuleni kupitia kwenye akaunti za shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa wanafunzi wetu wote wa shule za msingi na sekondari maeneo mengi hawapati elimu sawa sawa kwa sababu walimu hutumia zaidi ya siku mbili kila mwezi kufuata mishahara yao *NMB* ambazo ziko mbali na maeneo yao. Mheshimiwa Spika, maeneo mengi walimu bado wana madai yao mbali mbali ya likizo, masomo, matibabu na kadhalika. Naomba sana Mheshimiwa Waziri awasiliane na Wizara ya Fedha ili malimbikizo mengi ya walimu yalipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru sana kama Mheshimiwa Waziri atatamka kuhusu Msaada wa shilingi milioni 12.5 atakazotoa kwa shule ya Iguguno.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi kutangaza *interest* katika mchango wangu. Mimi nina shule tatu, *Colleta Kindergarten, Colleta Memorial Primary School* na *Bakiri Muluzi Secondary School*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uko katika Serikali kuzisaidia shule za binafsi katika uendeshaji wake. Wengi wetu wa wamiliki wa shule hizi hasa Wabunge ni watu masikini na uwezo wa chini, hivyo vyanzo vya ujenzi wa shule hizo hutegemea sana mikopo ya Benki katika kujenga. Kwa kufanya hivyo, gharama ya kujenga na kuendesha shule hizi ni mzigo mkubwa sana. Kwa kifupi, kumiliki shule binafsi na kutoa elimu bora kwa watoto wa kitanzania kuna hitaji moyo wa kujitolea kwa hali ya juu. Aidha, sekta hii binafsi imechangia sana maendeleo ya Taifa letu kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha na kukatisha tamaa ni pale Serikali inaposhindwa kuzisaidia shule binafsi kwa maelezo kuwa eti tunatoza ada kubwa. Huu ni uonevu wa hali ya juu kwa kuwa karo zinazotozwa na shule binafsi za Tanzania hazifikii hata robo ya ada ambazo hutozwa na nchi jirani kama Kenya, Uganda, Zambia na Malawi, ndiyo maana Serikali inafidia gharama karibu zote za shule za Serikali na gharama zenyewe *actually* ni kubwa sana kulingana na bajeti ya mwaka huu 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifikirie upya kwa maana ya kuzisaidia shule binafsi ili ziweze kuendelea kutoa elimu iliyo bora na kuchangia maendeleo ya taifa letu. Kutofanya hivyo ni kuziua shule hizo na hivyo kufifisha maendeleo ya elimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nitoe lawama kwa Mkaguzi Mkuu wa Elimu Kanda ya Mashariki, kama sikosei anaitwa Mama Karunga au linafanana na hilo. Mama huyo ana lugha isiyoridhisha kwa wadau wake wanaomsadia katika kuboresha elimu. Kazi yake iwe ni kusaidiana na wadau na wala sio kuwakomoa hasa

anapombwa maelezo au kusaidia kutatua jambo linalohusu elimu anayosimamia. Nipo tayari kutoa ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi - Mheshimiwa Sitta, Naibu Mawaziri wake wote wawili kwa kufanikisha elimu nchini. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye kugusa maeneo yote yanayohitaji kuboreshwa katika elimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utahusu jinsi ya kutatua tatizo la upungufu wa walimu hasa katika shule za sekondari. Tunaishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kuchukua hatua za haraka ili kukabiliana na upungufu wa walimu baada ya nchi yetu kuwa na shule za sekondari 1,084 nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika wakati mikakati hiyo ya Wizara ikiendelea, napendekeza tuwaajiri pale inapowezekana walimu wastaafu ambao bado wana nguvu ya kufanya kazi kwa miakataba ya mika miwili miwili. Walimu hao wapo kila sehemu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mahakama iliwahi kutumia mbinu hii pale ilipobaini kuwa ilikuwa na upungufu mkubwa wa Mahakimu miaka ya 1980 – 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chombo cha kushughulikia ajira na huduma ni muhimu kipatikane katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2007/2008. Walimu wanasumbuka sana kwa vile wanazunguka na kupigwa dana dana na mamlaka nyingi kuhusu maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo muhimu ambayo Waziri ameyaorodhesha kama maamuzi muhimu, kipengele (g) anaongelea juu ya ya kuangalia uwezekano wa kuwa na chombo kimoja cha ajira na huduma kwa walimu kwa lengo la kuboresha huduma kwa walimu. Mimi nashauri kuwa badala ya kuangalia uwezekano, tuseme kuwa katika kipindi hiki tutaimarisha *Teachers Service Commission* kama chombo cha kushughulikia ajira, nidhamu na huduma kwa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukatisha masomo wanafunzi wa kike kwa sababu ya uja uzito, Wilaya yangu na Wilaya ya Ulanga katika Mkoa wa Morogoro ni Wilaya zenye matatizo makubwa ya ukatishaji wa masomo kutokana na matatizo ya mimba. Iko haja ya kuleta Muswada wa Sheria ambao utakuwa tofauti na sheria ya kujamiiana. Sheria hiyo ijikite kwa wanafunzi tu kwa kutoa adhabu kali kama mhusika ni mtu mzima na kutoa adhabu ya fimbo hadharani (*Corporal Punishment*) kama mhusika ni mwanafunzi mwenzake.

Baada ya adhabu ya kuchapwa fimbo kama 12 hivi, yule kijana wa kiume kwa udhamini wa wazazi wake aruhusiwe kuendelea na shule na yule msichana naye akishajifungua aruhusiwe kurudi shuleni hata ikibidi kurudia darasa la nyuma ili kuweza ku-*catch up*. Kama mtu mzima akihusika kumpa mimba mwanafunzi, basi adhabu kama zilivyo kwenye sheria ya kujamiiana zitumike. Kwa bahati nzuri siku hizi kuna ushahidi wa *DNA* ambao unakubalika.

Kwa hiyo, lile tatizo la kukwepa kuhusika halitakuwepo. Tayari sheria ya kukubali ushahidi wa vinasaba (*DNA*) imeishapitishwa. Kwa hiyo, kesi za namna hiyo zitaendeshwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja!

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii nzuri yenye tija na matumaini ya kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila elimu, maisha bora hayatapatikana, unyanyaswaji kwa wananchi hautakwisha. Elimu inaongeza pato la Taifa, kaya na mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pole kwa wale wote waliopotelewa na ndugu zao. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie yafuatayo: Kwanza nianze na Elimu ya Msingi. Naomba niongelee matatizo ya walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ieleze bayana fungu la kujiendeleza kitaaluma ili tuboreshe elimu kwa wanafunzi wetu. Katika kitabu cha hotuba eneo hili la kujiendeleza sijaliona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya walimu, uhamisho, usafiri na gharama za matibabu, walimu washughulikiwe matatizo yao kwa haraka. Ikiwezekana tatizo la matibabu lipewe kipaumbelee. Wapo walimu ambao wanahangaika sana kupata huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bukombe tuna upungufu wa walimu. Mahitaji yetu ni walimu 2,384, waliopo ni 1199, kuna upungufu wa walimu 1,185 ambapo uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi Bukombe ni 1:79 badala ya 1:40. Ninaomba Bukombe ipelekewe walimu wa kutosha ili tutoe matunda mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Waratibu Elimu Kata (MEKs); Waratibu hawa hawana vitendea kazi vya kutosha na Kata wanazoongoza ni kubwa sana.

Naomba Serikali iwasaidie usafiri ili waweze kuratibu vizuri shule zao. Mahitaji ya ofisi za MEKs yanapatikana wapi? Naomba Serikali inisaidie kujua fedha za kuendesha ofisi zao ziko katika kasma gani ili nifahamu tuwasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya sekondari, kuna tatizo la ucheleweshaji wa maslahi ya walimu. Naomba Serikali iharakishe maslahi yao ili waendeele kuipenda kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Walimu ambao waliazimwa toka Halmashauri ya Wilaya ili wakafundishe shule zetu za kata, mafao yao yakoje? Je, yatalipwa kwa wakati? Naomba Serikali ilianganalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa walimu wetu wapo vijijini kwenye Kata zetu, naomba Serikali ifungue Chuo Kikuu Huria Bukombe ili tuwasaidie walimu tarajali kujiendeleza. Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ituonee huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango mzuri wa MMES, kwa kuwa fedha ni za maendeleo, nashauri Serikali fedha hizi zipitite mlango mmoja kwa *DED* ili iwe rahisi kusimamia. Naomba pia Serikali ianganalie uwiano wa kutoa fedha hizi za MMES. Naomba Serikali izingatie umbali na mfumko wa bei katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa maabara, maktaba, hostel. Nyumba za walimu 1500 (Uk. 18)(h & i), Bukombe ikumbukwe.

Aidha, suala la watoto yatima/wasiojiweza wanaofiwa na wazazi wao wakiwa shuleni, ushauri katika kuwapata vijana hawa, kwa kuwa kunakuwa na chaguo la kwanza, la pili na ikiwezekana na la tatu, badala ya kuainisha vijana kabla ya matokeo, wanafunzi hawa watambuliwe mara baada ya matokeo na kila chaguo linapotokea, wanaofiwa na wazazi wao wakiwa shuleni, Wakuu wa shule wasidie kuainisha ili nao wahudumiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyo/chuo cha ualimu, napenda kuishauri Serikali kama inawezekana, vijana hawa wasaidiwe kusomeshwa kama zinavyofanya Wizara nyingine ili tumalize tatizo hili au Serikali iandae mkakati kwenye taasisi za fedha kwa udhamini wa Serikali wakopeshwe ili wasome kama inavyofanya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Aidha, naishukuru Serikali kwa kutupatia Chuo cha Ualimu (*Shycom*). Ombi la Wabunge wa Mkoa na viongozi pamoja na wananchi, Chuo hiki kichukue masomo mbali mbali (nyanja) badala ya kuegemea masomo ya biashara peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia kuondoa/kupunguza tatizo la walimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya jumla, naishukuru Serikali kutupatia gari la ukaguzi, jenereta katika shule ya sekondari Runzewe, vitabu vya sayansi kwa shule za Ushirombo na Runzewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo la vitabu, naomba Serikali iendeele na juhudi zake kama ilivyodhamiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Idara ya utamaduni iimarishwe, madarasa na nyumba za walimu, MEM na MMES na *Capital Grant* ziendelee kutusaidia. Nashukuru pia Mfuko wa *TASAF II*, kwani umetusaidia sana.

Mheshimiwa Naiibu Spika, Mungu akijalia, hadi Desemba, 2007 tutakuwa tumejenga hosteli nane kati ya shule 20 za Serikali Bukombe. Naomba Serikali ituongeze fedha za Mfuko huu kwani mgawo wetu umekwisha.

Aidha, naipongeze sana Wizara, mambo yake ni makini, mahiri na viwango, yaliyomo yote ni mazuri. Mungu awabariki. Naunga mkono hoja!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitaanza kuwaita Wizara waanze kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naibu Mawaziri kila mmoja atapewa dakika 20. Halafu Waziri mtoa hoja atapewa dakika 50. Kwa hiyo, sasa tunaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo na Ufundi na kwa ridhaa yako, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema na mapenzi yake mema kwangu, kwa kuniwezesha kutimiza majukumu yangu sawa sawa. Aidha, ninawapongeze wananchi wote wa Mkoa wa Tanga, kwa namna walivyoshirikiana kujenga shule za Sekondari na kuwezesha kupeleka idadi kubwa ya wanafunzi. Hongera zao nyingi ziwafikie na ninawasihi tuongeze ari ili nasi tufikie hatua nzuri zaidi kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa nami nichangie kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo: Kwa kuwa orodha ni ndefu ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, tumegawana kuzijibu nami nitajibu chache. Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Wilson M. Masingi, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzungwanko, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, walizungumzia kwa kina upungufu wa maabara katika shule za sekondari za kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikijenga maabara na itaendelea kufanya hivyo kadri fedha zitakavyopatikana ili kutimiza lengo la kuwa na maabara kwa kila shule. Kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008, Wizara itajenga maabara 84 ikilinganishwa na ujenzi wa maabara 42 kwa mwaka uliopita.

Uamuzi wa shule zipi zitajengwa maabara utatolewa na mikoa husika. Tunawashauri Waheshimiwa Wabunge, washiriki katika kubaini shule za kujengwa maabara hizo.

Mheshimiwa Magreth A. Mkanga, amezungumzia zaidi juu ya masuala ya Elimu ya Walemavu. Hoja ya kwanza aliyoitoa ilikuwa ni Asasi zikiwemo shule za *mission* na za watu binafsi zinazotoa elimu kwa wenye walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES) na Mpango wa Elimu ya Msingi, imeainisha utaratibu wa kutoa ruzuku za maendeleo kwa shule zisizo za Serikali zinazotoa elimu kwa wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa orodha ni ndefu ya ruzuku ilivyotolewa, tumempatia Mheshimiwa Magreth A. Mkanga orodha yote ikiwa ni pamoja alichogiza kwamba apatiwe mgawanyo wa vifaa vya kufundishia, tumempatia mezani kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banywika, Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Dr. O. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Ledian M. Mng'ong'o na Mheshimiwa Benito W. Malangalila, wamezungumzia juu ya kupandishwa hadhi kwa baadhi ya shule ili ziweze kuwa *High School ('A' Level)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa shule za kuanzisha masomo ya *High School ('A' Level)*, hufanyika baada ya ukaguzi wa shule kuridhika ukamilifu na utayari wa shule hizo kuanzisha masomo hayo. Sifa au vigezo vinavyotazamwa ni pamoja na madarasa yanayotosha kutegemea michepuo inayokusudiwa kuanzishwa; mabweni au hosteli; nyumba za walimu; maabara kwa masomo ya sayansi na huduma muhimu za jamii.

Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Felix N. Kijiko na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, wamezungumzia juu ya ujenzi wa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuanzia mwaka 2004 kupitia Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES), imekuwa ikitoa ruzuku ya ujenzi wa nyumba za walimu. Aidha, bajeti ya mwaka huu 2007/2008, Wizara imelenga kujenga nyumba 1,500. Ujenzi utaendelea kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, pamoja na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, wameomba umiliki wa shule za sekondari kisheria uwe chini ya Serikali za Mitaa na kuziongezea uwezo wa wataalam na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo katika Mpango wa Madaraka *D by D* wa kupeleka kwenye Halmashauri. Mchakato huo pia umeanza kwa shule za sekondari na utatekelezwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, amezungumzia upungufu wa vifaa vya maabara. Kweli kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya maabara katika shule za sekondari. Hata hivyo, Wizara yangu kupitia Mpango wa Elimu ya

Sekondari (MMES), hutoa ruzuku ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa ya maabara kadri fedha zinavyopatikana.

Mheshimwia Jacob D. Shibiliti, alizungumzia pamoja na mambo mengine juu ya kujenga mabwalo na majiko. Wizara inajenga mabwalo katika shule za mabweni. Hata hivyo, Wizara inashauri Halmashauri na wananchi kwa ujumla wa shule husika, waweke mipango ya ujenzi wa mabwalo ya chakula sanjari na majengo mengine.

Mheshimiwa Christopher K. Chiza, ameshauri kuwa shule za bwani zitumie kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya matone (*Drip Irrigation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge umepokelewa na utafanyiwa kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, hasa kwa shule zenye michepuo ya kilimo.

Mheshimiwa Pindi H. Chana, amezungumzia juu ya wanafunzi kufukuzwa shule kwa utovu wa nidhamu na hivyo kumnyima mtoto haki ya kupata elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunakubaliana kuwa ni haki ya mtoto kupata elimu. Hata hivyo, ni vyema wanafunzi wa shule kufuata taratibu na kanuni ambazo zinalenga katika kuwajengea maadili mema. Endapo mzazi hataridhika na adhabu iliyotolewa kwa mwanawe, anaweza kukata rufaa katika mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni vyema wazazi wakasaidia kuhakikisha kuwa watoto wetu wanakwenda shuleni wakiwa na tabia nzuri bila kujiingiza katika makundi mabaya ya uhalifu na hasa uvutaji bangi na unga.

Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Juma H. Killimbah na Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, walizungumzia uchakavu wa majengo wa shule nyingi. Wanashauri Shule ya Sekondari Msalato na Tumaini zifanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inao utaratibu wa kukarabati majengo ya shule za sekondari kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mwaka wa fedha 2006/2007, Wizara ilipanga kukarabati shule za sekondari 16. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, Wizara imepanga kukarabati shule 15 na Msalato ikiwemo.

Mheshimiwa Felix N. Kijiko, ameendelea kuzungumzia juu ya matumizi ya *solar unit*. Tumepokea ushauri wake na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Hasnain M. Dewji, amezungumzia uhaba wa maji ya kunywa katika baadhi ya shule. Ni kweli kuna matatizo ya upatikanaji wa maji kwa baadhi ya shule zetu. Hata hivyo, Wizara inashauri na kutoa wito kwa shule kutazama uwezekano wa kuvuna maji ya mvua ili kupunguza tatizo hili.



Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe wito kwa wote tunaopenda kuvuna maji, tukajifunze Bukombe, wao kila shule mpya iliyojengwa wameonesha namna ya kuvuna maji. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Diana M. Chilolo anataka Serikali ioneshe kwa vitendo dhamira ya Serikali ya kuinua kiwango cha michezo kwa kurudisha mashindano mbalimbali ya michezo shuleni. Somo la michezo linatiliwa mkazo sana. Wakuu wa Shule wameshaagizwa kuendesha mashindano ya ndani kati ya shule na shule. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mpango Mkakati umeshapangwa na namna ya kuendesha mashindano hayo. Mara baada ya bajeti yetu, Wakuu wa Shule watapatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Lekule M. Laizer, amezungumzia juu ya uhaba mkubwa wa Walimu na kwamba kule Longido hawatulii. Wizara yangu hupanga Walimu kwa mikoa na mikoa hupanga Walimu katika shule ili kukabiliana na upungufu wa Walimu. Hata hivyo, kutokaa katika shule kuna sababu nyingi, mojawapo ikiwa ni kukosekana kwa huduma muhimu na vivutio kama vile nyumba, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, ameshauri Kamati za Ujenzi za Shule zitumie wazazi wenye ujuzi wasaidiekujenga shule. Tumepokea ushauri wake.

Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, ameulizia *capitation grants* inafika lini shuleni na ni kiasi gani? Dhamira ya Serikali ni kufidia ada ya Sh.20,000 kwa kila mwanafunzi lakini Wizara haijaweza kufikia kiasi hicho kwa sababu ya ufinyu wa bajeti na ongezeko kubwa la wanafunzi wa shule za kutwa. Kiasi kinachotolewa hutegemea sana upatikanaji wa fedha na idadi ya wanafunzi wa shule za kutwa. Fedha hii hutumwa inapopatikana kutoka Hazina.

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, alitaka kujua idadi halisi ya Walimu katika fani zenye upungufu katika kipindi cha miaka kumi. Mpaka Machi, 2007 tulikuwa na Walimu 29,858 waliokuwa kwenye shule za sekondari. Wizara inatengeneza andiko la MMES ili kuweka takwimu za Walimu kwa kipindi kilichotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea na Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, ameshauri watoto wajengewe uzalendo wakiwa wadogo. Wizara inayo mikakati mbalimbali ya kujenga uzalendo kwa watoto wadogo. Mtaala wa elimu ya awali umezingatia matendo ya michezo ambayo hujenga umoja, ushirikiano na upendo. Aidha, mtaala wa Elimu ya Msingi kupitia somo la Haiba na Michezo inasisitiza haki, wajibu na kuheshimiana. Masuala haya huchangia katika kujenga uzalendo.

Mheshimiwa Diana M. Chilolo, alizungumzia pia upatikanaji wa vyeti vya wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka 1990. Ni kweli mwaka 1990, Wizara haikuchapa vyeti hivyo kwa wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi. Mwaka 1993 Serikali ilichapa vyeti na kuvisambaza katika Mikoa yote ili vifikishwe katika

Halmashauri na shule za msingi ambazo zilikosa pamoja na wahitimu wa mwaka 1990. Wale ambao hawajapata vyeti vyao wawasiliane na Maafisa Elimu wa Wilaya ili kuvipata vyeti hivyo.

Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, alizungumzia juu upatikanaji wa vitabu vya kiada. Kupitia Utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi MEM, shule zinapelekwa ruzuku ya uendeshaji ambapo hutumika kununulia vitabu vya kiada na ziada. Utaratibu huu umewezesha uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu.

Mheshimiwa Ledian M. Mng'ong'o, ameomba huduma muhimu za maji na chakula zitolewe shuleni. Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama *TASAF*, *WFP*, *Plan International* na *World Vision*, Serikali imekuwa ikiendelea na huduma muhimu za ujenzi wa matanki ya maji. Aidha, tunahimiza Kamati za Shule kusimamia zaidi na kushirikiana ili kuhakikisha majengo hayo yanakuwa bora na yenye kuwa na vifaa vinavyohusika.

Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, kuwepo kwa msongamano katika shule za bweni za jamii ya wafugaji isiyolingana na miundombinu iliyopo. Shule za bweni zinakusudiwa kuwahudumia watoto wanaotoka katika jamii ya wafugaji ambapo mwamko wao wa elimu uko chini. Wizara inatoa wito kwa Halmashauri kuhakikisha kwamba, wanafunzi wanaoandikishwa katika shule hizi wawe wamelengwa tu. Halmashauri zinashauriwa pia kuwahamasisha wananchi washiriki katika kuongeza miundombinu ili kupunguza msongamano uliopo sasa.

Mheshimiwa John P. Lwanji, ameiomba Serikali ianzishe utaratibu wa kutoa chakula cha mchana kwa wanafunzi wa shule za msingi, kuliko utaratibu wa hivi sasa wa shule chache. Serikali kwa kushirikiana na *WFP*, ilianzisha Mradi wa Lishe Shuleni katika maeneo yenye ukame na uhaba wa chakula ili kupunguza mdondoko, kuimarisha mahudhurio na afya za wanafunzi.

Kutokana na umuhimu wa utoaji wa chakula cha mchana, Wizara inahimiza Halmashauri zote kuzielekeza Kamati za Shule na Serikali za Vijiji, kuanza kutoa huduma za chakula katika shule zao.

Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu, anashauri *REOs* wapewe magari waweze kufuatilia utekelezaji wa mipango yao ya elimu ya MMES na MEM. Wizara inatambua umuhimu wa vyombo vya usafiri katika kufanikisha usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya elimu. Wizara inatoa wito kwa Makatibu Tawala, kuhakikisha kwamba *REOs* wanapata usafiri kila wanapohitaji kwenda kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya familia yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kalambo na wananchi wa Mkoa wa

Rukwa, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutufikisha siku ya leo na kutuwezesha kufanya kazi hizi. Pili, napenda kutoa pole kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa, aliyefariki tarehe 26 Juni, 2007. Namwomba Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amen*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba niwape pole jamaa wa marehemu wote waliofariki katika ajali mbaya za magari zilizotokea Singida, Moshi na Mbeya katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti. Majeruhi nawaombea kheri wapone haraka. Pia nawapa pole Wabunge wote waliofiwa na wapendwa wao kipindi hiki. Naomba Mungu awape subira na uvumilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii niwapongeze Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Florence E. Kyendesya, kwa kuchaguliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kuchangia hoja ya Wizara yangu kwa kujibu baadhi tu ya hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri na kama Waheshimiwa Wabunge walivyoweza kuchangia kwa siku hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge aliyechangia mwanzo alikuwa ni Mheshimiwa Anna R. Lupembe, ambaye alizungumzia kuhusu ada katika Vyuo vya Ualimu.

Uhaba wa Walimu tunaufahamu, unatokana na uwezo mdogo wa vyuo vyetu. Hoja ya Wanachuo wanaotoka katika familia zenye kipato duni kutoweza kulipia gharama za mafunzo ya Ualimu, Wizara inalifanyia kazi suala hili ili tuweze kuona tunapunguza tatizo hili kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine alilolizungumzia ni kuhusu Chuo cha Ualimu Sumbawanga, kipandishwe *grade* ili kiweze kutoa stahhada. Mgawanyo wa vyuo kutoa mafunzo ya cheti na stahhada unafanywa kwa kuzingatia mahitaji ya Kitaifa. Aidha, ili chuo kiweze kutoa Walimu wa Stahhada, maandalizi ikiwa ni pamoja na wakufunzi wenye Shahada ya Chuo Kikuu na vifaa vya kufundishia yanatakiwa. Lakini hata hivyo, andiko lipo linafanyika la MMES, ambalo litazingatia upanuzi wa vyuo vyetu ili viweze kuchukua idadi kubwa ya Walimu.

Mheshimiwa Profesa Feetham F. Banyikwa, alizungumzia mambo mengi hasa Programu ya Mafunzo Maalum ya muda mfupi kwa wahitimu wa kidato cha sita kwamba ni nzuri na isibezwe na mtu yeyote. Programu hii ni nzuri tu kwa sababu tunapoiningia katika mfumo huu wa kuleta mapinduzi katika elimu ni lazima tutegemee mpango huu ili tusiende kuchukua watu kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa pongezi za Mheshimiwa Profesa Feetham F. Banyikwa, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuwaendeleza Walimu wa Mafunzo Maalum ya muda mfupi.

Mheshimiwa Banyikwa pia alizungumzia uhaba wa Walimu katika shule za msingi za Ngara na shule za sekondari. Suala hili tumelizingatia, tutaendelea kutoa Walimu katika Wilaya ya Ngara lakini tunachoomba, wananchi na Halmashauri wajipange kuwapokea Walimu katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Juma H. Killimbah na Mheshimiwa Raynald A. Mrope, walizungumzia kuhusu masuala mbalimbali. Waliipongeza Wizara na wanapendekeza Walimu hawa wanaojiendeleza, waendelezwe zaidi ili kuweza kufikia stahada na shahada ili wanafunzi waweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizo tumezipokea. Walimu hawa watajumuishwa katika utaratibu wa mafunzo kazini na wale wenye msukumo na nia na ari ya kujiendeleza, watapata mafunzo mazuri na watajiendeleza na watahitimu na kuwa Walimu wazuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia walizungumzia kuhusu Vituo vya Walimu (*Teacher Resources Centers*) viimarishwe. Mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kutumia vituo hivi vya Walimu tumeyapokea na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa pia hawa walisema kwamba, uandaliwe Mpango Maalum wa Mafunzo Kazini, ambao ni pamoja na *upgrading* ya Daraja A kwenda stahada na hadi kufikia shahada na wale wa stahada kwenda shahada. Hili tumelizingatia na hivyo ndivyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia walisema kwamba, Walimu waelimishwe juu ya umuhimu wa kuvuta subira hasa kuhusu ujenzi wa nyumba za Walimu. Suala hili ukiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wetu wa Elimu imefafanua vizuri na imezungumzia suala la ujenzi wa nyumba za Walimu hasa katika maeneo ya pembezoni, ambayo ni maeneo ya mazingira magumu. Nyumba za Walimu za kutosha zitajengwa huko na tunaomba waendeleo kuwa na subira.

Mheshimiwa Pindi H. Chana, alizungumzia kuhusu vyuo visivyo na umeme, Wizara iweke mkakati wa kuviunganisha na umeme wa Gridi ya Taifa au vipate umeme wa *solar*. Baadhi ya vyuo hutumia *generator* vile ambavyo havijaunganishwa kwenye gridi lakini hili alilolizungumza tutalizingatia na kuhakikisha kwamba, tunatumia umeme wa *solar* ili tuweze kupata teknolojia Tehama katika Vyuo vya Ualimu. Vyuo vinavyotumia *generator* vitapewa wa *solar*, ikiwa ni pamoja na Chuo cha Ualimu cha Tandala.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia pia programu ya kuandaa Walimu kwa muda mfupi iwe ni ya mpito. Ni kweli kabisa mpango huu ni wa mpito tukishamaliza tukapata Walimu wa kutosha tutaingia katika Mpango Maalum ambao ni wa kawaida kwa ajili ya kupata Walimu waliohitimu vizuri.

Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, anasema Wizara ikifanye Chuo cha Shycom kuwa Chuo cha Biashara. Kuanzia mwaka huu 2007/2008, Chuo hicho kitaanza

kutoa mafunzo ya Stahada ya Biashara kwa sababu ni mchepuo ambao tumeurudisha. Wala asiwe na wasiwasi kuhusu jambo hili na Walimu wataingia hivi karibuni tu.

Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Juma H. Killimbah, walizungumzia kuhusu Serikali ioneshe dhamira ya kuinua michezo na kurudisha mashindano shuleni na vyuoni. Hili tumelizungumzia katika hotuba na mpango thabiti umepangwa ili tuweze kuhakikisha kwamba, michezo inarudishwa mashuleni na katika Vyuo vya Ualimu na mashindano yataendelea katika ngazi ya shule na shule, kata na kata na hata katika tarafa na katika likizo ndefu tuweze kufanya mashindano katika Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, matengenezo ya Vyuo vya Ualimu nayo haya tumeyazingatia. Vipo vyuo mbalimbali vitakavyokarabatiwa. Tunavyo vyuo vitano ambavyo vitapewa fedha kwa ajili ya kukarabatiwa mwaka huu.

Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, alisema Chuo cha Ualimu Kasulu kiendeleze kutoa mafunzo ya Daraja A, kwa sababu wanachuo wa Stashahada hawajai. Halafu pia kuwe na mkondo wa sayansi katika chuo hiki. Maombi haya tumeyazingatia na tutaangalia ni jinsi gani ya kuweza kuyatekeleza yote haya ili tuweze kupata Walimu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, yapo mambo mbalimbali waliyotoa kama maoni kwa mfano, tunahitaji kuwa na Walimu wenye sifa zinazotakiwa katika kutoa elimu bora. Hili limezingatiwa na Wizara hii na ukiangalia Hotuba ya Waziri imezungumza sana juu ya suala la mafunzo ya Walimu kazini kwa sababu hii ni njia mojawapo ya kuweza kuboresha Walimu wetu ili waweze kufanya kazi nzuri ya kuboresha elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni Mpango Maalum wa Mafunzo Kazini (*in-service*). Hili suala nalo tumelizingatia kwa ajili ya Walimu wa Shule za Msingi na Shule za Sekondari watakuwa na *in-service training* na *upgrading courses* ili tuweze kupata Walimu wazuri zaidi. Walizungumzia kuhusu chombo kimoja cha ajira ya Walimu ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi sana wamechangia katika hili. Suala hili ni la muda kidogo, tumekuwa tukisikia Waheshimiwa Wabunge wengi wakizungumzia. Ni kweli lazima Walimu wawe na chombo kimoja na Wizara yangu inalishughulikia ili kuhakikisha kwamba Walimu wanashughulikiwa na chombo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, walizungumzia pia kuwa na mkakati utakaofanikisha wanafunzi katika shule za msingi na sekondari kusoma na kufaulu masomo ya lugha hasa Kiswahili na Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo la kushindwa masomo ya lugha, Wizara yangu inachukua hatua zifuatazo: Kwanza ni kuangalia mitaala na Walimu katika vyuo vyetu vya ualimu. Hili suala linashughulikiwa na wako Walimu katika Chuo cha Mpwapwa wanafanya kazi ya kuangalia mitaala na kuiboresha. Aidha, Mpango wa Mafunzo ya Walimu Kazini unaolenga kuimarisha mbinu za kufundishia na kujifunzia unatolewa ili kuboresha Walimu hawa.

Mheshimiwa George M. Lubeleje, amezungumzia mambo mengi lakini hasa kuhusu *induction course*, kozi ya Walimu wetu hawa wanaomaliza *form six*. Katika kipindi cha kufanya mageuzi makubwa ya elimu ni lazima kuangalia upya jinsi ya kuandaa Walimu. Njia hizi ni pamoja na kuangalia muda wa mafunzo bila kuathiri ubora wa Walimu wanaopatikana. Kati ya mwaka 2005/2006 na 2006/2007, wahitimu wa kidato cha sita wapatao 9,054 wamepata mafunzo maalum ya muda mfupi na mafunzo waliyozingatiwa ni hasa mbinu ya kufundisha na kujifunzia, ujana na makuzi, taaluma ya elimu na ualimu na muundo wa utawala wa shule. Maeneo haya yanafundishwa kwa umakini na ni dhahiri yanawapa mbinu za kutosha za kumudu shughuli za ufundishaji katika shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine alilouliza kwamba, je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ukarabati? Wizara ilitenga shilingi 115 milioni kwa mwaka 2005/2006, kwa ajili ya ukarabati wa majengo mbalimbali. Fedha hizi ni kwa ajili ya majengo mengi ya utawala, pamoja na mabweni lakini kwa nyumba za Walimu bado fedha zinatafutwa ili ziweze kufanya kazi hiyo. Aliuliza je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule ya sekondari ambayo itakuwa ya Chuo cha Ualimu Mwapwa? Mpango huo upo na shule ya mazoezi itajengwa kwa sababu tunajua kumfundisha Mwalimu ni pamoja na kuhakikisha kwamba, anafanya mazoezi yatakayomsaidia yeye kuhitimu na kuwa Mwalimu aliye bora kuliko Mwalimu ambaye hajafanya mazoezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naingia katika hoja za vyuo vya *VETA*. Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, pamoja na Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, walizungumzia kuhusu Chuo cha *VETA* katika Mkoa wa Lindi na kwamba kitaanza lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Vyuo vya Lindi, Manyara, Pwani na Dar es Salaam, unafanyika kwa mkopo kutoka Serikali ya Korea ya Kusini. Msanifu wa Majengo amekamilisha michoro ya vyuo hivyo chini ya mradi huu. Aidha, zabuni za kuwapata wajenzi zimeshatangazwa kwa *international tendering* na zitafunguliwa mwishoni mwa mwezi huu wa Julai, 2007 na ujenzi utanza 2007. Ujenzi na ufungaji wa vifaa vya mafunzo utakamilika mwishoni mwa mwaka 2009 hivyo mafunzo yataanza baada ya kumalisha kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Wabunge waliochangia katika ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya zao nao ni Mheshimiwa Profesa Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Balizi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga na Mheshimiwa John S. Malecela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujibu hoja hizi kwa pamoja, Wizara yangu imeunda Kamati Maalum ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Uanzishwaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya. Kamati hiyo inaandaa mpango wa utekelezaji na itakamilisha taarifa yake mwezi Novemba, 2007. Taarifa hiyo itaainisha utaratibu mzima wa utekelezaji na

Wilaya zipi zipewe kipaumbele. Baada ya kazi hii kukamilika, Waheshimiwa Wabunge wote mtapewa taarifa ili kila mtu afahamu yuko katika mpango wa kuanzia lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu inawasiliana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuvigeuza baadhi ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) na asasi zisizo za Kiserikali kuwa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa na Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, walizungumzia vyuo vinavyojulikana kama *polytechnics* kwamba, vijengwe katika Mikoa ili viwe chimbuko la stadi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya lengo la vyuo vya aina hiyo ni kuleta uainisho kati ya mafunzo yanayotolewa katika ngazi ya juu ili wahitimu katika ngazi hiyo ya ufundi stadi (*Vocational Training*), waweze kupatiwa fursa ya kuendelea na mafunzo katika ngazi ya juu. Aidha, Kamati Maalum (*Task Force*) imeundwa ambayo inajumuisha wataalam kutoka *VETA*, Baraza la Elimu ya Ufundi (*NACTE*), kwa lengo la kuandaa taratibu zitakazowezesha wahitimu katika ngazi ya ufundi stadi kuendelea na mafunzo ya juu kupitia vyuo vya ufundi vilivyopo (*Technical Colleges*). Kamati itakamilisha kazi hii mwishoni mwa mwaka huu na tutajulishwa ili tuweze kuona ni jinsi gani vijana wetu watakavyoweza kupanda katika masomo.

Mheshimiwa Mariamu S. Mfaki alisema Wizara iangalie uwezekano wa kukopesha wahitimu wa *VETA* vifaa vya kuanzishia miradi wanapomaliza masomo. Suala hili limezingatiwa na Vyuo vya Mikumi, Mtwara na Dodoma. Kwa kuanzia vimeanza kutoa vyombo vya kuanzia maisha wakati wakishamaliza lakini utaratibu huu tunategemea utasambazwa katika vyuo vyote.

Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, naye pia alizungumzia Vyuo vya *VETA* kushirikiana na *SIDO* katika kuwawezesha wahitimu wa *VETA* kujiajiri ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo ya kununulia vifaa vya kuanzishia maisha.

Mheshimiwa William H. Shellukindo, alitoa ushauri mzuri sana na akatoa mafunzo kuhusu *VETA* ili iweze kusomeka sio mafunzo ya ufundi pekee bali pia ni mafunzo ya stadi za kazi ambayo najua na Wizara ya Kazi nayo itakuwa inazingatia hilo. Hilo tutalizingatia na tutahakikisha kwamba na mitaala yake inalenga katika kufundisha watu waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Hassan J. Killimbah alizungumzia wanafunzi wenye vipaji maalum watambuliwe. Hili tumelizingatia, tumepokea ushauri na tumeuzingatia.

Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, alizungumzia juu ya *skill development levy* iweze kusaidia kuboresha Vyuo vya *VETA* na ikiwezekana kujenga vyuo hivi. Suala hili limezingatiwa na Wizara yangu inatazama uwezekano wa kuomba Wizara ya Fedha kuongoza mgao wa *SDL* kutoka asilimia mbili hadi asilimia nne.

Mheshimiwa Charles N. Keenja amesema kuwa, hakuna mipango mikubwa ya kuendeleza elimu na mafunzo ya ufundi stadi katika bajeti hii. Kwa sababu suala hili la *VETA* lina mipango ambayo ni thabiti, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tunapenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, tayari Wizara yangu imeanza kuandaa mpango wa muda mrefu wa kuendeleza mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, aliomba Chuo cha Katandala kiweze kupewa hadhi ya Chuo cha Mkoa. Hili suala tunalifanyia kazi pamoja na kwamba kipo Chuo cha Mpanda ambacho ni cha Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *VETA* kubinafsishwa hilo halipo kwa sababu Serikali haina mpango huo. Lengo ni kuiendeleza *VETA* kiwe ni chombo cha wananchi kitakachofanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji anasema Vyuo vya *VETA* viwe na wataalam watakaokuwa wanatoa mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hili tumelizingatia. *VETA* imeshaanza kuwafundisha Walimu wa ufundishaji mafunzo maalum ili kuwawezesha kufundisha wanafunzi wenye ulemavu. Katika mwaka huu wa fedha, Vyuo vya *VETA* vitafundisha wanafunzi wenye ulemavu wapatao 102 kwa lengo ya kuwaandaa ili waweze kujiajiri au kuajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, amezungumzia kuhusu *VETA*, nalo hili tumelizingatia. Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Chuo cha Ufundi Stadi *VETA* Mtwara hakina Walimu. Walimu wa *VETA* Mtwara wako masomoni pale Chuo cha Morogoro, wako watano wakimaliza wanaendelea kwa sababu wako pale kwa muda lakini chuo hiki hakina matatizo.

Mheshimiwa Felister A. Bura, anasema watoto wenye uwezo wanaomaliza darasa la saba, kidato cha nne waweze kujiunga na Vyuo vya *VETA*. Mpango huo unazingatiwa vizuri tu na tutaendelea kuhakikisha wanajiunga na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Omar Ali Mzee anatoa pongezi kwa *VETA* kwa ubunifu na jinsi wanavyofanya kazi zao kwa hali bora. Serikali ivipe msukumo wa kutosha ili kuendeleza kazi walizojipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inashukuru kwa pongezi za Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wengine walioipongeza Wizara kwa kazi nzuri tunazozifanya lakini ni pamoja na ushirikiano wao. Mimi nawahakikishia kwamba, ushauri mliutoa kwetu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, *VETA* inafanya kazi vizuri pamoja na vyuo vya ualimu tunauzingatia na sisi tutahakikisha kwamba, tunafanya kazi yetu vizuri ili kuweza kukidhi yale matarajio mnayokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hapa. Asante sana na naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mnaona Wizara ya Elimu ilivyo na nidhamu, namwomba sasa mtoa hoja.



**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge lako Tukufu ili na mimi nizungumzie kuhusu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wale wote walioniwezesha kuwa hapa mbele yenu nikiwa kama Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa sababu bila wao kunichagua kuwa Mbunge wao, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asingeniona. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Lakini pia naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na Mheshimiwa Spika, watoto wangu pia kwa sababu bila wao mimi nisingeweza kwa sababu naamini kabisa nyuma ya mama aliyefanikiwa yupo maba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi ambavyo wamechangia kikamilifu hotuba yangu kwa kutoa ushauri, maoni na mawazo, ambayo kwetu sisi tumeona ni ya msingi sana na tutayafanyia kazi katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa jinsi muda ulivyo, sitaweza kupitia hoja zote hivyo, natanguliza kuomba radhi lakini naahidi hoja zote zitafanyiwa kazi zitatolewa majibu, ufafanuzi na hatimaye mtapata majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwataja Waheshimiwa Wabunge wote, walichaongia kwa kuongea kama ifuatavyo: Mheshimiwa Anna R. Lupembe, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Magret Agness Mkanga, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Ledian M. Mng'ong'o, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Fred M. Tungu, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu na Mheshimiwa Benedict K. Losurutia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia hotuba kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Balozzi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Dr.

Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Shally J. Raymond, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Victor K. Mwambalasa, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Lawrence K. Masha, Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Manju S. O. Msambya, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said. *(Makofi)*

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Maria I. Hewa na Mheshimiwa Omar Ali Mzee. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi kama wengine sikuwataja lakini nia ilikuwa ni nzuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na jumla ya wachangiaji 88, nimewataja ambao walichangia kwa kuongea na kwa maandishi lakini pia walichangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa pongezi nyingi mlizotupa. Tunawashukuru sana na tunaona hizi pongezi zitatusaidia kwani tunamwomba Mwenyezi Mungu, mwaka kesho ndiyo tufanye vizuri zaidi kwani mmetupa moyo sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi na wadau wote katika kuchangia ujenzi wa shule za sekondari. Juhudi hizo ndizo zimewezesha wanafunzi wengi kujiunga katika shule za msingi lakini na hasa katika shule za sekondari kwa miujiza tuliyoiona. Shule 488 mwaka 2006, yaani mwaka 2006 na sasa hivi shule 1,084 na hapa ninapooonea tayari zimeshaongezeka tunasema 1,089. Mpaka kuja kufikia Jumatatu zitakuwa zimefikia 1,090. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema Kambi ya Upinzani baadhi ya maneno waliyoandika ninaamini kabisa kesho ukiwauliza watayakataa na hii inadhihirisha kutokana na uchangiaji wa Waheshimiwa Wabunge, ambao wao wenyewe wamekiri kwamba ni mafanikio na tuwe tunakubali pale ambapo Serikali imefanya vizuri. *(Makofi)*

Kwanza, walisema kwamba mipango haikuandaliwa vizuri ni kama ya zimamoto. Tulichokifanya kinatokana na Mpango wa MMES na mipango iliyoandaliwa vizuri sana kwa umahiri na kwa kufanya utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali daima haipangi mipango yake kwa staili ya zimamoto. Kimsingi MEM na MMES ni mipango inayotokana na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu, yaani *SDP Education Sector Development Program* ya mwaka 1997, iliyotokana na tafiti mbalimbali za kina na aidha utayarishaji wa *SDP* ulihusisha wadau mbalimbali zikiwemo Kamati za Shule, Wazazi, Wahisani na Taasisi zisizo za Serikali. Hivyo basi, MEM na MMES ni mipango thabiti ya awali iliyo na dira na mwelekeo katika kuleta ubora wa elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu letu sisi Watanzania kukimbia wakati wenzetu wanatembea kwa mfano, takwimu zinazoonesha kuwa uandikishaji wa wanafunzi wa sekondari katika nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2004 ukijumuisha, yaani nchi zote tatu zikijumuishwa pamoja na Tanzania yenyewe. Tanzania ilikuwa na 21%, yaani wanafunzi 432,599 katika sekondari ikiwa nyuma ya Uganda iliyokuwa na 34% ambayo ni sawasawa na wanafunzi 697,507 na Kenya 45% ambayo ni sawasawa na wanafunzi 923,100. Lakini ukiangalia kwa uwingi wa watu (*population*), Tanzania ndiyo inayoongoza ikifuatiwa na Kenya na Uganda lakini wakati huo ndiyo tukawa wa mwisho. Kwa hiyo, kama nilivyosema, lazima tukimbie wakati wenzetu wakitembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu ilitangaza kwenye Kitabu chake kuwa tutakuwa na ujenzi wa nyumba 1,500 zenye gharama ya bilioni 13.1 na vifaa vya kujifunzia na kujifundishia vya bilioni 15 na mafunzo kazini ya walimu ya bilioni moja, zote hizi ni juhudi za kuimarisha ili tuwe na elimu bora. Kwa hiyo, si kweli kwamba wanafunzi wanaingizwa madarasani bila kuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba, wanapata elimu bora. Kwa hiyo, hilo nataka kulihakikisha Bunge lako ili lijue hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninataka kuzungumzia suala la kupeleka fedha mikoani. Mwaka 2006 katika Bunge hilihili, tulitumia utaratibu wa kupeleka fedha mikoani. Kwa upande wa vyumba vya madarasa tulipeleka 70% kwa Mikoa yote, halafu 30% ikaongezwa kwenye Mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo na ndivyo hivyo hivyo tutakavyofanya mwaka huu. Kwa upande wa vyumba 800 vya madarasa tutakavyojenga,

70% itakwenda kwenye Mikoa yote lakini 30% itapelekwa kwenye Wilaya zenye hali ngumu au ambazo ziko nyuma na utaratibu unaotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi tuliona kwamba utaratibu ambao tulikuwa tukiutumia kwa kupeleka fedha ni vizuri tukaendelea nao huohuo kwa sababu madarasa hayo 800 ambayo yatajengwa tumeona ni vizuri yakaenda kuimarisha zile shule ambazo tayari zimeshaanza kujengwa. Kwa msingi huo, kwa kuwa shule zile zinazoendelea kujengwa zinajulikana, fedha zitapelekwa moja kwa moja kwenye shule ambazo zinajengwa. Kwa hiyo, kutakuwa hakuna haja ya kubadilisha utaratibu wa kupeleka fedha, kitu cha maana tu ni kwamba tutakapowaomba mlete taarifa wapi ambapo fedha zinatakiwa kwenda, basi tunawaomba mlete kabla ya 15 Septemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumevitaja wakati huohuo kwa sababu tumeona tuwape muda kidogo Waheshimiwa Wabunge warudi majimboni ili wakashirikiane na Uongozi wa Mikoa katika kuamua wapi na shule gani zitasaidiwa kupewa yale madarasa 800. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge mkienda kule, mshirikiane kuamua wapi madarasa yataongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa nyumba za walimu, hizo nyumba 1,500 tumeona kwamba zigawanywe kwa Mikoa yote, kwa sababu kwa vyovyote vile nyumba za walimu zina matatizo, yaani zina upungufu katika mikoa yote. Kwa hiyo, nyumba 1,500 kila mkoa utapata nyumba 70 za walimu. Ombi letu kwenu Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, mkifika mkaamue hizo nyumba 70 zitajengwa wapi ili kuona kwamba Wilaya ambazo walimu hawakai kutokana na uhaba wa nyumba, ndiyo mkazo utiliwe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunaomba hili nalo mkatusaidie kwa sababu mwaka 2006 tulipata malalamiko, baada ya kupeleka fedha mikoani baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawakuhusishwa kwa hiyo, ikatuletea matatizo sana kwamba hawakushirikishwa na kadhalika. Safari hii tunaomba Uongozi wa Mikoa yote Tanzania, ihusishe viongozi katika kuamua wapi nyumba za walimu zikajengwe na wapi madarasa yakaongezwe ili kupunguza malalamiko. Lakini pia tumechukua ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ambao mmetaja wazi kabisa kwamba ni vizuri tukatumia utaratibu wa kutumia majeshi yetu pale inapowezekana, kwa mfano, JKT au Maaskari Magereza na wote ambao wanashughulika na mambo ya ujenzi. Kwa hiyo, ushauri wenu tumeuzingatia na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililozungumzwa kwa uchungu sana ni suala la mdondoko wa wanafunzi na mdondoko wa wanafunzi kama inavyoonesha kwenye *base* katika kile kitabu cha takwimu tulichowapa ziko sababu nyingi. Wanafunzi wengine wanaacha shule kwa sababu ya utoro tu lakini wapo wengine kweli ni suala la mamba, lakini wengine ni utoro tu wanaacha katikati, kwa kweli ni jambo la uchungu. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amelizungumzia kwa uchungu sana na viongozi wetu wote wa ngazi za juu wameliongelea kwa uchungu sana. Kwa hiyo, sisi kama Wizara ya Elimu, kwa kweli tunatoa wito kwa wazazi, tuanzie wazazi, wafuatilie maendeleo ya wanafunzi wao shuleni, haitoshi kumfikisha mtoto shuleni na

kumlipia ada halafu mwenyewe ukapotea. Kuna umuhimu wa kufuatilia maendeleo ya watoto wetu shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo linasababisha mdondoko wa wanafunzi kwa wingi ni ukosefu wa chakula la mchana. Tunatoa wito kwa viongozi wote wa Wilaya na Mikoa kuhakikisha kwamba, shuleni walimu na Kamati za Shule wanashirikiana katika kuhakikisha kwamba, wanafunzi wanapata chakula la mchana angalau uji kwa sababu wengine wanakimbia shule kutokana na matatizo ya njaa.

Suala lingine ambalo liliongelewa kwa uchungu sana ni suala la chombo kimoja cha walimu ambacho Naibu Waziri amezungumzia kwa kifupi, lakini niliona kwa kuwa ni suala ambalo limezungumziwa sana ni vizuri nitaje waliohusika katika kulitaja. Nao ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mwenyekiti wetu wa Huduma za Jamii, Mheshimiwa Magret Agness Mkanga, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Castor R. Ligallama.

Nakumbuka hata Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba alisema kwamba, ataondoka na shilingi yangu hata kabla ya wakati kufika lakini nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, suala hili linafanyiwa kazi sasa hivi na Serikali itaamua kuhusu suala hilo kadri ambavyo itaonekana inafaa. Nataka kuwahakikishia walimu kwamba, suala hili linafanyiwa kazi, kwa hiyo, natoa wito kwa walimu wote kufanya kazi kwa bidii sana wakijua kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne inawajali na inawasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilizungumziwa kwa uchungu sana lilikuwa ni suala la mimba shuleni, ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. Walilizungumzia pia Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, ambaye naye alitoa matamshi ambayo wengi hapa tukaogopa jinsi ya kushughulikia watu wenye mamba na Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, ambaye naye alilizungumzia kwa uchungu sana suala hili.

Lakini kama nilivyosema, ukiangalia kwenye hotuba katika sehemu ya kurasa za maamuzi muhimu, tumezungumzia kwamba, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imeibua mjadala huo wa jinsi ya kushughulikia upunguzaji na hata kumaliza suala la mimba shuleni. Lakini pia kuona ni jinsi gani tutakazia kuwabana wanaohusika na kuwapa mimba watoto shuleni. La mwisho katika uamuzi huo tumesema kwamba, kuibua mjadala, kuangalia kama kuna uwezekano wa kuwarudisha watoto shuleni watakojifungua.

Lakini kama nilivyosema, tumeibua mjadala na tunaomba Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge, mtuletee maoni yenu kwa njia ya mawasiliano ya barua, hata kwa njia ya ana kwa ana, tunataka kuona hili suala litafikia wapi ukiangalia jinsi wasichana wengi wanavyopoteza elimu yao kutokana na kujifungua au kupata mimba wakiwa shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kumalizia hotuba hii kwanza, kwa kuwashukuru Wabunge wote ambao mmechangia na kusema kwamba maoni yenu tumeyasikia na labda mniwie radhi, kuna suala la kuongeza mikondo, hili ni lazima niliseme hapa. Ni kwamba ili kupunguza gharama za ujenzi wa shule hasa ukiangalia miundombinu ile muhimu kama Maabara, Maktaba na Majengo ya Utawala, tuliona ni vizuri turuhusu kama Wizara ya Elimu tuongeze mikondo ili shule ziwe na mikondo minane. Nadhani hili wengi walikuwa wanapenda kulisikia. Kuanzia sasa Wizara ya Elimu imeruhusu Shule ziendeleze kuongeza mikondo mpaka ifike mikondo minane, zaidi ya hapo itabidi uwasiliane na sisi kwa sababu si vizuri kama walivyoongea Meshimiwa Bujiku P. Sakila na Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba. Mmoja alizungumzia kwamba si vizuri shule ikawa na mikondo mingi lakini Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba akazungumzia kwamba ni vizuri kutumia mali vizuri zaidi kwa kuongeza mikondo. Kwa msingi huo, tumeona kwamba ni vizuri shule ikaendelea mpaka ikawa na mikondo minane lakini zaidi ya hapo itabidi kuomba kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, namalizia kwa kusema ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, tutawaandikieni vizuri mtapata majibu. Ninaomba kwa ruksa yako niwataje wachache ambao niliwaacha ambao wameona kwamba si haki nisiwataje hapa.

Mheshimiwa Ephraim N. Madeje, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Martha J. Umbulla na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami. *(Makofi)*

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza, nawashukuru sana kwa yote. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa tunaendelea na hatua nyingine.

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 46 - Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 - *Administration and General*..... Sh. 9,920,695,500

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga, Mheshimiwa Magreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya. Tunaanza na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *Vote Number 46, Sub Vote 1001* na Kifungu 250100 - Mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Naomba tu anisaidie katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba pia uwezekano Chuo cha Ualimu cha Matogoro kukifanya kiwe Chuo cha Ualimu katika Madaraja yote, yaani *Diploma, Advanced Diploma* na *Degree*. Sasa sijasikia majibu, naomba anisaidie.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Mheshimiwa Mbunge, tumelisikia lakini naamini kabisa na ninakumbuka nilipokuwa nikitoa hoja ni kwamba, tuna andiko la Mpango wa MMES, ambalo linaangalia upanuzi wa Shule za *A – Level* pamoja kuongeza nafasi za Vyuo vya Ualimu. Namwomba avute subira suala hilo linafanyiwa kazi. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Sub-vote 1001* - Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kusema kweli nimefurahishwa sana na mipango ilivyosomwa kwenye kitabu hiki. Nimefurahishwa pia na watu wengi wanapozungumzia juu ya shilingi trilioni moja kwa elimu. Lakini nikiangalia kwenye *Vote* hii mbona namhurumia Mheshimiwa Waziri kwamba, anataka kweli mwaka kesho mambo yatakuwa mazuri lakini hana fedha. Fedha aliyopewa mwaka 2006 imepungua sasa ni 4.9% ya bajeti, fedha ambayo amepewa kwa ajili ya maendeleo ni 89% anategemea *source* ya *World Bank* zaidi ya 68%. Madarasa ambayo anataka kujenga 1,631 kufuatana na kitabu ingawa aliponiambia alipokuwa anajibu wakati akizungumza juu ya madarasa 800, sasa ndiyo napata matatizo zaidi.

Lakini watoto atakaopata mwaka huu 2007 wanaomaliza darasa la saba ni laki nane na zaidi. Sasa mimi nashangaa atafanyaje hii kazi au kuna mikakati nje ya bajeti ambayo itafanya watoto laki nane na zaidi waingie kidato cha kwanza? Madarasa tu ukifanya kwa haraka haraka ni zaidi ya arobaini elfu na wewe unajenga elfu moja. Kwa hiyo, napenda nielezwe hivi fedha ambazo tunaambiwa shilingi trilioni moja ukiongeza hela ambayo inakwenda elimu ya juu shilingi bilioni mia mbili sitini na tisa kufuatana na vitabu. Jumla inayokwenda kwenye Wizara yake shilingi bilioni mia mbili sitini na tano, ukiongeza pamoja pale unapata shilingi bilioni sitini na mbili, hizi nyingine inayobaki shilingi bilioni mia nne na sitini na tano ziko wapi? Labda zile zingechukuliwa apewe Mheshimiwa Waziri ili aweze kufanya kazi ambayo ametuambia atafanya hapa. La sivyo nasema tunaondoka hapa Waheshimiwa Wabunge hatuna chochote cha kurudisha kwa wananchi wetu kwa Wizara hii ya Elimu, licha ya maneno mazuri pamoja na mipango mizuri naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Kuhusu hoja aliyoitoa Mheshimiwa John M. Cheyo nataka tu nijibu kama ifuatavyo: Kwanza, angeangalia ukurasa wa 17 wa hotuba ya bajeti, siyo idadi hiyo aliyoisema, kwa hiyo, idadi aliyoitoa ni ya mwaka 2006. Lakini pia nataka kusema kwamba, fedha zilizotengwa kwa ajili ya Sekta ya Elimu zipo ambazo tayari

zimeshaonekana kwenye hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa ajili ya shule za msingi. Hizi zilizobaki zinazotajwa leo ni kwa ajili ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kumjulisha Mheshimiwa Mbunge aliyezungumza kwamba, ndiyo maana tunazungumzia umuhimu wa wananchi kuchangia na napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mimi nimefika Bariadi. Katika sehemu ambayo wananchi wameamka ni Bariadi na hasa Jimbo analotoka Mheshimiwa Mbunge. Nimekuta vijiji wamegawana nyumba za walimu tatu na wao kutokana na uamuzi wao wameamua wananchi wale wachimbe msingi wakiwasaidia *engineers* na akinamama wanaokota mawe, ndiyo maana tunaomba ushiriki wa wananchi. Kwa hiyo, tunakuomba Mheshimiwa Mbunge utusaidie ili wananchi waendeleo na moyo huo huo, kwa sababu nchi hii itajengwa na wenye moyo. (*Makofi*)

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina matatizo na dhana ya wananchi kuchangia na kama alivyosema wananchi wa Bariadi huchangia sana na mengine sitaki kuyasema. Mimi mwenyewe mwaka huu nitaongeza mchango wangu, baada ya kuangalia bajeti haina chochote nitaongeza. Lakini *issue* ni kwamba, ...

**MWENYEKITI:** Shilingi milioni ngapi, mara ya mwisho ilikuwa shilingi milioni mbili tu?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ni kwamba, tutaendelea mpaka lini tunapanga mipango ambayo tunategemea *almost double taxation* kwa wananchi, ambayo inategemea tu mchango wa wananchi au fedha kutoka nje. Ndiyo hiyo *issue*, napenda kuona kwamba, angalau mwaka huu tuendeleo, mwaka unaokuja kidogo michango itaanza kupungua na wananchi watapata nguvu ya kuchangia zaidi na zaidi. Lakini kama kila siku Wizara hii inatengewa asilimia nne ya bajeti ili wananchi wachangie, hii hairidhishi ndiyo maana nasema kwamba, Mheshimiwa Waziri ni wa kumhurumia maana yake Serikali haimpi hela na tuondoke hapa tunajua hilo kwamba, hakuna hela ambayo itaweza kusaidia elimu, ni mchango tu. Hili ndilo tatizo nililionalo, lakini hakuna mtoto wa Bariadi ambaye mimi nitasimama kusema kwamba usichangie, hapana nitachangia, lakini tunataka Serikali itushike mkono na kwenye mahesabu haya, ndiyo tatizo nililionalo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama una la kuongeza, ongeza.

Waheshimiwa Wabunge ukweli ni kwamba, nchi hii itajengwa na wananchi. Kwa hiyo tunaendelea. (*Makofi*)

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *Vote 46*, programu ya 10, *subvote 1001* - Mshahara wa Waziri. Nilichangia kwa maandishi, sasa naomba kama ombi langu limezingatiwa kwamba katika ugawaji wa fedha hizi za kusaidia ujenzi wa shule za msingi na sekondari, kiwango kinachotolewa kinafanana nchi nzima. Lakini kwa mikoa iliyo mbali sana na Dar es Salaam ambako kuna viwanda au sehemu za viwanda, fedha hii unakuta ni kidogo sana, haisaidii kwa vile bei ni kubwa sana ya bidhaa kama sementi, mabati, misumari na



vinginevyo. Kwa mfano, Mkoa wa Kagera, mfuko wa sementi Mjini Bukoba ulikuwa shilingi elfu kumi na nane, nadhani sasa hivi utakuwa unafikia shilingi elfu ishirini lakini hapo mfuko huo haujafika Mrongo, Mgoma, Mrusagamba na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nimeomba ni namna gani wanafikiria kuangalia tatizo hili ili fedha igawiwe kulingana na hali ya mikoa, tusilinganishe kwa vile ukilinganisha Dar es Salaam na Morogoro unakuta kwamba, kwa kweli maeneo yale yanaumia sana? Kwa hiyo, nimeomba kuwe na utaratibu wa kugawa hizi fedha kulingana na mahitaji halisi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaheshimu sana ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutalifanyia kazi lakini hasa tutakapoingia mkataba mpya na *World Bank*. Kwa sasa hivi tumeomba tuendelee na utaratibu ambao ni fedha za mwisho katika utaratibu tuliokubaliana nao. Tutakapoanza utaratibu mpya, yote haya yatazingatiwa. Naheshimu ushauri wake. *(Makofi)*

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuongea. *Program 10, subvote 1001, kifungu kidogo 250100 - Basic Salaries and Pensionable Posts*. Wakati nachangia na wakati pia Naibu Waziri akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ruth Msafiri tarehe 22 Juni, 2007 kuhusu udhibiti wa mitihani ya darasa la saba, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu na naomba kunukuu: “Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tayari Wizara yangu imeshafanyia kazi marekebisha na mwaka kesho kutakuwepo na mtihani mara baada ya wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza. Itakapofika mwezi wa tatu, kutakuwa tena na mtihani na mtihani huo utakapobaini waliofanya vibaya, watarudishwa kwa sababu hicho kitakuwa ni kigezo kizuri cha kuweza kudhibiti badala ya kungoja mpaka watakapofika kidato cha pili.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu hapa ni kwamba, naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kama kweli hii ni sera kwamba kuanzia mwaka kesho kutakuwa na mtihani wa pili kwa kidato cha kwanza ili kuwadhibiti wale walioiba mtihani. Kama hivyo ndivyo, nadhani ni makosa kwa sababu yule mtoto hajaiba ule mtihani na kwamba wanaohusika ni Baraza la Mitihani au walimu. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, atoe tamko kama kweli Serikali kuanzia mwaka 2008, mtakuwa mnatoa mtihani wa pili kwa wanafunzi wote wa kidato cha kwanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumjibu Mbunge Suzan Lyimo, kuhusu wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza kama alivyozungumza katika hoja yake. Ni kwamba, kweli siku za nyuma, udanganyifu ulikuwa mkubwa sana kiasi ambacho wale waliokuwa wanapelekwa kwenye shule maalum, baada ya kuonekana hawafanyi vizuri kama walivyotegemewa kwa shule ambayo ni ya vipaji maalum, walikuwa wakipewa mtihani fulani pale pale shuleni ili kupima uwezo wao na wale waliokuwa wakifanya vibaya kinyume na mategemeo, walikuwa wakipelekwa kwenye shule za kawaida na siyo kurudishwa nyumbani. Kwa hiyo, nilitaka nisawazishe hivyo tu.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kutokana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kabisa kwamba, yale maelezo ya awali ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayakuwa *correct*. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri, atuambie kama yale aliyoyasema ni hivyo kwa sababu wazazi wengi wamekuwa na masikitiko makubwa sana kuhusu hilo tamko la Mheshimiwa Naibu Waziri? Sasa naomba kama Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anamaanisha hayo aliyosema, Mheshimiwa Waziri au yeye alikuwa anamaanisha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza katika shule zote kwa sababu alichosema Mheshimiwa Waziri ni wale wa *special school* lakini alichokijibu hapa Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwa zile shule zote za Serikali.

**MWENYEKITI:** Kwa *protocol* yetu haituruhusu kwa sababu aliyesema sasa ndiye Waziri wa Wizara hii. (*Makofi*)

**MHE. MAGRETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea. *Vote 46*, programu ya 10, *subvote 100*, *item 250100*, sina haja ya kughasighasi mshahara wa mtu, lakini naomba maelekezo tu. Jana nilipokuwa najaribu kuchangia nilieleza kushangazwa na kutoridhika na kutopatikana kwa ramani ambazo kwa muda mrefu nimeelekezwa kwamba zipo na Wizara zimekwishachora. Sasa hivi zinaelekea kwenye Halmashauri, hazipo kwa sababu bado kuna matatizo, majengo yote ya shule yanayojengwa, vyoo vinavyojengwa, bado havifuati vipimo au staili itakayowasaidia watoto wenye mahitaji maalum kuweza kutumia. Jana nililizungumzia sana hilo. Sasa nataka kufahamu hivi hizi ramani ziko wapi na kama ni Halmashauri ni nani huyo wa kumwuliza; huyo *Engineer* wa Halmashauri ndiye anazikalia au *DO*? Naomba msaada hizi ramani ziko wapi? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilipochangia kwa maandishi niliomba kwamba, katika mfumo wa elimu ya msingi, ninaamini kama sikosei na naomba nirekebishwe kama nitakosea ni kwamba, kuna vitengo fulani fulani kunakuwa na waratibu. Sasa kwa muda nimejaribu kuchunguza chunguza, waratibu wa elimu maalum katika ngazi ya Wilaya hawapo. Watoto wenye matatizo maalum wanaongezeka katika sehemu zetu. Kwa hiyo, ili kusaidia watendaji walio Makao Makuu, ambao ni sita tu ndani ya kitengo cha elimu maalum, nilikuwa nimeuliza kwamba, wakati haujafika ili tuwe na Waratibu wa Elimu Maalum ndani ya Wilaya zetu? Kwa hiyo, nikifafanuliwa hayo tu itakuwa ni rahisi kwenda kufuatilia utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Magreth Mkanga. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwanza tunamshukuru sana Mheshimiwa Magreth Mkanga, kwa jinsi ambavyo amekuwa kila wakati, akitukumbusha umuhimu wa kutilia mkazo elimu maalum. Jambo ambalo sisi kama Wizara tumelizingatia na ukiangalia kwenye maamuzi muhimu utaona kwamba mojawapo ni la Andiko Maalum tunaloliandaa kwa ajili ya Elimu Maalum. Kati ya hayo

mambo yatakayokuwa ndani ya andiko hilo ni hilo hilo la kuangalia akina nani waiangalie Elimu Maalum kwa ukaribu zaidi. Kwa hiyo, ushauri wake ndiyo huo huo unaofanyiwa kazi. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, avute tu subira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ramani. Ramani zipo jambo nitakalolifanya sasa hivi na watendaji wananisikia ni kuhakikisha kwamba, Wilaya zote zinapewa ili kweli michoro hiyo izingatiwe wakati wa ujenzi wa shule. Tuna shule nyingi, mimi nimekwenda Tabora, Mwanga, zile ambazo zina wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ni kweli wanahitaji miundombinu, ndiyo maana tumeona tuandae Mkakamti Maalum wa kuzingatia mahitaji ya vijana wanafunzi wenye mahitaji maalum. Yote yamezingatiwa. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Vote* 46, programu ya 10, *subvote* 1001, kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri. Mchango wangu nimeutoa kwa maandishi, nilizungumzia mambo mbalimbali pamoja na suala la gari kwa ukaguzi katika Wilaya ya Misungwi. Nimeeleza hayo na bahati nzuri kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 22, ameeleza yale aliyotekeleza mwaka 2006/2007, magari kumi na sita na Wilaya akazitaja, lakini pia katika ukurasa wa 23 ametaja anategemea kununua magari kumi na tano. Nilikuwa nimeomba sana ifikiwi Wilaya ya Misungwi ina matatizo makubwa, kijiografia imekaa vibaya kweli, ukichukuliwa kuanzia Fela uende mpaka Mwawile-Mahando ni umbali mrefu kweli. Nimefika ofisini kwake *especially* kwa wakaguzi, nilimkuta Mama Mteleka, nikawaeleza haya masuala wakasema labda bajeti hii. Sasa sikusikia wakati wa majibu, napenda basi Mheshimiwa Waziri alione hilo na naomba jibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kumjibu Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, kuhusu hoja yake aliyoitoa kuhusu mahitaji makubwa ya gari katika Wilaya yake ya Misungwi. Ni kweli tutanunua magari kumi na tano, lakini mara nyingi huwa tunatoa kipaumbele kwa Wilaya ambazo zina mazingira magumu ili kuwawezesha wakaguzi kufika sehemu nyingi. Kwa hiyo tunapokea, tuangalie hilo ombi, mambo yakikubali kufuatana na mazingira ya kule, basi ombi lake litafanikiwa lakini tunalifanyia kazi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> .....	Sh. 593,716,500
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> .....	Sh. 1,436,240,900
Kif. 2001 – <i>Chief Education Officer</i> .....	Sh. 4,110,732,700
Kif. 2002 – <i>Inspectorate</i> .....	Sh. 4,600,063,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - <i>Basic Education</i> .....	Sh. 12,742,015,100
--	--------------------

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Japokuwa sijatajwa kama nimechangia, lakini nasema nimechangia kabisa kwa maandishi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Haya umeshaingizwa kwenye orodha. Lngine?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 3001, kifungu 250100 - Mshahara wa Waziri. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inayofuata.

**MWENYEKITI:** Hakuna mshahara wa Waziri huko.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** 260200 – *Educational Materials, Supplies and Services*.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani? Anza ni programu gani, *subvote* gani na *item* gani?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** *Subvote* 3001, kifungu 260200...

**MWENYEKITI:** Mmh, *Educational Materials, Supplies and Services*?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Hapana.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia kwa kusema kuwa japokuwa Serikali imetoa shilingi milioni tisa kwa ajili ya kuwajengea bweni watoto wasioona na wenye mtindio wa akili, pesa hizo bado hazitoshelezi.

Inatakiwa Serikali ifanye mpango mwingine tena waweze kuongeza pesa nyingine kwa sababu zile wamezituma kwa ajili ya watoto wale ishirini na saba niliowataja. Lakini katika Mkoa wa Kigoma watoto ambao wana mtindio wa akili na wale wasioona ni wengi.

Kwa hiyo, nikawa nimeionba Serikali, iweze kuongeza pesa nyingine ili wajenge mabweni siyo bweni moja. Kwa sababu watakaposikia kuwa wamejenga lile bweni moja, itabidi wale watoto wote ambao wapo mitaani waletwe kusoma. Kwa hiyo, naiomba Serikali waongeze pesa ili waweze kujengewa mabweni mengine. Vilevile nimezungumzia kuwa, kwa kuwa walimu wana hali ngumu hata kama wakiongezewa mishahara...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sijapata, naomba ukae chini. Kwanza, kifungu hicho hakihusiki na mabweni wala watoto wenye mazingira maalum. Kinahusika na mambo ya vifaa, madaftari, penseli na nini, tena shule za msingi siyo chenyewe hata kidogo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Secondary Education* .....Sh. 103,757,460,700

Kif. 5001 – *Teacher Education*.....Sh. 18,286,193,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

Kif. 1001 – *Administration and General*.....Sh. 644,000,000

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 1001, kifungu kidogo 6281 - *Strengthening of NECTA*. Wakati Kamati ya Huduma za Jamii, inatembelea Baraza la Mitihani kule *Mbezi One*, tuliona maendeleo yake ni mazuri, lakini tatizo lilikuwa ni fedha. Wale *contractors* walikuwa wanadai karibu shilingi 11,000,000,000 na *actually* kuanzia wakati ule, *interest rate* bado inapanda. Lakini ukiangalia fedha zilizotengwa ni ndogo sana, shilingi 320,000,000 na nadhani lile jengo lilikuwa karibu tayari kabisa na kwamba nilikuwa nategemea fedha hizi zingelipwa basi angalau kwa mwaka huu mitihani ya kidato cha nne iweze kusahihishiwa pale kutokana na nyongeza kubwa ya wanafunzi, yaani watahiniwa. Sasa naomba Waziri atuambie hali ikoje? Je, hizi fedha wanadhani kwamba wale *contractors* wanaweza kukabidhi lile jengo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ili niweze kumjibu Mheshimiwa Suzan A. J. Lyimo kama ifuatavyo: Ni kweli shilingi 320,000,000 hazitoshi. Wizara ya Elimu inalifahamu suala hili lakini imechukua utaratibu mwingine kabisa tofauti na huu ili kukabiliana na mahitaji. Kwa hiyo, linafanyiwa kazi katika ngazi za juu. Nashukuru.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *Subvote* 1001, kifungu 6324, ni leo asubuhi Naibu Waziri alizungumza sasa hivi wanaanzisha na kuendeleza maktaba za Wilaya lakini cha kusikitisha Mkoa wa Lindi hata Maktaba ya Mkoa hatuna. Je, Waziri anatoa tamko gani, kuwaambia wananchi wa Lindi ambao wanahitaji maendeleo na wanataka kuruka kabisa sambamba na Mikoa mingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki S. Lulida, katika kanuni zetu hatupaswi kuuliza maswali yanayodai kuongeza fedha. Iliyopo hapa ni *Construction of Dodoma Library*; Lindi haipo hapa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Policy and Planning*.....Sh. 21,056,110,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Chief Education Officer*.....Sh. 2,540,000,000

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa msizurure wakati wa Kamati. Mimi nafikiri yule anataka kuongea kumbe amesimama tu. Mheshimiwa nani yule. (*Kicheko*)

Haya Mheshimiwa Juma H. Killimbah.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia *subvote* 2001 - *Chief Education Officer*. Nazungumzia kifungu kidogo 4394 - *Family Life Education*. Nilikuwa naangalia hapa 2005/2006, kulikuwa kuna bajeti yake iliwekwa, lakini 2006/2007 hakuna chochote kilichowekwa. Sasa napenda tu labda Mheshimiwa Waziri anieleze kulingana na hali ya sasa hivi tuliyonayo, wimbi la mimba mashuleni na kila kitu; tunaona hatuna haja kweli ya kuwa na fungu hili la kuweza kutoa elimu kwa ajili ya hiyo?

**MWENYEKITI:** Anauliza ile *Family Life Education* sasa imekwenda wapi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Juma H. Killimbah kama ifuatavyo: Fedha za ushauri nasaha na yote yanayohusiana na matatizo ya maambukizi ya UKIMWI, zipo kwenye kifungu kinachofuata pale chini 5492 ambapo kuna shilingi 2,000,000,000, ndipo hapo zitakapopatikana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Inspectorate*.....Sh. 200,000,000

Kif. 3001 – *Basic Education*.....Sh. 14,352,014,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4001 – *Secondary Education*.....Sh. 70,470,000,000

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nisaidiwe hapa kwenye *subvote* 4001, kifungu kidogo 4301 - *Construction of Lab and Supply of Lab Equipment*. Hapa sioni pesa yoyote iliyotengwa, sasa napata wasiwasi kutokana na mkakati mzima wa Wizara; je, *lab* hizi zitatengenezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, sana sana unaweza kuuliza kwamba, hizo *laboratories* zitatengenezwa wapi, hapa hakuna fedha. Mheshimiwa Waziri, unaweza kujibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za ujenzi wa maabara na vifaa vyake vyote vipo kwenye zile shilingi 70,470,000,000 ambazo ziko kwenye kifungu 4390.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge umeelewa kwamba, badala ya kifungu 4301, Mheshimiwa Waziri amekwenda kwenye kifungu 4390 - *Secondary Education Development Programme*, kwenye *SEDP* zipo shilingi 70,470,000,000.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi niko katika kifungu hicho hicho 4001 - *Secondary Education*. Nina hoja katika vifungu viwili: Kifungu cha kwanza ni kile kifungu kidogo cha 4325, kinachozungumzia kuhusu *improvement performance of girls in secondary schools*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ajenda yetu ni kuendeleza sana watoto wa kike katika masuala ya elimu. Lakini kifungu hiki sasa kinaonesha kimeanza kujenga tabia ya kutopewa fedha kabisa toka bajeti ya mwaka 2006/2007 mpaka mwaka huu. Kwa hiyo, naomba hapo nipewe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lingine ni kile kifungu kidogo cha 4390 - *Secondary Education Development Programme (SEDP)*. Ninaambatanisha kifungu hicho na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu ujenzi wa hosteli kwa ajili ya sekondari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kujua tunao mgogoro mkubwa sana kati yetu sisi wananchi wa Sekondari ya Maposeni, ambapo mkataba wa shule yetu ya Sekondari ya Maposeni na Wizara ya Elimu mwaka 2003 ilikuwa ni Ubalozzi wa Japan kujenga bwani la watoto wa kike na Wizara kutoa vitanda kwa ajili ya watoto wale. Suala hilo halijafanyika mpaka leo hii. Sasa naomba kufahamu Wizara itatekeleza lini ahadi hiyo ambayo ilitia sainsi kati yetu na Serikali ya Japan na Japan ilishatimiza lengo lake? Mpaka leo watoto wale hawajaanza kulala kwenye ile hosteli mpaka majengo yale yameanza kuharibika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo.

**MWENYEKITI:** Kwanza tukubaliane kwamba vifungu 4325 na 4374 havina fedha kwa mwaka huu. Kwa hiyo basi, Waziri jibu kifungu 4390.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa ufafanuzi wako ni kweli fedha zote zimehamishiwa kwenye kifungu 4390, yaani *SEDP*; shilingi bilioni tano ambazo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 65 ambazo ni fedha kutoka nje. Hata suala ambalo amelizungumza Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ni kweli kabisa suala hilo tunalifahamu na mimi ninaamini kabisa Mheshimiwa Mbunge ameliongelea ili watu wa Jimboni kwake Peramiho wasikie ambapo ni jambo zuri sana. Kwa sababu tulishaongea, tulipeleka shilingi milioni nne, tuliandika na tukatumia *minus works* na nilikwenda na kumbukumbu ambazo zipo Wizarani nikamwonesha. Lakini pia nikamwahidi kwamba, tutapeleka shilingi milioni tano. Kwa hiyo, nadhani hayo ameyazungumza ili wapiga kura wasikie ni jambo zuri tu. Namshukuru sana. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri anielewe. Fedha hizo zimekuwa zikitengwa na kupelekwa kwenye Shule ya Sekondari ya Maposeni katika utaratibu wa *minus works*, kwa maana ya *maintenance*. Shule ile ni ya muda mrefu na kwa kweli inahitaji matengenezo. Sasa tunapopelekwa fedha ya ahadi ya Serikali kwa ajili ya vitanda katika kifungu kingine cha matengenezo ni kufanya shule ile ikose haki ya matengenezo na ishindwe kufikia lengo la kupata vitanda kulingana na utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Shule ya Sekondari ya Maposeni ipewe haki ya fedha za matengenezo kama shule nyingine, lakini ipewe fedha za vitanda kulingana na ahadi iliyotolewa na Serikali kwa utaratibu uliopangwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, tunazidi kuelewa kwamba, *maintenance* na vitanda bila shaka vitaonekana kwenye *Supply Vote* na siyo *development per se*. Mheshimiwa Waziri, kama unapenda kujibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshukuru Mheshimiwa Mbunge. Kitu cha maana hapa ni mawasiliano, kuhakikisha kwamba, fedha zile zinafika na maelekezo yanafuata pia. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nazungumzia *Sub-vote* 4001, lakini pia *items* zile zote tatu ambazo hazina fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, umetoa maelekezo, lakini mimi nimekuwa nashangaa kidogo, ingawa wenzangu wameshalizungumza, linanishangaza kwa sababu tuna *items* muhimu pale ujenzi wa maabara, halafu *improvement performance of girls in secondary schools, and teaching equipment for secondary*



*schools*. Sasa vifungu vyote havina fedha, lakini maelezo ni kwamba, fedha zote zipo kwenye *item* ya mwisho ya 4390.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani hili linatuchanganya Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tunapaswa tuyasimamie mambo haya. Kwa sababu sasa hivi tunaweza tusijue kabisa fedha kiasi gani zinaenda kwenye ujenzi wa maabara, fedha kiasi gani zinaenda *teaching equipment for secondary schools*, lakini pia fedha kiasi gani zinaenda kwa ajili ya *improvement performance of girls in secondary schools*?

Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri hii Wizara ya Elimu ndiyo inayopaswa itupe mfano katika kuandaa vitabu ili sisi Waheshimiwa Wabunge, tusipate shida tunapofuatilia, lakini pia tuwe na urahisi katika kusimamia. Kwa hiyo, naomba pengine Waziri atoe tamko kwamba, hili lilifanywa *deliberately* au pia ilikuwa ni *oversight*. Asante.

**MWENYEKITI:** Sasa kama ingekuwa kompyuta imependa kufuta hivi vifungu, vingekuwa vimefutika, lakini kwa sababu utaratibu wa Hazina wana-keep vifungu hata wakiweka *zero* wanaweka kusudi kila *item* isipotee kama *item*. Sasa kwa maana hiyo, nasema kuulizia vile vifungu vyenye *zero amount*, kanuni zetu zinakataza, hatuwezi kuongeza fedha sasa. Sana sana baadaye Waziri labda anaweza kutoa *breakdown* ya *item* 4390, labda kwa msingi huo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi nijibu hoja za Mheshimiwa Godfrey Zambi kama ifuatavyo: Mradi ule wa *Girls Secondary Schools, Education Support* uliisha. Ulikuwa unapata msaada kutoka *World Bank* na kulikuwa na Kitengo, yaani *Unit* pale Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ule Mpango uliisha, lakini tukaona lazima utafutiwe fedha ili wanafunzi ambao tayari walishaanza kunufaika wanufaike. Kwa hiyo ni humo humo katika shilingi bilioni 70 ambapo sisi wenyewe tumeona ni vizuri tumalizie kuwasomesha wale wanafunzi walioko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kuhusiana na ujenzi kama nilivyozungumza kwenye Hotuba ya Bajeti, nilipokuwa nikizungumzia ujenzi wa nyumba 1,500, nilisema pale kwamba, tutakuwa na shilingi bilioni 13 ambazo ni asilimia 59 ya shilingi 21,719,330,000, ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wote kwa ujumla. Kwa hiyo, sisi tulivyoona tumepata shilingi bilioni 21 za ujenzi ndiyo tukakubaliana kwamba, mwaka huu kipaumbele ni nyumba za walimu. Kwa hiyo, tukachukua shilingi bilioni 13.5 kwa ajili ya ujenzi huo na ndiyo tukakubaliana kwamba, tujenge madarasa 800 kwa sababu mwaka huu kipaumbele ni nyumba za walimu.

Halafu tukaona kwamba tuchukue pia shilingi bilioni 15 hapo hapo kwa ajili ya vifaa vya kufundishia katika hiyo bilioni 70. Kwa hiyo, tulipanga sisi wenyewe kutokana na vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, shilingi bilioni 70 tumeigawa sisi wenyewe kutokana na vipaumbele na kwa msingi huo wakati wowote anapotaka ufafanuzi zaidi tuko tayari.

Lakini kama nilivyomtajia, tumeshagawa kabisa *capitation grant* shilingi bilioni 19, chakula cha wanafunzi shilingi bilioni tano na fedha nyingine ziko kwenye fungu la kwanza.

Kwa hiyo, kila kitu tumekipanga. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa taarifa zaidi tunaweza tukakaa pamoja, tukamwonesha jinsi ilivyo. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa jinsi alivyotoa maelezo vizuri sana. Wizara italeta *breakdown* ya fedha zote zile kadri zitakavyopelekwa Mikoani kabla ya Kikao hiki kuahirishwa ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge, kufuatilia fedha hizo. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho, lakini nasema baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimeridhika. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001- *Teacher Education* ..... Sh.970,622,700

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitishwa bila mabadiliko.

Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi  
kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa hotuba yao nzuri na majibu yao mazuri na tunawatakiwa kila la kheri kwa sababu Wizara hii inawagusa watanzania wote na ndiyo kipaumbele cha Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sina matangazo mengine na nina suala fulani tutajadiliana kesho kuhusu utaratibu, nasema kama inatokea Waziri amejibu swali na Mheshimiwa Mbunge hakuridhika, kuna utaratibu wake ambapo anaweza kuja kutoa maelezo binafsi kwamba, wakati Waziri fulani anajibu swali sikuridhika na kitu fulani.

Sasa kwa hapa nadhani wanazungumzia swali aliloulizia Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo kuhusu majibu aliyoyatoa zamani Naibu Waziri, lakini sasa Waziri mwenye madaraka na Wizara hii ame-clarify suala zima. Kwa hiyo, nadhani hoja hiyo haipo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawashukuru kwa kazi njema ya leo, tumeifanya vizuri, nawatakiwa usiku mwema. Sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.52 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano  
Tarehe 11 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*